

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WAKUMI

Kikao cha Pili – Tarehe 31 Januari, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Karibuni kwenye kikao chetu cha pili.

Katibu!

NDG. THEONEST RUHULABAKE – KATIBU MEZANI

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMMAVU:**

Maelezo ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2018 *(The Public Service Social Security Fund Bill, 2018)*.

**NDG. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI
YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Mfuko

wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2018 (*The Public Service Social Security Fund Bill, 2018*).

NDG. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:-

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2018 (*The Public Service Social Security Fund Bill, 2018*)

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Ahsante. Swali letu la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na linaulizwa na Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini.

Na. 16

Mji wa Kibaha kuwa Manispaa

MHE. SILVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Mji wa Kibaha ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani na yapo maombi yaliyokwishapelekwa Serikalini kuomba Mji huo upewe hadhi ya kuwa Manispaa lakini hakuna majibu kwa ombi hilo hadi sasa:-

Je, ni kwa nini mpaka sasa Serikali haijaupa hadhi Mji huo kuwa Manispaa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maombi ya kuupandisha hadhi Mji wa Kibaha kuwa Manispaa kupokelewa mwezi Agosti, 2016; Ofisi ya Rais , TAMISEMI ilifanya uhakiki uliobaini kuwa Mji wa Kibaha ulikuwa na wakazi 128,488 (sensa ya Mwaka 2012), Kata 14, Mitaa 73 ambapo ni asilimia 56 tu ya wakazi ndio walikuwa wakipata huduma za maji safi na pia haukuwa na mpango kabambe wa uendelezaji wa Mji (*Master plan*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mwongozo wa Serikali wa mwaka 2014, vigezo vya kupandisha hadhi miji kuwa manispaa unatakiwa kuwa na wakazi si chini ya 300,000, Kata si chini ya 15, Mitaa si chini ya 75, wakazi wanaopata huduma za maji wawe si chini ya asilimia 75 ya wakazi wote wa mji na uwepo mpango kabambe wa uendelezaji wa Mji (*Master plan*). Kutokana na vigezo hivyo kutofikiwa, ilidhihirika kuwa Mji wa kibaha haukuwa umefuzu kupandishwa hadhi kuwa Manispaa. Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani alijulishwa matokeo hayo kwa barua yenye kumb. Na. CCB.132/394/01/16 ya tarehe 12 Juni, 2017.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Koka, swali la nyongeza.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Ikumbukwe kuwa Mji huo wa Kibaha ndio Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani wenye Wilaya sita na yenye idadi ya watu zaidi ya 1,100,000, Mji huu wa Kibaha umekuwa unaongoza katika ujenzi wa viwanda ukiwa na viwanda vikubwa sita, vya kati 16, vidogo 78, vinavyoendelezwa kujengwa vitatu na ambavyo vipo katika taratibu za ujenzi kwenye makaratasi 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipata kikwazo kikubwa hasa kwa wawekezaji hasa wanapotaka

kuendeleza viwanda wanapobaini kwamba huu ni mji tu na wala hauna hadhi ya Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo basi na tukizingatia kwamba Sera Kuu ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwenda katika uchumi wa kati ni viwanda na inatekelezwa vizuri na kipekee na kwa kuongoza kwa mji wa kibaha, ni kwa nini sasa Serikali isitoe upendeleo wa pekee na kuupatia mji huu hadhi ya manispaa ili tuweze kwenda kwa kasi kulingana na sera ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi wa Kibaha kwa utiifu na unyenyekevu kabisa wanaomba ombi lao hili lipewe uzito wa kipekee. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nimsifu Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini kwa jinsi anavyopangilia hoja zake kwa niaba ya wananchi wa Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa na mwongozo wa Serikali wa mwaka 2014 bado tunahimiza kwamba Halmashauri ya Mji wa Kibaha ifanye kila linalowezekana ili kuweza kutimiza vigezo hivi nilivyovitaja mwanzoni kwenye jibu la msingi ili waweze kufikia hadhi ya kupandishwa kuwa Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kwa kweli tunaungana nao wakazi wa Kibaha. Ni mji wa muda mrefu na sisi tunashangaa kwa nini hawajaweza kuwavutia watu wengi waongezeke kwenye Mji. Hii idadi ya watu wote waliotaja inafanana na idadi ya wakazi wa Mkoa mzima wa Pwani. Kwa mujibu wa sensa iliyofanyika mwaka 2012, Mji wenyewe wa kibaha ambao ndio uko kwenye Halmashauri ya Mji wa Kibaha ulikuwa na wakazi 128,488, hizo ndizo taarifa tulizonazo. Kwa hiyo pamoja na kutilia uzito

ombi lake bado tunahimiza kwamba Mji wa Kibaha wajitahidi kutimiza vigezo vilivyowekwa. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Bagamoyo imepata hadhi ya Mamlaka ya Mji Mdogo mwaka 2005 na miaka 10 baadaye mwaka 2015 baada ya kujitathimini na kuona tumetimiza vigezo tumeomba kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji. Je, Serikali inatupa jibu gani kuhusu Bagamoyo kupandishwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tulipokea maombi ya Mji wa Bagamoyo kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji sawa sawa na ambavyo tumepokea maombi mengi ya aina hiyo. Kwa sababu kupandisha hadhi Mji kuwa Halmashauri ya Mji kunaweza kusababisha ongezeko la mahitaji mengi ya kiutawala, bado maombi hayo yako kwenye mchakato na tutayafikiria muda utakapofika na kuzingatia na uwezo wa Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hussein.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja. Ningependa kujua Wilaya ya Nyangh'wale Makao yake Makuu ni Karumwa, lakini nikiuliza kila mara hapa kuhusu GNya Makao Makuu ya Wilaya Nyangh'wale ambayo ni Karumwa, leo hili swali ni mara ya tano, kila nikiuliza naambiwa GN iko tayari lakini cha ajabu mpaka leo hatujakabidhiwa katika Halmashauri yetu ya Nyangh'wale. Je, GN hiyo tutakabidhiwa lini?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kuhusu *GM*.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba uniruhusu nitoke na Mheshimiwa Amar mara baada ya kipindi hiki twende kwenye Idara yetu ya Sheria ili tuweze kumpatia majibu sahihi.

NWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, linaelekezwa Ofisi hiyohiyo ya Rais, TAMISEMI na linaulizwa na Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mbunge wa viti Maalum.

Na. 17

Ugatuaji wa Madaraka

MHE. SHALLY J. RAYMOND aliuliza:-

Halmashauri zina wataalam wa kusimamia na kutekeleza mipango yao na zina uwezo kisheria kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo, elimu, afya, maji kilimo na ardhi pasipo kuingiliwa. Viongozi na Watendaji wa Serikali ngazi za Mkoa na Wilaya huambiwa watawajibishwa kufikia malengo mathalani, katika ujenzi wa maabara, madarasa na kutengeneza madawati:-

Je, mipaka ipi ni ya kinadharia (*theoretical*) na ipi inatekeleza (*practical*) kiutendaji na uwajibikaji kati ya viongozi wa Serikali Kuu na Halmashauri za Majiji, Miji na Wilaya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugatuzi wa madaraka ya kisiasa, fedha na utawala kutoka Serikali Kuu kwenda kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa umetokana na mahitaji ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 145 na 146. Madhumuni ya ugatuzi ni kuwapa wananchi kupitia Mabaraza yao ya Madiwani, uwezo wa kufanya maamuzi kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Mitaa zimeundwa kwa mujibu wa Sheria Na.7 (Mamlaka za Wilaya) na Sheria Na.8 (Mamlaka za Miji)kwa malengo ya kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma mbalimbali za jamii kwa wananchi pamoja na kusimamia ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sheria kuweka utaratibu wa Serikali za Mitaa kujiamulia mambo yake kupitia vikao rasmi, hazijapewa uwezo wa kukataa maelekezo ya Serikali Kuu. Kwa mujibu wa Sera ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1998, Serikali Kuu ina majukumu ya kutunga sera, kutoa miongozo ya namna bora ya kutekeleza sera, kuandaa mikakati ya kitaifa, kuweka mazingira bora ya utekelezaji wa sera kwa kuzipatia Serikali za Mitaa rasilimali watu, rasilimali fedha na baadhi ya vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuweka viwango vya utekelezaji, kufuatilia utekelezaji ili kujiridhisha kuwa miongozo na viwango vinazingatiwa na kuchukua hatua dhidi ya utekelezaji usioridhisha inapobidi hasa inapobainika matumizi yasiyo sahihi ya fedha ikiwemo viwango duni vya miradi visivyolingana na thamani ya fedha iliyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali Kuu huwakilishwa na viongozi wa Mikoa na Wilaya katika kusimamia utekelezaji wa sera na miongozo, Viongozi Wakuu wa Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya hutekeleza majukumu yao ya kisheria ya kuziwezesha Serikali za Mitaa kutimiza majukumu yao kikamilifu ikiwemo kutekeleza maagizo halali na ushauri wa viongozi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikibainika kiongozi wa Mkoa au Wilaya ameshindwa kutimiza wajibu wake na hivyo kusababisha Mamlaka ya Serikali za Mtaa zisitimize vizuri majukumu yao, Mamlaka ya uteuzi huchukua hatua za kiutawala. Napenda kuisitiza kwamba Katiba, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi zikirejewa vizuri hakuna mgogoro wowote wa kimipaka wala kiutendaji utakaodhihiri.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali la nyongeza. Serikali iko moja nayo ni Serikali Kuu na hao wote waliotamkwa wanatekeleza kutokana na maagizo ya Serikali Kuu. Je, inakuwaje pale ambapo hela hazipelekwi za kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali inafuatilia vipi kuepusha migongano hiyo kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo fedha za kutekeleza mradi fulani hazijapelekwa zote mawasiliano yanafahamika kati ya waliopokea na waliopeleka. Kwa hiyo hayo yanakuwa ni maelezo sahihi wakati wa tathmini kwamba hatukuweza kutekeleza vizuri mradi huu au hatukukamilisha kwa sababu fedha imekuja nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hiyo ni mawasiliano ya ndani ya Serikali na mara nyingi imefanyika; lakini kitu kimoja kizuri kwa upande wa Serikali za Mitaa ni kwamba wanapopewa wakati mwingine fedha imezidi au imechelewa kuja imekuja mwishoni mwa mwaka wa fedha wenzetu wanaruhusiwa kubaki na fedha ile halafu mwezi

wa Saba wanakaa kwenye vikao vyao rasmi wanazipitisha kwa ajili ya matumizi yaliyovuka mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili kwamba tunafuatiliaje mgogoro; Serikali ina macho usiku na mchana. Kule kule ziliko Serikali za Mitaa wapo waangalizi wa Serikali ambao wanakusanya taarifa kila siku asubuhi na mchana kwa masaa yote. Kwa hiyo kama kuna harufu yoyote ya mgogoro Serikali Kuu huwa inapata taarifa hizo mara moja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Maida.

MHE. MAIDA H. ABDALLAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa miradi mingi ya maendeleo ngazi ya Halmashauri imekuwa ikisuasua na ikikwama kutokana na ucheleweshwaji wa fedha kutoka Hazina. Je, Serikali inatoa kauli gani katika ukamilishwaji wa miradi ya maendeleo iliyopitishwa na bajeti ya Serikali mwaka 2015/2016 na 2016/2017?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kusuasua kwa miradi; huku kunategemea na eneo na mradi na Halmashauri husika. Ziko Halmashauri ambazo tumekuwa tukizifuatilia na kuwashauri kuhusu matumizi ya fedha kwa wakati. Wakati mwingine wanakuwa na fedha kwenye akaunti lakini wakati mwingine watekelezaji kule kwenye mradi wanakuwa hawajui kama fedha zimekuja. Kwa hiyo matatizo mengine ni ya kimawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusesitiza, Halmashauri mara zinapopata fedha kutoka Serikali Kuu, zijipange kwa haraka na kwa wakati kutumia fedha hizo kwa ajili ya wananchi, wasiziache kwenye akaunti. Pale ambapo kuna ucheleweshaji wa aina yoyote wafanye mawasiliano haraka na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kusudi tuweze kufuatilia kwa wenzetu tuweze kusuluhisha suala hilo mara moja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Baadhi ya Wakuu wa Wilaya na Mikoa hapa nchini wamekuwa wakiwasimamisha hovy watumishi wa Serikali za Mitaa bila kufuata taratibu na sheria zilizopo. Je, nini kauli na msimamo wa Serikali katika suala hili? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kukanusha, hakuna sehemu yoyote ambayo Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa amesimamisha watu kazi hovy, hakuna! Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba usimamishaji wowote wa kazi unafuata masharti ya taratibu za kazi na sheria zinazomwongoza anayetoa amri hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, bado tupo Ofisi ya Rais, TAMISEMI, linaulizwa na Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Buyungu.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sjaruhusu swali langu lijibiwe naomba kusema tu kwamba madhara ya mikanda kuvuliwa sasa tumeyaona leo. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa, uliza swali!

MHE. KASUKU S. BILAGO: Naomba swali langu namba 18 sasa lijibiwe.

Na. 18

Wahitimu wa Elimu Maalum Kutopangiwa Vitengo Husika

MHE. KASUKU S. BILAGO aliuliza:-

Walimu wa Elimu Maalum wanapohitimu kwenye Vyuo vya Patandi na SEKOMU hawapelekwi kwenye shule za vitengo vya elimu maalum:-

(a) Je, Serikali haioni kama inapoteza rasilimali fedha na watu kwa kutoa elimu isiyo na tija kwa Walimu hao?

(b) Je, ni lini Serikali itawapanga walimu wenye elimu maalum kwenye shule na vitengo vyenye mahitaji hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo alilosema Mheshimiwa Bilago halihusiani kabisa na swali lake. Hata hivyo, nataka kumwambia kwamba kukatika kwa mkanda si kuvuliwa kwa mkanda. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Buyungu lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa mafunzo kwa Walimu ni miongoni mwa mikakati ya kuongeza tija ya kazi na ubora wa elimu inayotolewa, si kupoteza rasilimali fedha na rasilimaliwatu. Kwa muktadha huo, Chuo wa Walimu wa Elimu Maalum Patandi hudahili Walimu kutoka kazini ambao huhitimu kwa viwango vya astashahada na stashahada. Chuo Kikuu cha Elimu Maalum SEKOMU hudahili walimu kutoka kazini na pia Walimu wapya kwa kiwango cha shahada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vyuo vyote viwili, wahitimu waliodahiliwa kutoka kazini hurudi kwenye vituo vya vya kazi wakisubiri uhamisho kwenda kwenye shule za vitengo vya elimu maalum; na wahitimu ambao hudahiliwa kabla ya ajira huajiriwa na Serikali na kupangiwa shule zenye vitengo vya elimu maalum na wengine huajiriwa na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 2012 na 2015 Serikali iliajiri Walimu wapya 614 wa elimu maalum ambao walipangiwa kufundisha kwenye shule zenye vitengo vya elimu maalum. Hadi Desemba 2016 wapo Walimu 3,957 wa elimu maalum nchini sawa na asilimia 74.3 ya Walimu 5,324 wanaohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha Walimu wote wenye taaluma za elimu maalum wanatumika vizuri, naziielekeza Halmashauri zote ziwahamishie Walimu wa elimu maalum kwenye shule zenye vitengo vya elimu maalum ifikapo Desemba 31, 2018. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Maagizo yaliyotolewa na Serikali ya kuhamishia watoto wenye uhitaji wa elimu maalum ifikapo Desemba 31 mwaka huu hayatekelezeki; kwa sababu hata kwangu Wilaya ya Kakonko hakuna shule hiyo. Swali la kwanza, Serikali iko tayari kujenga shule ya watoto wenye uhitaji wa elimu maalum katika Wilaya ya Kakonko ikizingatiwa kwamba kuna watoto zaidi ya 200, Walimu wako watano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa maelezo hayo hayo ambayo nchi nzima itaathiriwa na agizo hili la Serikali, je, Serikali inaweza ikajiridhisha kwamba kila wilaya inapata shule ya watoto wenye vipaji maalum yenye mabweni ili kuwaokoa katika usumbufu wanaoupata? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, hajasahau taaluma yake licha ya kuwa Mbunge. Sasa naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasuku kama ifuatavyo:-

Serikali imeshatoa maagizo tangu mwaka jana kwamba kila halmashauri iteue shule angalau moja ili watoto wenye mahitaji maalum waweze kusomeshwa vizuri kwa mujibu wa mazingira ya mahitaji yao. Sasa kama kwenye wilaya yake hakuna hata shule moja, natoa agizo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo ili aweze kutekeleza agizo la Serikali lililotolewa tangu mwaka jana mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, amezungumza kwamba kwenye eneo lake la Ubunge wapo Walimu watano tu ambao wana taaluma ya elimu maalum. Namhakikishia kwa agizo ambalo limetolewa na Serikali leo; mimi nimesisitiza tu lilishatolewa siku nyingi, nasisitiza na kuwapa muda kwamba ifikapo Desemba 31, 2018 agizo hili linatekelezeka. Ndiyo maana tumewapa muda mrefu vinginevyo tungeweza kuwapa mwisho tarehe 30 mwezi wa Juni, lakini tumewapa muda mrefu hadi Desemba ya 2018 ili Halmashauri ziweze kujipanga vizuri kuhakikisha agizo linatekelezeka. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni kweli baadhi ya halmashauri zimetokeleza agizo la Serikali la kutenga shule moja kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum, lakini ni kweli pia kwamba shule hizi hazina vitendea kazi pamoja na Walimu wa kutosha na matokeo yake hata ufaulu wa watoto umekuwa ukitia shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano Shule ya Sekondari ya Viziwi Njombe ambayo matokeo ya *Form Four* ya mwaka uliopita shule nzima wamepata *division zero*. Sasa je, Serikali iko tayari pamoja na agizo hili kuhakikisha kwamba shule hizi zimepata Walimu wa kutosha na vitendea kazi ili hawa watoto waweze kuangaliwa kwa uzito ule ule wa watoto wengine ambao hawana mahitaji kama hayo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru amerejea kauli yangu kwamba agizo hili la kila Halmashauri kuwa na angalau shule moja ambayo watasoma watoto wenye mahitaji maalum. Napenda kumhakikishia kwamba agizo lile lililotolewa tangu mwaka jana lilienda sambamba na maagizo kwamba wahakikishe shule hizo zinakuwa na vifaa na vitendea kazi pamoja na Walimu ambao watawafundisha watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wake wa Njombe alioutoa, namwagiza Mkurugenzi wa Elimu pale ofisini kwangu afuatilie hiyo shule ya Njombe kuona je, ni ukosefu wa vifaa au ukosefu wa Walimu au ni tatizo la wanafunzi wenyewe lililosababisha wote wapate *division zero*? Hata hivyo, tunafuatilia na naagiza kwamba kila Halmashauri inapoteua shule ya watoto wenye mahitaji maalum wahakikishe kwamba kunakuwa na vifaa vya kutosha vya kuwafundishia. Ndiyo maana tunaita ni mahitaji maalum kwa sababu mtu ambaye ana ulemavu wa macho anahitaji vifaa maalum vya kusomea. Mtu ambaye ana ulemavu wa akili anahitaji vifaa maalum vya kusomea. Kwa hiyo wahakikishe vifaa vyote vinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wakati wa kupanga bajeti, kwa hiyo wahakikishe kwamba ikifika mwezi wa Saba tarehe moja, utekelezaji uanze kufanyika kwa mujibu wa maelezo ya Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo taarifa kwamba wako Walimu wa kufundisha shule za walemavu wamehitimu hawajaajiriwa bado. Tumefanya mazungumzo na Ofisi ya Waziri Mkuu, nimezungumza na Naibu Waziri anayeshughulika na walemavu, tuletewe orodha ya mahitaji ya Walimu kwa ajili shule za walemavu, tutapata kutoka Wizarani orodha ya wale ambao tayari wamehitimu. Tutawaajiri mara moja ili wanafunzi hao nao wapate elimu kama wanafunzi wengine. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa majibu yako.

Tunaendelea, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, anauliza swali lake kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 19

Kuanzishwa kwa shule ya Sekondari ya Mlundikwa

MHE. DESDERIUS J. MIPATA aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Nkandasi wamejitahidi kujenga shule ya Sekondari ya Kata ya Milundikwa hadi kufikia kidato cha sita lakini Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeamuru shule hiyo kuhamishwa mara moja kuanzia tarehe 1 Januari, 2017 kuachia Jeshi:-

(a) Wananchi walitumia muda na rasilimali zao kukamilisha ujenzi huo na sasa wanakwenda kuanza upya: je, ni upi mchango wa Wizara kwa ujenzi mpya wa shule?

(b) Wizara ya Elimu imeafiki kuhamishwa shule hiyo ya Kata; Je, ni upi mchango wa Wizara katika uhamishaji wa shule hiyo?

(c) Je, Serikali iko tayari kufanya uthamini wa miundombinu yote ya shule na majengo, yaliyojengwa na wananchi na thamani hiyo kuitoa katika fedha taslimu kwa ujenzo wa shule mpya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deusderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Jeshi la Kujenga Taifa kuhitaji eneo lao ilipokuwa imejengwa shule ya sekondari ya Milundikwa kuanzia Januari 2017, Serikali iliamishia shule hiyo kwenye eneo jipya la Kijiji cha Kasu A. Ushirikiano mzuri baina ya Serikali Kuu, Halmashauri, JKT, Mbunge na wananchi umewezesha ujenzi wa madarasa 13, vyoo matundu 26 na bweni moja kukamilika. Ujenzi wa maabara moja ya sayansi na bweni la pili uko katika hatua za mwisho ambapo wanafunzi 461 wakiwepo 92 wa kidato cha tano wanasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuchangia shilingi milioni mbili na wananchi wa Kata ya Nkandasi hususan Vijiji vya Katani, Kisula, Malongwe, Milundikwa, Kasu A na Kasu B kwa kujitolea kuchimba msingi, kukusanya mawe na mchanga, kuteka maji kwa ajili ya ujenzi kwa utaratibu wa 50 kwa 50 yaani wanaume 50, wanawake 50 kila siku ya ujenzi na kufyatua tofali za kuchoma laki mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi nayo ilitoa milioni arobaini na tisa kwa ajili ya ujenzi huo na Serikali Kuu kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa shilingi milioni mia mbili hamsini na tisa zilizotumika kujenga vyumba vya madarasa manne, vyoo matundu 22 na mabweni mawili ambapo ujenzi wa bweni la pili unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia ukamilishaji wa bweni la pili, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa mwezi Desemba, 2017 imepeleka shilingi milioni mia moja na Jeshi la Kujenga Taifa nalo lilichangia mabati 204, miche 300 ya miti kwa ajili ya mazingira na pia imetoa Walimu 10 wanajeshi ambao wanafundisha shuleni hapo. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali imependekeza shule hiyo itengewe shilingi milioni 230 ili kujenga maabara za sayansi mbili, jengo la utawala, bwalo na nyumba za Walimu endapo Bunge litaridhia.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mipata, swali la nyongeza.

MHE. DESUDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na nichukue nafasi hii kutambua juhudi kubwa sana na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya kwenye shule hii, lakini pia usimamizi mzuri uliotolewa na Mkuu wetu wa Wilaya na kwa hakika nimeridhika sana na majibu ya Serikali, lakini hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; shule hii ni ya bweni kwa kidato cha tano na cha sita. Haina nyumba ya *matron* wala haina uzio wa ulinzi wa wanafunzi. Naomba Serikali itoe hela zaidi kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na huduma ya vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Halmashauri ilijitahidi kuchimba kisima cha maji lakini kiko mbali kidogo na shule. Naomba Serikali itoe pesa zaidi kwa ajili ya kusogeza maji kwa ajili ya huduma ya wanafunzi hawa. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Mipata na Mheshimiwa Keissy,

wilaya yao ni miongoni mwa wilaya zinazoongoza katika ujenzi wa madarasa. Mwaka jana peke yake wamejenga madarasa 550 ambayo yanatakiwa kuzekwa sasa hivi. Kwa hiyo nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili hitaji la kwanza alilosema la nyumba ya *matron*, uzio; nilifika pale Milundikwa, nimeona kweli ni mahitaji halisi nayo tutayafikiri kadri ambavyo tunapata uwezo wa kifedha lakini kwa kushirikiana na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu kisima, shule ya sekondari ya Milundikwa tumeingiza kwenye orodha ya shule 100 ambazo zitapata ufadhili wa fedha kutoka kwa Sultan Qaboos wa Oman. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwakajoka, swali la nyongeza.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Tunduma ni mji unaokuwa sana na una msongamano mkubwa sana wa watoto; na mwaka wa jana Waheshimiwa Madiwani kwa kushirikiana na wananchi waliweza kuanzisha shule mpya nane ambazo zingine zina madarasa matatu, zingine zina madarasa nane lakini shule hizi mpaka sasa hivi hazijaanza kutumika kwa sababu *DC* amewasimamisha Madiwani. Kwa, hiyo kuna baadhi ya shughuli ambazo zilitakiwa zifanyike kama vioo na mambo mengine hayajafanyika kwa sababu wananchi pia walikuwa wanategemea Madiwani. Je, ni lini Serikali itatia mkazo kuhakikisha kwamba Madiwani wanarudi kazini ili shule hizi zianze kutumika haraka iwezekanavyo? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ilijitahidi ikajenga shule nane na hizi shule hazijaanza kutumika, ni kweli; lakini ni matokeo ya migogoro ambayo haina sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wenzetu wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma walipokaa kwenye kikao cha rasmi walikataa ushirikiano wa aina yoyote na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya. Sasa hilo likawa ni chanzo cha matatizo ambayo yamesababisha Waheshimiwa Madiwani wasiweze kutimiza majukumu yao. Suala lao tunalishughulikia kitaifa na namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalitatia hivi karibuni, ili kusudi waweze kuendelea kutekeleza majukumu yao kama kawaida. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kwa sababu ya muda. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua na linaelekezwa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Na. 20

Mradi wa TASAF III – Jimbo la Kaliua

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mradi wa *TASAF* awamu ya III katika vijiji ambavyo havijapata mradi katika Jimbo la Kaliua?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa dada yangu Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kunusuru kaya maskini ambao umodani ya *TASAF* awamu ya III unaendelea na utekelezaji wake katika halmashauri 159 pamoja na Unguja na Pemba. Mpango wa kunusuru kaya maskini una sehemu tatu ambazo ni uhaulishaji fedha kwa kutimiza masharti ya elimu na afya kwa watoto walioko shuleni na wale wanaotakiwa kuhudhuria kliniki pamoja na walengwa kufanya kazi za ajira ya muda. Sehemu nyingine ni kukuza uchumi wa kaya kwa kuweka akiba na kuanzisha miradi ya kuongeza kipato na uboreshaji wa miundombinu ya elimu na afya ili kuwawezesha walengwa kutimiza masharti ya elimu na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kunusuru kaya maskini unatekelezwa katika halmashauri 159 za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba lakini si katika vijiji, mitaa na shehia zote. Mpango ulipoanza utekelezaji mwaka 2013, rasilimali zilizokuwepo zilitosheleza kufikia asilimi 70 tu ya maeneo yote, ambayo ni sawa na vijiji, mitaa, shehia 9,989 na maeneo yaliyobaki yana vijiji, mitaa, shehia zaidi ya 5000. Kila halmashauri nchini imegusa kwa wastani wa asilimia 30 ya maeneo yake ambayo hayajafikiwa na mpango wa kunusuru kaya maskini na hili si kwa Jimbo la Kaliua pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba yapo maeneo yenye kaya zenye vigezo vya umaskini na uhitaji ambavyo bado havijafikiwa. Serikali ipo katika hatua za mwanzo za kuanza kuandaa sehemu ya pili ya *TASAF* awamu ya tatu ambayo itaendelea kwa miaka mingine mitano. Lengo la sehemu hii ya pili ni kuzifikia kaya zote maskini nchini na kuimarisha utekelezaji wa mpango na kuwasaidia wananchi kuwa na shughuli za kiuchumi na uzalishaji zaidi ili waweze kuondokana na umaskini.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba kumuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza Halmashauri ya Kaliua hatujafikiwa kuwa asilimia 70 tumefikiwa kwa asilimia 50 tu; kati ya vijiji 102 ni vijiji 54 tu. Katika vijiji ambavyo vilipata miradi kuna baadhi ya makosa ambayo yalifanyika katika kuanisha wale ambao walikuwa ni walengwa na baada ya kulalamika wakaambiwa waandike rufaa kwa sababu kuna wazee ambao wanastahili kupata mradi hawakupewa mradi wakaenda kupewa watu ambao wana uwezo. Leo ni mwaka wa pili waliambiwa waandike rufaa na mpaka leo rufaa haijarudi wala majina yao hayajaingizwa kwenye mradi, jambo ambalo limeleta manunguniko makubwa na masikitiko kwa sababu wanashindwa kuishi lakini wenzao ambao wana hali nzuri wanaendela kupata mradi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza swali.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba zile rufaa ambazo ziliandikwa na walengwa zinarudi ili waingizwe kwenye mradi waendeleo kunufaika na mradi huu wa kunusuru kaya maskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili mradi huu umeanza mwaka 2013, lakini kwa baadhi ya wilaya ikiwemo Kaliua tumeanza mwaka 2015, Januari. Naomba kuuliza Serikali kwa zile wilaya ambazo zilichelewa kupata mradi kwa miaka miwili, je, wataendeleza mradi kwa miaka 10 kama ilivyo kawaida au wataenda kufanya *evaluation* kama wanavyokwenda nchi nzima na kusahau kwamba sasa hivi mradi ni mwaka wa tatu wakati wengine ni mwaka wa tano? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa George Mkuchika.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Sakaya kwa jinsi anavyofuatilia kunusuru kaya maskini katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza kwamba kwake tumefikia asilimia 50 sio 70 kama katika maeneo mengine mimi kama Waziri ninayesimamia masuala ya *TASAF* nitafuatilia nione nini kimesababisha wao wawe chini kulingana na wilaya nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, anasema makosa yalifanyika katika kuwabaini walengwa na naomba nichukue nafasi kulieleza Bunge lako Tukufu, Watendaji wa *TASAF* hawana kauli juu ya nani asaidiwe. Wenye kauli juu ya nani asaidiwe ni watu katika mtaa, shehia, wao ndio wanaokaa wanasema hapa kijijini fulani bin fulani hali yake si nzuri. Kwa hiyo kwa yale maeneo ambayo makosa haya yamefanyika ni makosa ya wanavijiji na hasa viongozi wa vijiji kule Kaliua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo mmetuletea watu ambao hawakuhusika wamelipishwa fedha. Juzi nilikuwa Singida vijijini, watu walilipishwa milioni tatu laki tisa ambao hawahusiki, wamesharudisha milioni tatu bado laki tisa; na kila mahali wanarudisha. Katika maeneo mengine tumewawajibisha watendaji wa *TASAF* ambao walishiriki katika udanganyifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zile wilaya ambazo zilichelewa nalo siwezi kuwa na jibu la moja kwa moja hapa, nitalifanyia utafiti nijue walichelewa kwa sababu gani na nitachukua hatua stahiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Zitto Kabwe atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei.

MHE. ZITO Z. KABWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mchakato wa bajeti mpya ya Serikali ya Mwaka 2018/2019 unaendelea, kumekuwa na taarifa kwamba Serikali sasa inajiondoa katika mfumo wa *conditional cash transfer*, yaani kwenda kuwapa fedha wananchi na inaanzisha mfumo tofauti. Baadhi ya mikataba ambayo Wizara ya Fedha ilikuwa iingie na baadhi ya nchi wafadhili ikiwemo Benki ya Dunia, Wizara ya Fedha imesitisha kusaini kwa sababu Serikali haitaki

tena kuendelea kutoa hizi *conditional cash transfer*. Tunaomba taarifa rasmi ya Serikali ndani ya Bunge kuhusiana na jambo hili.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Waziri mwenye dhamana ya *TASAF* sina taarifa ya Serikali sasa hivi kujiondoa katika kuwapelekea hizi fedha. Taarifa nilizonazo ni kwamba sasa hivi tunafanya utafiti wa hizi fedha. Badala ya watu kwenda kupanga foleni pale wilayani kila siku tunaangalia uwezekano wa kupekea fedha zao kwa njia ya simu ili kuwaondolea usumbufu wa kwenda wilayani. Hilo ambalo anasema Mheshimiwa Zitto Kabwe kama analisema liko njiani, lakini halijafika mezani kwa Waziri mwenye dhamana ya *TASAF*. (*Makofi*)

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali kwa kuandaa mpango huu wa kunusuru kaya maskini. Katika jimbo langu Mheshimiwa Waziri alishawahi kuwa Mkuu wa Wilaya. Je, Mheshimiwa Waziri, kwa sababu anajua Bonde la Yaeda Chini kwa Hadzabe kule wana tatizo hili la umaskini. Je, ataweza kutuongezea angalau Vijiji vile Mungwamono, Eshkeshi na Endagechani tukapata zaidi msaada huu wa *TASAF*?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nakubali kwamba nilikuwa *DC* wa Mbulu 1983 mpaka 1988 na maeneo anayoyataja ya Yaeda Chini nimefika, wanakaa Wahadzabe, wanaishi kwa kuwinda tu badala ya kulima. Nataka nimwahidi kwamba kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, wanachotakiwa wao ni kuzitambua zile kaya

maskini, wakituletea sisi tutachukua hatua. Nilipita siku nyingi kule Yaeda Chini, Mheshimiwa Mbunge akinialika kwenda kuwahamasisha, nitashirikiana naye.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dokta Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo na linaelekezwa kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na. 21

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Mradi wa EPZA-
Bagamoyo**

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA aliuliza:-

Wananchi wapatao 1,025 wa Vijiji vya Kiromo, Zinga, Pande, Mlingotini na Kondo walifanyiwa uthamini wa mali zao tangu mwaka 2008 ili kupisha mradi wa EPZA Bagamoyo lakini hadi sasa hawajalipwa fidia:-

Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi hao fidia stahiki?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la ukanda maalum la kiuchumi la Bagamoyo (*Bagamoyo Special Economic Zone*) ni moja ya miradi ya kimkakati ya kitaifa. Awamu ya kwanza ya mradi huu inahusisha ujenzi wa bandari kubwa ya kisasa, eneo la viwanda kando ya bahari ambapo kwa kuanzia viwanda 190 vitajengwa na ujenzi wa miundombinu wezeshi na saidizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 mpaka mwaka 2010 Serikali ilifanya uthamini wa eneo lengwa lililokuwa na wananchi 2,273 na kubaini mahitaji ya fidia ya shilingi bilioni

58.771. Katika kipindi cha kati ya Agosti, 2012 na Februari, 2015 Serikali iliwalipa wananchi 1,155 jumla ya shilingi 26.66 kama fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kasi ndogo ya upatikanaji wa fedha ya fidia kutoka Bajeti Kuu ya Serikali mwaka 2017, Septemba, Serikali iliamua kubadilisha chanzo cha fedha za fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya utaratibu mpya wabia katika mradi wa Bagamoyo (*China Merchant na State Reserve Fund SGRF*) ya Oman watatoa fedha za fidia kwa makubaliano maalum na mbia mwenzao (Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwahakikishia wananchi wa vijiji vya Pande, Zinga, Kiromo, Mlingotini na Kondo kupitia kwa Mheshimiwa Mbunge wao, kuwa pindi majadiliano ya hawa wabia watatu yanayoendelea sasa yatakapokamilika watalipwa pesa zao mara moja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Mwezi Septemba, 2015 Serikali iliwalipa fidia wananchi wanaopisha mradi wa bandari katika Vijiji vya Pande na Mlingotini. Miongoni mwao wananchi 687 walibainika kwamba walipunjwa fidia zao; kwa hivyo Serikali iliwafanyia uhakiki mwezi wa kwanza mwaka jana ili kubaini fidia stahiki za wananchi hao. Je, ni lini wananchi hawa watalipwa fidia zao stahiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tarehe 22 Mwezi wa sita mwaka jana wakati anazindua kiwanda cha Elvin katika Kata ya Mapinga, Mheshimiwa Rais aliwatangazia wananchi wanaopisha mradi wa *EPZ* Bagamoyo kwamba wale wote ambao hawajalipwa fidia zao wanaweza

wakarudi sasa katika maeneo yao wayaendeleze maeneo yao. Je, ni lini EPZA na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo itawaruhusu wananchi hao kumiliki maeneo yao kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Rais?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofuatilia suala hili; lakini na yeye amekiri kwamba uhakiki ulifanyika kufuatilia wale waliopunjwa. Hapa tatizo kama nilivyosema kwenye suala la msingi ni ukosefu wa pesa za kutosha kutoka kwenye Bajeti ya Serikali kufidia maeneo ya kiuwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu Serikali imeshapata njia hii ya pili ya wabia watatu kutafuta pesa, nimshauri Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kusudi tupate fedha za kuweza kuwafidia kila mtu aridhike kusudi mradi wetu uweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusu tamko la Mheshimiwa Rais. Tamko la Mheshimiwa Rais ni maelekezo, watu wa EPZA, watu wa halmashauri na hapa kunapashwa kuingia wananchi, watakaa kusudi watekeleze tamko la Mheshimiwa Rais. Jambo ambalo ningependa Watanzania walielewe lile eneo limeamuliwa kwamba ni *Export Processing Zone*. Sasa kuna mchakato unapaswa ufanyike kusudi wewe ukawekeze vinginevyo; lakini kwa mamlaka niliyonayo EPZA na halmashauri na wananchi na wewe Mbunge tutakaa chini tuangalie namna ya kuwekeza kwa manufaa ya watu wote.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khadija Nassir.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Ripoti ya CAG inaonesha kwamba mdaiwa mkubwa wa viwanda vyetu vya ndani ni Serikali hususan halmashauri zetu. Je, Serikali ina mkakati gani

madhubuti ya kuanza kulipa madeni hayo ili kunusuru anguko la viwanda vyetu ambavyo tunavianzisha kwa nia njema? Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, Serikali inadaiwa na Serikali sasa tunaongeza jitihada za kuhakikisha kwamba kila stahili ya Serikali inakusanywa na kile kitakachokusanywa ndicho kitawalipa wale. Hatujawalipa wale kwa sababu na sisi hatujalipwa kuna watu hawapendi kulipa kodi, hata ukisoma *easy of doing business* Tanzania tunafanya vibaya kwa sababu watu hawataki kulipa kodi, lakini katika nchi nyingine huwezi kupewa haki nyingine hata kwenda kuchumbia kama huwezi kuonesha *tax clearance*.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini na linaelekezwa kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 22

**Utaratibu Unaotumika kwa Aliyepoteza
Cheti cha Taaluma**

MHE. COSATO D. CHUMI aliuliza:-

Kumekuwepo na matangazo mengi ya watu waliopoteza vyeti vya kitaaluma hasa vinavyotolewa na Baraza la Mitihani:-

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika pale mtu anapopoteza cheti ili aweze kupata cheti kingine?

(b) Je, anapata cheti halisi au nakala ya cheti?

(c) Baadhi ya wananchi wanalalamika kuwa kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa kwa Baraza la Mitihani wanapoombwa kuwasilisha cheti katika mamlaka fulani ambayo mtu ameomba kazi au nafasi ya masomo na hivyo kusababisha waombaji wengi kukosa nafasi kutokana na ucheleweshaji huo; je, ni taratibu gani mtu anatakiwa kuzifuata ili ombi lake lifanyiwe kazi ipasavyo na kwa wakati?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mhitimu aliyepoteza cheti hupatiwa cheti mbadala au uthibitisho wa matokeo kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi kuhusu upotevu wa cheti na kupata hati ya upotevu wa cheti na kupata hati ya upotevu. Lengo la kuripoti polisi ni kupata msaada wa kiuchunguzi ili kusaidia kukipata cheti kilichopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kutangaza gazetini kuhusu upotevu wa cheti kwa lengo la kuutarifu umma ili kusaidia kukipata cheti kilichopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, endapo hakikupatikana hata baada ya kutangazwa katika vyombo vya habari, mhitimu atajaza fomu ya ombi la cheti mbadala au uthibitisho wa matokeo na kuwasilisha Baraza la Mitihani la Tanzania. Fomu hiyo inapatikana kwenye Ofisi za Baraza la Mitihani Tanzania na pia kwenye tovuti ya Baraza ambayo ni www.necta.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne Baraza la Mitihani Tanzania hufanya uchunguzi wa uhalali wa umiliki wa cheti

husika na kutoa huduma stahiki. Wahitimu waliofanya mtihani kuanzia mwaka 2008 ambao vyeti vyao vina picha, hupatiwa vyeti mbadala (*Duplicate Certificate*) na waliofanya mtihani kabla ya mwaka 2008 hupatiwa uthibitisho wa matokeo ambao hutumwa kwa waajiri wao au mahali pengine kwa mahitaji yaliyotolewa na mwombaji. Hivyo, kundi hili la pili hawapewi cheti mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cheti mbadala kinachotolewa ni cheti halisi. Hata hivyo, kinaongezewa maandishi yanayosomeka *Duplicate* kuonesha kuwa cheti hicho kimetolewa kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwombaji wa cheti mbadala au uthibitisho wa matokeo hupatiwa huduma baada ya kukamilisha taratibu zinazohitajika na zilizowekwa.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza litalenga wale waliofanya mitihani kabla ya mwaka 2008 ambao hawapewi cheti mbadala. Kwa mujibu wa majibu ya Serikali badala ya kupewa cheti wanapewa uthibitisho na mara nyingi uthibitisho huu mtu anakuwa ameomba ili uelekezwe ama sehemu anayoomba kazi anayoomba kujiunga na masomo zaidi.

Sasa Serikali haioni umuhimu wa hata hawa ambao walipoteza Cheti ambao walihitimu kabla ya mwaka 2008, kuwafanyia utaratibu wa kuwapa hiyo *duplicate*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa mara nyingi watu wanaoomba Baraza la Mitihani liwasilishe hizo taarifa kama vyeti kule walikoomba kazi au masomo, vyeti hivyo mara nyingi uthibitisho upo kwamba, vimekuwa vinachelewa na hivyo kuwasababishia watu hao ama kukosa hizo nafasi za kazi walizoomba au nafasi za masomo.

Je, Serikali haioni haja ya kuwa na mifumo kama ya vyuo vya elimu ya juu ambapo mtu ambaye amepoteza cheti anaweza akapewa nakala hata mbili tatu akazitunza mwenyewe, midhali Serikali na Baraza la Mitihani limejiridhisha kwamba, huyo mtu kweli alihitimu masomo hayo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wahitimu waliomaliza shule kabla ya mwaka 2008, kwa sasa imekuwa ni vigumu kuwapatia vyeti mbadala kwa sababu wakati huo vyeti havikuwa vinabeba picha za wahitimu. Kwa hiyo tukitaka kubadilisha maana yake ni lazima tutafute picha za wale wote ambao wamemaliza shule kabla ya 2008. Kwa vyovyote vile ni kazi kubwa, hata hivyo, sio jambo ambalo haliwezekani kufanyika kwa hiyo, nalibeba tukajadiliane ndani ya Serikali kama linatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kuhusu kuchelewa kupatiwa nakala au cheti mbadala au uthibitisho kwa wale ambao wanakuwa wamepoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo ni kwamba, mara nyingi watu wanaenda kuomba vyeti mbadala au uthibitisho pale wanapokuwa na uhitaji. Ushauri wangu kwa Watanzania wote ni kwamba, kila mara unapopoteza cheti usisubiri mpaka uhitaji kutumia cheti hicho ndio ukaanze kutafuta mbadala au uthibitisho. Ukishapoteza anza taratibu za kuanza kutafuta, ili ikitokea kwamba, unahitaji iwe ni rahisi kwa sababu, tayari unakuwanacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa sasa kwa mwombaji yeyote yule, ukiomba inachukua angalau siku 30, lakini hizo ndiyo siku nyingi ambazo kinaweza kuchukua, ni *maximum*. Inaweza ikawa chini ya hapo na kwa sasa hivi

kwa kweli, Baraza la Mitihani la Taifa ni moja kati ya Taasisi za Serikali zinazofanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana kwa hiyo, mara nyingi hazifiki hata hizo siku ukikamilisha taratibu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pendekezo lake la kutumia utaratibu unaotumiwa na vyuo vikuu la kutoa nakala, naomba nilibebe, ni wazo zuri, tukaangalie namna ya kutekeleza, ili ikiwezekana tunapotoa cheti tutoe nakala kadhaa ili mtu aweze kutumia pale atakapopoteza. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa taarifa zinaeleza kwamba, vyeti vimekuwa vikizalishwa nje ya nchi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzalisha vyeti hapa nchini ili zoezi la kuvitoe liwe rahisi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo mimi vyeti vinatengenezwa hapa hapa nchini, tuna vifaa vya kisasa, Baraza la Mitihani lina vifaa vya kisasa sana na ni taasisi ambayo kwa ufanisi wake nchi nyingi sasa hivi zimeanza kuja kujifunza namna tunavyofanya. Kama Mbunge ana taarifa tofauti na hizi naomba tuonane baada ya Bunge hili ili nijue kwa nini yeye ana taarifa ambazo si sahihi.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, Mbunge wa Mwanga na linaelekezwa Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Na. 23

Utekelezaji wa REA Awamu ya I na II Wilaya ya Mwanga

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE aliuliza:-

Miradi ya *REA I* na *II* katika Wilaya ya Mwanga haikukamilika na fedha zilizokuwa zimepangwa hazikutumika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia umeme wananchi waliopitiwa na umeme huo bila kufungiwa?

(b) Je, Awamu ya III ya *REA* iliyozinduliwa Mwanga, mwezi Septemba, 2017 itaanza kutekelezwa lini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, Mbunge wa Mwanga, lenye Sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya vijiji 38 kati ya vijiji 44 vya Wilaya ya Mwanga vilipata umeme kupitia Awamu ya II ya Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini ambapo wateja zaidi ya 2,241 waliunganishiwa umeme. Aidha, vijiji sita vilivyosalia havikuweza kupatiwa umeme kutokana na Mkandarasi, Kampuni ya *SPENCON*, aliyekuwa anafanya kazi hiyo kushindwa kukamilisha kazi hiyo na mkataba wake kusitishwa mwezi Disemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) imempata Mkandarasi Kampuni ya *M/S Octopus Engineering Limited* atakayeikamilisha kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vilivyosalia kwa awamu ya pili. Kazi hizo zimeanza rasmi mwezi Januari, 2018 na zitakamilika ndani ya miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mradi wa REA Awamu ya Tatu katika Wilaya ya Mwanga ulianza mwezi Oktoba, 2017 chini ya Mkandarasi Kampuni ya *Urban and Rural Engineering Services Limited*. Kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 10.98; njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 urefu wa kilometa 24; ufungaji wa *transformer* 12 za kVA 50; pamoja na kuunganisha wateja wa awali 347. Gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 1.7 na shilingi bilioni 12.3; mradi huu utakamilika mwezi Juni, 2021.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Maghembe.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Wizara ya Nishati imesema mara nyingi ndani na nje ya Bunge kwamba katika vijiji ambavyo vinahusika na mradi wa REA watu wote walioko kwenye vijiji hivyo, hata wale ambao nyumba zao ni za majani watapewa umeme. Hata hivyo, katika utekelezaji wa miradi hii Awamu ya Kwanza na Pili katika Wilaya ya Mwanga ni familia chache sana zilizokuwa zimejitayarisha kupewa umeme ambazo zimefungiwa umeme huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa kwamba nia yake ni kuipa TANESCO biashara ya kuzifungia kaya hizo umeme kwa Sh.177,000/= baada ya mradi kukamilika. Je, sera hii tuliyotangaziwa hapa imefutwa lini ikaja hii ya TANESCO kuchagua watu wachache kuwapa umeme na wengine kuwaacha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tuliambiwa kwamba, mkandarasi huyu ambaye ameshindwa kazi ya kusambaza umeme pale awali hawezi tena kupewa kazi katika Wizara ya Nishati na Madini, hasa kazi ileile ambayo yeye alifukuzwa kwa kushindwa kutekeleza. Sasa katika Wilaya ya Mwanga aliyekuwa anatekeleza mradi huu kwa niaba ya SPENCON alikuwa bwana mmoja anaitwa *Mrs. Njarita & Company Limited*. Sasa Njarita huyo huyo

amepewa kazi ya kutekeleza mradi huo kwa jina lingine la *Octopus*. Je, inatuambia nini au inawezaje kututhibitishia kwamba, huyu aliyeshindwa kutekeleza huu mradi huko nyuma, sasa ataweza kutekeleza *round* hii? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe kwa maswali yake mawili ya nyongeza, lakini na kwa kazi nzuri anayofanya katika kufuatilia mahitaji ya nishati katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kwenye ziara wiki iliyopita katika Jimbo la Mheshimiwa Maghembe, kukagua maeneo mbalimbali ambako mradi huu wa *REA* Awamu ya Pili haukufanyika vizuri, lakini utakubaliana na mimi kwamba, ni kweli kuna mahitaji makubwa na kwa kuwa, hizi kazi zinatekelezwa kwa mujibu wa *scope* na kwamba, *scope* ile inakuwa haikidhi mahitaji, lakini Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutambua hilo imekuja na Mradi Mpya wa Ujazilizi (*densification*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa katika mkoa sita ya awali ya mfano. Ilipofika Mkoa wa Kilimanjaro na wao Mkandarasi Mshauri Elekezi yupo ndani ya mkoa ule kujaribu kufanya *feasibility study* kwa ajili ya mradi huu, *densification* kwa maeneo ambayo au kwa kaya ambazo hazijaguswa au taasisi za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie Mbunge hakuna ukweli wowote kwamba, zile kaya ambazo hazijaunganishwa nia ya kwamba, iipe kazi *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* ni Serikali ambayo nayo ina kazi ya kusambaza umeme, lakini kwa utaratibu mwingine, lakini si kweli kwamba, kaya hazifikiwi kwa sababu ya kuipa kazi *TANESCO*. *TANESCO* itaendelea na kazi ya kusambaza umeme, lakini kama umeme vijijini na ndio

maana Serikali imetambua uwepo wa ukubwa wa mahitaji imekuja na huo Mradi wa *densification*. Kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge zile kaya ambazo hazijaunganishwa, zile taasisi za umma ambazo hazijaunganishwa, zitaunganishwa kupitia mradi huu wa *densification* ambao umefanya vizuri katika Mikoa ya Songwe, Mbeya, Pwani, Arusha, Tanga, Iringa na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ameeleza kwamba mbona mkandarasi yuleyule ndio amepewa kazi na kwamba, Wizara itathibitishaje kwamba kazi zitafanyika. Ni kweli kazi ilifanywa na Kampuni ya *SPENCON* ambayo ndio ilikuwa *main contractor*. Huyu Kampuni ya *Njarita Octopus* walikuwa *Sub Contractor*. Uchunguzi uliofanyika na Serikali na Wakala wa Umeme Vijijini ulithibitisha kwamba, tatizo lilikuwa kwa *main Contractor* mwenyewe ambaye ni *Spenco* si hawa *Sub Contractor*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo nilipokuwa katika ziara tulikuwa na Mkandarasi huyu Njarita na sisi tumempa maelekezo na masharti, ndani ya miezi sita kazi zile zilizoshindwa kufanywa zimalizike na zikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nilipokuwa eneo la tukio mkandarasi alikuwa ameshaanza kazi na niliwaomba viongozi wa maeneo hayo, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri, pia nilizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mama yangu Anna Mghwira kwamba Ofisi yetu au Wizara yetu itasubiria taarifa za mara kwa mara za Mkandarasi huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wakandarasi hawa waliopewa kazi hii tutawafuatilia kwa kila hatua kuona kwamba, makosa yaliyojitokeza awamu zilizopita hayajitokezi tena. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, nakushukuru sana kwa majibu yako mazuri Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini angalia waliosimama humu kwa swali hili, wengi na muda sio rafiki

kwa hiyo, nitachukua wawili tu Waheshimiwa Wabunge. Najua ni tatizo na Serikali inaona, *REA III*, *REA II*, tufanye la maana.

Nitachukua watatu, mnisamehe Waheshimiwa, muda. Mheshimiwa Murad, Mheshimiwa Nnauye na Mheshimiwa Gekul.

MHE. SULEIMAN S. MURAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nina swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika masuala ambayo yanahusu umeme, Mwanga. Tatizo la Mwanga linafanana sana na tatizo la Mvomero. *REA* Awamu ya Pili ambayo Mkandarasi wake alikuwa *MDH Power* ameishia kwenye maeneo ya makao makuu ya vijiji, mradi ule haujafika kwenye kaya wala kwenye vitongoji vya ndani. Kwa namna hii maana halisi ya kupeleka umeme vijijini inapotea na nia na madhumuni ya Serikali ni wananchi wafaidike na wananchi ambao wana uwezo mdogo ni wale ambao wako ndani ya kwenye vitongoji. Je, Naibu Waziri yuko tayari sasa kutoa maelekezo kwa *contractor* huyu wa *REA* Awamu ya Pili aje amalizie mradi wake? Pia, yule wa Awamu ya Tatu ambaye ni *State...* (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, swali moja.

MHE. SULEIMAN S. MURAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, na yeye apewe maelekezo afike kwenye kaya zote. Na Mheshimiwa Naibu Waziri nakukaribisha Mvomero karibu sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Murad kwa swali lake la nyongeza na kazi anazoendelea kufanya za kufuatilia miradi ya umeme. Nakubaliana na yeye kwamba, huyu

Mkandarasi *MDH* kwa kweli hakufanya vizuri na hakuwa mkandarasi katika mkoa wake tu, lakini alikuwa mkandarasi pia katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi tumetoa maelekezo kwa *REA* kwa sababu, wakandarasi wote wa Miradi ya *REA* Awamu ya Pili ni Mikoa miwili tu Tanga na Arusha ambao wametimiza vigezo na wamemaliza kipindi cha uangalizi. Kwa hiyo mikoa mingi ina changamoto, Singida, Mbeya, Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Kwa hiyo, tumetoa maelekezo na tumewataka *REA* wafanye tathmini na tutachukua hatua na kwamba, maelekezo ni kwamba, awamu ya tatu isiruke kitongoji chochote wala taasisi ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, nimesema tangu awali kwamba, upungufu wa awamu ya pili tumeubaini, tathmini imefanyika, awamu ya tatu tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba, umeme huu au miradi hii inatimiza lengo lililotarajiwa na maelekezo ya Serikali kwamba, kila kitongoji kisirukwe. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nnauye na wa mwisho Mheshimiwa Gekul.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali chini ya Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri wanayofanya ya usambazaji wa umeme vijijini, hasa hii *REA* Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, kwa kuwa gharama za kuunganisha umeme wakati mradi unaendelea katika eneo ni Sh.27,000 na mradi ukishapita ni Sh.177,000; na kwa kuwa idadi nzuri na kubwa ya watumiaji wa umeme ni biashara nzuri kwa *TANESCO*, kwa nini sasa bei hii isiwe moja hiyohiyo ya 27,000 badala ya bei kupanda baada ya mradi kwisha? Kama haiwezekani, basi *REA* hawa waendeleo na kazi ya usambazaji wa nguzo na

miundombinu na *TANESCO* wafanye kazi moja tu ya kupeleka umeme na kukusanya kodi yao baada ya kupeleka umeme?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, Kaka yangu Nape Nnauye. Ni kweli bei ya kusambaza umeme ya vijijini ni Sh.27,000 kipindi cha mradi na hii ni hatua ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwamba, imegharamia gharama zote za uunganishwaji kwa umeme huu na kwamba mwananchi yeye gharama yake ni analipia *VAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wazo alilolisema kwamba, mara baada ya mradi kukamilika na miundombinu kukabidhiwa *TANESCO* ni kweli wananchi wanaunganishwa kwa bei ya Sh.177,000, lakini hata hivyo niseme hata hii bei pia, Sh.177,000 nayo ina mchango wa Serikali kwa sababu, mijini kwa bei hii wanaunganishwa kwa Sh.321,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wazo alilosema linapokelewa na litafanyiwa kazi na ni la msingi kwa sababu, Wizara yetu na Shirika letu la *TANESCO* na wadau wengine wa nishati kwamba, tunauza bidhaa ya umeme. Kwa hiyo, ni vema zaidi kwamba, tunapoiuza tupate wateja wengi, ili tupate mapato na kuendesha shughuli mbalimbali na uwekezaji mpya wa maeneo ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, nimelipokea na Serikali itaona utaratibu gani wa kufanya ili iweze kurahisisha. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiahidi mara nyingi sana kulipa fidia wananchi ambao maeneo yao yanapitiwa na umeme wa KV400. Miongoni mwa maeneo hayo ni Mkoa wa Manyara na katika Jimbo langu la Babati Mjini, wameahidi zaidi ya mara tatu na ahadi ya mwisho ni tarehe 17 Disemba, kwamba, mngewalipa. Hata hivyo, mpaka sasa Mheshimiwa Naibu Waziri mmekuwa mkisema kwamba, Wizara ya Fedha haiwapi pesa na Waziri wa Fedha yuko hapa. Naomba awatangazie wananchi wa Jimbo langu la Babati Mjini kwamba, ni lini wanawalipa fidia hiyo kwa sababu, wamechoka kusubiri?

MWENYEKITI: Lini mnawalipa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Pauline Gekul kwa swali lake zuri, lakini naomba niseme haijapata kutokea Wizara yetu ya Nishati ikasema Wizara ya Fedha haijatupa pesa, kwa sababu Serikali inafanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo ilijitokeza ni kwamba tulipata jedwali la thamani ya fidia. Wizara yetu ya Fedha kazi yake yeye hata inapoleta pesa ni kuangalia malipo yanafanyika kwa walengwa na kwa viwango sahihi. Kwa hiyo kulikuwa na changamoto ndogo ndogo tu za kumaliza kwa ajili ya kuthibitisha uhalali, kiwango na walipwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwambie Mheshimiwa Mbunge mradi huu wa KV400 msongo huu ni muhimu ambao unaunganisha na nchi ya jirani ya Kenya kwa kusafirisha umeme kwa maeneo mbalimbali. Kwa hiyo nimthibitishie kwamba fidia ya wananchi wa maeneo hayo italipwa muda si mrefu, ndani ya mwaka huu wa fedha na maandalizi yanaendelea vizuri. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Sussane Peter Masele, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Wizara ya Madini.

Na. 24

Kuwapatia leseni na vibali wachimbaji wadogo wadogo - Misungwi

MHE. SUSANNE P. MASELE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza kauli ya Mheshimiwa Rais kuhusu kuwapatia wachimbaji wadogo wadogo kipaumbele cha leseni na vibali vya kuchimba madini kwa kuonesha mfano kwa wachimbaji wadogo wa machimbo ya Dhahabu ya Ishokelahela, Misungwi?

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Susanne Masele naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama hapa, lakini vile vile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Imani kubwa aliyonipatia na akaona naweza kumsaidia kwenye Sekta hii ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Susanne Peter Masele Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wa Madini wadogo wa Ishokelahela Wilayani Misungwi walivamia na kuanza shughuli za uchimbaji wa madini ya dhahabu katika eneo la Leseni kubwa ya utafutaji wa madini inayomilikiwa na Kampuni ya *Carlton Kitongo Tanzania Limited* yenye ukubwa wa kilomita za mraba 12.4 tokea mwezi Julai, 2017. Kabla ya hapa wachimbaji hao walikuwepo lakini kwa kiasi kidogo. Mpaka kufikia sasa leseni hiyo imevamiwa na wachimbaji wadogo zaidi ya 1000 ambao wanachimba madini hayo ya dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leseni ya *Carlton Kitongo Tanzania Limited* ilitolewa tarehe 5 Agosti, 2014 na itamaliza muda wake wa awali tarehe 4 Agosti 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Wilaya ya Misungwi kwa kushirikiana na kampuni ya *Carlton Kitongo Tanzania Limited* ambaye ni mmiliki wa leseni hiyo waliamua kutenga eneo kwa ajili ya kuwaachia wachimbaji wadogo ambalo likuwa linamilikiwa na kampuni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubaliano hayo yalihitimishwa rasmi mwezi Desemba mwaka 2017 kati ya mmiliki wa leseni na vikundi ambayo viliungana kuunda kikundi kimoja kwa jina la *Basimbi and Buhunda Mining Group*. Nakala ya makubaliano hayo ipo Ofisi ya Madini Mwanza na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Misungwi. Vikundi hivyo vilipatikana baada ya Wizara kupitia Ofisi yetu ya Madini Mkoani Mwanza kutoa elimu ya umuhimu ya kujiunga katika vikundi na kuendesha shughuli za uchimbaji madini ili ziweze kuwa na tija zinazozingatia matakwa ya Sheria ya Madini na Kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza kauli ya Mheshimiwa Rais kuhusu kuwapatia wachimbaji wadogo kipaumbele cha leseni na vibali vya kuchimba madini, leseni za wachimbaji madini katika eneo hilo zitatolewa kwa vikundi hivyo mara tu baada ya taratibu za kisheria za kushughulikia maombi hayo kukamilika.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sussane Masele.

MHE. SUSANNE P. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, baada ya taratibu kukamilika, je, Serikali itachukua muda gani kuwapatia leseni wachimbaji hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, yamejitokeza madai kuwa zuio la mchanga pale bandarini makinikia halikuwagusa wachimbaji wakubwa tu hata wadogo pia.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wachimbaji hao wadogo wanasafisha mchanga wao hapa nchini ili kuendeleza uwekezaji na kutengeneza ajira zaidi kwa wachimbaji hawa wadogo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itachukua muda gani, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, taratibu za kuunda Tume ambayo ndiyo imepewa mamlaka ya leseni ya uchimbaji madini, iko katika hatua za mwisho za kuundwa. Mara itakapokamilika kazi hiyo itaanza mara moja, kwa hiyo, haitachukua muda mrefu sana baada ya Tume hiyo kuwa imeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la zuiro la mchanga, naomba nimhibitishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Watanzania, kwamba Sheria ya Madini haijazuia usafirishaji wa mchanga nje ya nchi isipokuwa zipo taratibu na sheria ambazo yule mtu anayetaka kusafirisha mchanga kama madini lazima azifuate kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba tumezuia yale makontena kwa sababu yalikuwa na mgogoro ambao Serikali tuliona kuna haja ya kujiridhisha kabla ya kuruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna wananchi ambao wana madini ya mchanga ambao wanataka kuyasafirisha kwenda nje ya nchi kama wengine ambavyo wanapata vibali na wao wafuate taratibu watapewa vibali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kapufi, atafuatia Mheshimiwa Kikwete.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Serikali iliahidi kutenga maeneo ya Ibindi, Dirifu,

Society na Kapanda kwa wachimbaji wadogo wa huko Mpanda, je, ni lini wachimbaji hawa watapatiwa leseni?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, lini watapewa leseni kwenye maeneo husika.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Kapufi kwa ufuatiliaji wake kwenye jambo hili. Kwa muda mfupi ambao nimeingia ofisini amekuwa mara nyingi akiniambia jambo hili juu ya wachimbaji wake wadogo wadogo. Naomba nitumie fursa hii kuwaambia Watanzania wote wakiwepo na wananchi wa Kibindi kwamba wale wote ambao wamejiunga kwenye vikundi wakaomba maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchimbaji madini Wizara ya Madini iko tayari kuwasaidia mara tu, Tume ya Madini itakapoanza kazi baada ya kuwa imekwishakuundwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mbunge wa Chalinze.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami nimpongeze Mheshimiwa Dotto kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo naomba niombe kuuliza au kupata kauli ya Serikali juu ya lini Serikali itaruhusu mwekezaji wetu *Gulf Concrete* awalipe fidia wananchi wapatao 80 wanaoishi katika maeneo mbalimbali ya Kata ya Lugoba ili waweze kuendeleza eneo lile na wao waweze kuondoka na kulinda afya zao?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTTO M. BITEKO): Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji wa *Gulf Concrete and Cement Product* ambaye yuko Chalinze kwenye Kijiji cha

Nguza amekuwa akichimba kwa muda mrefu kwenye eneo hilo; na kwa kweli anachimba kwenye eneo hilo ametengeneza ajira zaidi ya 170 kwa watu wa Chalinze ambako Mheshimiwa Mbunge anafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetoa mgogoro mdogo ambao sisi kama Wizara ya Madini tunaushughulikia. Mwekezaji huyu amechimba na akaingia kwenye eneo la mwekezaji mwingine ambaye ana leseni anaitwa *Global Mining*; ameingia kwenye eneo ambalo lina ukubwa kama hekta 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichofanya kwa sasa, tunataka tuumalize kwanza mgogoro huu ambao yeye *Gulf Concrete* ameingia kwenye eneo la mtu mwingine. Tukishamaliza twende kwenye hatua ya pili sasa ya kumsaidia Mwekezaji huyo ambaye kwa kweli ana tija kwa watu wa Chalinze na watu wa Mkoa wa Pwani aweze kulipa fidia ili aendeleze mradi wake.

MWENYEKITI: Nashukuru. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea tuko nyuma sana ya muda. Swali lililofuata linaulizwa na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini na linaelekezwa kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

Na. 25

Migogoro ya Ardhi Nchini

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA, aliuliza:-

Kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi nchini inayosababisha uvunjifu wa amani miongoni mwa wananchi na hata katika baadhi ya maeneo migogoro hiyo imesababisha vifo;

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kutatua migogoro hiyo?

(b) Kwa kuwa Maafisa Ardhi wengi ndiyo chanzo cha migogoro hiyo, je, ni Maafisa Ardhi wangapi wamechukuliwa hatua kwa kusababisha migogoro hiyo?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu kwanza kwa sababu ni mara ya kwanza mwaka huu niwatake heri ya mwaka mpya wote na tumshukuru Mungu kwamba tunaendelea kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa migogoro ya ardhi nchini na tayari imeweka mikakati mbalimbali ya kuitatua na kuzuia uwezekano wa kuibuka migogoro mipya. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kutoa elimu kwa watendaji wanaohusika na utatuzi wa migogoro ya ardhi kuanzia ngazi za Serikali za Mitaa hadi Serikali Kuu na kuzifanyia marekebisho sera na sheria mbalimbali zinazosimamia sekta ya ardhi;

(ii) Kuboresha Mabaraza ya Ardhi na kuyaongezea watumishi pamoja na vitendea kazi;

(iii) Kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya wilaya na vijiji; na

(iv) Kutekeleza mkakati wa kupima kila kipande cha ardhi nchini na kuboresha mifumo ya kutunza kumbukumbu za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imeanzisha utaratibu wa kushughulikia migogoro ya ardhi ambapo Mheshimiwa Waziri akiambatana na wataalam wa sekta ya ardhi amekuwa akikutana na wananchi papo kwa papo

na kutatua migogoro na changamoto zinazowakabili kwa mfumo ambao tunaita Funguka na Waziri wa Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi kwa namna moja ama nyingine husababisha pia na watendaji wa sekta ya ardhi wasio waaminifu; lakini Serikali imeendelea kuwachukulia hatua maofisa hao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 2014/2015 na 2016/2017, watumishi wanne wamesimamishwa kazi baada ya kufikishwa Mahakamani kutokana na ukiukwaji wa maadili ya Utumishi wa Umma; watumishi 16 walifukuzwa kazi kwa makosa mbalimbali ya kiutendaji; na watumishi 19 waliandikiwa barua za onyo na kutakiwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watendaji wa sekta ya ardhi walio chini ya usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Wizara imekuwa ikishirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika kuhakikisha kuwa hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya watendaji hao ambao wamekuwa wakisababisha migogoro kutokana na kutowajibika au kukiuka masharti ya ajira zao.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwakasaka.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Tabora Manispaa imeathirika sana na migogoro ya ardhi. Kuna kata ambazo zinapakana na maeneo ya jeshi, ambazo ni Kata za Cheyo, Mbugani, Tambuka Reli, Uyui na Micha. Maeneo yale yamekuwa na migogoro ya mipaka ya muda mrefu. Je, Wizara ya Ardhi imejipangaje kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi ili waweze kuoanisha sasa mipaka halisi ili kuweza kutatua migogoro hii ya mipaka katika kata hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Tabora kama nilivyosema manispaa imekuwa na migogoro mikubwa ya ardhi na hasa bomoa bomoa. Tabora imeathiriwa sana na zoezi la bomoa bomoa; si maeneo ya reli tu lakini hata maeneo mengine yanayopaka na mashule kama Tabora *Girls...*

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza swali.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Wananchi wale na maafisa kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wengine si waaminifu. Je, Serikali kwa kuwa hawa wananchi wengi waliobomolewa hayakuwa makosa yao, inawachukulia hatua gani hawa ambao wamesababisha wananchi wamepata hasara kubwa na sasa hawana hata amani na wamekuwa katika hali isiyoeleweka?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza amezungumza habari ya mipaka kuathiri maeneo yaliyopakana na Jeshi na ametaja kata ya Cheyo, Tambuka Reli na nyingine. Naomba tu nimthibitishie Mheshimiwa Mwakasaka kwamba Wizara ya Ulinzi ilishachukua hatua ya kuunda Kamati ambayo imepitia katika maeneo yote ambayo yana migogoro ya Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo hayo walikuwa wakifika wanaongea na watu wa eneo lile na kuweza kubainisha mipaka; kwa sababu kuna mengine ambayo wananchi lakini maeneo mengine Jeshi lilingia ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kabla ya kuanza kuweka mipaka upya au kuipitia kwanza wanachambua yale maeneo. Wakishamaliza shughuli hiyo ndiyo Wizara itaingilia

kati katika suala la kupanga. Hata hivyo, kwanza tuitambue tuibaini ili kuondoa ile migogoro. Zoezi limeshaanza katika baadhi ya wilaya na Kamati ile inafanya kazi vizuri kwa sababu inashirikisha uongozi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la bomoa bomoa katika maeneo ambayo yamevamiwa au watu wamebomolewa pengine hawakuwa na tahadhari; kwanza naomba nitoe tahadhari kwa wananchi wengi, kwamba maeneo mengi ya taasisi za umma yamevamiwa sana na wananchi na wengine wamejenga nyumba za kudumu kwa muda mrefu. Hata hivyo, unapoangalia kisheria na taratibu na ukubwa wa shule yanayotakiwa kuwa unakuta sehemu nyingi yamevamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa makosa ya watendaji wetu kuna wengine pia walithubutu kutoa hati katika maeneo ambayo ni ya shule. Kwa hiyo zoezi hili linafanyika ili kuhakikisha kwamba maeneo yote yanapimwa na yanatambulika na wale wote walioingia ndani basi sheria inachukua mkondo, wake kwa maana ikiwa ni pamoja na kuvunjiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao watakuwa wamevunjiwa kimakosa ni lazima uhakiki ufanyike tuweze kujua pengine hata ile hati aliyonayo si sahihi. Kwa hiyo kama tukikuta mtu amevunjiwa katika utaratibu ambao ni wa kimakosa basi tutaona namna ya kuweza kumpatia kiwanja mbadala. Nitoe rai tu kwamba wale wote walioko kwenye maeneo ya umma ni vizuri wakayaachia.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Machano Othman Said toka Baraza la Wawakilishi. Zanzibar linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Saada Mkuya na linaelekezwa kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Na. 26

Kufungua Ubalozi Nchini Cuba

MHE. SAADA MKUYA SALUM (K.n.y MHE. MACHANO OTHMAN SAID) aliuliza:-

Kwa muda mrefu Tanzania imekuwa na uhusiano mzuri kiuchumi, kiafya na kisiasa na Jamhuriya Muungano wa Watu wa Cuba, lakini Tanzania haina Ubalozi katika nchi hiyo:-

(a) Je, ni lini Tanzania itafungua ubalozi wake nchini Cuba hasa ikizingatiwa kuwa Cuba tayari wana Ubalozi nchini muda mrefu?

(b) Je, Serikali inajua kwamba kutokana na Tanzania kutofunga Ubalozi nchini Cuba, imesababisha sanamu ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere kutowekwa katika uwanja wa Viongozi muhimu wa Afrika katika Jiji la Havana?

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashaki, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Machano Othman Said, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Tanzania na Cuba imekuwa na mahusiano mazuri ya Kidiplomasia, Kisiasa, Kiuchumi, Kielimu, Kiafya na Kiutamaduni kwa muda mrefu yalioanzishwa na waasisi wa Mataifa haya mawili, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa Tanzania na Hayati Fidel Alejandro Castro Ruz wa Cuba. Kwa ujumla mahusiano haya mazuri yamedumu kwa miaka mingi kutokana na kuwa na maslahi mapana na nchi yanayozingatia usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya mafupi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Machano Othman Said, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutambua mahusiano mazuri na ya muda mrefu yaliyopo baina ya nchi hizi mbili ina mpango wa kufungua ubalozi katika Mji wa Havana Cuba. Hivi sasa taratibu za kufungua Balozi hizi zinaendelea, mara zitakapokuwa zimekamili ubalozi huo utafunguliwa kama ulivyopangwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Cuba kwa kutambua na kuthamini mchango mkubwa uliotolewa na mashujaa katika vita vya ukombozi wa bara la Afrika iliamua kujenga mnara wa kumbukumbu kuenzi juhudi na harakati hizo pamoja uzalendo wa viongozi hao akiwemo Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba Tanzania kutokufungua Ubalozzi nchini Cuba kumesababisha sanamu ya Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kutokuwekwa katika Uwanja wa Viongozi Muhimu Afrika katika Jiji la Havana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sanamu hiyo haikuwekwa katika uwanja huo kutokana na muonekano wake kutokuwa na uhalisia wa sura ya Hayati Baba wa Taifa, hivyo utengenezaji wake kuanza upya. Matengenezo ya sanamu hiyo yanaendelea na Serikali inafanya juhudi ili sanamu hiyo ikamilike na kuwekwa sehemu iliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa mahusiano ya Tanzania na Cuba yataendelea kuwa mazuri katika nyanja mbalimbali hapa nchini kama vile diplomasia, afya, elimu, michezo, utalii na biashara.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mkuya swali la nyongeza.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba mipango inaendelea kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kufungua Ubalozi. Hata hivyo, tunaomba tu awaambie Watanzania hii mipango imefikia hatua gani ili na wao wapate *confidence* kwamba Ubalozi huu utafunguliwa karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kwa upande wa mashirikiano, Zanzibar inashirikiana kwa karibu sana na Cuba hasa katika nyanja ya afya na imekuwa ikipeleka wanafunzi mbalimbali kwa ajili ya masomo ya muda mfupi na mrefu. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuchelewa kufungua Balozi hii katika Mji wa Havana kunawapa maisha magumu wanafunzi wale kwa maana wanakuwa hawajui wanapopata matatizo wakimbilie wapi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maswali mawili ya nyongeza ambayo yameulizwa na Mheshimiwa Saada Mkuya akitaka kujua hatua iliyofikiwa kwa sasa hivi. Naweza kumwambia tu utaratibu wa mwanzo huwa tunafanya kutafiti kutengeneza gharama za kuanzisha Balozi, uanzishwe wapi, watu wangapi wapelekwe, lakini mwisho kabisa ni lazima tuwe tumejiandaa kwamba tuna pesa ya kutosha na imewekwa kwenye bajeti ndipo hapo Ubalozi unaweza ukafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa pia anajua kwamba tuna Balozi nyingine sita ambazo zimefunguliwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ambazo bado tunataka tuhakikishe kwamba tumekamilisha mambo yote

yanayohusiana na *staffing*, gharama za nyumba na uendeshaji. Hatuwezi tu tukafungua kwa sababu tumesema, tukishakuwa tumejiandaa tutaweza kusema ni lini. Hata hivyo, utaratibu wa kuangalia aina ya watu watakaopelekwa na gharama za uendeshaji zimekwishakamilika, tunasubiria kwanza zile ambazo zimepangwa zikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili tunatambua kwamba mahusiano baina ya Tanzania na Cuba ni mazuri na Zanzibar kama yeye anavyojua kwamba ni sehemu pia ya Tanzania. Nataka kumhakikishia kwamba wale wanafunzi ambao wanasoma kule Cuba kwa kozi za muda mrefu na mfupi watakuwa wanaendelea kusimamiwa na Balozi yetu ya Canada maana ndiyo wanaosimamia wanafunzi au wafanyakazi wote wa Tanzania walioko Cuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimwambie mahusiano hayo hayako mazuri tu kwa upande wa Zanzibar ni mazuri kwa Tanzania nzima. Kwa kumpa tu taarifa mwaka jana Manesi 16 pamoja na Madaktari kwa mkataba wa miaka miwili wa kutoka Cuba watakuwa wanafanya kazi katika Hospitali yetu ya Muhimbili na Waziri wa Afya yuko hapa anaweza kukiri hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna mahusiano mazuri kwenye suala la elimu, kuna Madaktari na Wataalam wa afya ambao wanatoa mihadhara katika vyo vyetu vikuu. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia kwamba wale wanafunzi ambao wamepelekwa kutoka Zanzibar wataendelea kuhudumiwa na Balozi yetu ya Canada.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki na linaelekezwa kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 27

Hitaji la Vituo vya Polisi Tarafa ya Mamba na Gonja-Same

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Jimbo la Same Mashariki lina Kata 14 lakini lina Kituo kimoja cha Polisi kilichopo Kata ya Maore na vituo vidogo vilivyopo Kata ya Ndungu na Kihurio; vituo vyote hivyo vipo katika tarafa moja yenye kata tano, kata nyingine tisa ambazo zipo katika tarafa mbili zilizoko mlimani na zipo mbali sana na vituo hivyo vya Polisi zinapata shida sana kutoa ripoti za uhalifu. Kwa kuwa wananchi wa tarafa hizo mbili za mlimani tayari wametenga maeneo ya kuweka vituo vya Polisi:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuanzisha Vituo vya Polisi katika Tarafa ya Mamba/Vunta na Tarafa ya Gonja?

(b) Kama Serikali ipo tayari kuanzisha Vituo hivyo vya Polisi, je, ni lini Polisi hao wataanza kazi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, najibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na Vituo vya Polisi katika ngazi ya Kata na Tarafa nchi nzima, Mamba/Vunta na Gonja zikiwemo. Katika Tarafa ya Gonja kuna Kituo cha Polisi, Daraja B kinachotoa huduma za kipolisi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tarafa ya Mamba wananchi wamejitolea eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi ambapo kwa sasa majadiliano kati ya Jeshi la Polisi na wananchi kuhusu ujenzi wa Kituo cha Polisi, Daraja la B yanaendelea. Hata hivyo, kwa sasa Tarafa ya Mamba ina

Kituo kidogo Daraja la C ambacho kinatoa huduma kwa wananchi katika Tarafa hiyo. Aidha, Jeshi la Polisi hufanya doria mara kwa mara katika maeneo hayo ya milimani ambayo hafikiwi kirahisi na vyombo vya usafiri kutokana na jiografia yake.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naghenjwa.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba Naibu Waziri aliombe Bunge lako Tukufu radhi kwa kulidanganya. Amesema Tarafa ya Gonja ina Kituo cha Polisi cha Daraja B, naomba afanye *home work*, tarafa hii mimi ndiyo natoka na hakuna hata Kituo cha Daraja C, sasa hicho cha Daraja B amekitoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hata huko anakosema kipo Kituo cha Daraja C, iko nyumba haijawahi kuwekwa polisi hata siku moja. Naomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri aeleze Bunge lako Tukufu kwa nini anatoa taarifa za uongo ambapo hata wananchi katika Jimbo langu watahangaa kwamba hicho kituo Daraja B, kiko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, Waziri atakumbuka kwamba nimeshawaandikia Wizara yao barua mara mbili kuomba kituo hiki kilichopo Maore, Tarafa ya Ndungu ambacho kimejengwa mwaka 1959, kimechakaa *ceiling board* zimedondoka, vigae vilivyowekwa hata kabla ya Uhuru vimebomoka hata OCS hana mahali pa kukaa kufanyia kazi, aseme lini Serikali itaweza kukarabati kituo hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili amesema Polisi wanafanya doria kwenye Jimbo hili, atajua kwamba Polisi wa Kituo cha Maore chenye Daraja B kama anavyosema kipo Tarafa ya Ndungu hawana hata matairi kwenye magari yao, usafiri wao ni wa shida, sasa hiyo doria wanaifanyaje? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilichokieleza katika majibu yangu ya msingi, nilieleza kwamba kulingana na maeneo ambayo walileta maombi ya ujenzi wa vituo katika Tarafa ya Gonja kwamba kuna Kituo cha Daraja B sio C. Katika Tarafa ya Mamba nilichokisema ni kwamba wananchi wametoa eneo, kwa hiyo tupo katika mchakato wa ujenzi wa kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kituo cha Maore ni kweli Mheshimiwa Mbunge aliwahi kuwasilisha barua yake kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na ukarabati wa kituo hiki na barua yake tunaifanyia kazi na pale uwezo utaruhusu basi tutafanya marekebisha ya kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na ubovu wa magari kwa ajili ya doria, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba natarajia muda siyo mrefu kufanya ziara katika Jimbo lake nitamwomba na yeye kama atakuwa na nafasi tuambatane ili tukaone changamoto hizo. Tatizo la usafiri katika nchi yetu ni kubwa sana, kwa hiyo itategemea uzito tutakavyoona katika eneo hilo kulinganisha na maeneo mengine katika nchi nzima tuone uwezekano wa kusaidia usafiri ili waweze kufanya kazi zao vizuri hasa maeneo ya millimani ambapo hakuna mawasiliano mazuri ya usafiri.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, linaelekezwa Wizara hiyo hiyo ya Mambo ya Ndani ya nchi.

Na. 28

Tatizo la Kupotea kwa Watoto-Dar es Salaam

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS aliuliza:-

Tatizo la kupotea kwa watoto katika Jiji la Dar es Salaam limekuwa kubwa. Aidha, taarifa za kupotea kwa

watoto hao zimekuwa zikitolewa kwenye vyombo vya habari:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazochangia kuongezeka kwa tatizo hilo siku hadi siku?

(b) Je, kwa nini taarifa za upatikanaji wa watoto hao hazitolewi kwenye vyombo vya habari?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani kuondoa tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri ya Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na wimbi la upoteaji wa watoto katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Jiji la Dar es Salaam. Aidha, sababu za upotevu wa watoto hawa ni pamoja na uangalifu hafifu wa watoto kutoka kwa wazazi au walezi na jamii kwa ujumla, mazingira magumu wanayoishi baadhi ya watoto, imani za kishirikina, visasi kati ya familia na kupotea kwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kudhibiti matukio hayo kwa kutoa elimu kupitia programu ya Polisi Jamii kwa watoto mashuleni na wazazi kupitia mihadhara ya kijamii na vyombo vya habari. Jitihada hizo zimekuwa zikizaa matunda kwa kuongeza elimu ya usalama wetu kwanza miongoni mwa jamii na hivyo kuongeza umakini wa kulinda watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Disemba, 2017 kwa Mkoa wa Dar es Salaam walipotea watoto 184, ambapo watoto waliopatikana ni

176 na watoto ambao wanaendelea kutafutwa ni nane. Jeshi la Polisi linaendelea kutoa rai kwa taasisi na idara mbalimbali kama Ustawi wa Jamii kushirikiana na kuwa na programu za pamoja ili kutoa elimu ya kumlinda mtoto wa Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fakharia.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kulitamka vizuri jina langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza ambapo maswali ya msingi amenijibu vizuri na yameeleweka lakini kuna kifungu cha mwisho hapa ambacho kimenifanya niweze kupata maswali ya nyongeza. Amekiri kwamba watoto 184 walipotea na 176 wamepatikana na nane hawajapatikana lakini bado wanaendelea kutafutwa. Sasa napenda kumuuliza hivi Mheshimiwa Waziri kwa hao waliopatikana na hao waliokutwa nao, Serikali imechukua hatua gani ya kuwawajibisha kisheria? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wale watoto baada ya kupatikana ambapo alikuwa hayuko kwenye mazingira ya wazazi lazima afya itakuwa ni mgogoro. Je, Serikali au vyombo vimechukua hatua gani baada ya watoto hao kupatikana kupelekwa kwenye vyombo vya utibabu ili kuangaliwa hali yao na wazee kuweza kujiridhisha? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi kwamba, kupotea kwa watoto hawa 184 kulitokana na sababu mbalimbali ambapo

miongoni mwa sababu hizo ilikuwa ni mazingira magumu ambayo wanaishi baadhi watoto, imani na kishirikina, visasi, kukosekana uangalifu wazazi/walezi na sababu nyingine ni kupotea kwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sababu hizi ni tofauti na hatua ambazo zinachukuliwa zinategemea na sababu husika. Kwa zile sababu ambazo zimesababishwa na njia ya uhalifu basi hatua mbalimbali zimeshachukuliwa kwa mujibu wa sheria kwa watu ambao wamehusika na upotevu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbukuka juzi tu kulikuwa na tukio la kijana mmoja ambaye amejihusisha na utekaji wa watoto na kuomba fedha, kijana yule alikamatwa na kwa bahati mbaya alipata majeraha na akafariki. Nikuhakikishie kwamba Serikali kupitia Jeshi la Polisi iko makini sana kuhakikisha kwamba inalinda watoto wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuhusu hatua ambazo watoto hawa wanachukuliwa. Kama ambavyo nimesema kwamba kwa kuwa sababu ni tofauti kwa wale watoto ambao wamepatikana na madhara mbalimbali basi nao vilevile hufikishwa katika mamlaka husika kwa ajili ya kuweza kupata huduma mbalimbali ili kuwaweka katika hali nzuri ya kimaisha na kiafya.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali letu la mwisho kwa leo. Swali Na.29 linaulizwa na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar na linaelekezwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali, napenda nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Kaimu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, kwa juhudi na umakini wake katika shughuli hizi. Nimwambie tu dalili ya mvua ni mawingu na nyota njema huonekana asubuhi. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 29

Malipo Kuhusu Utaratibu wa Kuingiza Mafuta nchini

MHE. JAKU HASHIM AYOUB aliuliza:-

Utaratibu wa kuingiza mafuta nchini unaosimamiwa na *Petroleum Bulk Procurement Agent (PBPA)* kwa mfumo wa *Bulk Procurement System*, wakala hukusanya mahitaji kutoka kwa makampuni ya ndani na nje ya nchi lakini kampuni zote zikiweko zile zinazopeleka mafuta nje ya nchi zinalipa Dola za Marekani tatu hadi nne kwa tani kwa mafuta yanayopitia *transit* ya Dar es Salaam isipokuwa mafuta yanayopelekwa Zanzibar ambayo hutozwa Dola za Marekani 10 kwa tani.

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika kutoa nafuu ya malipo ya *Wharfage* kwa kampuni za nje zinazopitisha mafuta Dar es Salaam na kuitoa Zanzibar malipo makubwa?

(b) Mafuta yanayopitishwa *transit* ya Dar es Salaam kwenda Zanzibar yanalipiwa aina zote za ushuru, je, Serikali haioni kuwa inawabebesha wananchi gharama kubwa ya ununuzi wa mafuta kuliko nchi nyingine?

(c) Je, ni hatua gani Serikali inachukua katika kuhakikisha mafuta yanayopita *transit* ya Dar es Salaam yanalipwa kama mafuta mengine yanayopita *transit* ya bandari hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashimu Ayoub, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaotumika kupanga tozo za bandari hautoi upendeleo kwa upande

wowote. Tozo hizo zimewekwa kwa kuzingatia gharama za kutoa huduma, hali ya soko na umuhimu wa kuvutia shehena ya nchi jirani ili kutekeleza sera ya uchumi wa kijiografia na kufanya bandari ya Dar es Salaam kuwa kitovu yaani *hub* ya usafirishaji. Ushindani wa shehena ya mafuta ni mkali sana (*cut throat competition*) kwa bandari za TPA hususani Dar es Salaam na bandari za nchi jirani za Kenya, Msumbiji, Afrika Kusini, Namibia na Angola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kutokana na hali ya soko (*market place exigencies*), tozo za bandari kwa shehena ya nchi ya jirani hutofautishwa na shehena ya ndani ya nchi ili kuvutia shehena nyingi kuhudumiwa na bandari ya Dar es Salaam. Kwa hivi sasa gharama ya *Wharfage* kwa shehena ya Tanzania ya kupakuliwa (*imports*) ni asilimia 1.6 ya thamani ya mzigo ulioidhinishwa na TRA na kwa kiwango cha chini kilichowekwa cha Dola za Marekani 10 kwa tani moja.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania Bara na Zanzibar ni nchi moja na kwa hiyo shehena yoyote iendayo Zanzibar ikiwa ni pamoja na shehena ya mafuta hutambuliwa kama ni shehena ya nchini (*local cargo*) na sio shehena ya nchi jirani yaani *transit*. Kwa mantiki hii, tozo zinazotumika ni tozo za shehena ya ndani (*local cargo*) ambayo ni sawa kwa Bara na Zanzibar.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia majibu ya (a) na (b) hapo juu ni dhahiri kwamba matumizi ya tozo ni miongoni mwa mikakati maalum ya kibiashara na masoko kwa ajili ya kuvutia shehena za nchi jirani ambazo huleta faida ya uchumi na kijamii hapa nchini (*multiplier effect*) siyo tu kwa bandari bali kwa wadau wote wa bandari na wananchi kwa ujumla.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ayoub Jaku.

MHE. JAKU HASHIM AYUBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza mnyonge mnyongeni, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kitendo alichoonyesha

asubuhi hii leo cha uungwana na ungwana ni vitendo. Nikupongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa, tena makubwa, tena makubwa kwa mara ya tatu. Wizara yake anayoiongoza Mheshimiwa Waziri imekuwa ikiwaonea wananchi wa Zanzibar, Unguja na Pemba. Nipo tayari kumthibitishia hilo kwani mafuta yanayouzwa Zanzibar sasa hivi ni ghali kuliko hapa Dar es Salaam. Nimwombe tu kwa unyenyekevu, ni lini atakaa na watu wa upande wa Zanzibar kutatua tatizo hili? Kama anavyojua mafuta ni nguzo muhimu. Mafuta Zanzibar yanauzwa ghali, kodi zimekuwa nyingi na amekiri, nimpongeze kuwa Zanzibar wamechaji Dola 10, wakaiacha Rwanda Dola tatu, Zambia Dola tatu Burundi Dola tatu, kwa nini wanaonea Zanzibar kwa Dola 10? Mawaziri wengi husema Muungano huu wetu ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza swali.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima ujenge hoja kwanza. Bila kujenga hoja hawezi kuja kufahamu Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri, nimwombe ni lini atakaa na upande wa Zanzibar maana kuna barua mpaka leo Katibu wake Mkuu hajawajibu Wazanzibari, je, kalamu ya kuandikia hana au anaandika *spelling* moja moja? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni uonevu, mafuta Zanzibar yanauzwa ghali, sisi tunaumia. Mafuta ni nguzo muhimu ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ni lini utaketi na wafanyabiashara wa Zanzibar kuzungumzia suala hili?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. Kwanza nikiri kweli kwamba kuna changamoto katika hizi tozo ambazo zinatozwa na bandari, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Jaku kwamba tupo tayari kama Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Uchukuzi ya Zanzibar lakini vilevile

na Mamlaka ya Mapato kukaa na kuangalia hizi tozo ambazo ni kero sana kwa wananchi wetu wa Tanzania, tuweze kuzitatua kwa pamoja. Katika hilo, nitamkaribisha Mheshimiwa Jaku tukae pamoja tulijadili kwa kina tuliondoe tatizo hilo ambalo linasumbua wananchi kwa njia moja au nyingine. Hili linatatulika kwa mustakabali wa nchi yetu ya Tanzania. Ahsante.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Lini, lini, lini, Mheshimiwa Naibu hujataja?

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hapa ndiyo tumefika mwisho wa kipindi cha maswali, miona nimeminya sana lakini mnaelewa mimi siwezi kuwafundisha utaratibu wa kulinda muda. Tunarembaremba mno maswali, tunarembaremba mno majibu. Nenda *straight* swali lako na jibu *straight*, Watanzania hawa wanataka wayasikie kwa kifupi tu. Tumechukua muda zaidi ya nusu saa, tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wetu waliopo leo hapa Bungeni, naanza na wagei waliopo Jukwaa la Spika. Tunao wageni 46 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) ambao ni viongozi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Eric Shitindi. Karibuni sana Katibu Mkuu na timu yako. Nafahamu tuna Muswada muhimu sana leo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Wajumbe na wadau kutoka Shirika la Vyama vya Wafanyakazi (*TUCTA*) wakiongozwa na Rais wa Shirikisho hilo Ndugu Peter Nyamhokya. Karibu sana Mheshimiwa na timu yako. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Wakuu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa umoja wenu simameni tuwaone. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO). Karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kundi la pili ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kuna wageni watano wa Mheshimiwa Lathifah Chande kutoka Liwale Mkoa wa Lindi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni marafiki zake kutoka Kilolo, Mkoa wa Iringa pamoja na wageni wengine kutoka nchi ya Uholanzi - Netherlands. Karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ni wale waliotembelea Bunge letu kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 16 kutoka Chuo cha Habari Maalum kilichoko Mkoa wa Arusha. Karibuni sana kwenye mafunzo yetu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Walimu wanne na wanafunzi 49 wa Mafunzo ya Usanifu wa Majengo kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Uhandisi wa Miundo na Ujenzi, Kitivo cha Uhandisi na Teknolojia. Ahsanteni sana, karibuni sana, muone shughuli zetu za Bunge. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo lingine, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore, Mheshimiwa Shally Raymond, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Wakristo Wakatoliki, leo tarehe 31 Januari, 2018 kutakuwa na Ibada ya Misa mara baada ya kuahirishwa kwa Bunge saa 7.00 mchana katika Kanisa dogo lililopo ghorofa ya pili, ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wengine wote mnakaribishwa kushiriki Ibada hii Takatifu.

Hayo ndiyo matangazo niliyonayo hapa mezani. Baada ya hapo...

MWONGOZO WA SPIKA

WABUNGE FULANI: Mwongozo.

MWENYEKITI: Mniruhusu nikae basi.

WABUNGE FULANI: Kaa tu Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Kwa sababu ya muda nitachukua wachache, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Paresso.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Nina hoja ya msingi sana.

MWENYEKITI: Tuanze na Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68(7) juu ya jambo lililotokea Bungeni mapema sambamba na Kanuni ya 46(1) maswali kutojibiwa kikamilifu sambamba na Kanuni ya 64(1) kuhusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni na (a) inasema hakuna kutoa taarifa za uongo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na taarifa hizi kutaka mwongozo wako juu ya swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso wakati Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph Kakunda akijibu kwamba hakuna hata Mkuu wa Mkoa mmoja aliyemsimamisha Mwenyekiti wa Mtaa au na ngazi nyingine katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa kuwa watu hawa wapo wengi sana hata hapa Dodoma, tarehe 1 Aprili, 2017, Mwenyekiti wa Mtaa wa Mlimwa Kusini alisimamishwa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya wakati huo. Hii orodha ya watu wa aina hii ni kubwa ambapo Mheshimiwa Joseph Kakunda ama amelidanganya Bunge au amedanganywa na wataalam wake. Naomba mwongozo wako juu ya jambo hili ambalo limetokea leo mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati swali Na.19 linajibiwa na Mheshimiwa Mwakajoka anapata majibu ya swali lake la nyongeza alionyesha kwamba katika Wilaya yake kuna shule ambazo hazijafunguliwa kwa sababu shughuli za Madiwani zimesitishwa na Naibu Waziri akasema kwamba hicho kitu siyo kweli na akarudia mara tatu anakataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niweke mambo sawa kwamba Naibu Waziri jibu lake halikuwa sahihi kwa sababu hilo jambo limetokea Tunduma lakini jambo hilo hilo nimemwona kwenye Televisheni Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Bwana Mnyeti akimsimamisha Mwenyekiti wa Mtaa ambaye pia ni Mheshimiwa Diwani, anamlazimisha ajiudhuru nafasi moja hapa hapa lakini vilevile imefanyika Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkuu wa Manyara, Bwana Mnyeti, ambaye kumbukumbu zinaonesha amewahi kuitwa na Bunge hili kuja kwenye Kamati ya Maadili kwa kudharau Bunge, lakini juzi tulimwona kwenye *clip* mbalimbali akitoa maelekezo kwa Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto, akimweleza kwamba wewe ukija kwenye Kijiji B usizungumze mambo ya Kijiji B. Anasema Mkuu wa Wilaya ana masikio makubwa kuliko mtu mwingine katika Wilaya ile na Mbunge akisema jambo lolote anatakiwa awajibishwe mara moja na kama atashindwa yeye ataingilia kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba Bunge hili litoe kauli, matendo haya ambayo yanafanyika kwa Wateule ambao wanateuliwa na Mheshimiwa Rais, wakidhalilisha Mhimili wa Bunge, wao wapo juu ya sheria? Katiba imetoa mgawanyiko wa madaraka, kwamba kuna kazi za Serikali, kuna kazi za Bunge na kuna kazi za Mahakama. Hata hivyo, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa

Wilaya anafika mahali anamwambia kuanzia sasa sio Mtumishi wa Umma na hilo jambo limerudiwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wa Bunge hili ili tufuate utaratibu, tufuate sheria na Katiba ili kila mtu afanye kazi katika mazingira na mipaka ya kazi yake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba niwasilishe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paresso.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba mwongozo wako, kwa suala hili ambalo lipo mbele yetu ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba hakuna Wakuu wa Mikoa wa ambao wameweza kufanya kitendo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mheshimiwa Mnyeti, amewavua nafasi zao za Ukuu wa Shule na kuwasimamisha kwa madai kwamba hawajatimiza wajibu wao Walimu Wakuu katika Shule za Simanjiro, Kiteto na Babati Vijijini. Hivi karibuni, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania alitoa kauli katika vyombo vya habari kwamba michango mashuleni sio lazima, vyakula mashuleni sio lazima na kwa hali ya kawaida Wakuu hawa wa Shule wanaovuliwa nafasi zao sio kwamba wao wanasababisha watoto wafeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe mwongozo wako, ni kwa nini Serikali inatudanganya kwamba hakuna Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ambao wanawasimamisha kazi watumishi wakati hali hiyo ikiendelea hususan katika Mkoa wa Manyara? Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsanteni.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68(7) ya kuombea mwongozo sote tunaifahamu, kuhusu jambo lililotokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi na Kanuni hizi. Hiyo ndiyo Kanuni ambayo imeombewa mwongozo. Nijumuisha, inaonekana haya yametokana na jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Twende vizuri tu Waheshimiwa Wabunge, kwanza kuna uamuzi wa Spika kuhusiana na majibu ya nyongeza kutokidhi kile kiwango ambacho Mbunge anaona kwamba hakikufikiwa. Hasa uamuzi wa Spika ni kwamba anayeweza kulalamika kwamba swali lake halikujibiwa kikamilifu, ni mwenye swali na aliyeliza maswali ya nyongeza kwa swali hilo na sio mwingine. Wale tunaouliza maswali ya nyongeza huwezi ukasema yale majibu aliyopewa muuliza swali hayajitoshelezi. Kwa hiyo, Waheshimiwa hilo tuelewane kabisa.

MJUMBE FULANI: Ulinipa nafasi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, wewe hukuwa mwenye swali la msingi kama unadhani yaliyosemwa humu Bungeni na Serikali hayatoshelezi, wewe uliza swali lako litajibiwa na Serikali. *(Makofi)*

(Hapa baadhi wa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana lazima Kanuni hizi tuendeleo kuzisimamia sisi wenyewe. Yote haya Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa mliojigeuza, mimi nimemuita Paresso mkajigeuza, mkakaribishana tu, nimevumilia tu hayo yote, lakini nayakubali tu kwamba na ninyi mna haki ya kuyasema haya lakini mimi nawanyoosha kwenye mstari wa Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo mwongozo wangu, tumekaa vizuri na suala hilo. Sasa tunaendelea, Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa
Watumishi wa Umma kwa Mwaka 2017
(*The Public Service Social Security Fund Bill 2017*)**

(Kusomwa Mara ya Pili)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, karibu uwasilishe Muswada, Karibu sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2018 (*The Public Service Social Security Fund Act, 2018*) kama ulivyochapishwa upya sasa usomwe Mara ya Pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishwe Muswada huu kuwa sehemu ya sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni Mkutano wa Kwanza tangu mwaka huu uanze, naomba nikutakie wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wengine wa Bunge pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Wabunge wengine wote kheri ya mwaka mpya wa 2018.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Doto Biteko, kwa kuteuliwa na kuaminiwa na Rais kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbo, Mbunge wa Songea Mjini; Mheshimiwa Justin Monko, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini; na Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiluswa, Mbunge wa Jimbo la Longido kwa kuchaguliwa na wananchi wa Majimbo yao na kisha kuapishwa kuwa Wabunge wa Bunge hili. Nawatakiwa utendaji mwema katika kutekeleza majukumu yao ya Kibunge ndani na nje ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi ya pekee kumshukuru sana Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo anayoendelea kutupatia ambayo imetuwzesha kufanikisha uandaaji wa Muswada ambao uko mbele yako leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yake yaliyotuwzesha kufanikisha kuandaa Muswada huu. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Naibu Mawaziri wangu Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde na Mheshimiwa Stella Ikupa na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Eric Shitindi na watendaji wengine wote toka Ofisi ya Waziri Mkuu kwa msaada mkubwa waliotupatia katika maandalizi ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutambua kazi kubwa iliyofanywa na Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii kuanzia hatua ya utafiti zilizopelekea kufikia hatua hii ya leo. Nawashukuru sana *SSRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, nawashukuru sana Viongozi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na naomba kwa hisani yako niwataje kwa majina viongozi

Watendaji Wakuu wa Mifuko hiyo, Mheshimiwa Sanga, Mheshimiwa Eriyo, Profesa Kiharara, Mheshimiwa Msangi na Ndugu yetu Adam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile natoa shukrani za dhati kwa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (*TUCTA*) wakiongozwa na Rais wa Shirikisho hilo Ndugu yangu Tumaini Nyamhokya kwa kazi nzuri waliyofanya katika kupelekea kufanikiwa kwa kuwepo kwa Muswada huu. Aidha, nashukuru sana Chama cha Waajiri Tanzania (*ACTE*) kikiongozwa na mama yetu mpendwa Mama Janeth Nyimbo kwa kufanya kazi nzuri ya kutoa ushauri katika kufanikisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nilishukuru sana Shirika la Kazi Duniani kwa ushirikiano mkubwa walionyeshwa katika hatua zote za majadiliano ya hoja na mpaka kutufikishia kuweza kuleta Muswada wa kuunganisha Mifuko na hatimaye Muswada huu kuingia katika Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupongeze tena kwa mara nyingine, lakini nimpongeze pia Spika wa Bunge letu, Naibu Spika na Wenyeviti Wabunge kwa jinsi mnavyoendelea kutekeleza majukumu ya Bunge kwa ufanisi mkubwa. Aidha, namshukuru sana kaka yangu George Masaju, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ndugu Gerson Mdemu, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri na ushirikiano wao waliotupatia wakati wa uandaaji wa Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa dhati pia nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kusimamia shughuli za maandalizi ya Muswada huu ndani Serikali, lakini tulishirikiana pamoja na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe na Ndugu yangu George Mkuchika, wote kwa pamoja Mawaziri hawa tulifanya nao kazi usiku

na mchana na hatimaye kazi hii leo imeweza kuja mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, akisaidiwa na Mheshimiwa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wametupa ushirikiano na ambao umetupelekea kuchambua na kupitia Muswada huu na hatimaye tarehe 22 Januari, Kamati ilikamilisha kupitia na kuchambua Muswada wa Sheria wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na kuridhia Muswada huu uendelee kwa hatua ya kusoma Mara ya Pili na ya Tatu katika Mkutano huu wa Bunge. Hakika ushauri, maoni na mapendekezo ya Kamati yametusaia sana sana kuboresha Muswada kupitia marekebisha ambayo yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanywa na Mwenyekiti wa Kamati hii na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii katika Muswada huu ni jambo la kihistoria. Kwa dhati kwa niaba ya Serikali tutaheshimu sana kazi nzuri iliyofanywa na Kamati hii. Hii ni kutokana na namna Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati walivyoungana na kujitua kwa pamoja bila kujali itikadi zao katika kuchambua, kurekebisha na kuboresha Muswada huu ili kuhakikisha kwamba unakidhi lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho makubwa yaliyofanywa na Kamati yamepelekea kupokea maagizo ya Kamati na Muswada huu kuchapwa upya ili kujumuisha maboresho yote na hivyo kuleta urahisi wa usomaji wa Muswada wenyewe. Mwenyezi Mungu awabariki sana kwa kazi hii nzuri mliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kuwa tunamaliza sasa mwaka wa mwisho wa utendaji wa Kamati za Kudumu za Bunge, naomba nichukue nafasi hii kuzipongeza na kuzishukuru Kamati za Kudumu za Bunge zote kwa ushirikiano mkubwa waliotuonesha ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee, nawashukuru sana Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zifuatazo za Bunge ambao tulifanya nao kazi katika kipindi hiki cha awamu ya kwanza ya Kamati za Kudumu za Bunge ndani ya Bunge lako Tukufu. Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya UKIMWI lakini vilevile Kamati yako ya Sheria Ndogo. Hakika walitupa ushirikiano mkubwa na walionesha kwamba wanajali na kuhitaji kuboresha utendaji wa Serikali kwa ujumla kwa manufaa ya nchi yetu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitakwenda kwenye madhumuni ya Muswada. Muswada uliopo mbele yako unapendekezwa kutungwa kwa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa mwaka 2018. Sheria hii inapendekeza kuunganisha Mifuko ya *Pension ya PSPF, LAPF, GEPF* na *PPF* na kuanzisha mfuko mmoja wa hifadhi ya jamii mahsusi kwa ajili ya Watumishi wa Umma kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuanzisha mfuko mpya, sheria inayopendekezwa inafanya marekebisho makubwa (*consequential amendment*) kwenye Sheria ya Mfuko wa Taifa ya Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) ili kuufanya Mfuko huo kuwahudumia wafanyakazi wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu pia unapendekeza kufuta sheria zinazoanzisha Mifuko ya Pensheni ambayo ni Sheria ya Mafao ya Pensheni kwa Watumishi wa Umma (*PSPF*), Sheria ya Mafao ya Pensheni kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa (*LAPF*), Sheria ya Mafao ya Pensheni kwa Mashirika ya Umma (*PPF*) na Sheria ya Mafao ya Kustaafu (*GEPF*). Aidha, Sheria ya *SSRA* pia itarekebishwa ili kuendana na mabadiliko haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kuunganisha Mifuko ya Pensheni inalenga kukidhi kilio cha muda mrefu cha wafanyakazi kuhusu kuunganisha Mifuko hiyo ili kupunguza gharama za uendeshaji, kuondokana na ushindani usio na tija baina ya Mifuko ya Pensheni ambayo kimsingi inatoa mafao yanayofanana na hatimaye kuboresha mafao ya wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la hoja ya kuunganisha Mifuko ya Pensheni nchini ni madai ya muda mrefu ya wadau mbalimbali wa sekta ya hifadhi ya jamii, hasa wafanyakazi ambao katika nyakati tofauti kupitia vyama vyao waliomba na kuishauri Serikali kuunganisha Mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2014, 2015, 2016 na 2017, Shirikisho la Vyama Nchini (*TUCTA*) wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani na katika vikao baina yao na Serikali wamekuwa wakiomba Serikali kuunganisha Mifuko ya Pensheni ili kuondoa changamoto mbalimbali zinazotokana na uwepo wa Mifuko mingi ya Pensheni inayotoa mafao yanayofanana na kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2016 katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani katika risala yao *TUCTA* waliwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ombi lao la kuunganisha Mifuko ya Pensheni nchini. Mheshimiwa Rais alikubali ombi hilo na kuiagiza Ofisi ya Waziri Mkuu kuharakisha mchakato wa kuunganisha Mifuko hiyo. Hatua hii pia inakwenda sambamba na mapendekezo ya *ILO* ambayo kupitia tathmini ilishauri Mifuko ya Pensheni nchini iunganishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuitikia kilio cha maombi ya wadau wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii hatua ya kuunganisha Mifuko hii pia ni sehemu ya utekelezaji wa Ibara

174 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 inayoielekeza Serikali kuimarisha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa manufaa ya Watanzania wote kwa ujumla na hasa wafanyakazi wanaostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunganisha Mifuko kutasaidia kupunguza gharama za uendeshaji kutoka viwango vya asilimia 19 mpaka asilimia tisa iliyowekwa na Mdhibiti wa Sekta; kuondoa gharama za ushindani usiokuwa na tija; kupunguza migogoro baina ya Mifuko; kuboresha mafao ya wanachama ikiwemo kuongeza mafao mapya yaliyokuwa yakihitajika sana miongoni mwa wanachama; kuongeza tija katika sekta ya hifadhi ya jamii na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla. Aidha, hatua ya kuunganisha Mifuko itasaidia kuimarisha uwiano wa idadi ya wanachama wachangiaji na wastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya sheria hii inayopendekezwa uwiano ya idadi ya wanachama wachangiaji na wastaafu ilikuwa wastani wa 1:5 kwa Mfuko ambao ulikuwa chini kabisa. Baada ya kupitishwa kwa sheria hii inayopendekezwa na Bunge lako Tukufu tunatarajia uwiano wa idadi ya wanachama wachangiaji na wastaafu itaendelea kuongezeka kufikia kiwango cha kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu. Kabla ya kueleza mpangilio wa Muswada huu, naomba uniruhusu nibainishe kwa ujumla mambo muhimu ambayo yamezingatiwa katika Muswada wetu mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayopendekezwa kwa sasa inaweka mfumo madhubuti utakaomhakikishia mwanachama kulipa mafao ya msingi kama inavyoelekezwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, lbara ya 11(1) nitanukuu:-

“Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi na

kupata msaada wa jamii wakati wa uzee, wakati wa maradhi au hali ya ulemavu na katika hali nyingine za mtu kuwa hajiwezi". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayopendekezwa inabainisha kwa uwazi jumla ya mafao saba yatakayolipwa na Mfuko huu, mafao hayo ni pamoja na:-

- (i) Fao la Pensheni;
- (ii) Fao la warithi;
- (iii) Fao la ulemavu;
- (iv) Fao la uzazi;
- (v) Fao la ukosefu wa ajira;
- (vi) Fao la ugonjwa; na
- (vii) Fao la kufiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inaweka utaratibu bora na ulio rahisi wa wanachama wa mifuko inayounganishwa kuhamia kwenye mfuko mpya pasipo kuathiri mafao yao na uendelevu wa Mfuko mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sheria inapendekeza kutumia utaratibu wa *cut-off date* ambapo wanachama wa umma waliopo *NSSF* na wanachama waliopo katika sekta binafsi ambao kwa sasa wanachangia kwenye mifuko inayounganishwa hawatahamishwa na badala yake utaratibu mpya wa mifuko miwili utaanza kwa wanachama watakaoajiriwa baada ya sheria mpya kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inaweka bayana kwamba mafao na michango ya wanachama haitatozwa kodi kama ilivyokwishabainishwa hata katika sheria nyingine za kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inaainisha viwango vya uchangiaji na namna ya uchangiaji katika Mfuko mpya ambapo viwango vya uchangiaji itakuwa ni asilimia 20, mwajiri atachangia asilimia 15 na mwajiriwa atachangia asilimia tano (5) tu ya mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inaweka mfumo madhubuti utakaohakikisha mwanachama anapata mafao kwa wakati kama ifuatavyo:-

Itautaka Mfuko kumlipa mwanachama aliyekidhi vigezo mafao yake hata kama mwajiri hajawasilisha michango na baadaye Mfuko utafuatilia michango ambayo haijawasilishwa kutoka kwa mwajiri. Hii inatokana na ukweli kwamba jukumu la kufuatilia michango siyo jukumu la mwanachama. Wakati ukifika mwanachama alipwe michango yake hata kama mwajiri hajafuatilia michango yake kunakohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inaweka adhabu ya tozo ya asilimia tano (5) kwa Mfuko utakapochelewesha mafao ya mwanachama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inaweka mfumo rahisi na mfupi wa mashauri ya madai ya michango Mahakamani, ambapo mwajiri aliyeshtakiwa kwa kutowasilisha michango ya mwanachama, hatakuwa na fursa ya moja kwa moja ya kujitetea Mahakamani mpaka atakapowasilisha dhamana ya fedha taslimu sawa na kiasi cha michango ya mwanachama anayodaiwa na mwanachama huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii itamwezesha mwanachama kutumia mafao yake kujipatia mikopo ya nyumba na shughuli nyingine za kiuchumi kwa riba nafuu. Hatua hii itawasaidia wanachama kujiandaa na maisha kabla ya kustaafu. Baada ya sheria hii kupita, Ofisi yangu itaandaa utaratibu ambapo mikopo itakayotolewa, itatolewa na benki ambayo Mifuko itakuwa na hisa na

mikopo hiyo kwa wafanyakazi hao ambao ni wanachama itakuwa ni mikopo yenye riba nafuu ili kuhakikisha wanachama hawapati tena shida ya kujiandaa na maisha kabla ya kustaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inaainisha kwa uwazi haki na stahili za warithi pale mwanachama au mstaafu anapofariki. Masharti katika eneo hili yanalenga kuondoa changamoto mbalimbali zinazotokana na sheria za sasa za Mifuko kutokuwa wazi katika eneo la haki na stahili za warithi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayopendekezwa inaondoa kilio cha muda mrefu cha wastaafu katika utumishi wa umma kuhusu kukoma kwa mafao ama pensheni pale mstaafu anapofariki dunia. Sheria inayopendekezwa itaruhusu wategemezi kuendelea kupokea mafao kwa kipindi cha miezi 36 baada ya mstaafu kufariki dunia. Tofauti na ilivyo sasa ambapo mwanachama akifariki tu, malipo hukoma mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inapendekeza kuboresha masharti kuhusu fao la uzazi ambapo pamoja na kupata fedha taslim baada ya kujifungua, mwanachama pia atapata huduma ya matibabu kabla na baada ya kujifungua endapo huduma hizo hazilipwi na Mfuko wa Taifa wa Bima Afya, Aidha, mwanachama atakuwa na fursa ya kupata fao hilo mara nne katika kipindi chake chote cha ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayopendekezwa itaanzisha fao la upotevu wa ajira ili kuondoa changamoto ya muda mrefu ya wanachama kujitoa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Fao hili litatolewa kwa wanachama waliopoteza ajira baada ya kukidhi vigezo vilivyoainishwa ndani ya sheria. Vigezo hivyo ni pamoja na hivi nitakavyovisoma:-

- Mwanachama awe amechangia kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na nane;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- Awe ni Mtanzania; awe hajaacha kazi kwa matakwa yake mwenyewe;
- Mwanachama huyo awe hajafikia umri wa kupata pensheni au kiinua mgongo au mafao mengine ya muda mrefu;
- Awe ametoa uthibitisho kwa Mkurugenzi Mkuu kuwa hajaweza kupata kazi nyingine na awe hajafikisha umri wa miaka 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inaongeza wigo wa wanachama wa Mfuko mpya kwa kuwatambua wafanyakazi wote waliopo kwenye mashirika ambayo Serikali ina hisa kuwa wanachama wa Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria pia inaanisha muundo wa Bodi ya Wadhamini ili kuzingatia uwakilishi wa waajiri na wafanyakazi. Sheria hii pia inaboresha masharti kuhusu mafao ya Majaji na Viongozi wengine Waandamizi wa Serikali ambao wanashika nafasi za kikatiba kwa kutenganisha mafao yao ya pensheni na stahili nyingine wanazopata wakati wa kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la maboresho haya ni kuhakikisha sheria inayopendekezwa inajikita kwenye masuala ya pensheni tu stahili nyingine za viongozi hawa zitahamishiwa kwenye sheria zao za utumishi. Hatua hii inalenga kuondoa uwezekano wa fedha za Mfuko kutumika kulipa stahili zisizohusiana na mafao ya pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inatoa fursa kwa mwanachama anayetumikia kifungo jela kushirikishwa juu ya namna bora ya mafao yake yatakavyotumika ikiwa ni pamoja na kutunza familia yake akiwa anaendelea kutumikia kifungo kwa kuiandikia Bodi ya Mfuko na Bodi itafanyia maamuzi kuzingatia taarifa ya mfungwa husika. Sheria hii pia imeainisha kipindi cha mpito na mambo

yanayopaswa kusimamiwa na kutekelezwa katika kipindi hicho cha mpito ni kama haya yafuatayo:-

- Kutambua na kulinda haki, stahili na mafao ya wanachama wa Mifuko inayounganishwa na kuhakikisha kwamba yanahamishiwa kwenye Mfuko mpya kwa usalama;
- Kutambua na kusimamia uhamishaji wa rasilimali na miradi ya Mifuko inayounganishwa;
- Kutambua na kulinda haki za wanachama katika Mifuko ya hiari inayoendesha na Mifuko inayounganishwa;
- Kuandaa muundo mpya wa Mfuko mpya ikiwa ni pamoja na kuweka mfumo utakaosimamia usalama wa ajira za watumishi wa Mifuko inayounganishwa;
- Kufanya marekebisho katika Sheria ya *NSSF* ili kuwezesha Mfuko huu kuhudumia wafanyakazi wote walioko katika sekta binafsi. Aidha, kwa mujibu wa sheria inayopendekezwa, Mfuko wa *NSSF* utatoa hifadhi ya jamii kwa sekta isiyo rasmi (*informal sector*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inalenga kuimarisha mfumo wa usimamizi na udhibiti wa sekta ili kuiwezesha Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) kuendelea kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii katika kuhakikisha kwamba mabadiliko hayataathiri kwa namna yoyote ile haki na maslahi ya wanachama na wastaafu. Vilevile kuhakikisha ushiriki wa sekta katika miradi iliyopo na iliyopangwa kufanywa haiathiriwi na mabadiliko haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha lengo hili, sheria inapendekeza kufanya marekebisho Sheria ya Msimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii ili pamoja na mambo mengine kuipa nguvu ya kisheria miongozo mbalimbali inayotolewa na Mamlaka hiyo kwa kuitaka kutangazwa katika Gazeti la Serikali ili iweze kutambulika rasmi kama sehemu ya Sheria Ndogo za nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitakwenda kwenye mpangilio wa Muswada. Sheria hii inayopendekezwa imegawanyika katika sehemu kuu kumi na moja. Sehemu ya Kwanza, inaweka masharti ya utangulizi yakiwemo jina la sheria inayopendekezwa, matumizi yake na tafsiri ya maneno yaliyotumika katika sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili inapendekeza masharti yanayoanzisha mpango wa hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma wenye lengo la kutoa mafao mbalimbali ya hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma. Sehemu hii pia inaainisha wanachama na masharti ya uanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu inapendekeza kuanzishwa kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kwa madhumuni ya kutoa mafao ya hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne inapendekeza masharti kuhusu usimamizi na uangalizi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa umma. Sehemu hii inaanzisha Bodi ya Wadhamini ya Mfuko na kuainisha majukumu na mamlaka ya Bodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sehemu hii inaweka masharti kuhusu uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko na utaratibu wa ajira kwa watumishi wengine wa Mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano inaweka masharti kuhusu usajili wa wanachama, kiwango cha michango ya kila mwezi na utaratibu wa uwasilishaji wa michango kwenye Mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya sehemu hii, Muswada unapendekeza masharti kuhusu usajili na utunzaji wa taarifa na kumbukumbu za wanachama, usajili wa wanachama, kiwango na utaratibu wa uchangiaji, usalama wa michango na masharti mengine yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita ya Muswada inaainisha masuala yanayohusiana na mafao yatakayotolewa na Mfuko wa Watumishi wa Umma. Kwa madhumuni hayo, Muswada unaainisha kwa kina masharti kuhusu umri wa kustaafu na masharti ya sifa za kupata pensheni kwa wanachama na wategemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa masharti ya sehemu hii mafao yanayopendekezwa kutolewa chini ya sheria mpya ni pamoja na mafao ya pensheni, ulemavu usiotokana na kazi, warithi kwa kuboresha muda na utaratibu wa kutoa fao hilo, fao la uzazi, fao la upotevu wa ajira na fao la ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Saba ya Muswada inaweka masharti kuhusu fedha. Sehemu hii inapendekeza masharti kuhusu vyanzo vya mapato vya Mfuko, bajeti ya mwaka, hesabu za Mfuko na ukaguzi wa hesabu. Masharti kuhusu tathmini na uwekezaji wa fedha za Mfuko pia yameainishwa katika sehemu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nane inaweka masharti kuhusu mashauri ya kisheria pamoja na makosa na adhabu mbalimbali. Chini ya sehemu hii, Muswada unaweka masharti kuhusu urejeshwaji wa michango ambayo hajjalipwa, vipaumbele vya malipo ya michango, wajibu wa wajumbe na masuala yanayohusu kesi dhidi ya Bodi ya Wadhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tisa inahusu masharti ya jumla yakiwemo ujumuishwaji wa vipindi vya uchangiaji, kulinda maslahi ya wanachama na watumishi, ukaguzi na mamlaka ya Waziri kutengeneza Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi inaweka masharti ya mpito na ufutwaji wa sheria mbalimbali. Sehemu hii inaweka masharti yanayotambua mikataba na mashauri mbalimbali dhidi ya Mifuko inayounganishwa kuwa yatahamishiwa katika Mfuko mpya. Aidha, sehemu hii pia inaweka masharti yanayolenga kulinda maslahi ya

wanachama, wastaafu, warithi wa Mifuko inayounganishwa yasiathiriwe wakati wa kuunganisha Mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Moja inaweka masharti kuhusu marekebisho yatokanayo (*consequential amendment*). Katika sehemu hii, sheria mbalimbali zinapendekezwa kufanyiwa marekebisho. Sheria hizi ni:-

(i) Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii;

(ii) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii; Sheria ya Utumishi wa Umma;

(iii) Sheria ya Tume ya Utumishi wa Polisi na Magereza na Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Marupurupu ya Majaji.

Lengo la marekebisho katika sheria hizi ni kutambua na kuhamishia katika sheria hizo stahili za baadhi ya viongozi ambao hulipwa sambamba na mafao ya uzeeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Baada ya maelezo haya, naomba sasa Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa mwaka 2018 na kuridhia usomwe kwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu na hatimaye kuwa sehemu ya sheria za nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Waziri kwa jinsi ulivyoiwasilisha hoja yako na maeneo ya msingi ulivyoyaweka wazi.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BILL SUPPLEMENT

No. 1

26th January, 2018

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.4 Vol. 99 dated 26th January, 2018

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

THE PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND ACT, 2018

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Section Title

PART I PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title and commencement.
2. Application.
3. Interpretation.

PART II THE PENSION SCHEME

4. Establishment of Scheme.
5. Composition of Scheme.

PART III THE PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND

6. Establishment of Fund.
7. Objectives of Fund.

PART IV THE BOARD OF TRUSTEES OF THE FUND

8. Establishment of Board.
9. Functions of Board.
10. Proceedings of Board.
11. Management of Fund.
12. Committees of Board.
13. Delegation of powers of Board.
14. Remuneration and allowances of Board Members.
15. Appointment of Director General.

16. Other staff of Fund.

PART V
REGISTRATION, CONTRIBUTIONS AND PAYMENTS

17. Registration and maintenance of records by employer.

18. Contributions.

19. Additional contributions for delayed remittance of contributions by employer.

20. Treating unpaid contributions as paid.

21. Protection of contributions.

22. Refund of excess contributions.

23. Accounts of members.

24. Authority to withdraw from Fund.

PART VI
BENEFITS UNDER THE SCHEME

25. Retirement age.

26. Qualifying conditions.

27. Special lump sum.

28. Rights to benefits.

29. Benefits payable.

30. Rates of retirement pension.

31. Refund of contributions due to emigration.

32. Maternity benefits.

33. Invalidity pension.

34. Rate of invalidity pension.

35. Unemployment benefit.

36. Death gratuity.

37. Survivors' benefits.

38. Basis and duration of survivors' benefit.

39. Cessation of payment of pension.

40. Pensions, gratuity and allowances for persons holding certain public offices.

41. Benefits conferred on Chief Justice.

42. Collateral for home mortgage.

43. Delayed payment of benefits.

44. Restriction on double benefits.

45. Pension when serving sentence.

46. President may exempt from certain conditions.

47. Prohibition on cession and attachment of benefits.

48. Unclaimed benefits.

PART VII
FINANCIAL PROVISIONS

- 49. Sources of fund.
- 50. Fund to be held by Board.
- 51. Annual Budget estimates.
- 52. Accounts and Supplementary Budget.
- 53. Investment of monies of Fund.
- 54. Annual accounts and audit.
- 55. Reserve account.
- 56. Exemption from tax.
- 57. Actuarial valuation report.
- 58. Restoration of financial soundness of Fund.
- 59. Bank accounts of Fund.
- 60. Government guarantee.
- 61. Reports.

PART VIII
LEGAL PROCEEDINGS, OFFENCES AND PENALTIES

- 62. Contributions to be debt to Board.
- 63. Certificates as evidence.
- 64. Summary recovery.
- 65. Joinder of cases of non-payment of contributions.
- 66. Notice of claim.
- 67. Priority for payment of contributions.
- 68. Offences and penalties.
- 69. General penalty.
- 70. Liability for acts of bodies of persons.
- 71. Protection for acts done in good faith.
- 72. Suits against Board.

PART IX
GENERAL PROVISIONS

- 73. Contribution under former schemes.
- 74. Totalization of periods and benefits.
- 75. Inspectors.
- 76. Powers to make regulations.

PART X
REPEALS, SAVINGS AND TRANSITIONAL PROVISIONS

- 77. Repeal and savings.

- 78. Existing contracts.
- 79. Pending disciplinary proceedings.
- 80. Members, pensioners and beneficiaries of former schemes.
- 81. Voluntary schemes.
- 82. Vesting of assets and liabilities.
- 83. Rights and obligations.
- 84. Investments.
- 85. Pending legal proceedings.
- 86. Transition period.
- 87. Provision regarding employees.

PART XI
CONSEQUENTIAL AMENDMENTS
(a) *Amendment of Fire and Rescue Force Act,
(Cap. 427)*

- 88. Construction.
- 89. Addition of section 29A.
- 90. Addition of Schedule.

(b) *Amendment of the Judges (Remuneration and Terminal Benefits) Act
(Cap. 424)*

- 91. Construction.
- 92. Amendment of Schedule.

(c) *Amendment of the National Social Security Fund Act,
(Cap. 50)*

- 93. Construction.
- 94. Amendment of section 2
- 95. Amendment of section 6.
- 96. Repeal of section 20A.
- 97. Amendment of section 21.
- 98. Amendment of section 22.
- 99. Amendment of section 23.
- 100. Amendment of section 24.
- 101. Amendment of section 26.
- 102. Amendment of section 27.
- 103. Amendment of section 33.
- 104. Repeal and replacement of section 39.
- 105. Repeal of section 40.
- 106. Amendment of section 49.

- 107. Amendment of section 55.
- 108. Amendment of section 72.
- 109. Addition of section 74A.
- 110. Addition of section 92A.

*(d) Amendment of the Police Force and Prisons Service Commission Act,
(Cap. 241)*

- 111. Construction.
- 112. Addition of section 19A.
- 113. Amendments of Schedule.

*(e) Amendment of the Public Service Act,
(Cap. 298)*

- 114. Construction.
- 115. Repeal and replacement of section 26.
- 116. Repeal of section 27.
- 117. Repeal and replacement of section 28
- 118. Amendment of schedule.

*(f) Amendment of the Social Security (Regulatory Authority) Act,
(Cap. 135)*

- 119. Construction.
- 120. Amendment of section 5.
- 121. Amendment of section 7.
- 122. Addition of section 25A.
- 123. Amendment of section 38A.
- 124. Amendment of section 29.
- 125. Repeal and replacement of section 30.
- 126. Amendment of section 54.
- 127. Amendment of section 58.

SCHEDULE

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly was published as a Special Supplement No.8A of 19th October, 2017 and was First Read in the National Assembly on 17th day of November, 2017. This Bill is now re-published for purposes of Second Reading and Third Reading.

Dar es Salaam,
KIJAZI
25th January, 2018
Cabinet

JOHN W.H.
Secretary to the

A BILL
for

An Act to provide for establishment of the Public Service Social Security Scheme; to provide for contributions to and payments of social security benefits in respect of the service of employees in the public service; to repeal the Public Service Retirement Benefit Act, the LAPF Pensions Fund Act, the GEPF Retirement Benefits Fund Act and the PPF Pensions Fund Act and to provide for other related matters.

ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I

PRELIMINARY PROVISIONS

Short title and
commencement

1.-(1) This Act may be cited as the Public Service Social Security Fund Act, 2018.

(2) The Act shall come into operation on such date as the Minister may, by notice published in the *Gazette*, appoint.

Application

2. This Act shall apply in Mainland Tanzania in respect of all employers and employees in the Public Service.

- Interpretation **3.** In this Act, unless the context otherwise requires-
- “actuary” means a person who is professionally qualified as an actuary and approved by the Minister in the manner prescribed in the regulations;
- “actuarial valuation” means valuation of assets and liabilities of a scheme of the Fund made by an actuary;
- “actuarial valuation report” means a report prepared by an actuary who effected actuarial valuation in accordance with the guidelines issued by the Authority;
- “administration expenses” means all cost incidental or in relation to registration of members, collection of members' contributions and disbursement of members' benefits;
- “annual pensionable emoluments” means the emoluments which is taken for the purposes of computing any pension granted to the member under this Act if he had retired from the Service in circumstances described in section 36;
- Cap 135 “Authority” means the Social Security Regulatory Authority established by section 4 of the Social Security (Regulatory Authority) Act;
- Cap 197 “Bank” means the Bank of Tanzania established under the Bank of Tanzania Act;
- “benefit” means a social security benefit payable under this Act;
- “Board” means the Board of Trustees of the Public Service Social Security Fund established by section 8;
- “child” includes a step-child, a child born out of wedlock and an adopted child;
- “commuted pension” means the lump sum payment payable to a member pursuant to section 30;
- “compulsory retirement age” means the age referred to in section 25, upon the attainment of which a member shall retire;
- Cap. 2 “constitutional office” means an office which is established by or under the Constitution of the United Republic of Tanzania;
- “contract terms” in relation to employment, means the terms whereby a person is employed on contract for a period of service with an eligibility for payment of a sum of money upon satisfactory completion of that period of service;

- “dependant” in relation to a deceased member, means-
- (a) where the deceased member was a male, his widow or if he was married to two or more wives, his widows; and
 - (b) where the deceased member was a female, the husband of such deceased member;
 - (c) every child of the deceased member who was wholly or substantially dependent upon the deceased member's income for his livelihood immediately preceding the death of the deceased member; or
 - (d) the immediate parents of the deceased member, who satisfies the deceased member's employer that they were wholly or substantially depend upon the deceased member's income for their livelihood.
- “Director General” means the Director General of the Public Service Social Security Fund appointed under section 15;
- “effective date” means the date declared as such by the Minister for commencement of this Act upon the expiration of transition period;
- “employee” means a person employed in the Public Service;
- “employee's contribution” means that portion of a statutory contribution declared under section 49 to be the employee's contribution;
- “employer” means a person or organization in the public service, with whom an employee entered into a contract of service and who is responsible for the payment of salaries of such employee;
- “employer's contribution” means a portion of statutory contribution declared under section 49 to be the employer's contribution;
- “Fund” means the Public Service Social Security Fund established by section 6;
- “former Funds” means the Public Service Pension Fund, GEPF Retirement Benefit Fund, the PPF Pensions Fund and the LAPF Pension Fund;
- “former schemes” means the Public Service Pension Scheme, GEPF Retirement Benefit Scheme, the PPF Pensions Scheme and the LAPF Pension Scheme;
- “incapable of work” means in relation to any person, incapacity for work by reason of some specific

- disease or bodily or mental disablement, and also includes references to any person deemed to be so incapable under this Act;
- “member” means an employee who is registered by the Scheme under this Act;
- “Minister” means the Minister responsible for social security matters;
- Cap.1 “month” has the meaning ascribed to it under the Interpretation of Laws Act;
- Cap. 50 “National Social Security Fund” means the Fund established under National Social Security Fund Act;
- “paid” means paid in money or money's worth, and where it has reference to a date of payment means the date on which the payment was made in cash, or as the case may be, the bills of exchange or promissory note was met;
- “pensionable emoluments” means the salary specified to be used in calculating pension or related benefits;
- Cap. 298 “Public Service” has the meaning ascribed to it by the Public Service Act and includes judicial service, parliamentary service, police force and prisons service and service in the specified corporations;
- “qualifying pensionable service” means-
- (a) any period of service rendered by a member since his becoming a member of the scheme and includes periods of absence from duty or leave with not less than half salary; and
 - (b) any period of service rendered by a member immediately prior to his becoming a member of the scheme during which he was employed by a Government on contract terms or on other than temporary terms daily paid or casual basis and during which he was governed by any employees' terminal benefits scheme under which the terminal benefit or retirement took the form of payment of a pension, and includes any periods of absence from duty or leave with not less than half salary;
- “qualifying period” means service which may be taken into account in determining whether or not that a member is eligible by length of service for a pension or gratuity;
- “reserve account” means a pool of funds built up for

- payment of obligations of the scheme;
- “salary” means gross salary excluding bonus, commission, cost of living allowance, overtime payments, directors’ fees or any other additional emolument of a member payable upon rendering service under the contract of service;
- “Scheme” means the Public Service Social Security Scheme established by section 4;
- “Service” means the service in the Public Service;
- “Service of Tanganyika” means Service in a capacity under the Government of Tanganyika or under the then East African Community before the 1st day of July, 1977 on permanent and pensionable terms under the General Fund Service and being a citizen of Tanganyika;
- “totalization of periods of contribution” means the totalization of period of contribution and benefits provided for under section 74;
- “transition period” means the period referred to under section 86;
- “trustee” means a member of the Board including the Chairman; and
- “voluntary retirement age” means the age referred to in section 25, from which age a member may retire before attaining compulsory retirement age;
- “year” means a period of consecutive twelve months.

PART II THE PENSION SCHEME

Establishment of Scheme

4. There is hereby established a Scheme to be known as the Public Service Social Security Scheme.

Composition of Scheme

5.-(1) The Scheme shall be constituted by:

- (a) all employees in the Public Service employed after the commencement of this Act;
- (b) all employees who at the time of commencement of this Act are members of the former schemes; and
- (c) all employees employed after the commencement of this Act in any specified corporation.

(2) For the purposes of this section-

- (a) all pensioners of the former schemes shall,

subject to the provisions of this Act, be deemed to be pensioners of the Scheme; and

(b) "corporation" means any company or corporation established or registered under the laws of Tanzania which the Government or its agent owns more than thirty percent of the total shares of the company or corporation.

(3) Notwithstanding subsections (1)(c) and 2(b), the Minister may, by notice published in the *Gazette*, specify any other company or corporation in which the Government owns shares to be a corporation whose employees shall be members of the Scheme.

PART III

THE PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND

Establishment
of Fund

6.-(1) There is hereby established a Fund to be known as the Public Service Social Security Fund which shall constitute of:

- (a) all contributions required to be made under this Act;
- (b) the funds of the former Funds vested in the Board under subsection (2);
- (c) assets of the former Funds;
- (d) monies earned by carrying out any project, scheme or enterprise financed pursuant to this Act;
- (e) monies earned or arising from any investments acquired by or vested in the Fund; and
- (f) all other monies or investments which may, in any manner, become payable to or vested in the Board in respect of any matter incidental to its powers and duties.

(2) The monies of the former Funds shall, with effect from the date of commencement of this Act, be transferred to the Fund and be vested in the Board.

(3) There may be charged on and paid out of the Fund all such sums of monies as may be granted by way of pension or other benefits, including the expenses of administration, as are authorised by this Act.

Objectives
of Fund

7. Objectives of the Fund shall be to:

- (a) ensure that every person who is an employee in the Public Service receives his retirement pension

benefits as and when due;

- (b) assist improvident individuals by ensuring that they save in order to cater for their livelihood during old age; and
- (c) establish a uniform set of rules, regulations and standards for the administration and payments of retirement pension and other benefits for the Public Service.

PART IV
THE BOARD OF TRUSTEES OF THE FUND

Establishment
of Board

8.-(1) There is established a Board to be known as the Board of Trustees of the Fund which shall be composed of members set out in the First Schedule to this Act.

(2) The Board shall be a body corporate with perpetual succession and a common seal and in its corporate name, be capable of:

- (a) suing and be sued;
- (b) purchasing or otherwise acquiring, holding, charging or disposing of its movable and immovable property;
- (c) borrowing and lending;
- (d) entering into contract; and
- (e) performing such other functions under this Act which may be lawfully performed by a body corporate.

(3) Notwithstanding the provisions of subsection (2), the Attorney General shall have the right to intervene in any suit or matter instituted by or against the Board.

Cap. 5

(4) Where the Attorney General intervenes in any matter pursuant to subsection **(3)**, the provisions of the Government Proceedings Act, shall apply in relation to the proceeding of that suit or matter as if it was instituted by or against the Government.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana na chimbuko la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kabla ya kuendelea, napenda kutoa maelezo machache kuhusu dhana na chimbuko la Mfuko

wa Hifadhi ya Jamii kwa ujumla wake nikioanisha na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni kwa ajili ya kumwezesha mwanajamii aweze kuishi maisha yenye thamani na staha ndani yake na kumpa uwezo wa kuendelea kumudu maisha yake wakati wote hasa pale anapokumbwa na majanga katika maisha kama vile kukosa ajira, kuugua, kuacha kazi kwa sababu ya umri yaani uzee, likizo ya kujifungua, ulemavu na majanga mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya jamii ni haki ya msingi ambayo inatambulika kimataifa na viwango vyake vimeainishwa katika Mkataba wa Shirika la Kazi Dunia (*ILO*) 102 wa mwaka 1952 pamoja na pendekezo lake la 201 la mwaka 2012. Tanzania kama nchi mwanachama iliridhia na kusaini mkataba huo, basi haina budi kuufuata na kuweka sheria na taratibu ili kuhakikisha unakuwepo mfumo madhubuti wa kutoa huduma hiyo kwa wananchi wake. Aidha, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu wa mwaka 1948, Kifungu cha 22 nacho kimeainisha suala la Hifadhi ya Jamii kwa wananchi wake katika nchi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatambulika kwamba kwa mujibu wa utaratibu wa mkataba wowote lazima upate ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utekelezaji wa maridhio ya Bunge hilo utafanya mapitisho ya sheria mbalimbali zikiwemo sheria zilizokuwa zinasimamia Mifuko inayopendekezwa na sheria hii kufutwa ambayo ni Mifuko mitano. Kwa maana ya Sheria ya Mfuko wa *NSSF* ya mwaka 1997; Sheria ya Usimamizi wa Mfuko wa *GEPP*, 2012; Sheria ya Mfuko wa *LAPF*; Sheria ya Mfuko wa *PPF*; na Sheria ya Mfuko wa *PSPF*. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetambua Hifadhi ya Jamii kama sehemu ya haki ya kila mwananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la uunganishwaji wa Mifuko hiyo ilitokana na maombi ya watumishi wa umma kupitia Vyama vyao vya Wafanyakazi na kuwasilishwa katika Shirika la Vyama vya Wafanyakazi yaani *TUCTA* ambapo

walieleza mapendekezo hayo wakati wa Maadhimisho mbalimbali ya Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani ambayo hufanyika kila mwaka Mei Mosi. Aidha, wakati wa maadhimisho hayo kuanzia mwaka 2014 (Mbeya), 2016 (Dodoma), 2017 (Kilimanjaro), *TUCTA* ambao ndio sauti ya wafanyakazi nchini imekuwa ikitoa mapendekezo hayo kwa Mgeni Rasmi mara nyingi amekuwa ni Mheshimiwa Rais kwamba Mifuko hiyo iunganishwe kwa ajili ya kuweka uwiano wa makato pamoja na maslahi mbalimbali yatolewayo na Mifuko hiyo kwa wanachama na watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya uunganishwaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma wa mwaka 2017 unalenga kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kwa malengo ya kutoa mafao ya hifadhi ya jamii kwa watumishi walio katika utumishi wa umma, kufuta Sheria ya Mfuko wa Mafao ya Hitimisho la Kazi la Watumishi wa Umma, Sura 407; Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa *LAPF*, Sura 407; Sheria ya Mfuko wa Pensheni ya *PPF*, Sura 372; Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa *GEPF*, Sura 51 kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Muswada unapendekeza pia marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Taifa wa Jamii kwa madhumuni ya kuweka masharti kuhusu mafao ya hifadhi ya jamii kwa watumishi walio katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekuwa ikitimiza majukumu ya utoaji wa huduma ya hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma na watumishi walio katika sekta binafsi kupitia Mifuko mbalimbali kama ambavyo imetajwa hapo awali kwa maana ya *PSPF*, *LAPF*, *GEPF* pamoja na *PPF* kwa mujibu wa sheria za uanzishwaji wake na ina-save kwa watumishi walio katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya Serikali na uchambuzi uliofanywa na Kamati imebainika kwamba kuunganishwa kwa Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii

kutakuwa na manufaa mengi kwa wananchi na wanachama wa Mifuko pamoja na Taifa kwa ujumla wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza gharama mbalimbali za uendeshaji wa Mifuko. Kamati imebaini kwamba kuunganisha Mifuko hiyo, gharama nyingi zitapungua zikiwemo gharama zifuatazo:-

Kupungua kwa idadi ya gharama za Bodi ya Wadhamini; kupunguza gharama za Menejimenti ya Mifuko; kupunguza gharama za uendeshaji wa Ofisi za Mikoa na Kanda; kupunguza gharama za mifumo ya TEHAMA; kupunguza gharama za ushindani na kupunguza kwa migogoro baina ya Mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hii Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) imekuwa ikilazimika kuendesha zoezi la uhakiki (*reconciliation*) kwa michango ya wanachama ambalo hili nalo lilikuwa linatumia gharama kubwa kusababisha ongezeko la gharama hizo katika gharama za uendeshaji wa Mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji na uimarishaji wa huduma kwa wanachama. Kamati imebaini kwamba kuunganishwa kwa mifuko hii kutapelekea huduma kwa wanachama kuwa bora na imara kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo itakayoendelea kutolewa na Mamlaka kuhusu utoaji wa huduma hizo kwa wateja wa Mifuko. Sheria hii inayopendekezwa imeainisha vifungu mbalimbali vinavyolinda maslahi ya wanachama ikiwa na pamoja na Kifungu namba 20 cha Muswada kinachotoa masharti ya kuzuia wanachama kuhusishwa na ucheleweshaji wa michango ambalo ni jukumu la mwajiri la kuhakikisha michango ya mwajiriwa inapelekwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuboresha huduma za wanachama, Kifungu cha 43(3) kinampa haki kamili mwanachama kuweza kudai kulipwa fidia na Mfuko

ambapo kama Mfuko huo utamcheleweshea stahiki yake ya mafao ndani ya siku 90 na kubainika kwamba ucheleweshaji huo haujasababishwa na mwanachama bali ni Mfuko husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vya Sheria vya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeboreshwa ili kuipa Mamlaka uwezo wa kuchukua hatua stahiki kwa watumishi wa Mifuko ambao watakiuka masharti ya kisheria na maelekezo ya Mamlaka. Kwa kufanya hivyo, huduma za wateja wa Mifuko hazitaathirika kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Muswada. Kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2016, mnamo tarehe 17 na 18 Kamati ilifanya mkutano wa wadau kwa lengo la kupokea maoni (*public hearing*) kwa kusaidia Kamati kufanya uchambuzi wa Muswada huu. Wadau mbalimbali walifika katika mkutano huo ambao ni pamoja na:-

National Organization for Legal Aids; Legal and Human Rights Centre; Chama cha Wanasheria Tanzania; Chama cha Walimu Tanzania; Chama cha Waajiri; Chama cha Wafanyakazi (TUCTA); Chama cha Wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Tanzania na Shirika la Kazi (ILO). Aidha, wadau wengine walitoa maoni yao kwa maandishi wakiwemo Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA) na Chama cha Wafanyakazi wa Mahakama ambayo yamesaidia Kamati kuboresha Muswada huu na kutoa maoni na ushauri huu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hoja nzito zilizoibuliwa, siku ya tarehe 19 ilikuwa ni siku ya kufanya maridhiano ya Serikali kupata ushauri elekezi (*consultation*) ili kuwa na dhana ya uwajibikaji wa pamoja. Kamati ikaona ni busara kuwapa nafasi Serikali. Napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa katika mashauriano ya hoja mbalimbali zikiwemo zile zilizohitaji ushauri elekezi, Serikali ilikubaliana na Kamati kwamba marekebisho yote yatawasilishwa na Serikali kwenye Jedwali la Marekebisho (*Schedule of Amendments*) kama Kamati ilivyopendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Spika na wewe kwa kusaidia Kamati kutekeleza wajibu wake, naipongeza Serikali kwa kuwa wasikivu na kupokea maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kuyapokea kwa ajili ya kuyafanyia kazi. Ni imani yangu na Kamati nzima kwamba tumeisaidia Serikali na wananchi wa Tanzania katika kuiboresha sheria hii ambayo ipo katika mchakato wa kutungwa kwa ajili ya manufaa ya wafanyakazi wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa namna ambavyo amekuwa akitoa ushirikiano wa dhati kwangu mimi pamoja na Kamati nzima. Kwa jinsi alivyokuwa msikivu, mwelewa na hata pale tulipohitaji ufafanuzi wa Serikali alitoa ushirikiano bila kusita wakati wa kuuchambua na kuujadili Muswada huu. Kwa kweli Mheshimiwa Jenista ni mfano wa kuigwa, hongera sana dada yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati. Napenda kutoa maoni na ushauri na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo kwa lengo la kuboresha Muswada. Kamati imebaini makosa ya uchapaji, *spelling and grammatical errors* na inashauri marekebisho yafanywe kwa maeneo yote yenye makosa ili kuweka maana stahiki katika vifungu vilivyoonekana kuwa na makosa ya uchapishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza kifungu cha tatu (3) kuhusu *Interpretation* kufuta neno '*leader*' katika maana ya neno *qualifying period* na badala yake kuweka neno '*member*'. Aidha, kifungu hicho Kamati inashauri kufuta marejeo namba 87 kwa maana ya *transitional period* badala yake kitumike kifungu namba 86 ili kuondoa makosa ya uchapaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha tatu (3) cha tafsiri ya maneno mbalimbali liongezwe neno '*Parliamentary Service*' kwa maana *Public Service* ili kutambua utumishi wa Bunge ni mtumishi wa umma na ni

mwanachama wa mfuko huu unaopendekezwa kuanzishwa. Aidha, kuongezwa tafsiri ya maneno kama vile *Special lump sum, pension, unemployment benefit, funeral benefit and sickness benefit* ambayo yametumika hajapatiwa tafsiri yake katika orodha ya maneno yaliyotafsiriwa kwa Muswada huu. Aidha, Kamati inashauri maneno haya yapatiwe tafsiri pia zijumuishwe katika Kanuni ambazo zitatungwa na Waziri mwenye dhamana kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza pia neno '*month*' tafsiri iliyopewa iboreshwe kwa kuwa siyo miezi yote ina siku thelathini kama ilivyotafsiriwa, kuna mwezi ambao siku ni ishirini na nane, ishirini na tisa na mingine siku thelathini na moja. Kamati inapendekeza isomeke *calendar month or a written calendar* badala ya *a period of thirty days consecutively* kama ilivyotafsiriwa katika Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho cha tatu (3) katika tafsiri ya neno '*qualifying pensionable service*' kuna neno *continuous* katika vipengele vyote yaani "a" na "b", kwa kuwa mwanachama anaweza akawa hajafanya kazi kwa kipindi fulani kutokana na sababu mbalimbali na baadaye akarejea kazini katika sekta ya umma au katika sekta binafsi, ambapo atakapofikia umri wa kustaafu akawa anastahili kulipwa mafao yake kwa kujumlisha muda aliotumikia na kuchangia katika Mfuko wa hifadhi ya jamii. Aidha, katika tafsiri ya neno '*totalization*' neno '*fully contributed*' lifafanuliwe ili lisiweze kuleta mkanganyiko na liweze kueleweka sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tafsiri ya neno '*salary*' Kamati inashauri neno hilo litafsiriwe vyema na ikiwezekana tafsiri inayotumika na Msimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya jamii (SSRA) itumike. Kamati inashauri marupurupu mengine kama vile posho zisijumuishwe katika tafsiri hiyo kwani posho hizo hubadilika mara kwa mara kadiri inavyoonekana inafaa. Aidha, Kamati inashauri pia maneno "*Employers Association*" na "*Employees Association*" yaongezwe katika orodha ya tafsiri ya meneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika orodha ya tafsiri ya maneno kuna neno la *'full pension'* kwa kuwa tafsiri hiyo haijakamilika kama ambavyo imetafsiriwa na Sheria ya SSRA. Kamati inashauri tafsiri hiyo izingatie tafsiri itakayorejewa katika kanuni za ukokotozi zitakazotengenezwa kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, neno *'Actuarial valuation'* limepewa tafsiri yake katika orodha ya maneno na limetumika katika kifungu cha 91(a)(i) kwa maana tofauti na tafsiri iliyopo katika maneno mengine. Kamati inashauri tafsiri hiyo iangaliwe upya ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza katika matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tafsiri ya neno *'qualifying period'* Kamati inapendekeza neno *'leader'* lifutwe na badala yake litumike neno *'member'* ili kufanya marekebisho ya kiandishi na kuleta tafsiri sahihi kwa kuwa wachangiaji wa Mfuko huo wa Hifadhi ya Jamii wote wanatambulika kama wanachama (*members*) na siyo kiongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika tafsiri ya neno *'transition period'* kumefanyika marejeo ya kifungu cha 87 kinachozungumzia *provision regarding employees Cap.298*, Kamati inashauri ibadilishwe na badala yake marejeo yafanyike katika kifungu cha 86 ambacho kinazungumzia *transition period*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha sita (6) kinachohusu *Establishment of the Fund*. Katika Kifungu kidogo 6(1)(c), Kamati inashauri kifutwe na kiandikwe upya ili kuondoa mkanganyiko uliopo katika kifungu hicho tajwa na kifungu cha 80(2) na 105 vya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 15 kinachohusu *Appointment of the Director General* wa Mfuko huu. Kifungu cha 16(2) kinachohusu *other staff of the fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 18 kinachohusu *contributions*, Kamati inapendekeza kufuta maneno yanayosomeka '*such amount as the Minister may, by order in the Gazette, determine*'. Katika Kifungu cha 18(8) Kamati inapendekeza kuondoa neno '*may*' na kuweka neno '*shall*'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 19 kinachohusu *Additional contributions for delayed remittance of contributions by employer*. Kifungu 19(1) kina mkanganyiko na kifungu 18(3) katika kuainisha nani ni mwajiri. Kamati inashauri kifanyiwe kazi ili kuondoa mkanganyiko huo. Aidha, katika kifungu hicho rejea ifanyike katika Kifungu cha 18(6) badala ya kifungu cha 21(2) na kifungu 19(3). Kifungu cha 19 kinachohusu *Additional contributions for delayed remittance of contributions by employer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 29(1) kinachohusu *Benefits payable*, Kamati inashauri iongeze aina mbili ya mafao kutoka nane (8) yanayotolewa na Mfuko hadi kufikia kumi (10) kwa kuongeza fao la *education benefit* na *gratuity benefit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 33 kinachohusu *invalidity benefit*. Kifungu cha 37 kinachohusu "*Survivors benefits*", kifungu 37(1) (a) na (b). Kifungu cha 38 kinachohusu *Basis and duration of survivor's pension*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 40 kinachohusu *pensions, gratuity and allowances for persons holding certain public office*. Kamati inapendekeza viongozi waliotajwa katika kifungu hiki aongezwe Katibu wa Bunge (*Clerk of National Assembly*) kwenye orodha ya viongozi wanaopata mafao maalum kwa kuwa nafasi hiyo ni nafasi ya kikatiba kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 87 (1) ambapo imetamka uwepo wa Katibu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Katika kifungu hiki kuongezwe neno '*and Security*' kati ya neno '*Intelligence*' na neno '*service*' ili kuweza kurekebisha jina la Mkurugenzi

wa Idara ya Intelijensia kuweza kuleta maana sahihi ya cheo hicho katika sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 47(2)(c) kinachohusu *Prohibition on cession and attachment of benefits*, Kamati inashauri kiangaliwe upya ili kuondoa ubaguzi wa jinsia kwani kimemtaja mke na kuacha mume. Aidha, marekebisho yafanyike ili kumtambua mnufaikaji pasipo kuainisha jinsi ya mnufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 56 kinahusu *exemption from tax*. Kifungu cha 57(4) *Actuarial Valuation Report*, Kamati inashauri neno 'may' lifutwe na kuweka neno 'shall' ili kuweza kuwa na sharti la lazima kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kurekebisha upungufu uliobainika kwenye taarifa ya mtaalam wa uthamini wa hali halisi ya Mifuko (*Actuarial Valuation*) ya hifadhi ya jamii. Kwa kubaki hivyo, mamlaka inapewa mwana wa kuamua kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla. Umuhimu wa *SSRA* kuongezewa majukumu ya usimamizi ya hifadhi ya jamii. Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 ilipelekea Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutunga Sheria Na.8 ya mwaka 2008 pamoja na mambo mengine ilitoa masharti ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (*Social Security Regulatory Authority*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu mengine, Mamlaka hii ya usimamizi ilipewa jukumu la kusimamia Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kwa kutoa miongozo ya utendaji sahihi, kusimamia utendaji wa Mifuko, kutetea na kulinda maslahi mbalimbali ya wanachama, kutoa ushauri wa kisera kwa Waziri mwenye dhamana, kusajili wasimamizi wa uwekezaji wa fedha za Mifuko ya jamii na majukumu mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa, bado kuna majukumu mengi na makubwa kwa Mamlaka

hii ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuwa majukumu hayo bado yapo ikizingatiwa kwamba Mifuko hii inakwenda kuunganishwa hivyo Mamlaka inapaswa kuhakikisha kumbukumbu za wanachama wa Mifuko yote zinabaki vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza pia masuala yote yanayohusiana na hifadhi ya jamii, iwekwe chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Mifuko ya Bima ya Afya ikiwemo Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (*NHIF*), Bima ya Afya ya Jamii (*CHF*) na mifuko mingine yenye dhana ya hifadhi ya jamii iwekwe chini ya msimamizi mmoja. Kwa kufanya hivyo, kutaondoa mkanganyiko na unufaikaji wa mafao zaidi ya mara moja ikiwemo fao la matibabu na fao la ugonjwa yanayotolewa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wanaotoka katika Mifuko hiyo kuwahahakikishia ajira zao. Kamati inaona kuwa kuunganishwa kwa Mifuko hii kutapelekea suala la ajira za wafanyakazi katika Mifuko hiyo kuathirika na wengine kupoteza nafasi zao za awali na hata kupoteza ajira zao kabisa. Kamati inashauri, Wizara yenye dhamana ikishirikiana na Mifuko husika pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Jamii kuhakikisha wanalinda ajira za wafanyakazi hao bila kujali nafasi zao za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani ya Kamati kuwa, kuanzia sasa ofisi za Mifuko hii zitakuwa hadi ngazi ya Wilaya ambako wanachama wengi wapo wakiwemo Walimu, Wauguzi, Askari na kada nyingine mbalimbali hasa kutoka katika sekta ya umma. Hivyo basi Kamati inasisitiza watumishi wote waliokuwa katika Mifuko hiyo ajira zao zilindwe kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachama katika Mifuko hiyo wasihame na michango yao ili kuiwezesha Mifuko hiyo kujiendesha. katika kuhakikisha Mifuko hii inakuwa na muda mrefu wa uhai wake, ni maoni ya Kamati kwamba, katika

uunganishaji na usajili wa wanachama wa Mifuko uanze na wafanyakazi wapya katika sekta zote mbili kwa maana kwamba, mara baada ya sheria hii kusainiwa na Mheshimiwa Rais, basi wafanyakazi watakaoajiriwa katika sekta zote mbili waanze kutenganishwa usajili wao ili mfanyakazi wa sekta ya umma asajiliwe katika Mfuko wa umma na mfanyakazi wa sekta binafsi asajiliwe katika Mfuko wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwa wakati huu, wanachama waliopo katika Mifuko hiyo minne inayounganishwa wote wabaki katika Mfuko wa umma na wale waliopo katika mfuko wa *NSSF* waendeleo kuchangia huko bila kujali ni mfanyakazi wa sekta gani, utaratibu huu unafahamika kama *cut-off date* ya mwanachama. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kuboresha uwiano wa wanachama wastaafu kutoka uwiano wa 1:5 hadi kufikia uwiano wa 1:10, kutapunguza idadi ya wanachama kuanza kufuatilia taarifa zao wakati wa kupata stahiki za mafao yakiwemo mafao ya uzazi na kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sababu kubwa zaidi ni kwamba michango ya wanachama hao imewekezwa katika miradi mbalimbali iliyogharamiwa na michango yao ambapo kuwahamisha na uwekezaji huo itailetea usumbufu Serikali na wanachama wake pia na kwa mfumo ulivyo makusanyo ya michango ya watumishi sasa (*current collections*) ndiyo inambeba kwa kumlipa mtumishi anayestaafu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifafanue fao la upotevu wa ajira (*Unemployment Benefit*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko kufuatilia michango ya wanachama kwa waajiri. Mara baada ya mwajiriwa kupeleka taarifa zake kwa mwajiri na kuanza kulipwa mshahara wake huanza kukatwa michango yake kwa ajili ya kupeleka michango yao. Kamati inashauri Mifuko hiyo iweke utaratibu wa kufuatilia michango hiyo kwa waajiri ili kifungu cha kulipa faini kilichopo katika sheria hii kiweze kutumika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi katika kampuni yenye hisa za Serikali kuchangia katika mfumo wa umma. Nchi yetu imekuwa na kampuni za aina mbalimbali zile za binafsi na kampuni ambako Serikali imeingia ubia na mwekezaji. Kamati inashauri Kampuni zote ambako Serikali ina hisa zake bila kujali kiasi cha umiliki wa hisa hizo, ikiwemo *TBL, TCC, Airtel* na Kampuni nyingine, wafanyakazi wake wote wawe wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, kutaweza kuimarisha Mfuko huu lakini pia kuweza kulinda maslahi ya wananchi wetu ambao ni waajiriwa katika kampuni hizo kwa kuhakikisha kwamba ni kwa kiasi gani wafanyakazi wa Kitanzania wananufaika na Kampuni hizo na kuwekewa hazina yao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kulipa madeni ya mifuko. Mifuko inayounganishwa kwa sheria hii imekuwa ikiidai Serikali madeni makubwa ya kuanzia mwaka 2000 na kurudi nyuma ilipoamua kuwalipa wastaafu mafao licha ya Serikali kutopeleka mafao ya watumishi hao katika Mifuko wanakonufaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilisha utoaji wa fao la elimu. Katika Mifuko hii inayounganishwa kwa sheria hii, kuna Mifuko iliyokuwa inatoa fao la elimu kwa wanachama na hata wategemezi wa wanachama wa Mifuko hiyo. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 29(1) cha orodha ya mafao yanayoainishwa na Mfuko huu fao la elimu limeachwa na kwamba halitatolewa tena kwa wanachama wa Mfuko huu. Kamati inaunga mkono hoja ya kuondolewa kwa fao la elimu katika orodha ya mafao kwani sasa Serikali inaihudumia jamii nzima ya Tanzania kwa kutoa elimu bila malipo kuanzia elimu ya msingi. Nashauri kama itakuwa hivyo basi wale waliokuwa wananufaika, waendeleo kunufaika mpaka waishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria iwatambue Katibu wa Bunge na Makatibu Wakuu wa Wizara. Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania imemtambua Katibu wa Bunge katika Ibara ya 87(1) kwamba kutakuwa na *Accounting Officer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri sheria hii iwajumuishe Makatibu Wakuu wote wa Wizara ili waweze kunufaika na Mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa umma. Kwa kufanya hivyo, kutaondoa dhana ya matumizi mabaya ya madaraka yao kwa manufaa binafsi na kutalinda hadhi ya maisha na utu wao mara baada ya ajira zao kukoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa mara nyingine tena napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada huu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Anthony Mavunde na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, Katibu Mkuu Eric Shitindi na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati na kupelekea kuwasilisha vyema Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru tena wadau wote waliofika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri yenye umahiri wakati wote wa uchambuzi wa Muswada huu. Wajumbe wamefanya kazi nzuri ya kuhakikisha uchambuzi wa Muswada huu unakuwa wenye tija kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman B. Hussein na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati Ndugu Chacha

Nyakega pamoja na Katibu wa Kamati hii Ndugu Agnes Nkwera na Msaidizi wa Kamati Ndugu Waziri Kizingiti kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru Kaimu Mshauri Mkuu wa Mambo ya Sheria wa Bunge Ndugu Pius Mboya pamoja na wasaidizi wake Ndugu Leorcard Kapongwa, Ndugu Maria Mdulugu na Ndugu Nesta Kawamala kwa uchambuzi wa kisheria walioufanya kuisadia Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa na kwa kuzingatia muda.

MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII KWA WATUMISHI WA UMMA WA MWAKA 2017 (*THE PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND, 2017*) KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2017 (*The Public Service Social Security Fund, 2017*). Uwasilishaji huu wa maoni na mapendekezo ya Kamati ni kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, uliipa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii jukumu la kushughulikia Muswada huu wa Sheria. Naomba

kutoa shukrani zangu za dhati kwa kuendelea kuonesha imani kubwa kwa Kamati ninayoiongoza na kuipa kazi ya kuufanyia kazi Muswada na kuwasilisha maoni na mapendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu. Nina imani Kamati imefanya kazi kwa weledi mkubwa na kuweza kuutendea haki Muswada na kuisaidia Serikali kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza shughuli hiyo muhimu ya uchambuzi wa Muswada, Kamati ilipata fursa ya kupokea Maelezo ya kina kuhusu Muswada wa Sheria inayopendekezwa yaliyowasilishwa mbele ya Kamati na Ofisi ya Waziri Mkuu-Waziri, Sera, Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Watu Wenye Ulemavu Mheshimiwa Jenister Joakim Mhagama, (Mb) ambaye alieleza kuhusu Madhumuni, Sababu na Mpangilio wa Muswada huu siku ya **tarehe 16 Januari, 2018**. Maelezo hayo ya kina yalitanguliwa na Semina ya kutoa uelewa mpana kwa Wajumbe wa Kamati kuhusu dhana nzima ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii pamoja na chimbuko la hoja ya kuunganisha mifuko hii. Semina hiyo ilitolewa na wataalamu wa masuala ya Hifadhi ya Jamii iliawezesha wajumbe wa kamati kuwa katika nafasi nzuri ya kuelewa dhana na msingi mzima wa uunganishwaji wa mifuko na sababu za mapendekezo ya sheria hii ambapo Wajumbe waliweza kuwa katika nafasi nzuri ya kuuchambua na kuweza kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya kuuboresha Muswada.

2.0 DHANA NA CHIMBUKO LA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII

Mheshimiwa Spika, Kabla ya kuendelea napenda kutoa maelezo machache kuhusu Dhana na Chimbuko la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa ujumla wake ikioanishwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Dhana ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni kwa ajili ya kumuwezesha mwanajamii aweze kuishi maisha yenye thamani na staha ndani yake na kuwapa uwezo wa kuendelea kumudu maisha yake wakati wote na hasa pale akapokumbwa na majanga katika maisha yake kama vile kukosa ajira, kuugua, kuacha kazi kwasababu ya

umri (uzee), likizo ya kujifungua, ulemavu na majanga mengine.

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya jamii ni haki ya msingi ambayo inatambulika kimataifa na viwango vyake vimeainishwa katika **Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Na.102 wa Mwaka 1952** pamoja na pendekezo lake **Na.201 la Mwaka 2012** na Tanzania kama nchi mwanachama aliliridhia kwa kusaini Mkataba huo, basi nchi haina budi kuufuata kwa kuwekwa utaratibu wa kuhakikisha kunakuwepo na mfumo madhubuti wa kutoa huduma hiyo kwa wananchi wake. Aidha, Mkataba wa kimataifa wa haki za binadamu wa **Mwaka 1948 kifungu cha 22** nacho kimeainisha suala la Hifadhi ya Jamii kwa wananchi wake katika nchi yeyote.

Mheshimiwa Spika, inatambulika kwamba, kwa mujibu wa utaratibu Mkataba wowote lazima upate ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katika utekelezaji wa maridhio hayo Bunge liliweza kufanya mapitisho ya Sheria mbalimbali zikiwemo Sheria zilizokuwa zinasimamia Mifuko inayopendekezwa na Sheria hii kufutwa ambayo ni Mifuko mitano (5) kwa maana ya sheria ya mfuko wa NSSF ya Mwaka 1997, Sheria ya usimamizi wa mfuko wa GEPF ya mwaka 2012, Sheria ya mfuko wa LAPF, Sheria ya mfuko wa PPF na Sheria ya Mfuko wa PSPF.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ibara ya 11(1) pia imetambua Hifadhi ya jamii kama sehemu ya haki ya kila mwananchi wa Tanzania. Kwa kufanya hivyo Muswada huu umetoa mapendekezo ya aina nane (8) za Mafao ikiwemo fao la kustaafu, fao la urithi kwa mtumishi atakayefariki na kuacha wategemezi wake, fao la pensheni endapo mtumishi atafikisha miaka 60 kazini na ndiyo ukomo wa utumishi kwa mujibu wa sheria, fao la uzazi kwa mtumishi atakayejifungua mtoto akiwa bado kazini, fao la upotevu wa ajira, fao la ugonjwa endapo mtumishi ataugua ugonjwa ambao utamsababishia kushindwa kuendelea kufanya kazi katika utumishi wa umma na kupata kipato chake cha kila siku,

fao la kifo na fao la mazishi kwa mwanachama wake. Aidha, utolewaji wa mafao hayo hautaingiliana kati ya unufaikaji wa fao moja na fao lingine kwa wakati mmoja kwa mujibu wa usimamizi wa sheria hii inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la uunganishwaji wa Mifuko hiyo lilitokana na maombi ya watumishi wa Umma wenyewe kupitia vyama vyao vya wafanyakazi na kuwasilishwa na Shirikisho la Vyama vya wafanyakazi yaani **TUCTA** ambapo walieleza mapendekezo hayo wakati wa maadhimisho mbalimbali ya Sikukuu ya wafanyakazi Duniani ambayo hufanyika kila mwaka tarehe **01 Mei** ijulikanayo kama **Mei Mosi**.

Aidha, wakati wa maadhimisho hayo kuanzia mwaka 2014 jijini Mbeya, 2016 Mjini Dodoma, 2017 Mjini Moshi – Kilimanjaro TUCTA ambayo ndiyo sauti ya wafanyakazi nchini, imekuwa ikitoa mapendekezo hayo kwa mgeni rasmi (**mara nyingi amekuwa Mheshimiwa Rais**) kwamba Mifuko hiyo iunganishwe kwa ajili ya kuweka uwiano wa makato pamoja na maslahi mbalimbali yatolewayo na mifuko hiyo kwa wanachama hasa watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, mbali na sababu ya kuweka uwiano wa makato na maslahi ya mwanachama katika mifuko ya hifadhi ya jamii, mapendekezo mengine yaliyokuwa yakitolewa ni pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji. Aidha, mapendekezo yao yalikuwa ni kuwepo kwa mifuko miwili tu, mmoja ukihudumia sekta ya Umma na wa pili kwa ajili ya sekta binafsi. Licha ya kupunguza gharama pia kuondokana na ushindani usio na tija baina ya mifuko iliyopo na kuifanya Sekta ya Hifadhi ya Jamii kuwa bora zaidi kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitueleza kwamba, katika kusikiliza hoja ya wafanyakazi wa umma iliamua kulichukua pendekezo hilo na kulifanyia kazi. Aidha, kabla ya kutekeleza mapendekezo ya uunganishaji wa mifuko ya Hifadhi ya jamii ambacho kimekuwa ni kilio cha wafanyakazi wengi wa umma hapa nchini kwa muda mrefu Serikali ilifanya utafiti

wa kuona jinsi gani mifuko hiyo inaweza kuunganishwa na nini faida zake, lakini pia kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wafanyakazi wenyewe kupitia majukwaa au vyama vyao, waajiri na hata baadhi ya idara za Serikali, kupeleka Waraka wa Baraza la Mawaziri pamoja na kuandaa Muswada wa Sheria wa kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kuunda Mifuko miwili kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali. Muswada huo ulisomwa kwa mara ya Kwanza mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya **tarehe 17 Novemba, 2017**.

3.0 DHUMUNI LA MUSWADA NA UUNGANISHWAJI WA MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2017 (*The Public Service Social Security Fund, 2017*) **unalenga kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kwa malengo ya kutoa mafao ya hifadhi ya jamii kwa watumishi walio katika Utumishi wa Umma na kufuta sheria ya Mfuko wa mafao ya Hitimisho la kazi kwa Watumishi wa Umma, Sura 407 Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa LAPF, Sura 407 Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa PPF, Sura 372 na Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa GEPF, Sura 51 kwa ajili hiyo. Aidha, Muswada unapendekeza pia marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa madhumuni ya kuweka masharti kuhusu mafao ya hifadhi ya Jamii kwa watumishi walio katika sekta binafsi.**

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu imekuwa ikitimiza majukumu ya utoaji wa huduma ya Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma na Watumishi walio katika Sekta binafsi kupitia mifuko mbalimbali kama ambavyo imetajwa hapo awali kwa maana ya PSPF, LAPF, GEPF pamoja na PPF kwa mujibu wa Sheria za uanzishwaji wake na NSSF kwa watumishi walioko katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Serikali na uchambuzi uliofanywa na Kamati imebainika kwamba, kuunganishwa kwa Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii kutakuwa

na manufaa mengi kwa wanachama wa mifuko hiyo pamoja na Taifa kwa ujumla wake kama ifuatavyo;

3.1 Kupunguza gharama mbalimbali za uendeshaji wa Mifuko

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sheria ya mifuko ili uweze kutoa huduma bora kwa wanachama wake lazima uingie gharama za kuendesha mfuko huo. Kwa hali ilivyo sasa mifuko mitano (5) inayowahudumia wafanyakazi katika sekta zote mbili na inatoa mafao ambayo kwa kiasi kikubwa yanafanana, na kwa mujibu wa mfumo wa uendeshaji wa kila mfuko unapaswa kuwa na mfumo wa kitaasisi ambapo mfumo hiyo inapelekea gharama kubwa za uendeshaji wa mifuko husika. Kwa sasa nchi yetu ina mifuko mitano (5) kama ambavyo imetajwa hapo awali na mifuko hiyo ilikuwa inatumia kiasi kisichopungua **shilingi Bilioni 235.8** kwa mwaka kwa ajili ya uendeshaji wa mfuko husika kwa wanachama katika ofisi za kanda na mikoza.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba kwa kuunganisha mifuko hiyo gharama nyingi zitapungua zikiwemo gharama zifuatazo;

i) Kupungua kwa idadi na gharama ya Bodi ya wadhamini

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazoisimamia Mifuko hii ilitoa masharti ya kuanzishwa kwa bodi ya wadhamini kwa kila mfuko. Kamati imebaini kwamba katika uendeshaji wa Mifuko hii kila mfuko ulikuwa na bodi yake ya wadhamini yenye wajumbe wasiopungua tisa (9), kwa mantiki hiyo kwa mifuko yote wajumbe waliopo ni takribani 45. Wajumbe hawa wanapaswa kulipwa kila baada ya miezi mitatu (3) ada ya ujumbe (**Directors Fees**) pamoja na gharama nyingine kwa mujibu wa miongozo ya Msajili wa Hazina, ambapo gharama za bodi hizi zilikuwa ni kubwa ikilinganishwa na uhalisia. **Jedwali namba 1** linaonesha gharama za uendeshaji wa bodi ya udhamini kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 hadi 2015/2016.

Jedwali Na. 1
Gharama za uendeshaji wa Bodi ya Wadhamini kwa
Mwaka 2013/2014 hadi 2015/2015 (Tsh.Bilioni)

MFUKO	LAPF	PPF	PSPF	NSSF	GEPP	WASTANI
MWAKA	GHARAMA	ZA	UENDESHAJI	ZA	MFUKO	KILA
2013/2014	0.8	1.9	1.4	3.6	0.3	1.06
2014/2015	1.8	2.6	1.8	3.9	0.3	2.08
2015/2016	1.5	1.6	1.7	4.2	0.4	1.88

Chanzo: Taarifa ya SSRA

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa jedwali la matumizi ya fedha kwa bodi ya wadhamini kwa mifuko yote mitano (5) ni kiasi cha shilingi **Bilioni 1.67** kwa mwaka kwa wajumbe wasiozidi 45 kama ada ya ujumbe wa bodi na malipo mengine. Ambapo baada ya Kamati kufanya uchambuzi wake wa kina ikabaini kwamba, katika mifuko inayounganishwa (Mifuko minne) ili kupata mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa watumishi wa umma, Bodi ya wadhamini kwa wajumbe wake 36 ilikuwa inatumia kiasi cha **shilingi Bilioni 4.46** kwa wastani wa kiasi cha **shilingi Bilioni 1.115** kwa mwaka kwa ajili ya kuhudumia Bodi ya wadhamini yenye wajumbe watano (9) kwa kila mfuko.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuunganisha mifuko hii itapunguza gharama za Bodi ya wadhamini kwani katika mifuko hiyo kumekuwa na utofauti mkubwa wa gharama kati ya bodi moja na nyingine. Kwa mfano **mwaka 2014/2015** mfuko wa **LAPF** ilitumia kiasi cha **shilingi Bilioni 1.8** wakati mfuko wa **GEPP** ilitumia kiasi cha **shilingi Bilioni 0.3** tofauti ya shilingi **Bilioni 1.5** sawa na **asilimia 83.3** kwa gharama za uendeshaji wa Bodi ya wadhamini, Kamati ilijiuliza je, miongozo kutoka kwa Msajili wa Hazina ya usimamizi na uendeshaji wa Bodi za mifuko ya Hifadhi ya jamii ni tofauti kulingana na aina ya mfuko? Na je, majukumu ya Bodi yanatofautiana kati ya mfuko mmoja na mwingine?

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kwamba hii ilikuwa ni gharama kubwa sana kwa bodi hizo na ikumbukwe kwamba hizi ni fedha za wanachama na faida inayopatikana kutokana na uwekezaji wa fedha za wanachama hao katika miradi mbalimbali. Kamati iliona gharama hizi ni kubwa na utofauti wake ni mkubwa, hivyo basi kwa ajili ya kupunguza gharama hizo Kamati inaunga mkono hoja ya Serikali ya kuunganisha mifuko hiyo mine (4) na kuwa mfuko mmoja na mfuko wa NSSF kwa ajili ya watumishi wa sekta binafsi.

ii) Kupungua kwa gharama za menejimenti ya Mifuko

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, maamuzi ya Serikali kuunganisha mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii kutoka Mifuko Mitano (5) hadi miwili kutapunguza gharama za uendeshaji katika suala zima la menejimenti. Kwa kuwepo mifuko mitano ya hifadhi ya jamii ilikuwa inalazimu kila mfuko kuwa na timu yake ya menejimenti ambapo kila mfuko ulikuwa na timu yake ya uongozi akiwemo Mkurugenzi Mkuu na wastani wa wakurugenzi wa Idara mbalimbali sita (6) kwa ajili ya uendeshaji wa mfuko husika. Kwa uwepo wa wakurugenzi hao ambao ni wajumbe wa menejement kila mjumbe alistahili kupata mshahara na stahiki mbalimbali kwa mujibu wa sheria za mifuko husika, rejea **Jedwali namba 2**.

Jedwali Na. 2

Mishahara na stahili za viongozi wa Menejimenti (Tsh.

Bilioni)

MFUKO	LAPF	PPF	PSPF	NSSF	GEPF	WASTANI KWA MWAKA
MWAKA	GHARAMA	ZA	UENDESHAJI	KWA	KILA	MFUKO
2013/2014	1.7	3.7	2.8	7.3	0.5	3.20
2014/2015	3.6	5.2	3.5	7.8	0.7	4.16
2015/2016	3.1	3.1	3.4	8.4	0.9	3.78

Chanzo: Taarifa ya SSRA

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha ya menejimenti kwa wajumbe wake, mishahara na stahili katika mifuko hii mitano ilikuwa ni makubwa na ambayo yalikuwa yanapanda kila mwaka, mathalani, mfuko wa LAPF mwaka 2013/2014 ilitumia kiasi cha **shilingi Bilioni 1.7** ikilinganishwa na mwaka 2014/2015 ambapo mfuko ulitumia kiasi cha shilingi **Bilioni 3.6** ambalo ni ongezeko la **shilingi Bilioni 1.9** sawa na **asilimia 52.7** kwa mwaka huo. Aidha, mifuko yote matumizi ya menejimenti kwa mwaka wa fedha 2013/2014 hadi Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 gharama za uendeshaji wa ilikuwa ni kwa wastani wa shilingi **Bilioni 0.96** ambayo sawa na **asilimia 23** ya ongezeko ikilinganishwa na matumizi ya menejimenti kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona matumizi haya ni makubwa sana na hakuna sababu ya kuendelea kuwa na mifuko mingi ambayo kimsingi haina tija kwa wanachama na taifa kwa ujumla, kwani fedha hizo zilizokuwa zinatumiwa ni michango ya wanachama ambao wanajiwekea akiba yao ya maisha kwa dhana ya hifadhi ya jamii.

MFUKO	LAPF	PPF	PSPF	NSSF	GEPF	WASTANI
	iii)	Kupunguza gharama za uendeshaji				ofisi za
	Mikoa na Kanda					MWAKA
MWAKA	GHARAMA ZA	UENDESHAJI	KWA	KILA	MFUKO	
2013/2014	1.7	5.2	3.5	7.8	0.7	4.16
2014/2015	3.6	5.2	3.5	7.8	0.7	4.16
2015/2016	3.6	5.2	3.5	7.8	0.7	4.16

Mheshimiwa Spika, mujibu wa uendeshaji wa mifuko hii ya hifadhi ya jamii inayopendekezwa kufutwa na sheria hii ili kufanikisha utekelezaji wa utoaji wa huduma bora kwa wanachama wake mifuko ilianzisha ofisi mbalimbali ikiwemo za Kanda na Mikoa. Kwa mujibu wa taarifa za msimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii mifuko yote ina jumla ya ofisi **114** zinazojumuisha ofisi za makao makuu, kanda, mikoa na wilaya. Mifuko yote ina ofisi katika mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Tanga, Mbeya na Iringa. Aidha, mifuko ya NSSF, LAPF, GEPF na PPF ina ofisi katika mikoa yote na baadhi ya wilaya nchini.

iv) **Kupunguza gharama za mifumo ya Tehama**

Mheshimiwa Spika, Kati ya gharama nyingi za uendeshaji wa mifuko ya hifadhi ya jamii ni pamoja na eneo

la Tehama kwa ajili ya uendeshaji wa mifuko hiyo. Kwa kuunganisha mifuko hii kutaweza kupunguza gharama za kulipia mifumo hiyo ya Tehama kwa zaidi ya asilimia 60. Ni matumaini ya Kamati kwamba, mifuko hii ikiunganishwa gharama zilizoainishwa hapo awali na nyingine nyingi zitaendelea kupungua na kuweza kuimarisha maisha ya mifuko hii.

v) Kupunguza Gharama za Ushindani

Mheshimiwa Spika, kamati ilibaini kwamba, mfumo wa sasa unaruhusu kufanya ushindani kwa ajili ya kujipatia wanachama. Ili mfuko husika uweze kumudu ushindani huo ulikuwa unalazimika kufanya matangazo kwa njia mbalimbali za habari kama vile matangazo ya Televisheni, machapisho ya vipeperushi, matangazo ya radio na hata kuandaa makongamano yaligharimu fedha nyingi za mifuko. Kwa mujibu wa kumbukumbu za msimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kila mfuko ulitumia kiasi cha **shilingi Bilioni 1.0** katika ushindani wa kujitafutia wanachama. Kamati ina maoni kwamba kwa kuunganisha mifuko hii dhana ya ushindani baina ya mifuko itapungua kama siyo kuondoka kabisa na kupunguza gharama za kujinadi ili kuvutia wanachama.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kwamba, pamoja na dhana ya ushindani kuondoka kutokana na uunganishwaji wa mifuko hii, ni muhimu Serikali ikatambua kwamba dhana ya ushindani itaendelea kuwepo katika mifuko hii miwili ya hifadhi ya jamii, kwani kuna wananchi wengine ambao hawapo katika sekta ya binafsi au sekta ya umma watapenda kujiunga na mifuko hiyo kwa mfumo wa uchangiaji wa hiari (**Supplementary Schemes**) ambapo mfumo huu unaruhusu mwananchi kuchagua mfuko apendao na kuchangia kwa hiari.

3.2 Kupunguza kwa Migogoro baina ya Mifuko

Mheshimiwa Spika, kutokana na utitiri wa mifuko ya hifadhi ya jamii ilipelekea hali ya mifuko hiyo kuingia katika

migogoro ya kugombaniana wanachama kutokana na baadhi ya wanachama kuandikishwa katika mfuko zaidi ya mmoja na kupelekea usumbufu mkubwa wakati mwanachama huyo anapostaafu na kuanza kufuatilia mafao yake. Na kwakuwa mifuko hii ilikuwa inafanya kazi kipekee (*Independent Operation*) bila kuingiliana na mfuko mwingine kimfumo wa uendeshaji, hivyo kupelekea baadhi ya wanachama kukosa stahiki zao kama mwanachama halali wa mfuko.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na changamoto hii, Mamlaka ya usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (**SSRA**) imekuwa ikilazimika kuendesha zoezi la uhakiki (*Reconciliation*) wa michango ya wanachama ambalo nalo lilikuwa linatumia gharama kubwa na kusababisha ongezeko la gharama hizo katika gharama za uendeshaji wa mifuko. Hivyo basi, ni dhahiri kuwa uunganishwaji wa mifuko hii kutaondoa changamoto ya wanachama kujiandikisha katika mifuko mingi ambayo ingeweza kuleta migogoro wakati wa utekelezaji wa utoaji wa huduma kwa ufanisi mkubwa.

3.3 Uboreshaji na uimarishaji wa huduma kwa wanachama

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, kuunganishwa kwa mifuko hii kutapelekea huduma kwa wanachama kuwa bora na imara kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo na itakayoendelea kutolewa na Mamlaka kuhusu utoaji wa huduma hizo kwa wateja wa mfuko. Sheria hii inayopendekezwa imeainisha vifungu mbalimbali vinavyolinda maslahi ya mwanachama ikiwa ni pamoja na **Kifungu cha 20** cha Muswada kinachoainisha masharti ya kuzuia mwanachama wa mfuko kuhusishwa na ucheleweshwaji wa michango yake ambalo ni jukumu la muajiri kuhakikisha michango ya mwajiriwa wake inapelekwa katika mfuko kwa wakati na badala yake muajiri achukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma kwa wanachama, **Kifungu cha 43(3)** kinampa haki kamili

mwanachama kuweza kudai kulipwa fidia na mfuko endapo mfuko huo utamcheleweshea stahiki yake ya mafao ndani ya **siku sitini (60)** na kubainika kwamba ucheleweshaji huo haujasababishwa na mwanachama bali ni mfuko husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vifungu hivyo Sheria ya Msimamizi wa mfuko ya Hifadhi ya Jamii imeboreshwa ili kuipa mamlaka uwezo wa kuchukua hatua stahiki kwa watumishi wa mfuko ambao watakiuka masharti ya Sheria na maelekezo ya mamlaka, kwa kufanya haya yote huduma kwa wateja wa mfuko hazitaathirika kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, kutokana na manufaa hayo yaliyoainishwa na Kamati yakiwemo kuwepo kwa taarifa za wanachama wa nchi nzima katika mifumo miwili tu badala ya kutawanyika katika mifumo mitano (5), kupungua kwa gharama za uendeshaji wa mfuko, kuondoa dhana ya ushindani uliokuwa unajitokeza ambao kwa wakati mwingine ulikuwa hauna tija kwa wanachama na hata nchi, Kamati imebaini kwamba, Sekta ya Hifadhi ya Jamii itaweza kudhibitiwa na kusimamiwa kwa urahisi, kuboresha uwekezaji utakaotokana na fedha za Hifadhi ya Jamii, kumaliza malalamiko ya wanachama kutokana na sababu mbalimbali na kuwapa uhakika wa maisha wafanyakazi wakati na baada ya ajira zao kukoma kwa sababu yoyote ile, hoja ya kuunganisha mfuko hii ni njema kabisa kama tu itasimamiwa ipasavyo.

4.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, mnamo **tarehe 17 na 18 Januari, 2018** Kamati ilifanya Mkutano na Wadau kwa lengo la kupokea Maoni yao (**Public Hearing**) ili kuisadia Kamati katika Uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Wadau mbalimbali walifika katika Mkutano huo Wadau hao ambao walifika mbele ya Kamati ni pamoja na National Organization for Legal Aids, Legal and Human Rights Centre (LHRC), Chama cha

Wanasheria Tanzania (Tanganyika Law Society (TLS), Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Chama cha Waajiri Tanzania, Chama cha Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Chama cha Wahariri wa Vyuo Vikuu Tanzania (THTU), Shirika la Kazi Duniani (ILO), Aidha Wadau wengine walitoa maoni yao kwa maandishi wakiwemo Chama cha Wanasheria wanawake (TAWLA) na Chama cha wafanyakazi wa mahakama walitoa maoni yao kwa njia ya maandishi ambayo yamesaidia Kamati kuboresha Muswada huu na kuiwezesha Kamati kutoa maoni na ushauri unaotolewa leo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja nzito zilizoibuliwa na Kamati wakati wa majadiliano, Serikali iliomba Kamati siku ya **tarehe 19 Januari, 2018** ambayo ilikuwa ni siku ya kufanya mashauriano na Serikali kupata ushauri elekeze (*Consultation*) ili kuwa na dhana ya uwajibikaji Serikalini (*Collective Responsibility*) na Kamati ikaona ni busara kuwapa nafasi hiyo ili kupata majibu sahihi na yenye kujenga kutoka kwao kwa muktadha mzima wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kibali chako, uliiruhusu Kamati kuendelea na kazi kwa siku ya Jumamosi **tarehe 20 Januari, 2018** ili kufanya mashauriano na Serikali kwa lengo la kuzingatia maoni ya Kamati na Maoni ya wadau mbalimbali yaliyotolewa kwa ajili ya maboresho na ambayo Kamati iliona ni mazuri kwa ajili ya uboreshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, katika mashauriano ya hoja mbalimbali zikiwemo zile zilizohitaji ushauri elekezi Serikali ilikubaliana na Kamati kwamba marekebisho yote yatawasilishwa na Serikali kwenye Jedwali la marekebisho (*Schedule of Amendments*) kama Kamati ilivyokuwa imependekeza.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza wajibu wake na ninaipongeza Serikali kwa kuwa wasikivu na kupokea Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na

kuyapokea kwa ajili ya kuyafanyia kazi. Ni imani yangu na Kamati nzima kwamba, tumeisaidia Serikali na wananchi wa Tanzania katika kuiboresha Sheria hii ambayo ipo katika mchakato wa kutungwa kwa ajili ya manufaa ya wafanyakazi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Jenister Mhagama Waziri, kwa namna ambavyo amekuwa akitoa ushirikiano wa dhati kwangu mimi pamoja na Kamati nzima, kwa jinsi alivyokuwa msikikivu, muelewa na hata pale tulipohitaji ufafanuzi wa Serikali Mheshimiwa Waziri alitoa bila kusita wakati wa kuuchambua na kuujadili muswada huu. Kwakweli Mheshimiwa Jenister ni mfano wa kuigwa, hongera na asante sana.

5.0 MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo kwa lengo la kuboresha Muswada huu:-

5.1 MAONI KUHUSU VIFUNGU

a) Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini makosa ya uchapaji na sarufi (*spelling and grammatical errors*) na inashauri Marekebicho yafanyike kwenye maeneo yote yenye makosa hayo ili kuweka maana stahiki katika vifungu hivyo vilivyoonekana kuwa na makosa ya kiuchapishaji.

b) Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza Kifungu cha 3 kuhusu *Interpretation* kufuta neno "*leader*" katika maana ya neno "*qualifying period*" na badala yake kuweka neno "*member*". Aidha, katika kifungu hicho hicho Kamati inashauri kufuta marejeo namba 87 katika maana ya neno "*transition period*" na badala yake kitumike kifungu namba 86 ili kuondoa makosa ya kiuchapaji.

c) Katika Kifungu cha 3 cha tafsiri ya maneno mbalimbali "*Interpretation*" iongezwe neno "*Parliamentary service*" katika maana ya "*public services*" ili kutambua Utumishi wa Bunge kuwa ni mtumishi wa Umma na ni mwanachama wa mfuko huu unaopendekezwa kuanzishwa. Aidha, kuongezwe tafsiri ya maneno kama vile "*Special Lumpsum*", "*Pension*", "*unemployment benefit*", "*funeral benefit*" na "*sickness benefit*" ambayo yametumika na hayajapatiwa tafsiri yake katika orodha ya maeneo yaliyotafsiriwa katika Muswada huu. Aidha, kamati inashauri maneno haya yapatiwe tafsiri pia zijumuishwe katika Kanuni ambazo zitatungwa na Waziri mwenye dhamana kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hii.

Kamati inapendekeza pia neno "*Month*" tafsiri iliyopewa iboreshwe kwakuwa siyo miezi yote ina siku thelathini (30) kama ilivyotafsiriwa, kuna mwezi ambao siku ni ishirini na nane (28), ishirini na tisa (29) na mingine mpaka siku thelathini na moja (31). Kamati inapendekeza isomeke "*Calendar Month or a written calendar*" badala ya "*a period of thirty days consecutively*" kama ilivyotafsiriwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu hicho hicho cha 3 katika tafsiri ya neno "*qualifying pensionable service*" kuna neno "*continuous*" katika vipengele vyote yaan "*a*" na "*b*", kwakuwa mwanachama anaweza akawa hajafanya kazi kwa kipindi fulani kutokana na sababu mbalimbali na baadae akarejea kazini katika sekta ya umma au katika sekta binafsi, ambapo atakapofikia umri wa kustaafu akawa anastahili kulipwa mafao yake kwa kujumlisha muda aliotumikia na kuchangia katika mfuko wa hifadhi ya jamii. Aidha, katika tafsiri ya neno "*Totalization*" neno "*fully contributed*" lifafanuliwe ili lisiweze kuleta mkanganyiko na liweze kueleweka sawasawa.

Mheshimiwa Spika, Katika tafsiri ya neno "*Salary*" Kamati inashauri neno hilo litafsiriwe vyema na ikiwezekana tafsiri inayotumika na Msimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii (SSRA) itumike. Kamati inashauri malupulupu mengine kama

vile posho zisijumuishwe katika tafsiri hiyo kwani posho hizo hubadilika mara kwa mara kadiri inavyoonekana inafaa. Aidha, Kamati inashauri pia maneno "*Employers Association*" na "*Employees Association*" yaongezwe katika orodha ya tafsiri ya meneno mbalimbali ili kutambua na kuweka bayana maana ya vyama hivyo vya waajiri na waajiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika orodha ya tafsiri ya maneno kuna neno la "*full pension*" kwa kuwa tafsiri hiyo haijakamilika kama ambavyo imetafsiriwa na Sheria ya SSRA. Kamati inashauri tafsiri hiyo izingatie tafsiri itakayorejewa katika kanuni za ukotozi zitakazotengenezwa kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hii. Aidha, neno "*Actuarial valuation*" limepewa tafsiri yake katika orodha ya maneno na limetumika katika **kifungu cha 91(a)(i)** kwa maana tofauti na tafsiri iliyopo katika orodha ya maneno. Kamati inashauri tafsiri hiyo iangaliwe upya ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza katika matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, katika tafsiri ya neno "*qualifying period*" Kamati inapendekeza neno "*leader*" lifutwe na badala yake litumike neno "*member*" ili kufanya marekebisho ya kiuandishi na kuleta tafsiri sahihi kwa kuwa wachangiaji wa mfuko huo wa hifadhi ya jamii wote wanatambulika kama wanachama (*members*) na siyo kiongozi.

Aidha, katika tafsiri ya neno "*transition period*" kumefanyika marejeo ya **kifungu cha 87** kinachozungumzia "*provision regarding employees Cap.298*", Kamati inashauri ibadilishwe na badala yake marejeo yafanyike katika **kifungu cha 86** ambacho kinazungumzia "*Transition Period*".

d) **Kifungu cha 6** kinachohusu "*Establishment of the Fund*" katika **Kifungu kidogo 6(1)(c)** Kamati inashauri kifutwe na kiandikwe upya ili kuondoa mkanganyiko uliopo katika kifungu hicho tajwa na **kifungu cha 80(2)** na **105** vya muswada huu.

e) **Kifungu cha 15** kinachohusu "*Appointment of the Director General*" wa mfuko huu, Kamati inashauri kifutwe

na kuandikwa upya ili masharti yake yaweze kumuondoa Mkurugenzi huyo kabla ya kipindi chake cha miaka mitano (5) kuisha kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Sheria iainishe vipindi vya Mkurugenzi Mkuu kushika wadhfa huo yaana kwa vipindi viwili tu (*two terms*) kulingana na utendaji bora wa kazi yake pamoja na masharti mengine kuzingatiwa.

f) **Kifungu cha 16(2) kinachohusu "Other staff of the Fund"** Kamati inashauri maneno yanayosomeka "*under subsection (2)*" yafutwe kwani hayana msingi wowote kuwepo katika kifungu hicho kwakuwa kinachoainishwa kipo katika kifungu hicho hicho kidogo.

g) **Kifungu cha 18 kinachohusu "Contributions"** Kamati inapendekeza kufuta maneno yanayosomeka "*such amount as the Minister may, by order in the Gazette, determine*" kwakuwa Waziri mwenye dhamana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma amepewa Mamlaka makubwa ambayo yanaweza kutumika vibaya dhidi ya michango ya wanachama na hasa maamuzi ambayo yanaweza kuwa kandamizi kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, katika **Kifungu cha 18(8)** Kamati inapendekeza kuondoa neno "*May*" na kuweka neno "*Shall*" ili kuweka masharti kuwa endapo Bodi itajiridhisha kwamba michango ya mwanachama ilikatwa na mwajiri hakupeleka katika mfuko basi Bodi ilazimike kuingiza michango hiyo katika mfuko wa mwanachama na gharama hizo ziwe juu ya mwajiri pamoja na adhabu kwa mujibu wa sheria hii.

h) **Kifungu cha 19 kinachohusu "Additional contributions for delayed remittance of contributions by employer"** kifungu 19(1) kina mkanganyiko na kifungu 18(3) katika kuainisha nani ni mwajiri, Kamati inashauri kifanyiwe kazi ili kuondoa mkanganyiko huo. Aidha, katika kifungu hicho rejea ifanyiwe katika **Kifungu cha 18(6)** badala ya **kifungu cha 21(2)** kama ilivyo katika muswada ili kuondoa makosa ya kiuchapaji. Aidha, kiongezwe **kifungu cha 19(3)** kinachoweka sharti la Mkurugenzi wa mfuko kulazimika kutoa taarifa kwa

mwanachama kila ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha wa Serikali yaani mwezi Juni.

i) **Mheshimiwa Spika**, Katika kifungu cha 19 kinachohusu *“Additional contributions for delayed remittance of contributions by employer”* Kamati inapendekeza kiongezwe kifungu cha 19(3) na kisomeke kama ifuatavyo, *“The Director General shall make available to each member a statement of his contributions at the end of each financial year”*. Kamati iina maoni kuwa ni vyema kuweka sharti hili ili kuhakikisha linakuwa ni jukumu la Mkurugenzi wa mfuko kuwapa wanachama taarifa za michango yao kila mwisho wa mwaka badala ya kusubiri maombi kutoka kwa mwanachama kama ambavyo inapendekezwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuweka sharti hili kutasaidia kuwapa taarifa wanachama wa mfuko kila mwaka na kupunguza usumbufu na malalamiko yanayotokana na mwajiri kutopeleka michango ya mwanachama kwa wakati na kupelekea mtumishi anapostaafu kuanza kusumbuka kupata haki yake ya msingi ya uzeeni aliyoitumikia kwa miaka mingi katika utumishi wake.

j) **Kifungu cha 29 (1)** kinachohusu *“Benefits payable”* Kamati inashauri iongeze aina mbili ya mafao kutoka nane (8) yanayotolewa na mfuko hadi kufikia kumi (10) baada ya kuongeza fao la elimu (*education benefit*) na fao la mkono wa kwaheri (*gratuity benefit*).

k) **Kifungu cha 33 kinachohusu “Invalidity benefit”** kamati inashauri Serikali ifafanue vizuri ili kiweze kueleweka katika sheria hii na pia masharti ya kustahili kulipwa yaondolewe, kwani kilivyoandikwa sasa kinaleta mkanganyiko wa mtumishi ambaye amepata ulemavu kazini na hakutarajia kupata ulemavu huo chini ya muda ambao anastahili kulipwa fao hilo.

l) **Kifungu cha 37 kinachohusu “Survivors benefits” kifungu 37(1) (a) na (b)** katika vifungu hivyo

ametajwa mjane *“widow”* kama mnufaikaji wa mafao endapo mume wake aliyekuwa mwanachama atafariki basi ataendelea kunufaika na uchangiaji wa mume wake na kipengele hicho hakijamtambua mgane (*widower*) aliyefiwa na mke wake ambaye alikuwa mwanachama wa mfuko kuendelea kunufaika. Kamati inashauri liongezwe neno *“widower”* ili mgane aweze kutambulika na sheria hii kama mmoja wa wanufaika endapo mkewe atafariki.

m) **Kifungu cha 38 kinachohusu *“Basis and duration of survivors pension”*** Kamati inashauri kifanyiwe marekebisho ya utambuzi wa umri wa mtoto na kuongeza kutoka miaka 15 hadi miaka 18 ambayo inatambulika na sheria ya mtoto. Aidha, wanufaika wote kwa maana ya mgane, mjane au mtoto walipwe mafao kwa kutumia kanuni kama ilivyo kwa mwanachama wa mfuko kwa kuwa angekuwa hai angenufaika kwa kutumia kanuni husika ya mfuko ambayo itawekwa kwenye Kanuni za sheria hii.

n) **Kifungu cha 40 kinachohusu *“Pensions, gratuity and allowances for persons holding certain public office”*** Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza viongozi waliotajwa katika kifungu hiki aongezwe Katibu wa Bunge (*Clerk of National Assembly*) kwenye orodha ya viongozi wanaopata mafao maalum kwa kuwa nafasi hiyo ni nafasi ya kikatiba kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 **Ibara ya 87 (1)** ambapo imetamka uwepo wa Katibu wa Bunge. Aidha, Katika kifungu hiki kuongezwe neno *“ and Security”* kati ya neno *“ Intelligence”* na neno *service* ili kuweza kurekebisha jina la Mkurugenzi wa Idara ya Intelijensia kuweza kuleta maana sahihi ya Cheo hicho katika sheria hii.

o) **Kifungu cha 47 (2)(c) kinachohusu *“Prohibition on cession and attachment of benefits”***, Kamati inashauri kiangaliwe upya ili kuondoa ubaguzi wa jinsi kwani kimemtaja mke na kuacha mume. Aidha marekebisho yafanyike ili kumtambua mnufaikaji pasipo kuainisha jinsi ya mnufaika.

p) **Kifungu cha 56 kinachohusu “Exemption from Tax”** Kifungu hiki kimeelezea ukatwaji wa kodi lakini kamati ina maoni kuwa kifungu hiki hakijawekwa sawa kwakuwa hakifafanui kuwa nani atapaswa kukatwa kodi hiyo ni mfuko au michango ya mwezi au mafao ya mkupuo anayolipwa mwanachama. Aidha, Serikali ikakiandike upya kifungu hiki ili kiweze kuainisha kwamba atakayekatwa kodi ni mfuko kutokana na uwekezaji wake kwa kutumia fedha za wanachama na kodi hiyo isikatwe kwa mwanachama wa mfuko.

q) **Kifungu cha 57(4) kati ya vifungu vinavyohusu “Actuarial Valuation Report”** Kamati inashauri neno “**may**” lifutwe na kuweka neno “**shall**” ili kuweza kuwa na sharti la lazima kwa mamlaka ya usimamizi wa mifuko kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika kwenye taarifa ya mtaalamu wa uthamini wa hali halisi ya mifuko (**Actuarial Valuation**) ya hifadhi ya jamii. Kwa kubaki hivyo, mamlaka inapewa mwanya wa kuamua kuchukua hatua au isichukue hatua.

5.2 MAONI YA JUMLA

i) **Umuhimu wa SSRA kuongezewa majukumu ya Usimamizi ya Hifadhi ya Jamii**

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya **Mwaka 2003** ilipelekea Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutunga Sheria Na.8 ya Mwaka 2008 pamoja na mambo mengine ilitoa masharti ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (**Social Security Regulatory Authority**). Pamoja na majukumu mengine Mamlaka hii ya Usimamizi ilipewa jukumu la kusimamia Mifuko yote ya hifadhi ya jamii kwa kutoa miongozo ya utendaji sahihi, kusimamia utendaji wa mifuko, kutetea na kulinda maslahi mbalimbali ya wanachama, kutoa ushauri wa kiseru kwa waziri mwenye dhamana, kusajili wasimamizi wa uwekezaji wa fedha za mifuko ya jamii na majukumu mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa, bado kuna majukumu mengi na makubwa kwa Mamlaka hii ya Usimamizi wa Sekta ya hifadhi ya jamii kwa kuwa majukumu hayo bado yapo ikizingatiwa kwamba mifuko hii inakwenda kuunganishwa hivyo Mamlaka inapaswa kuhakikisha kumbukumbu za wanachama wa mifuko yote zinabaki kuwa sahihi na huduma zinaendelea kutolewa kwa wanachama wanaostahili katika mifuko hiyo. Kuunganishwa kwa mifuko hii kusiwe sababu au kigezo cha huduma kusimama. Hivyo Uangalizi wa SSRA ni muhimu sana kwa wakati huu kuliko wakati mwingine wowote. Aidha, katika kuanza kutekeleza Sheria hii, Serikali inahitaji kufanya tathmini ya hali halisi ya mifuko (*Actuarial Valuation*) yote ili iweze kuandaa kikokotoo (*Formular*) ambapo kazi hii inahitaji kusaidiwa na mamlaka husika ambayo ni SSRA.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza pia masuala yote yanayohusiana na Hifadhi ya Jamii, iwekwe chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Mifuko ya Bima ya Afya ikiwemo Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF), Bima ya Afya ya Jamii (CHF) na mifuko mingine yenye dhana ya hifadhi ya jamii iwekwe chini ya msimamizi mmoja. Kwa kufanya hivyo kutaondoa mkanganyiko na unufaikaji wa mafao zaidi ya mara moja ikiwemo fao la matibabu na fao la ugonjwa yanayotolewa na Mfuko wa Hifadhi ya jamii na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

ii) Watumishi wanaotoka katika mifuko hiyo kuwahahakikishia ajira zao

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa kuunganishwa kwa mifuko hii kutapelekea suala la ajira za wafanyakazi katika mifuko hiyo kuathirika na wengine kupoteza nafasi zao za awali na hata kupoteza ajira zao kabisa. Kamati inashauri, Wizara yenye dhamana ikishirikiana na mifuko husika pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Jamii kuhakikisha wanalinda ajira za wafanyakazi hao bila kujali nafasi zao za awali. Wizara ifanye tathmini ya idadi ya wafanyakazi wenye sifa wanaohitajika kwa ajili ya

kuhakikisha wanabaki katika ajira na kuhakikisha uanzishwaji wa Mifuko hii unakuwa wa ufanisi mkubwa bila kuleta taharuki yoyote kwa wafanyakazi na wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, ni imani ya Kamati kuwa, kuanzia sasa ofisi za mifuko hii zitakuwa hadi ngazi ya wilaya ambako wanachama wengi wapo wakiwemo walimu, wauguzi, askari na kada nyingine mbalimbali hasa kutoka katika Sekta ya Umma. Hivyo basi Kamati inasisitiza watumishi wote waliokuwa katika mifuko hiyo ajira zao zilindwe kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za utumishi wa umma.

iii) Wanachama katika mifuko hiyo wasihame na michango yao ili kuiwezesha mifuko hiyo kujiendesha

Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha mifuko hii inakuwa na muda mrefu wa uhai wake, ni maoni ya Kamati kwamba, katika uunganishaji na usajili wa wanachama wa mifuko ianze na wafanyakazi wapya katika Sekta zote mbili kwa maana kwamba, mara baada ya Sheria hii kusainiwa na Mheshimiwa Rais, basi wafanyakazi watakoajiriwa katika sekta zote mbili waanze kutenganishwa usajili wao ili mfanyakazi wa Sekta ya umma asajiliwe katika mfuko wa umma na mfanyakazi wa Sekta binafsi asajiliwe katika mfuko wa Sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwa wakati huu, wanachama waliopo katika mifuko hiyo minne inayounganishwa wote wabaki katika mfuko wa umma na wale waliopo katika mfuko wa NSSF waendeleo kuchangia huko bila kujali ni mfanyakazi wa Sekta gani, utaratibu huu unafahamika kama **Cutt off date** ya mwanachama.

Mheshimiwa Spika, Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kuboresha uwiano wa wanachama wastaafu kutoka **uwiano wa 1:5** hadi kufikia **uwiano wa 1:10**, kutapunguza idadi ya wanachama kuanza kufuatilia taarifa zao wakati wa kupata stahiki za mafao yakiwemo mafao ya uzazi na kustaafu. **Aidha, sababu kubwa zaidi ni kwamba michango ya wanachama hao imewekezwa katika miradi mbalimbali**

iliyogharamiwa na michango yao ambapo kuwahamisha na uwekezaji huo itaitelea usumbufu Serikali na wanachama wake pia na kwa mfumo ulivyo makusanyo ya michango ya watumishi sasa (*Current Collections*) ndiyo inambeba kwa kumlipa mtumishi aliyestaafu.

iv) **Serikali ifafanue Fao la upotevu wa ajira (*Unemployment Benefit*)**

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa Muswada huu, Kamati ilibaini kwamba katika orodha ya mafao kuna fao la upotevu wa ajira (*Unemployment Benefit*) kwa mwanachama ambaye amechangia michango kwa kipindi kisichopungua miezi 18, hajaacha kazi kwa hiari pamoja na masharti mengine, atalipwa **asilimia 33.3** ya mshahara wake kwa kipindi cha miezi sita (6), ambalo kimsingi Kamati inakubaliana nalo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri fao hilo lifafanuliwe vizuri ili umma uweze kuelewa kwani kumekuwa na upotoshwaji mkubwa katika jamii kuwa sasa watanzania wote waliokosa ajira watalipwa fao la ukosefu wa ajira. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kubadili jina la fao hilo kuitwa **FAO LA UKOSEFU WA AJIRA** na badala yake liitwe **FAO LA UPOTEVU WA AJIRA** kwa maana kwamba mtu alikuwa mwajiriwa na mwanachama wa mfuko, ila kutokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wake amepoteza ajira yake. Kwa kufanya hivyo Serikali itakuwa imefuta dhana potofu iliyoko kwa wananchi ya kwamba waliokosa ajira wote kwa Sheria hii wanaingizwa katika orodha ya wanufaika wa mafao kupitia fao la ukosefu wa ajira.

v) **Mifuko kufuatilia michango ya wanachama kwa Waajiri**

Mheshimiwa Spika, Mara baada ya mwajiriwa kupeleka taarifa zake kwa mwajiri na kuanza kulipwa mshahara wake huanza kukatwa michango yake kwa ajili ya kupeleka katika mfuko wa hifadhi ya jamii ambalo ni

jukumu la muajiri kuhakikisha michango hiyo inapelekwa katika Mfuko husika kwa wakati. Aidha, imezoeleka kwamba muajiri ndiye anapaswa kupeleka michango hiyo na endapo haijapelekwa kwa wakati mfuko haufanyi juhudi yoyote ile ya kufuatilia michango ya mwanachama wake. Hali hii inapelekea kutengeneza mazingira ya usumbufu kwa mwajiriwa wakati wa kufuatilia stahiki yake na hasa mara baada ya kustaafu na kuonekana kuna baadhi ya miezi makato hayo hayakupelekwa na mwajiri.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri mifuko iweke utaratibu wa kufuatilia michango hiyo kwa waajiri ili kifungu cha kulipa faini kilichopo katika sheria hii kiweze kutumika vizuri na ikawa sehemu ya mapato kwa mfuko.

vi) Wafanyakazi wa Kampuni zenye hisa za Serikali kuchangia katika Mfuko wa Umma

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu imekuwa na kampuni za aina mbalimbali zile za binafsi na kampuni ambako serikali imeingia ubia na muwekezaji. Kamati inashauri Kampuni zote ambako Serikali ina hisa zake bila kuja kiasi cha umiliki wa hisa hizo, ikiwemo TBL, TCC, Airtel na Kampuni nyingine, wafanyakazi wake wote wawe wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma. Kwa kufanya hivyo, kutaweza kuimarisha mfuko huu lakini pia kuweza kulinda maslahi ya wananchi wetu ambao ni waajiriwa katika kampuni hizo kwa kuhakikisha kwamba ni kwa kiasi gani wafanyakazi wakitanzania wananufaika na Kampuni hizo na kuwekewa hazina yao ya kijamii.

vii) Serikali kulipa madeni ya Mifuko

Mheshimiwa Spika, mifuko inayounganishwa kwa sheria hii imekuwa ikiidai serikali madeni makubwa ya kuanzia Mwaka 2000 na kurudi nyuma (*Pre 1999*) ilipoamua kuwalipa wastaafu mafao licha ya Serikali kutopeleka mafao ya watumishi hao katika mifuko wanakonufaika nayo. Hali hii imepelekea mifuko hiyo kuendesha kwa hasara kubwa na

madeni makubwa na wakati mwingine kuwasababisha wanachama hasa wastaafu kuwekwa kwenye foleni ya kusubiri pensheni zao kwa foleni. Aidha, Serikali imekuwa ikchukua fedha za mifuko kwa njia ya kukopa na kufanya miradi mbalimbali ya maendeleo kwa nchi, mikopo hiyo nayo imegeuka kuwa changamoto mojawapo inayoikabili Mifuko iayounganishwa kwa Sheria hii.

viii) Kukamilisha utoaji wa fao la elimu

Mheshimiwa Spika, Katika Mifuko hii inayounganishwa kwa Sheria hii, kuna mifuko iliyokuwa inatoa fao la elimu kwa wanachama na hata wategemezi wa wanachama wa mifuko hiyo. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 29(1) cha orodha ya mafao yanayoainishwa na mfuko huu fao la elimu limeachwa na kwamba halitatolewa tena kwa wanachama wa mfuko huu. Kamati inaunga mkono hoja ya kuondolewa kwa fao la elimu katika orodha ya mafao kwani sasa Serikali inaihudumia jamii nzima ya Tanzania kwa kutoa elimu bila malipo kwa elimu ya msingi yaani kuanzia Shule ya Msingi hadi Kidato cha nne kuanzia mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri, Serikali, kama haitaongeza fao la elimu, basi Serikali iruhusu mifuko hii kuendelea kutoa fao hilo la elimu kwa wale wanachama walioko tayari katika mfumo wa kupewa fao hilo ili waweze kumaliza masomo yao badala ya kuwakatika na kuweza kukatisha ndoto zao. Ikumbukwe kwamba kuna watoto ambao wamepoteza wazazi wao na kutokana na fao hili kuwepo wameweza kuendelea na masomo katika shule walizokuwepo wakati wa uhai wa wazazi au walezi wao.

ix) Sheria iwatambue Katibu wa Bunge na Makati Wakuu wa Wizara

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imemtambua Katibu wa Bunge katika **Ibara ya 87 (1)** kwamba kutakuwa na Katibu wa Bunge ambaye atakatoka miongoni mwa watumishi wenye madaraka ya

juu Serikalini. Aidha, katika utendaji wa Wizara Mtendaji Mkuu ni Katibu Mkuu (**Accounting Officer**) wa Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii inayopendekezwa kwa ajili ya Mfuko wa Jamii kwa Watumishi wa Umma imelenga kuwapa huduma watumishi wote waliopo katika Sekta ya Umma wakiwemo Makatibu Wakuu wa Wizara ambao wanateuliwa miongoni mwa watumishi wa umma waliohudumu kwa muda mrefu na kukatwa michango yao wakiwa watumishi katika ngazi za chini kabla ya ukatibu mkuu. Aidha, Makatibu Wakuu ndiyo maafisa masurufu na ni wasimamizi wa watumishi wengi walio chini yao (**Subordinates**) ambao wamejumuishwa katika Mfuko wa Hifadhi ya jamii lakini wasimamizi wao hawajapewa fursa hii muhimu sana kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, **Kamati inashauri sheria hii iwajumuishe Makatibu Wakuu wote wa Wizara ili waweze kunufaika na Mfuko huu wa Hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma. Kwa kufanya hivyo kutaondoa dhana ya matumizi mabaya ya madaraka yao kwa manufaa binafsi na katalinda hadhi ya maisha na utu wao mara baada ya ajira zao kukoma.**

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada huu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Jenister Joachim Mhagama (Mb), Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu Mhe. Anthony Mavunde (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Ikupa Stella Alex, (Mb), Ndg. Katibu Mkuu, Ndg. Erick Shitindi na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati na kuwasilisha vyema Muswada huu mbele ya Kamati

pamoja na kutoa ufafanuzi wa kina kila ulipohitajika. Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watendaji wake kwa kazi nzuri waliyofanya ya kutoa kutoa mwongozo mahiri wa kisheria wakati wote wa uchambuzi wa Muswada.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru tena Wadau wote waliofika mbele ya Kamati kuwasilisha Maoni yao. Aidha, nawashukuru hata Wadau ambao walishindwa kufika mbele ya Kamati kutokana na sababu mbalimbali lakini waliweza kutuma maoni yao kwa Maandishi. Napenda kuwaeleza kuwa Michango yao imesaidia kupata sheria hii muhimu kwa Maslahi mapana ya Watumishi wa Umma na hata Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri yenye umahiri wakati wote wa uchambuzi wa Muswada huu. Wajumbe wamefanya kazi nzuri ya kuhakikisha uchambuzi wa Muswada huu unakuwa wenye tija kwa maslahi ya Taifa zima. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Peter J. Serukamba, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Mussa A. Zungu, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Peter Ambrose Lijualikali	Mjumbe
5. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Kasuku Samson Bilago, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Lucia Ursula Michael Mlowe, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb	Mjumbe
12. Selemani Said Bungara, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Zitto Zuberi Kabwe, Mb	Mjumbe

14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Bernadetha K. Mushashu, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Grace Victor Tendega	Mjumbe
18. Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo	Mjumbe
19. Mhe. Hussein Nassor Amar	Mjumbe
20. Mhe. Juma A. Juma	Mjumbe
21. Mhe. Sonia Juma Magogo	Mjumbe
22. Mhe. Nuru Awadh Bafadhili	Mjumbe
23. Mhe. Rehema Juma Migira	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda sana kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega pamoja na Katibu wa Kamati hii Ndg. Agnes Nkwera na Msaidizi wa Kamati Ndg. Wazir Kizingiti kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. Aidha, namshukuru Kaimu Mshauri Mkuu wa Mambo ya Sheria wa Bunge Ndg. Pius T. Mboya pamoja na wasaidizi wake Ndg. Leorcard Kapongwa, Ndg. Maria Mdulugu na Ndg. Nesta Kawamala kwa Uchambuzi wa kisheria walioufanya kuisadia Kamati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Peter Joseph Serukamba, Mb

MWENYEKITI

Januari, 2018

MWENYEKITI: Tunaendelea, tupokee sasa maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu, karibu Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU(SERA, BUNGE, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasoma naomba niweke rekodi sawa kwamba wazo la kuunganishwa kwa Mifuko lilitoka Kambi Rasmi ya Upinzani na lilikuwa ni hoja ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kwa mwaka huu wa 2018 kusimama hapa kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa sheria uliopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutulinda sote na kutuvusha salama katika mwaka uliopita wa 2017 na kutujalia kuuona mwaka huu mpya wa 2018 tukiwa salama. Kwa sababu hiyo, nakutakia wewe na Waheshimiwa Wabunge wote, kheri ya mwaka mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zaburi ya 1:1 na 3 inasema kwamba, heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki; na kila alitendalo litafanikiwa. Mzaburi anaendelea kusema katika mstari wa nne (4) kwamba, sivyo walivyo wasio haki, hao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na nukuu hiyo ya Biblia Takatifu ili itutie nguvu sisi tulioonewa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa hebu keti kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, jana nilisema na leo nalazimika kusema tena, hizi taarifa pamoja na kwamba tunatoa maoni yetu lakini ni taarifa ambazo lazima zizingatie Kanuni kwa kutumia lugha za kibunge. Nilisema jana na nimekusihi Mheshimiwa Ester, nimekuandikia ki-*note* kwamba *stick* kwa hayo ambayo yamo kwenye hotuba hii. *Paragraph* hizo ambazo zimeondolewa sasa naamrisha usizisome. Baada ya hiyo uliyosoma kwenye Zaburi ufuate sasa unasema Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo, endelea kuanzia hapo. Karibu.

(Hapa baadhi wa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

MHE. ESTER A. BULAYA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU(SERA, BUNGE, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti na Mtemi wangu ninayekuheshimu sana, kwa sababu hutaki hata Maandiko ya Biblia niliyoya-*quote* niyasome na huyaamini nitaamua kuyaondoa ila mimi ninayaamini ndio maana nimeyaandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo na *quote* hizo za Biblia ulizozikataa za utangulizi, sasa naomba nitoe maoni ya jumla kuhusu Muswada wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Jamii ni haki ya kila Mtanzania. Haki hii imeanishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 11(1) na Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003. Haki hii pia imeainishwa kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu wa mwaka 1948 pamoja na Mikataba ya Shirika la Kazi Duniani (ILO), Ibara ya 102 ya mwaka 1952.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya jamii ni haki ya kila mtu na si kwa wale tu walio katika sekta iliyo rasmi, kwa sababu mpaka sasa kulingana na takwimu za Sensa ya Watu na Makazi zilizotolewa mwaka 2012 ni kwamba idadi ya Watanzania wote ni milioni 44.9 ambao kati yao, ni watu milioni 1.7 tu ndio waliojiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii, hii ikiwa ni asilimia 6.5 tu ya nguvukazi yote ya watu milioni 23.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizo, Tanzania haiwezi kujitokeza kifua mbele na kujidai kwamba jamii yake imehifadhika. Sababu kubwa asilimia ndogo ya watu waliojiunga na skimu za hifadhi za jamii ni ufinyu wa ajira kwa sekta za umma na sekta binafsi. Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba badala ya Serikali kung'ang'ania kuweka sheria za kupunguza na kuibana mifuko ya jamii, ingepanua fursa za ajira kwa Watanzania na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuajiri kwa wingi ili kupunguza umasikini wa kipato kwa Watanzania, lakini pili, kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanaweka akiba itakayowasaidia pindi umri wao wa kufanya kazi utakapokoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, jambo la msingi ambalo Kambi ya Upinzani inaamini ni kwamba akiba ni kitu kinachomsaidia mtu wakati wa shida au wa matatizo na siyo kitu cha kufanikisha mazishi ya mtu huyo baada ya kufariki kutokana na kushindwa kutatuliwa kwa matatizo au shida iliyokuwa ikimkabili. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali, pamoja na Wabunge wote kwa ujumla, kuhakikisha kwamba mifuko ya jamii chini ya sheria hii inaweka mazingira ya wanachama kuweza kunufaika na michango yake wakati wowote anapopata shida kubwa kabla ya kustaafu na siyo kuweka masharti magumu ya kumfanya mwanachama ashindwe kunufaika na michango yake mpaka wakati wa kustaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ikiwa hatutaweka utaratibu wa kumfanya mwanachama

kunufaika na michango yake wakati anapopata shida akiwa hai, yamkini tunaweza kuwa tunatengeneza mazingira ya kuwachangisha wanachama fedha za kuja kugharamia mazishi yao na siyo kuwasaidia kuboresha maisha yao. Hii ni bayana kwa kuwa umri wa kuishi kwa Mtanzania sasa hivi unakadiriwa kuwa ni miaka 61 na takribani umri huo huo mtumishi anapaswa kustaafu na kulipwa mafao yake. Kwa *logic* ndogo, mafao hayo ni ya kumzikia na siyo ya kumtegemeza kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mamlaka ya Udhubiti na Uhifadhi wa Jamii (*SSRA*) inasema kwamba hadi Juni, 2015, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini ilikuwa na jumla ya wanachama 2,132,000 kufikia Juni, 2016 wanachama waliongezeka kufikia 2,464,000. hii ni kutokana na ushindani uliopo baina ya mifuko. Watu hao ni wale waliopo katika ajira ya sekta iliyo rasmi tu na nguvu kazi kubwa iliyobaki ya takribani 20,000,000 inashughulika na sekta isiyo rasmi na wote wako katika hali hatarishi kwa vile hawana kinga yoyote ya hifadhi ya jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa *PPF* hadi Juni, 2015 ilikuwa na jumla ya watumishi 352, *PSPF* ilikuwa na watumishi 186, *LAPF* ilikuwa na watumishi 195 na mifuko hiyo yote ina matawi zaidi ya kumi nchi nzima. Hapa ni dhahiri kwamba kutokana na kile kinachoitwa *downsizing* ili kazi zifanyike kulingana na nafasi zitakazotengenezwa na mfuko mpya wa taasisi inayoanzishwa kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hilo, kuna ushindani kwa mifuko kutoa mafao yanayofanana. Mfano, fao la Bima ya Afya linalotolewa na Mfuko wa Bima ya Afya na fao la kuumia ukiwa kazini linalotolewa na Mfuko Maalum wa Fidia ya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia mafao yatakayotolewa chini ya sheria hii, ni dhahiri kwamba ushindani wa mafao baina ya mifuko utaendelea kuondoa baadhi ya mafao na kuyaacha kwenye mifuko ambayo

haijafutwa kwa mujibu wa sheria hii. Maana yake ni kumzidishia mzigo wa makato mtumishi wa umma ambaye mshahara wake ni mdogo, kwani inamlazimu kuchangia mifuko miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Hifadhi ya Jamii kwenye Kamati iliyochoambua Muswada huu, alisema kuwa pamoja na mambo mengine, ni kuboresha mafao ya wanachama. Hili ni jambo jema kama litaonekana katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafao ya wanachama yanaboreshwa kwa kuwa na kikokotoo (*formula*) kinachojulikana na kukubalika baina ya wahusika wote kwa maana ya wanachama. Tukumbuke kuwa fedha hizo siyo mali ya Serikali, bali ni mali ya wanachama na Serikali kupitia kwenye sheria hii ni mtunzaji na mwendelezaji wa fedha hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada umetoa kitu kinachoitwa *full pension* na ikatolewa tafsiri yake, kwa bahati mbaya sana hiyo ndiyo ilikuwa ni kikokotoo au kanuni au *formula*, lakini wadau waliipinga, kwani badala ya kuboresha mafao ilikuwa inayakandamiza. Kabla ya kuunganisha mifuko hii, mifuko mingi ilikuwa na vikokotoo kama vile *PSPF* 540 na 580 kwa waajiriwa walioanza kazi baada ya 2014; *LAPF* 540, *PPF* na *GEPF* 580.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile moja ya sababu kuu ya kuunganisha mifuko hii ni kuboresha mafao ya wafanyakazi, hivyo tunatarajia sheria hii ije na kikokotoo cha chini ya 540 au 580 na kionekane kwenye muswada huu wa sheria na siyo kwenye kanuni za Mheshimiwa Waziri na *SSRA*. Hivyo hatutarajii kabisa kupunguza kile kilichokuwepo badala ya kukiboresha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingi zinajengwa kuhusu uimara wa mifuko na mabadiliko ya kupunguza mafao kwa kutumia kanuni, lakini hoja hizi ni dhaifu kama

Serikali itaacha kuchota fedha za wanachama na kuweka katika miradi ambayo haikufanyiwa upembuzi yakinifu na mwisho wa siku miradi hushindwa kutoa kile kilichokusudiwa kama ambavyo ilioneshwa katika taarifa ya ukaguzi wa CAG kuhusiana na utendaji wa mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo ya mwaka 2015/2016 inasema kwamba watumishi wa umma wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2014 ilionesha kuwa mfuko una jumla ya fedha shilingi trilioni 1.3 na deni halisi lilikuwa shilingi trilioni 12.46, hivyo kufanya upungufu wa shilingi trilioni 11.1. Taarifa ya sasa inaonesha Mfuko wa PSPF unaidai Serikali kiasi cha shilingi trilioni tatu. Madeni haya yanatokana na mikopo ya moja kwa moja, dhamana na michango ambayo haikuwahusisha kulingana na matakwa ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali bado ni ile ile ya CCM, je, ni kitu gani kitakachotoa uthibitisho kuwa tabia hiyo ya Serikali itabadilika katika sheria hii inayotungwa ili kuondokana na tabia yake ya kukopa moja kwa moja kwenye mifuko na kushindwa kurejesha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili jambo la kuacha mambo muhimu yanayohusu maisha ya watu kwenye kanuni ambayo kwanza ni jukumu la Waziri au Serikali. Hii siyo sahihi kabisa. Inatakiwa suala muhimu kwa maisha ya wafanyakazi kama hili liamuliwe na Bunge zima kwa kujadiliwa na kufikia mwisho, kwani Wabunge ndiyo walinzi wa wananchi ikiwemo wanachama wa mifuko ya hifadhi. Mfano, kifungu cha 18(2)(b): *“or such amount as the Minister may by order in the Gazette determine...”* Kifungu cha 29(2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya jamii ni kinga ya maisha kwa wanachama wake mara tu baada ya kutoka kwenye ajira na mfuko uliokuwepo ambao ulikuwa unawapa wanachama kuchagua kulingana na aina ya mafao yaliyokuwa yanatolewa na mfuko husika. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa jambo la busara kama wanachama waliopo sasa katika mifuko waendeleo na utaratibu walioingia nao mikataba ya kupatiwa huduma na

utaratibu mpya wa mifuko miwili uwahusu wanachama wapya au watumishi wapya katika sekta za umma na binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ya wanachama kuhama na sera ya mafao waliyojiunga nayo kwenye mifuko iliyovunjwa, imepewa mwanga kidogo kwenye kifungu cha 80(4) cha muswada huu, lakini bado kuna hoja, kama ndivyo hivyo, ni kweli kuwa mafao yaliyokuwepo kwa mifuko inayounganishwa bado yataendelea kutolewa kwa wanachama wa zamani katika mifuko mipya inayoanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu zilizotolewa na wadau ni kwamba *PPF* ambayo asilimia 75 ya wanachama wake ni kutoka sekta binafsi, asilimia 25 ndiyo sekta za umma. Kwa hiyo basi, katika kuunganisha mifuko, ilitakiwa *NSSF* na *PPF* kuwa taasisi moja ambayo ingetumika kama sekta binafsi, badala yake asilimia 25 za wanachama ambao wako sekta za umma ndio wameunganishwa na wenzao katika mifuko mingine na iliyobaki, asilimia 75 wanahamishiwa *NSSF*. Hapa kuna shida ya kimaheسابu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya muswada huu unapendekeza kutunga sheria ya kutoa mafao ya hifadhi ya jamii kwa watumishi walio katika utumishi wa umma na kufuta sheria zilizopo zilizokuwa zinatoa huduma hiyo kwa watumishi hao. Ni kweli kwamba Mifuko hiyo ya Pensheni ya *PSPF*, *LAPF*, *GEPF* na *PPF*, mbali ya kutoa huduma kwa watumishi wa umma, pia ilikuwa inatoa huduma kwa watu ambao sio watumishi wa umma. Kwa maana nyingine ni kuwa taasisi hizo zina wanachama wasiokuwa watumishi wa umma na pia kuna watumishi wa umma ambao walikuwa ni wanachama wa *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, ili kuondoa mtafaruku unaoweza kujitokeza kutokana na uanzishwaji wa sheria hii, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa muda wa mpito uliowekwa kwenye muswada huu katika kifungu cha 86 kinaweza kusababisha usumbufu na hivyo kuleta matatizo miongoni mwa wanachama, kwani watu wanaostaafu kila wakati na wengine tayari wako

kwenye kusubiri mafao yao. Hivyo, kwa kipindi hicho cha mpito cha miezi sita ni wapi watatakiwa kudai au kuhudumiwa ili wapatiwe stahiki zao? Ni bora kuwekwa muda maalum wa kufanya uhamisho wa wanachama wote wanaotakiwa kuhamishwa kutoka mfuko wa awali kwenda mfuko mpya ili kuondoa usumbufu ambao utajitokeza katika utekelezaji wa zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama muswada unavyosema kuwa unafuta mifuko minne ambayo ilikuwa inatoa huduma kwa watumishi wa umma na kuunda mfuko mmoja kwa lengo kuu la kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima na pale pale kuleta tija kiutendaji kwa kutoa mafao na pensheni zilizolingana kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha (3) cha muswada kinachohusu tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika kwenye muswada, neno "*authority*" au kwa kiswahili "mamlaka" kwa maana iliyotolewa kuwa ni Mdhibiti wa Mifuko (SSRA) limetumika mara kadhaa katika vifungu mbalimbali vya muswada. Kwa mujibu wa kifungu cha 6(1) cha Sheria ya SSRA kinasema kazi kubwa ya mamlaka itakuwa ni kusimamia na kudhibiti utendaji wa mifuko ya hifadhi. Hii ilikuwa sahihi kutokana na kuwepo kwa mifuko mingi ambayo ilikuwa inashindana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa dhana pana ya Serikali ni kuwa mifuko miwili ambayo haishindani katika kutoa mafao na kwa mfumo huu unaoanzishwa na Muswada wa Sheria hii ni kuwa utakuwa na bodi inayopewa mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 8 na kifungu cha 9 katika kusimamia uendeshaji wa mfuko. Hivyo basi, itakuwa haina tija yoyote kwa Mdhibiti kudhibiti taasisi ambazo hazina ushindani wa aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuanzisha mchakato wa kuifuta Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi za Jamii kwani kuendelea kuwepo ni kuongeza gharama zisizokuwa za lazima kwa mfuko, kwani sheria inailazimisha mifuko kuchangia asilimia

kadhaa kwa mamlaka kila mwaka ili mamlaka ifanye kazi zake. Jambo hilo lilikuwa sahihi pale ambapo kulikuwa na mifuko zaidi ya mitano ya hifadhi ambayo ilikuwa inashindana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 8 kwa ujumla wake kinasema kuwa bodi itakuwa ni chombo huru chenye uwezo wa kushtaki au kushtakiwa, kununua na kuuza mali zake zisizohamishika na zinazohamishika, kukopa au kukopesheka na kuingia kwenye mikataba, lakini pia inasema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatakiwa kuingilia pale ambapo bodi itakuwa imeshitaki au kushitakiwa. Kwa kuwa bodi ni chombo au taasisi huru na yenye uwezo wa kuingia mikataba ya aina yoyote, ni kwa nini inapotakiwa kushtakiwa ni lazima utaratibu wa kushitaki Serikali ufuatwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinahalalisha kile kitu kinachopigiwa kelele mara kwa mara na watendaji kufanya kazi kwa kutojali, kwa kuwa kuna kinga ya Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa ili kuleta uwajibikaji kila mtu awajibike kulingana na matendo yake. Hakuna kifungu chochote kinachosema kuwa kabla ya kukopa au kukopesheka, kununua au kuuza mali au kuingia kwenye mikataba ya kibiashara ni lazima Mwanasheria Mkuu atoe ruhusa. Hivyo, kwa nini wakishalikoroga wanataka kinga ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali? Kambi Rasmi ya Upinzani inaungana na wadau waliopendekeza kufutwa kwa kifungu cha 8(3), (4) na (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 24 cha muswada kinatoa ruhusa kwa mwanachama kujitoa katika mfuko, lakini kwa sharti la kupata kibali cha bodi, baada ya bodi kujiridhisha kuwa mwanachama amekidhi matakwa yaliyowekwa. Jambo hili linaweza kuwa zuri hasa kwa watumishi wa mikataba ya muda mfupi, kwani sasa hivi siyo lazima kuzeeka kazini eti unafanya kazi Serikalini. Kuna watumishi wa Serikali kwa muda wa miaka mitano kama vile alivyo Rais na timu yake ya wasaidizi na pindi anapoingia Rais mwingine naye anaingia na timu yake ya wasaidizi,

waajiriwa wa kwenye migodi na madini ambao wanafanya kazi kwa mikataba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya wenzetu wa Kenya, Sheria Namba 45 ya mwaka 2013, kifungu cha 45, ina fao la kujitoa na haina mgogoro kabisa. Umuhimu wa kuwa na fao la kujitoa kama Sheria ya PPF na PSPF pamoja na NSSF zilivyokuwa zinahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba kanuni zilizoletwa na SSRA kujaribu kuzuia fao hili zilileta mtafaruku mkubwa sana kwa wanachama hasa wale waliokuwa wameajiriwa katika sekta ya madini na Mheshimiwa Waziri wa sasa ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii alikubaliana na wanachama na hoja binafsi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge; Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Selemani Jafo kuhusiana na fao hili; na Mheshimiwa Spika Anna Makinda kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, walikubali Mheshimiwa Selemani Jafo afanye utafiti wa kuleta taarifa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa taarifa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ina uhakika kuwa fao hilo bado linahitajika na ni muhimu sana kwa wanachama wa mifuko ya hifadhi kuwa nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 29 kinachoeleza mafao yatakayokuwa yanatolewa na mfuko huu, kifungu kidogo (e) kimesema kuwa kutakuwa na fao la kutokuwa na ajira *(an employment benefit)*. Hata hivyo fao hili halijatolewa ufafanuzi wowote kwenye sheria, zaidi ya kueleza kwamba Waziri mwenye dhamana atalitungia kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze kwa kina fao hili ni lipi? Linagusa kundi lipi? Kwa masilahi yapi? Tunayasema haya kwa sababu inasemekana kwamba fao hili lina lengo la kuchukua nafasi ya fao la kujitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba umuhimu mkubwa wa kuwa na fao la kujitoa kama ilivyokuwa linatolewa na mifuko iliyokuwepo, bado ni la msingi na lazima, kwani mwanachama anakuwa tayari ana akiba yake na hivyo huo unakuwa ni mtaji wa kumtoa kwenye umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 29(1)(f) kinatoa fao la ugonjwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaomba ipatiwe ufafanuzi wa hili. Fao la ugonjwa na tofauti yake...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ni kengele ya pili, Mheshimiwa.

MHE. ESTER A. BULAYA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie sentensi. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunaona ni njia ya kutaka kuliita fao la afya ili lisiingiliane na kile kinachotolewa na *NHIF*. Kama lengo ni kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo kuwa na matumizi mazuri ya fedha za wanachama, ni bora kama ambavyo tulieleza hapo awali, mafao yanatolewa na Mfuko wa Bima ya Afya yawekwe pia kwenye mfuko huu unaoanzishwa na sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa muda, naomba yote ambao yamebakia, sijayasoma yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, ila nasikitika kwa kutokubali Zaburi na wewe ni Mkristo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hakuna haja ya kusikitika. Zingatia kanuni tu, tutakuwa pamoja.

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MUSWADA
WA SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII KWA
WATUMISHI WA UMMA WA MWAKA 2017 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(The Public Service Social Security Fund Act, 2017)

*(Yanatolewa chini ya kanuni ya 86(6) ya kanuni za
Bunge, Toleo la mwaka 20016)*

A. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika,
kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kwa mwaka huu wa 2018 kusimama hapa kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria uliopo mezani, naomba kwa heshima, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutulinda sote na kutuvusha salama katika mwaka uliopita wa 2017 na kutujalia kuuona mwaka huu mpya wa 2018 tukiwa salama. Kwa sababu hiyo, nakutakia wewe Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge wote, heri ya Mwaka Mpya.

Mheshimiwa Spika,
Zaburi ya 1 mstari wa kwanza na wa tatu inasema kwamba: "Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki, wala hakusimama katika njia ya wakosaji, wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki; na kila atendalo litafanikiwa. Mzaburi anaendelea kusema katika mstari wa nne kwamba: "Sivyo walivyo wasio haki, hao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo"

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

Mheshimiwa Spika,
baada ya salamu hizo za utangulizi sasa naomba nitoe maoni ya jumla kuhusu Muswada wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika,

Hifadhi ya Jamii ni haki ya kila Mtanzania. Haki hii imeanishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 11(1) na Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003. Haki hii pia imeianishwa kwenye mkataba wa kimataifa wa haki za binadamu wa mwaka 1948 pamoja na mikataba ya shirika la kazi duniani (ILO) ibara ya 102 ya mwaka 1952.

Mheshimiwa Spika,

Hifadhi ya Jamii ni haki ya kila mtu na si kwa wale tu walio katika sekta iliyo rasmi . Kwa sababu mpaka sasa kulingana na takwimu za sensa ya watu na makazi zilizotolewa mwaka 2012 ni kwamba idadi ya watanzania wote ni milioni 44.9 ambao kati yao watu milioni 1.7 tu ndio waliojiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii, hii ikiwa ni asilimia 6.5 tu ya nguvu kazi yote ya watu milioni 23.7

Mheshimiwa Spika,

kwa takwimu hizo, Tanzania haiwezi kujitokeza kifuambele na kujidai kwamba jamii yake imehifadhika. Na sababu kubwa asilimia ndogo ya watu waliojiunga na scheme za hifadhi za jamii ni ufinyu wa ajira kwa sekta za uma na sekta binafsi. Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba badala ya Serikali kung'ang'ana kuweka sheria za kupunguza na kuibana mifuko ya jamii ingepanua fursa za ajira kwa watanzania na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuajiri kwa wingi ili kupunguza umasikini wa kipato kwa watanzania lakini pili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanaweka akiba itakayowasaidia pindi umri wao wa kufanya kazi utakapokoma.

Mheshimiwa Spika,

pamoja na hayo yote, jambo la msingi ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini, ni kwamba; akiba ni kitu kinamchomsaidia mtu wakati wa shida au matatizo; na sio kitu cha kufanikisha mazishi ya mtu huyo baada ya kufariki kutokana na kushindwa kutatuliwa kwa matatizo au shida iliyokuwa ikimkabili. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali pamoja na wabunge wote kwa jumla kuhakikisha kwamba mifuko ya jamii chini ya sheria hii

inaweka mazingira ya mwanachama kuweza kunufaika na michango yake wakati wowote anapopata shida kubwa kabla ya kustaafu na sio kuweka masharti magumu ya kumfanya mwanachama ashindwe kunufaika na michango yake mpaka wakati wa kustaafu.

Mheshimiwa nasema hivi kwa sababu ikiwa hatutaweke utaratibu wa kumfanya mwanachama kunufaika na michango yake wakati anapopata shida akiwa hai, yamkini tunaweza kuwa tunatengeneza mazingira ya kuwachangisha wanachama fedha za kuja kugharamia mazishi yao na sio kuwasaidia kuboresha maisha yao. Hii ni bayana kwa kuwa umiri wa kuishi kwa mtanzania sasa hivi unakadiriwa kuwa ni miaka 61; na ni takribani umri huo huo mtumishi anapaswa kustaafu na kulipwa mafao yake. Kwa logic ndogo, mafao hayo ni ya kumzika sio ya kumtegemeza aishi.

Mheshimiwa Spika,

Aidha, Mamlaka ya uthibiti wa hifadhi ya jamii (ssra) inasema kwamba hadi juni, 2015 mifuko ya hifadhi za jamii hapa nchini ilikuwa na jumla ya wanachama 2,132,350. Na kufikia Juni, 2016 wanachama waliongezeka na kufikia 2,464,399, hii ni kutokana na ushindani uliopo baina ya mifuko na watu hao ni wale walipo katika ajira ya sekta iliyo rasmi tu na nguvu kazi kubwa iliyobakia ya takribani milioni 20 inashughulika na sekta isiyo rasmi na wote wako katika hali hatarishi kwa vile hawana kinga yeyote ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika,

Takwimu zinaonesha kuwa PPF hadi juni 2015 ilikuwa na jumla ya watumishi 352, PSPF ilikuwa na watumishi 186, LAPF ilikuwa na watumishi 195 na mifuko hiyo yote ina matawi zaidi ya zaidi 10 nchi nzima. Hapa ni dhahiri kwamba kutakuwa na kile kinachoitwa **“down sizing”** ili kazi zifanyike kulingana na nafasi zitakazo tengenezwa na mfumo mpya wa taasisi inayoanzishwa kwa mujibu wa sheria hii. Mbali ya hilo kuna ushindani kwa mifuko kutoa mafao yanayofanana, mfano; fao la bima ya afya linalotolewa na Mfuko wa Bima ya afya -**National Health Insurance Fund- (NHIF)** na fao la kuumia ukiwa kazini linatolewa na mfuko maalumu wa fidia ya wafanyakazi -**Workers Compensation Fund (WCF)**

Mheshimiwa Spika,

Kwa kuangalia mafao yatakayotolewa chini ya sheria hii ni dhahiri kwamba ushindani au duplication ya mafao baina ya mifuko itaendelea au kuondoa baadhi ya mafao na kuyaacha kwenye mifuko ambayo haijafutwa kwa mujibu wa sheria hii maana yake ni kumzidishia mzigo wa makato mtumishi wa umma ambaye mshahara wake ni mdogo, kwani ina mlazimu kuchangia mifuko miwili.

Mheshimiwa Spika,

Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Hifadhi za jamii kwenye kamati iliyouchambua muswada huu alisema kuwa, pamoja na mambo mengine ni kuboresha mafao ya wanachama. Hili ni jambo jema kama litaonekana katika muswada huu.

Mheshimiwa Spika,

Mafao ya wanachama yanaboreshwa kwa kuwa na kikokotoo (formula) ambacho kinajulikana na kimekubalika baina ya wahusika wote, kwa maana ya wanachama. Tukumbuke kuwa fedha hizi sio mali ya Serikali bali ni mali ya wanachama na Serikali kupitia kwenye shirika hili ni mtunzaji na muendelezaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika,

Muswada ulikuwa umetoa kitu kinachoitwa "full pension" na kikatolewa tafsiri yake na kwa bahati mbaya sana hiyo ndiyo ilikuwa ni kikokotoo au Kanuni au formula, lakini wadau waliipinga kwani badala ya kuboresha mafao ilikuwa inayakandamiza. Kabla ya kuunganisha mifuko hii, mifuko mingi ilikuwa na vikokotoo tofauti kama vile: pspf 540 na (580 kwa wajiriwa walioanza kazi baada ya 2014, lapf 540, PPF na gepf 580. Kwa vile moja ya sababu kuu za kuunganisha mifuko hii ni kuboresha mafao ya wafanyakazi, hivyo tunatarajia sheria hii ije na kikotoo cha chini ya 540 au 580 na kionekane kwenye muswada huu wa sheria na sio kwenye kanuni za Mheshimiwa Waziri na SSRA. Hivyo hatutarajii kabisa kupunguza kile kilichokuwepo badala ya kukiboresha. Kuna hoja nyingi zinajengwa kuhusu uimara wa mifuko na mabadiliko ya kupunguza mafao kwa kutumia kanuni, lakini

hoja hizo ni dhahifu kama Serikali itaacha kuchota fedha za wanachama na kuwekeza katika miradi ambayo haikufanyiwa upembuzi yakinifu na mwisho wa siku mradi unashindwa kutoa kile kilichokusudiwa kama ambavyo ilioneshwa katika taarifa za ukaguzi na CAG kuhusiana na utendaji wa mashirika hayo. Taarifa hiyo ya mwaka 2015/16 inasema kwamba;

" Taarifa ya tathmini ya uwezo wa wa Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma ya mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2014 ambayo iliandaliwa na Muhana & Co Actuaries & Consultants ilionyesha kuwa Mfuko una jumla ya fedha za Shilingi milioni 1,306,707; na deni halisi lilikuwa Shilingi trilioni 12.46 Hivyo kufanya upungufu wa shilingi trilioni 11.15. Taarifa ya sasa inaonesha Mfuko wa PSPS unaidai serikali kiasi cha Tsh. 3 Trillion. Madeni haya yanatokana na mikopo ya moja kwa moja, dhamana, na michango ambayo haikuwasilishwa kulingana na matakwa ya kisheria".

Mheshimiwa Spika,
Serikali bado ni ile ile ya CCM, je ni kitu gani kitakachotoa uthibitisho kuwa tabia hiyo ya Serikali itabadilika katika Sheria hii inayotungwa ili kuondokana na tabia yake ya kukopa moja kwa moja kwenye mifuko na kushindwa kurejesha?

Mheshimiwa Spika,
Kuna hili jambo la kuacha mambo muhimu yanayohusu maisha ya watu kwenye kanuni ambazo kwazo ni jukumu la Waziri(Serikali), hii sio sahihi kabisa inatakiwa suala muhimu kwa maisha ya wafanyakazi kama hili liamuliwe na Bunge zima kwa kujadiliana na kufikia mwisho kwani wabunge ndio walinzi na wawakilishi wa wananchi ikiwemo wanachama wa mifuko ya hifadhi. Mfano kifungu cha 18(2) (b) Or such amount as the minister may, by order in the Gazette determine", kifungu cha 29(2) n.k

Mheshimiwa Spika,
Hifadhi ya jamii ni kinga ya maisha kwa wanachama wake mara tu baada ya kutoka kwenye ajira, na mfumo uliokuwepo ambao ulikuwa unawapa wanachama kuchagua kulingana na aina ya mafao yaliyokuwa

yanatolewa na mfuko husika. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inaona litakuwa jambo la busara kama wanachama waliopo sasa katika mifuko waendeleo na utaratibu walioingia nao mikataba ya kupatiwa huduma, na utaratibu mpya wa mifuko miwili uwahusu wanachama wapya au watumishi wapya katika sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Spika,

Hoja hii ya wanachama kuhama na sera ya mafao walijiunga nayo kwenye mifuko inayovunjwa imepewa mwanga kidogo kwenye kifungu cha 80(4) cha muswada huu. Lakini bado kuna hoja kama ndio hivyo ni ukweli kuwa mafao yaliyokuwepo kwa mifuko inayounganishwa bado yataendelea kutolewa kwa wanachama wa zamani katika mifuko mipya inayoanzishwa?

Mheshimiwa Spika,

Kwa takwimu zilizotolewa na wadau ni kwamba PPF ambayo asilimia 75 ya wanachama wake ni kutoka sekta binafsi na asilimia 25 ndio sekta ya umma, kwa hiyo basi katika kuunganisha mifuko ilitakiwa NSSF na PPF kuwa taasisi moja ambayo ingehudumia sekta binafsi. Badala yake asilimia 25 za wanachama ambao wako sekta ya umma ndio wameunganishwa na wenzao katika mifuko mingine na iliyobakia 75% wanahamishiwa NSSF. Hapa kuna shida ya kimahesabu!!!!

B. MAPITIO YA MUSWADA

Mheshimiwa Spika,

Madhumuni ya muswada huu unapendekeza kutungwa kwa sheria ya kutoa mafao ya hifadhi ya jamii kwa watumishi walio katika utumishi wa umma, na kufuta sheria zilizopo zilizokuwa zinatoa huduma hiyo kwa watumishi hao.

Mheshimiwa Spika,

Ni ukweli kwamba mifuko hiyo ya Pensheni ya PSPF, LAPF, GEPF na PPF mbali ya kutoa huduma kwa watumishi wa umma pia mifuko hiyo ilikuwa inatoa huduma kwa watu ambao sio watumishi wa umma. Kwa maana nyingine ni

kuwa taasisi hizo zina wanachama wasiokuwa watumishi wa umma na pia kuna watumishi wa umma ambao walikuwa ni wanachama wa NSSF.

Mheshimiwa Spika,

Kwa muktadha huo ili kuondoa mtafaruku unaoweza kujitokeza kutokana na uanzishwaji wa sheria hii, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa muda wa mpito ullokwewa kwenye muswada katika kifungu cha 86 kunaweza kusababisha usumbufu na hivyo kuleta matatizo miongoni mwa wanachama kwani watu wanastaafu kila wakati na wengine tayari wako kwenye kusubiri mafao yao, hivyo kwa kipindi hicho cha mpito wa miezi sita ni wapi wanatakiwa kudai au kuhudumiwa ili wapatiwe stahiki zao?

Ni bora kuwekwe muda maalum wa kufanya uhamisho kwa wanachama wote wanaotakiwa kuhamishwa kutoka mfuko wa awali kwenda mfuko mpya, ili kuondoa usumbufu ambao utaweza kujitokeza katika utekelezaji wa zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika,

Kama muswada unavyosema kuwa unafuta mifuko minne ambayo ilikuwa inatoa huduma kwa watumishi wa umma na kuunda mfuko mmoja, kwa lengo kuu la kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima na pale pale kuleta tija kiutendaji kwa kutoa mafao na pensheni zinazolingana kwa watumishiwa umma.

Mheshimiwa Spika,

Katika kifungu cha 3 cha muswada kinachohusu tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika kwenye muswada, neno "authority" au kwa Kiswahili mamlaka na kwa maana iliyotolewa kuwa ni mdhibiti wa mifuko yaani (SSRA) limetumika mara kadhaa katika vifungu mbalimbali vya muswada. Kwa mujibu wa kifungu cha 6(1) cha sheria ya SSRA kinasema kazi kubwa ya Mamlaka itakuwa ni kusimamia na kuthibiti utendaji wa mifuko ya hifadhi. Hii ilikuwa sahihi kutokana na uwepo wa mifuko mingi ambayo kwayo ilikuwa ni shindani.

Mheshimiwa Spika,
Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwa kuwa dhana pana ya Serikali ni kuwa na mifuko miwili ambayo haishindani katika kutoa mafao, na kwa mfuko huu unaoanzishwa na muswada wa sheria hii, ni kuwa utakuwa na bodi inayopewa mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 8 na kifungu cha 9 katika kusimamia uendeshaji wa mfuko. Hivyo basi itakuwa haina tija yoyote kwa mdhibiti kudhibiti taasisi ambazo hazina ushindaji wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika,
Kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuanzisha mchakato wa kuifuta mamlaka ya udhibiti wa hifadhi za jamii kwani kuendelea kuwepo ni kuongeza gharama zisizokuwa za lazima kwa mfuko, kwani sheria inailazimisha mifuko kuchangia asilimia kadhaa kwa mamlaka kila mwaka ili mamlaka ifanye kazi zake. Jambo hilo lilikuwa sahihi pale ambapo kulikuwa na mifuko zaidi ya mitano ya hifadhi ambayo ilikuwa inashindana.

Mheshimiwa Spika,
Kifungu cha 8 kwa ujumla wake kinasema kuwa Bodi itakuwa ni chombo huru chenye uwezo wa kushitaki au kushtakiwa, kununua na kuuza mali zake zisizohamishika na zinazohamishika, kukopa au kukopesha na kuingia kwenye mikataba. Lakini pia inasema Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatakiwa kuingilia pale ambapo bodi itakuwa imeshtaki au kushtakiwa.

Mheshimiwa Spika,
Kwa kuwa bodi ni chombo huru au taasisi huru na yenye uwezo wa kuingia mikataba ya aina yoyote, ni kwanini inapotakiwa kushtakiwa ni lazima utaratibu wa kuishtaki Serikali ufuatwe? Kwa mujibu wa sheria ya Mwenendo wa Mashtaka (Government Proceeding ACT) ili upeleke shauri lako mahakamani ni lazima utimize matakwa ya kifungu cha 6(2) kinachosema kuwa;

"No suit against the Government shall be instituted, and heard unless the claimant previously submits to the Government Minister, Department or officer

concerned a notice of not less than ninety days of his intention to sue the Government, specifying the basis of his claim against the government, and he shall send a copy of his claim to the Attorney General. Notice of intention to sue, as the first procedure to sue the government, a notice of not less than ninety days of his intention to sue the Government, before commencing proceedings in court”,

Kwa utaratibu maalum ili kukidhi matakwa ya sharia hiyo, kwa wanachama wa kawaida ambao kwa njia moja au nyinge wanakuwa na mikataba na mashirika haya, ni kweli haki itapatikana?

Mheshimiwa Spika,
Kifungu hiki kinahalalisha kile kitu kinachopigiwa kelele kila mara cha watendaji kufanyakazi kwa kutokujali, kwa kuwa kuna kinga ya Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa ili kuleta uwajibikaji kila mtu awajibike kulingana na matendo yake. Hakuna kifungu chochote kinachosema kuwa kabla ya kukopa au kukopesha, kununua au kuuza mali au kuingia kwenye mikataba ya kibiashara ni lazima Mwanasheria Mkuu wa Serikali atoe ruhusa. Hivyo kwanini wakishalikoroga wanataka kinga ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali?

Mheshimiwa Spika,
Kambi Rasmi ya Upinzani inaungana na wadau waliopendekeza kufutwa kwa vifungu vidogo vya 8(3), 8(4) na 8(5).

Mheshimiwa Spika,
Kifungu cha 11 cha muswada kinachosema kuhusu *“Management of the Fund”*, kifungu hicho kinasomeka kuwa;
“The Board shall be responsible for the administration and management of the fund.....”

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba Bodi ya wakurugenzi jukumu lake ni kusimamia (supervisory role) na

sio la uendeshaji (administrative and management role). Jambo hili limegusiwa katika kifungu cha 15(3) kinachosema kwamba;

“the Director General shall,subject to the directions of the Board, be responsible for the day to day administration of the Fund”.

Hii ni sawa sawa kabisa na Bunge linavyofanya kazi zake dhidi ya Serikali. Kwa muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kifungu hicho kitoe jukumu la uendeshaji kwa Mkurugenzi na timu yake ya utendaji badala ya Bodi ya Wakurugenzi. Kila mmoja ahukumiwe kwa nafasi yake na mgawanyo wa madaraka uwe wazi, tukumbuke kuwa Mtendaji Mkuu na Mwenyekiti wa bodi kwa mujibu wa sheria hii wote ni wateule wa Rais, rejea kifungu cha 8(1) kwenye Jedwali la kwanza kifungu cha 1(1) (a) na kifungu cha 15(1).

Mheshimiwa Spika,
Kifungu cha 15(4) cha muswada kinasema kuwa; “The Director General shall hold office for a term of five years and.....”. Hapa limetumika neno “shall”, hii ni kinga ya nguvu hadi kipindi cha miaka mitano kifike kama bado yuko hai na mwenye afya njema. Maana yake hata kama utendaji kazi wake utakuwa upo chini ya kiwango kwa tafsiri pana sio rahisi kutenguliwa. Japokuwa kifungu cha 15(2) kinasema atapewa masharti ya kazi, lakini mktaba au masharti ya kazi hayawezi kwenda tofauti na sheria iliyopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika,
Kifungu cha 24 cha muswada kinatoa ruhusa kwa mwanachama kujitoka katika mfuko, lakini kwa sharti la kupata kibali cha Bodi, baada ya bodi kujiridhisha kuwa mwanachama amekidhi matakwa yaliyowekwa. Jambo hili linaweza kuwa zuri hasa kwa watumishi wa mikataba ya muda mfupi, kwani sasa hivi kazi sio lazima kuzeeka kazini eti unafanya kazi Serikalini, kuna watumishi wa Serikali kwa muda wa miaka mitano kama vile alivyo Rais na timu yake ya wasaidizi na pindi anapoingia Rais mwingine nae anaingia na timu yake ya wasaidizi, waajiriwa wa kwenye

migodi ya madini ambao wanafanya kazi kwa mikataba n.k. Mheshimiwa Spika, ukiangalia sheria ya hifadhi ya jamii ya wenzetu wa Kenya kwa sheria Na.45 mwaka 2013 kifungu cha 45 ina fao la Kujitoa na haina mgogoro kabisa.

Mheshimiwa Spika,

Umuhimu wa kuwa na fao la kujitoa kama sheria ya PPF na PSPF pamoja na NSSF zilivyokuwa zinahitaji, tukumbuke kwamba kanuni zilizoletwa na SSRA kujaribu kuzuia fao hili zilileta mtafaruku mkubwa sana kwa wanachama hasa wale waliokuwa wameajiriwa katika sekta ya madini, na Mheshimiwa Waziri wa sasa akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii ulikubaliana na wanachama na hoja binafsi zilizoletwa na waheshimiwa John Mnyika na Mhe Selemani Jaffo kuhusiana na fao hili na Mheshimiwa Spika Anne makinda kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Kamati ya huduma za Jamii walikubali Mheshimiwa Selemani Jaffo afanye utafiti na kuleta taarifa Bungeni. Hivyo, kwa taarifa hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani ina uhakika kuwa fao hilo bado linahitajika na ni muhimu sana kwa wanachama wa mifuko ya hifadhi kuwa nalo.

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 27 kinasomeka kuwa kuwa kuwa na kitu kinaitwa "Special lumpsum" lakini vitatolewa vigezo vya wanaostahili hiyo "Special Lump sum", kama ambavyo hapo awali niliongelea kuhusu wafanyakazi walio katika sekta za madini na watumishi ambao utumishi wao Serikali unaendana na mihula ya Serikali kuwa madarakani kabla ya kufanyika kwa uchaguzi. Kama hakutakuwa na kazi inayotakiwa kuendelea na mtumishi huyo anaacha utumishi wa umma, nini kinatakiwa kifanyike kuhusiana na mafao yake? Je ni kweli ataendelea kulipwa mafao ya kutokuwa na ajira hadi kutimiza umri wa kulipwa pensheni? Au kifungu cha 27 (d) kinachosema kuwa "has retired on abolition of his office".

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 29 kinachoeleza mafao yatakayokuwa yanatolewa na mfuko huu, kifungu kidogo cha (e) kimesema kuwa kutakuwa na fao la kutokuwa na ajira (unemployment

benefit). Hata hivyo fao hili halijatolewa ufafanuzi wowote kwenye sheria,zaidi ya kuelekeza kwamba waziri mwenye dhamana atalitungia Kanuni. Kambi rasmi ya upinzani inaitaka serikali ieleze kwa kina fao hili ni lipi , litagusa kundi lipi na kwa maslahi yepi? Tunayasema haya kwa sababu inasemekana kwamba fao hii lina lengo la kuchukua nafasi ya fao la kujitoa (withdrawal benefit).

Mheshimiwa Spika,

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba umuhimu mkubwa wa kuwa na fao la kujitoa kama lilivyokuwa linatolewa na mifuko iliyokuwepo bado ni la msingi na lazima kwani mwanachama anakuwa tayari na akiba yake na hivyo huo unakuwa ni mtaji wa kumtoa kwenye umasikini wa kipato.

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 29(1) (f) kinatoa fao la Ugonjwa au "sickness benefit", Kambi Rasmi ya Upinzani inaomba ipatiwe ufafanuzi wa hili fao la ugonjwa na tofauti yake na fao la afya. Hapa tunaona ni njia ya kukataa kuliita fao la afya ili isingiliane na kile kinachotolewa na NHIF. Kama lengo ni kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo kuwa na matumizi mazuri ya fedha za wanachama ni bora kama ambavyo tulieleza hapo awali Mafao yanayotolewa na Mfuko wa Bima ya Afya yawekwe pia kwenye mfuko huu unaoanzishwa na sharia hii.

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 32(1) cha sheria kinasema kuwa mwanachama ana haki ya kupata mafao la uzazi, jambo ambalo ni jema sana, lakini maelezo yake yanabagua wanachama. Ukweli ni kuwa wanachama wanaume nao wanawake zao ambao nao wanakuwa katika mchakato wa uzazi kama wanachama wanawake. Ili kuweka uwiano ulio sawa kwa wanachama wa jinsia zote ni muhimu kukawepo na fao litakalokuwa ni kwa wanaume kama mafao hayo ya uzazi ni maalum kwa wanachama wa jinsia ya kike tu, ili wanachama wanawake na wanaume wanufaika na fao la uzazi.

Mheshimiwa Spika,
Kifungu cha 45(1) cha muswada kinaipa Bodi mamlaka ya kugawa pensheni ya mwanachamba ambaye atakuwa anatumikia kifungu kwa kadri itakavyoona inafaa hadi pale atakapomaliza kutumikia adhabu yake ya kifungu. Kambi Rasmi ya Upinzani iungane na wadau kwamba mtu kuwa gerezani haina maana kuwa hauna uwezo wa kuelewa ni vipi mali zako zitumike na ni nani wanastahili na nani hawastahili. Hivyo basi, tunashauri kifungu hicho kiondoe mamlaka ya kugawa pensheni yake kwa bodi na yarudishwe kwa mhusika mkuu wa pensheni.

Mheshimiwa Spika,
Kifungu cha 46 kinataja nafasi za utumishi wa umma kuwa wao inawapasa kupata kibali maalum kutoka kwa Mheshimiwa Rais kuhusiana na mafao yao, lakini kada zote hizo zinafuata sharia ya utumishi wa umma katika kutimiza majukumu yao japokuwa ni wateule wa Rais. Kama ambavyo tumeeleza hapo awali kwamba fao la kujitoa ni muhimu, na kama kanuni/kikokotoo cha pension au mafao kitakuwa shirikishi na kuwekwa wazi kuna umuhimu gani wa Rais kutoa kibali?

Mheshimiwa Spika,
Kifungu hicho kikisomwa pamoja na sharia ya SSRA kifungu cha 38A(A) kuwa mhusika ni lazima aandike barua kwenye kamati na barua hiyo iambatane na mapendekezo kutoka kwa majiri wake wa mwisho wakati anaacha kazi. Tukumbuke kwamba kada zote zilizotajwa kwenye musdwada katika kifungu cha 46 ni wasaidizi wa Rais hivyo katika hili Rais anakuwa na nafasi mbili, moja ni ushauri na pale ni kutoa maamuzi. Hii sasa ni jambo la ajabu katika utendaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika,
Kifungu cha 56(1) cha muswada kinachosema kuwa;
“No income tax on the contributions and benefitis payable under the scheme shall be levied on the fund”
Kwa maana kwamba, mfuko ndio hautatakiwa kulipa kodi lakini mafao ya wanachama yatakayokuwa yanalipwa

yatakiwa kukatwa kodi ya mapato, Kambi Rasmi ya Upinzani inashukuru kwani Serikali katika kikao na wadau ilikubali kuondoa maneno, "**on the fund**".

Mheshimiwa Spika,

Kuendelea kuwepo kwa maneno hayo ni kwamba wanachama watakuwa wanalipishwa michango mara mbili kwenye mishahara yao jambo ambalo lilikuwa ni kinyume cha utaratibu wa kikodi.

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 57(1) cha muswada kinailazimisha Bodi kumtafuta mthamini kufanya tathmini ya mfuko kila baada ya miaka mitatu kulingana na kanuni zilizotolewa na Mdhibiti. Kifungu cha 57(2) kinasema kuwa bodi inaweza kumuomba mdhibiti ili akubaline na bodi kutokufanyika kwa uthamini wa mfuko kama kifungu cha 57(1) kinavyotaka. Mheshimiwa Spika, madhara ya kutokufanyika kwa tathmini kwa wakati inaweza kupelekea madhara ya kufilisika kwa mfuko kama ambavyo ulivyokuwa mfuko wa PSPF. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kifungu hicho cha 57(2) kifutwe.

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 57(3) kinasema kuwa taarifa ya tathmini ya ubora wa mfuko inapelekwa kwa mdhibiti na Waziri badala ya msimamizi wa mfuko ambaye ni Bodi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa itakuwa ni vyema na taarifa toka kwa mdhamini juu ya ubora wa mfuko nakala ipewe Bodi sambamba na Mdhibiti na Waziri ili kabla ya hatua kuchukuliwa bodi na Mtendaji Mkuu vijitathmini utendaji wake.

Mheshimiwa Spika,

Vifungu vya 66 na 67 vya muswada vinatoa uhuru kwa Mkurugenzi Mkuu(ambaye anafanya kazi kwa maelekezo ya Bodi) wa PSSSF kuomba kibali cha Mahakama ili kukamata mali za mwajiri na kuzinadi ili kulipia michango ambayo alitakiwa kulipa lakini akashindwa kulipa. Wakati kifungu cha 72 kinazuia mali za mfuko kukamatwa na kunadiwa bila ya kuwepo kibali cha Waziri. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza,

sheria hii waajiri wote ni taasisi za Serikali na taasisi za Serikali nyingi kuzishtaki ni lazima Mwanasheria Mkuu wa Serikali ahushiswe. Aidha, Mfuko kwa muktadha huo ni kwanini mali zake zisikamatwe kama kutakuwa na amri ya kufanya hivyo? Kambi Rasmi ya Upinzani inaona hii ni “double Standard” inayowekwa katika muswada huu.

Mheshimiwa Spika

Kifungu cha 89(d), 108(h) na kifungu cha 112(b) kinachofanya marekbisho ya jedwali la pili la sheria ya Utumishi wa umma kwa kufuta kifungu cha 26 cha sheria na kukiandika upya. Kifungu hicho kinasema kuwa;

“one motor vehicle given once, of a value not exceeding such amount as the President may from time to time determine”

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki ambacho kinawaweka Waheshimiwa Majaji wastaafu kutegemea fadhila za Rais, jambo hili kwa mtazamo wetu linaweza kutumika kama kigezo cha kuwalazimisha kufanya yale ambayo Mheshimiwa Rais anataka yafanyike katika kadhia nzima ya utoaji wa haki. Hivyo basi tunaona sheria imtoe Rais na itamke aina ya gari au Jaji Mkuu aliyepo ndiye awe mhusika mkuu katika hilo.

Mheshimiwa Spika,

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....
Esther A. Bulaya(Mb)

**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Ofisi ya
Waziri Mkuu (Sera,Bunge,Kazi, Vijana, Ajira
na Wenye Ulemavu)**

31/1/2018

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo, wakati natangaza wageni, sikumtangaza kiongozi mmoja tuliyenaye hapa na kwa sababu ya muswada huu na ule

utatu wetu katika shughuli za wafanyakazi nchini, napenda nitambue uwepo wa Dkt. Aggrey Mlimuka, Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi baada ya kipindi cha maswali, mliona tulichua muda ambao tungelikuwa katika shughuli hizi mapema. Kwa maana hiyo, nitakuja kutumia madaraka yangu niongeze muda wa 30, tufanye kazi ya kibunge. Hii kazi ya leo ni muhimu sana. Sasa nataka niwahoji, kwamba badala ya kutumia kuchangia kwa dakika 15 kila mmoja wetu mtakaopata nafasi, kwa kuwa mko wachache, mnaonaje kama tutachangia kila mmoja wetu kwa dakika saba?

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoaja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Sasa wachangiaji tulionao hapa nataka tuelewane. Waheshimiwa tulionao hapa, tutatumia muda huo kidogo tulionao. Tutaanza na Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Serukamba, atafuatiwa na Mheshima Stephen Masele na Mheshimiwa Kasuku Bilago. Muda ninavyouona, hatutafika, lakini tuone, maana nusu saa nitaiongeza lakini tutafika tu. Tuanze na hawa watatu.

Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER. J SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza na naomba kwanza niishukuru Serikali kwa kuleta muswada huu. Kipekee kabisa namshukuru Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma historia ya muswada huu, ilianza mwaka 2004 huko, lakini wote hawakufanya *decision* hii, Rais huyu amechukua maamuzi haya magumu lakini maamuzi mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilitaka kusema kwamba sheria hii tunayotunga leo, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, *guarantor* ni Serikali, tusije tukasahau hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kusoma *standard* za *ILO*, *minimum* ya pensheni ya *ILO* ni asilimia 40; Ulaya Magharibi ni asilimia 42 mpaka asilimia 74; Ulaya Mashariki ni asilimia 46 mpaka asilimia 63. Latin America ni asilimia 46 mpaka 77; Tanzania kwa wale ambao labda hawajui ni kati ya nchi chache zenye kiwango kikubwa sana cha pensheni. Tanzania ni asilimia 72.5. Tumewazidi wengi katika *continent* hii. Naipongeza sana Serikali kwenye hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeamua kusema hili kwanza? Nataka tuelewane, sisi Kamati tumewaomba Serikali wako wachache watesema *otherwise*, lakini *unanimously* Kamati tulisema *formula* iwekwe kwenye kanuni. Sababu zetu ni moja, mbili, tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza, tumesema watakapotunga sheria hii wakafanya *actuarial valuation*. *Actuarial valuation* inafanywa na *SSRA*, siyo na mifuko yenyewe. Huweze kumwambia mtu aku-*access* wewe mwenyewe. *Regulatory* akafanye hiyo kazi, *access* hiyo mifuko, baada ya pale wakutane kwenye utatu mtakatifu, waweze kuandaa *formula* na lazima *formula* hii iwezeshe mifuko hii kuendelea kuwapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya maamuzi haya kwa sababu ya kutatua matatizo tuliyokuwa nayo ili wafanyakazi wa Tanzania wasipate shida. Kwa hiyo, bado naomba Serikali ifanye kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nimemsikiliza dada yangu wa upinzani, aliyekuwa anasoma, nadhani hajasoma muswada huu mpya. Serikali imeamua haitahamisha *member* yeyote. *Members* watabaki kule walikokuwa. Wanasheria wenzangu mnajua, hatutungi *retrospective law*. Waajiriwa wapya ndio watakwenda kwenye hiyo mifuko mipya. Hii ni kwa sababu ungewahamisha leo, unawahamisha na *contribution*, *investment* zao unafanyaje? *Liabilities* zao anabaki nazo nani? Kwa hiyo, ilikuwa ni lazima wabaki, halafu tuweke *cutOff*, wale wanaokuja mbele, wataingia kwenye sheria hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa *SSRA*, watu wanaweza wasilione, ndiyo maana tumependekeza mifuko yote ya hifadhi ya jamii iwe chini ya mtu mmoja, *NHIF* iende huko, *CHF* iende huko na mifuko yote ili kuwe na *regulator* ambaye anasimamia shughuli hii. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya mfuko wa jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tumelisema kwenye kamati na naomba *personally* niliseme, ni suala la Makatibu Wakuu. Makatibu Wakuu ndio Maafisa Masurufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe umekaa Serikalini; kwa kweli niwapongeze kwanza hata hao Makatibu Wakuu na watu wa Serikali. Maana wangukuwa wanajifikiria wao, wasingelela hii sheria. Kwa sababu sheria hii ilikuwa inawa-*benefit* wao, hasa waliokuwa kwenye *PSPF*. Kwa sababu ya kuangalia mbali, kuangalia Taifa, wameileta hii sheria. Naomba sana Makatibu Wakuu wenyewe hawafiki 20. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea yule ambaye amefanya kazi mpaka siku ya kustaafu ni Katibu Mkuu. Hawa ndio wanatunza pesa, *otherwise* tusipowa-*consider*, naomba Serikali mkatafakari, wataanza kujitafutia pensheni yao pembeni. Tunazuia haya, maana haiwezekani mimi ni Katibu Mkuu, aliye chini yangu amekuwa *taken care*, bado hatueleweki.

Naiomba Serikali iende kulitafakari namna tunachoweza kufanya kuhusu Makatibu Wakuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu umesema tupunguze muda, ukiangalia sheria hii, kwanza naipongeze Serikali kwa sababu karibu *amendments* zote ambazo Kamati tulitoa, kwa kweli zimeingizwa. Unaweza ukaona aliye na ule muswada wa Oktoba na huu, tofauti ni kubwa sana. Serikali imeanzisha mafao mapya, lakini imehakikisha mafao yanayotolewa mifuko yote ni sawa, lakini *under section 29* inasema, bodi ikiona inataka kuanzaisha fao lingine, wao ndiyo wataangalia wataweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la wale waliokuwa wana-*benefit* hasa kwenye fao la elimu. Kama Serikali inaona hilo fao hapana, naombeni wale watoto ambao wazazi wao labda hawapo, ni maskini, wamefariki, waliokuwa wanasomeshwa kwenye *arrangement* hizo, tusiwaache barabarani. Wale ni watoto wa Tanzania, twende tuhakikishe mifuko hiyo inayowachukua, iende iwafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naiomba Serikali ihakikishe inasimamia wafanyakazi wote wasipoteze ajira zao. Naamini wakifanya *job evaluation*, wakaangalia mifuko yote miwili, wakaangalia *NHIF*, wakaangalia *Workers Compensation*, bado unaweza ukawa-*rearrange* wafanyakazi walioko kwenye hii mifuko yote na kila mtu akapata kazi na kama Taifa tukaenda mbele. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na niwaomba Waheshimiwa Wabunge, tunaandika historia, tunatunga sheria ambayo itafanya hifadhi ya jamii Tanzania iendelee kuwepo kwa muda mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka niliyonayo naongeza muda wa nusu saa kuanzaia saa 7.00 mchana hadi saa 7.30 mchana ili tuvutevute wachangie na wengine. Mheshimiwa Masele atafuatiwa na Mwalimu Bilagoni na Mheshimiwa Zitto ajiandae.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. Kipekee kabisa, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Manaibu Waziri, kwa kuwa wasikivu na kupokea ushauri ambao sisi Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiutoa kwa Serikali kupitia Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza mambo mawili; la kwanza, maamuzi ya Serikali ya kuiacha *NSSF* ku-*deal* na

private sector pamoja na *informal sector*. Utafahamu kwamba kwa *population* ya Tanzania, Watanzania wengi wako kwenye *informal sector* na wengi hawaratibiwi na mfuko wowote. Kwa hiyo, maamuzi haya yanaifanya sasa Watanzania walio wengi ambao wako kwenye *informal sector* kupata fursa ya kuratibiwa na mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama kabisa *NSSF* iki-*deal* na *informal sector* itaweza kutoa mafao ambayo yatawanufaisha Watanzania wengi ambao ni wanyonge na ambao hawana uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sheria hii, wale watumishi ambao ni wa Serikali na walioko kwenye mifuko hii ambayo tunaiunganisha kupitia Muswada huu ambao tutatunga sheria, watafaidika na mafao mengi ambayo yako kwenye *minimum requirements* za *ILO*. Mimi nitajielekeza sehemu moja hasa kwenye *section number 29* ambapo kuna orodha ya mafao ambayo yapo kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama orodha hii, kuna fao la matibabu halipo. Vilevile ukitazama kwenye sheria iliyoanzisha *NSSF*, tukiichukulia kama ni *standard*, fao lile lipo. Sasa nilikuwa naomba kushauri Serikali...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masele, samahani niko hapo kwenye *section 29*.

MHE. STEPHEN J. MASELE: *Section 29*, ukiangalia pale *subsection (1)(a)* “*retirement benefits, survivors benefits, invalidity benefits, maternity benefits, unemployment benefits, sickness benefits and death gratuity.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza Serikali ilete *amendments* iongeze *medical benefits* ama *health insurance benefits* ili watumishi wa umma ambao watakuwa wakichangia kwenye mfuko huu mpya tutakaouanzisha waweze kunufaika na fao hili moja kwa moja bila kuchangia tena kwenye *NHIF*. Ziko hoja

zinazungumzwa kwamba Watumishi Umma wote watakuwa wananufaika na *health Insurance* kupitia *NHIF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizama kwa makini, unaona kwamba watumishi hawa wa Umma watakuwa wanachangia mara mbili; wanakatwa kwenye *NHIF* ili waweze kupata huduma, lakini kwa kuwa wao wako chini ya mfuko huu, pia watakatwa huku ambapo wakikatwa huku, moja kwa moja wana-*qualify* kupata huduma ya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naishauri Serikali, ilete mabadiliko hapa, iongeze *medical insurance*; na kupitia kukatwa huko kwa watumishi wa umma, huu mfuko sasa upeleke hizo fedha kule *NHIF* ili ukagharamie matibabu ya wanachama ama *members* ambao watakuwa ni wanachama wapya wa mfuko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewaondolea wanachama ama Watumishi wa Serikali ama watumishi wa umma kuchangia mara mbili. Hivi ilivyo, watakoachangia kwenye mfuko huu watakuwa wanakatwa na upande wa *NHIF* ili wale *members* pia watakatwa. Kwa hiyo, mtumishi huyu atakuwa anakatwa mara mbili kwa jambo lile lile ambalo anaweza kulipata kwa kuchangia katika mfuko huu ambao tunatunga sheria leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naishauri Serikali na ninaamini Mheshimwa Waziri na Mwanasheria Mkuu, watalizingatia hili, walete mabadiliko ili tuweze kuwaondolea michango ya mara mbili watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ulikuwa umeegemea hapo. Naomba niunge mkono muswada huu, naomba Serikali izingatie maoni haya ili kuwaondolewa mzigo watumishi wa umma. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Masele kwa mchango wako mzuri, una mantiki. Acha Serikali iuangalie

kwa undani zaidi. Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Bilago, Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Benardetha Mushashu.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. Kwanza ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kwa hiyo, nimeusoma muswada huu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote katika yote, ili tuutendee haki muswada huu ni lazima kikokotoo kiingie kwenye kanuni. Kama kikokotoo hakitaingia kwenye muswada huu kikaenda kwenye kanuni, Mheshimiwa Waziri anaweza akaja na yake ambayo hayatakuwa na maslahi kwa wafanyakazi waliokuwa wakiyapata kwenye mifuko iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kufutwa kwa *full pension*, ile tafsiri ya *full pension* ni baada ya kuona kikokotoo cha 100 kwa 580 kinapigiwa kelele hakikubaliki kubaliki. Kwa hiyo, ikaonekana kiondolewe halafu eti mtu akafanya *actuarial valuation* ndiyo aweze ku-*determine* kikokotoo, ni hatari sana. Mfanyakazi hawezi kuingia kwenye *scheme*; unamwingiza mfanyakazi kwenye *scheme* hajui mwisho wa siku atanufaikaje na *scheme* hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu kiwe *in black and white* kwenye sheria. Hizi sheria tunazo-*merge* zote zilikuwa zina *formula*. Kabla hujajunga unaangalia *formula* ya PSPF inanifaa kwa kiasi gani? *Formula* ya NSSF inanifaa kwa kiasi gani? *Formula* ya PPF, kwa hiyo, mfanyakazi anasema *should I go to PSPF or NSSF or PPF?* Baada ya kuona maslahi yanayo muhusu. Sasa tukienda kuficha kwenye kanuni, halafu sheria iwe kimya kabisa, haina mafao yoyote, haionyeshi mwisho wa siku itatusaidia nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili halileti afya na kama Waziri anaona, ili kikokotoo kifahamike ni baada ya *actuarial valuation*, alitakiwa afanye *actuarial valuation* ndiyo alete hoja ya kuunganisha kwamba hawa nimewaona

wakiungana, nimeridhika kwamba watakuwa na afya ya kutosha kunufaisha wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuja unaunganisha ambapo hujui kwamba baada ya *actuarial valuation* watakuwa na afya kiasi gani? Ukikuta baada ya kuungana, hali zao ni mbovu, ni mbaya kabisa, tutarudi humu tena kuja kushughulikia hii kitu? Kwa hiyo, hilo naliomba kabisa Waheshimiwa Wabunge tukubaliane, tusipitishie sheria ambayo iko kimya, yaani hata leo tukitoka, unakwenda kumuuliza mwenzako ambaye ni mfanyakazi aliyeko nyumbani, hivi tutafaidikaje na huu mfuko? Nikistaafu nitalipwa bei gani? Huwezi kumwambia bei atakayolipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna hii *cutoff point* ambayo inataka wafanyakazi waliokuwa katika sekta fulani wabaki huko tu-*board* na hawa wapya kwenye mfuko huu mpya. Basi ikiwezekana, vikokotoo vyao walivyokuwa navyo vibaki. Kila watu wa *board in* kwenye mfuko huo na vikokotoo vyao. Kwa hiyo, waliokuwa na 540, waendeleo na 540 yao mpaka watakapo-*phase out*, waliokuwa na 580 nao waingie humo wa-*board in* mpaka watakapomaliza. Kikokotoo kipya kitakachokuja kianze na wafanyakazi wapya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema kabisa ya kuunganisha mifuko hii, tusingahau baadhi ya *benefits* ambazo zilikuwa kwenye mifuko ya zamani. Mfanyakazi aliyekuwa ana-*benefit* kwenye mfuko aliokuwanao tusiipoteze ile *benefit* kwa sababu tu ya kuanzisha mfuko mpya. Mfuko mpya kama tunauanzisha na tunapoteza baadhi ya *benefits*, haina sababu ya kuunganishwa. Kuunganishwa kuboreshe kutoka pale tulipokuwa kwenda sehemu nyingine bora zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fao la elimu limeondolewa wakati mifuko mingine ilikuwa inatoa hilo fao. Fao la afya (*health insurance*) nalo linaondolewa wakati lilikuwepo. Sasa hivi vitu tusipoviangalia vitatuletea

confusion. Sasa mtu anajiuliza, huu mfuko mpya unanifaa kweli au haunifai? Kwa sababu hata kuwa na *option*, yaani ni kama tunatengeneza kitu ambacho utake, usitake utaingia tu. Kwa hiyo, hiki ni kitu cha hatari sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19 ambacho kimtoza *fine* anayechelewesha makato, mwajiri ambaye amechelewesha makato. Tukubaliane ile *fine* inayotozwa imnufaishe na mfanyakazi yaani *at the end of the day* wanapo-*calculate* mafao yake, waangalie tulinfuikaje na *fine*? Iliwe *fine* tu inaunufaisha mfuko halafu *member* hatanufaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18(2) kwenye (b) pale, kuna mahali ambapo tunazungumzia viwango vya kutoza, asilimia tano kwa mfanyakazi na asilimia 15 kwa mwajiri. Pale chini pamesema hivi, baada ya kusoma (b): *“or such amount as the Minister may by order published in the Gazette determine taking into consideration of the actuarial valuation.”* Maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku watafanya *actuarial valuation* waone labda mfuko una afya mbaya, Waziri akaamua kuongeza makato. Inawezekana, yaani hii inampa *room* Waziri kuongeza makato wakati tulishaweka kwenye sheria ni 5% by 15% ya Mwajiri. Hivi kwa nini tusiondoe hiki kifungu? Yaani kila siku akiamka tu akiona mifuko ina afya mbaya, anakwenda kuongeza makato. Mfanyakazi anaishi bila ya kuwa na uhakika atamaliza anakatwa kiasi gani? Kama ni 5% ibaki 5% na 15 ibaki 15. Kama anaiongeza, aiongeze kwa mwajiri, Mtumishi abaki na ile ile ya kwake. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Zitto Kabwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mashashu.

MHE. ZITTO Z. R. KABWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia muswada huu muhimu sana. Nadhani katika mambo ambayo tunaweza

tukasema kwamba tumeyafanya katika Bunge hili la Kumi na Moja ni pamoja na muswada huu kwa sababu ni Muswada ambao una mabadiliko makubwa sana ambayo tunakwenda kuyafanya katika mfumo mzima wa hifadhi ya jamii ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja la jumla ambalo napenda nilizungumze, ni kwamba hapa tumekaa tunazungumzia jambo la 9% tu ya *work force* ya Tanzania. Kwa sababu mfumo wetu wa hifadhi ya jamii katika nchi yetu unagusia watu tu ambao wameajiriwa katika sekta rasmi ambao ni watu 2,100,000. Watu 700,000 walioajiriwa na Serikali na Mashirika yake na watu 1,400,000 ambao wameajiriwa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja huko siku za usoni tunakokwenda tujaribu kuona ni namna gani ambavyo tutakuwa na utekelezaji wa kisera na kisheria katika hifadhi ya jamii ili tuweze kuwafikia Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii napenda kutoa mfano huu sana kwa watu wa korosho. Leo hii korosho ine bei nzuri sana na wananchi wamepata fedha nyingi sana, lakini kesho na keshokutwa bei ya Soko la Dunia ikiporomoka, watu watalia kwa sababu hatuna mfumo wa hifadhi ya jamii kwa wakulima ambapo tungeweza kuwapa wakulima fao la bei pale ambapo bei zimekuwa zimetetereka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo la msingi sana ambalo ni lazima tulitazame lazima tuondoke kuzungumzia 9% ya watu, tuje kuzungumzia Watanzania wengi zaidi ambao hawaguswi kabisa na *schemes* za hifadhi ya jamii ambazo tunazo katika nchi yetu hivi sasa

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo napenda kulizungumzia, limegusiwa kidogo na Mheshimiwa Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini kuhusiana na *SHIB* (Fao la Matibabu). Katika sheria hii mpya kuna hiyo *provision* ya *sickness benefit* ambayo ndani ya sheria haijaelezwana inakuwa namna gan? Kwa sababu ni miongoni mwa vifungu viwili

ambavyo Serikali inasema Waziri na *SSRA* watavitolea ufafanuzi wakati mafao mengine yote ndani ya sheria yamewekewa ufafanuzi wa namna gani ambavyo itatekelezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kustaajibisha kidogo, ukienda kwenye *consequential amendments* ambazo Serikali inazo ndani ya muswada huu, *section 97*, Serikali inafanya *amendment* ya Sheria ya *NSSF*. Sheria ya *NSSF section 21* inatoa *health insurance benefit* kwa wanachama wa *NSSF*. Sheria hii ambayo Serikali inaileta hapa, inaondoa *health insurance benefit* kwa wanachama wa *NSSF*. Hili ni jambo la hatari, kwa sababu sasa hivi *NSSF* ina zaidi ya wanachama 600,000. Kwa hiyo, Serikali hii inakwenda kutunga sheria kuwaondoa watu 600,000 kwenye takwa la kisheria la *health insurance*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa mkanganyiko ambao Serikali imeupata kwamba inataka *health insurance* zote ziwe *provided for* na *NHIF*, inaeleweka. Tunachopaswa kukifanya kwenye sheria ni kuweka *provision* inayosema kwamba fao hilo la *health insurance* litatolewa na *NHIF*, kwa *NSSF* kuchukua ile michango ambayo imefanyiwa mahesabu na *actuarial* kwamba ni *percent* ngapi ya michango ambayo inalipia *health insurance*, michango ile ipelekwe *NHIF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiwa na kadi ya *NSSF* wewe ni mwanachama wa *NSSF*, *automatically* unakuwa mwanachama wa *NHIF*. Hii ndiyo njia bora zaidi ambayo Serikali ilipaswa kufanya na inapaswa kufanya. Nawashauri Waheshimiwa Wabunge, kama *amendment* hii haitaletwa, tusiipitisha sheria hii kwa sababu tunakwenda kuwaondoa watu 600,000 kutoka kwenye *health insurance*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu ambalo ni vizuri pia Serikali ifahamu kufuatia hoja ambayo Mheshimiwa Bilago, Mbunge wa Kakonko amezungumza kwamba tunapotunga Sheria za Pensheni, wale ambao tayari wanafaidika na sheria sasa hivi, hawapaswi kufanywa kuwa

worse off. Wale wapya ambao wanaingia wakati sheria inatungwa, ndio wanapaswa kuendana na yale masharti mapya. Kwa hiyo, ni muhimu sana jambo hili liweze kueleweka vizuri ili tusiweze kuwafanya watu wetu kuwa katika hali mbaya zaidi badala ya kuwaboresha zaidi. (Makofi)

Jambo la mwisho na ambalo limezungumzwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ni jambo ambalo sisi kama Taifa ni lazima tuli-*face*, hatuna namna ya kulikwepa kama ambavyo tumelikwepa kwa miaka minne iliyopita, ni hiki kinachoitwa fao la kujitoa au kujitoa kwenye mafao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nje vijana wengi sana wanataka fao hili liwepo kwamba hiyo ni *innovation* ambayo ipo Tanzania. Inaeleweka kabisa dhamira ya Serikali yoyote, dhamira ya dola yoyote ni kujenga mazingira ambayo una mfumo madhubuti wa hifadhi ya jamii. Mfumo ambao hautakufanya baadaye uwe na wazee ambao hawana *pension*. Lazima ujenga hayo mazingira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuja na *innovation* ya *unemployment benefit*. Tumejadili sana hii kwenye Kamati na Serikali imeongeza kifungu cha 35 kuifafanua. Maelezo ambayo Serikali imetupa ya kwamba wafanyakazi ambao wanatoka kwenye mafao, ambao wamekosa kazi walipwe asilimia 33 ya mshahara kwa muda wa miezi sita. Baada ya miezi sita fedha ile inayobakia iingie kwenye *supplementary scheme*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maelezo ambayo Serikali imeyaeleza kwenye Kamati, haijayaweka kwenye sheria kama mafao mengine namna ambavyo yamefafanuliwa kwenye sheria, ila ndiyo maelezo ambayo tumepewa na masharti yamewekwa kwenye *section* 35. Mimi nadhani tulitazame hili jambo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inalazimisha Mwajiri kuchangia asilimia 10 ya mshahara wa mfanyakazi kwenye mfuko...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Benardetha Mushashu, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

MHE. BENARDETHA MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi Wakuu wa mifuko kwa kuandaa na kutuletea huu muswada. Naipongeza sana Serikali, nimeangalia huu muswada waliotugawia leo asubuhi, naona wamezingatia maoni ya wadau pamoja na marekebisho makubwa yaliyofanywa na Kamati. Ahsanteni sana Serikali kwa kuwa wasikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu unalenga kuunganisha hii mifuko yote mitano tukabakia na mifuko miwili, mmoja wa Umma na mwingine wa binafsi kwa lengo la kuboresha mafao ya wafanyakazi. Kwa hiyo, ni kitu kizuri, nakiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Ibara ya 18 ya muswada huu inayozungumzia michango kwamba mwajiri atachangia asilimia 15 ya mshahara na mwajiriwa atachangia asilimia tano; lakini ukiangalia 18(b) hii imempa Waziri mamlaka ya kuweza kubadilisha viwango kadri atakavyoona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikitokea tukawa na Waziri wakati fulani ambaye hajali wafanyakazi, unaweza ukakuta huyu Waziri ameamua kupanga kwamba *contribution* ya mfanyakazi iende mpaka asilimia 30. Hii inaweza ikawa shida, kwa sababu kwenye mshahara huo huo labda ukute alikuwa ni mwanafunzi anakatwa Bodi ya Mikopo, anakwata *PAYE*, anakatwa na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafurahi kwamba sasa hivi kwenye kipengele hicho wamebadilisha wakasema kwamba mpaka ifanywe *actuarial valuation*. Sasa nataka

nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba hiyo *actuarial valuation* inafanywa kwenye mfuko au inafanywa kwa mfanyakazi aonekane ana nguvu kiasi gani ya kuweza kuchangia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 20 inazungumzia juu ya michango isiyowasilishwa. Hali ilivyo sasa hivi ni kwamba unakuta wastaafu wengi wanapostaafu, wanalipwa mafao kidogo sana kwa sababu michango ilikatwa kutoka kwenye mishahara yao, lakini haikuwasilishwa kwenye mifuko. Katika kipengele cha 20 kimeainisha kwamba huyu mtu sasa awe michango yake imeshawasilishwa kwenye mifuko au haijawasilishwa, mfuko utatakiwa umlipe mafao yake yote na ule mfuko wenyewe ndiyo uendelee kudaiana na mwajiri Hiki ni kitu kizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa napendekeza ilivyoandikwa pale kwenye kipengele cha 20 kinachosema; *“Where the Director General is satisfied that an employee’s contribution has been deducted from his earnings, but the employer has failed to remit the contribution together with the paid employer’s contributions to the fund, he shall treat the unremitted contributions as wholly or partially paid to the purpose...”* Nilikuwa napendekeza neno *“partially”* liondoke pale, linaleta ukakasi kusudi tuhakikishe kwamba huyu mwajiriwa atalipwa mafao yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 29 inazungumzia mafao atakayopata mwanachama; ni mafao saba. Naipongeza Serikali kwa sababu wameweka mafao ya yule ambaye atakuwa amestaafu, lakini vile vile kuna namna ambapo huyu hajafikia umri wa kustaafu, atafaidika. Napenda kuuliza kwamba kuna *invalidity benefits* ambayo inahusu watu wenye ulemavu. Ni kitu gani kitalipwa na hii mifuko ya hifadhi ya jamii na kitu gani kitalipwa na *Workers Compensation Fund*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa *unemployment benefit*, nawashukuru sana kwa kuliweka hili fao. Kwa mara ya kwanza katika Tanzania tutakuwa sasa

tumetoa faraja kwa mtu aliyepoteza ajira. Pia naomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie zaidi, ni kitu gani huyu mtu anategemewa kupata kwenye *unemployment benefit*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 56 inazungumzia juu ya msamaha wa kodi kwenye mafao. Hii ibara imekaa vizuri kwa sababu huyu mtu amehangaika, sasa amefikia kustaafu, ukute na ile *pension* yake ya kila mwezi au ile *gratuity* anayoipata ikatwe kodi. Kwa hiyo, kipengele hiki kimesomeka kwamba huyu mtu hatakatwa kodi. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila ningependa kuona, inaweza ikatokea wakatunga Sheria za Kodi ambazo zinalazimisha sasa kwamba ile *pension* ambayo iko kwenye sheria hii iende kukatwa kodi. Napenda kuona kwenye muswada huu au sheria hii waweke kipengele kinacholinda *pension* ya mfanyakazi kwamba hata zikitungwa sheria nyingine za kodi zisilazimishe *pension* ya mfanyakazi kukatwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa muswada huu ni mapendekezo ya wafanyakazi na mategemeo ya wafanyakazi ni kwamba mifuko hii iunganishwe; gharama za uendeshaji zipungue, kusudi wao waweze kupata mafao makubwa zaidi. Sasa bahati mbaya kikokotoo kweli hakipo kwenye huu muswada na Mheshimiwa Waziri anasema watakiweka kwenye kanuni. Napendekeza kanuni zikishatungwa zipelekwe mbele ya Kamati itakayokuwa inahusika hizi... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Kanyasu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza naomba niwapongeze sana Kamati kwa namna ambavyo

wameutendea haki muswada huu. Nilipousoma mwaka 2017 na nilipokuja kusikiliza marekebicho, nimeona Kamati wamefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri pamoja na Watendaji wote katika Wizara hii. Kama walivyosema wenzangu, kimsingi tunaiona nia ya Serikali ya kuunganisha mifuko hii na kuondoa gharama za uendeshaji kama ambavyo zimetajwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na Mwenyekiti wa Kamati. Kwa hiyo, tunaiona hiyo nia na hilo lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu hapa, nilidhani baada ya Serikali kuondoa gharama hizo ambazo tumeziona kwenye maelezo ya Mheshimiwa Waziri, basi zingekuja chini zikawa na faida kwa mwanachama wa mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyomalizia kusema Mheshimiwa Mama Mushashu, kwa kweli tulitarajia kuona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba mwisho wa siku sasa haya mafao yanakwenda kuongezeka kwa asilimia ngapi au yanakwenda kuimarika kwa asilimia ngapi? Sasa linabaki kuwa kwenye *Pandora box* kitu ambacho nadhani tutahitaji pia baadaye kuanza kuhangaika na Mheshimiwa Waziri. Kwa ujumla wake, napongeze sana, marekebicho yamezingatia sana maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika *section 35* kama walivyosema wenzangu, ni vizuri sana kufikiria kuhusu *medical insurance* na fao la elimu. Hivi tunapozungumza, watumishi wengi ambao walikuwa wamesoma Diploma, hawapati mikopo tena kwenye Bodi ya Elimu na wengi walikuwa wanakimbilia kwenye mifuko hii kwenda kuomba mikopo na baadaye wanakwenda vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokuwa tume-*merge* na tukaliondoa hili kama ambavyo iko sasa, maana yake ni kwamba liko kundi la watu hawatasoma tena kulingana na gharama za elimu zilivyo juu. Kwa hiyo, ni vizuri sana kwenye

section 29 kurudisha fao hili la elimu, kwa sababu mifuko ilikuwa inatoa na wanachama walikuwa wakijunga katika mifuko hii kwa sababu waliona kuna kitu wanakihitaji kwenye mfuko huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naipongeza sana Serikali kwenye *section 43*. Mafao ya wastaafu yalikuwa yanaweza kuchelewa mpaka mwaka mzima na hakuna mtu aliyekuwa anajali. Ninao mfano wa watu ambao nimewasaidia, walicheleweshewa mafao yao kwa zaidi ya miezi sita, miezi nane na wako wengine mpaka leo wanasubiri na hakuna *interest*, wala hakuna mtu aliyekuwa anajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuweka *provision* hii katika *section 42* na *43* maana yake tunaweka *commitment* kwa mifuko hii kuhakikisha kwamba hii miezi sita ya maandalizi na hizi siku 60 zilizotajwa katika sheria wasipolipa wajue kwamba watalipa kwa *interest*. *Interest* haimasaidii sana mstaafu, kwa sababu mstaafu akili yake ikimpelekea kufikiri kustaafu, mara nyingi hufikiri aweze kupata malipo yake na kuendelea na maisha yake mengine. Naipongeza Serikali kwa kuweka *commitment* hii kwa sababu itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mimi natoka kwenye maneo ya wachimbaji na mgogoro wangu mkubwa siku zote umekuwa ni fao la kujitoa. Ninaishukuru Serikali, maelezo aliyoyasema Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Waziri, yanaleta picha kwamba kuna namna inalishughulikia. Hivi tunavyozungumza, wako wafanyakazi wengi walioko kwenye madini ambao wana zaidi ya miaka mitano, ambao wanasubiri sheria hii ili iwafungue namna ya kuendelea mbele, kwa bahati mbaya sana hajjawa *clear* bado. Bado imekuja ikiwa imefumbwa fumbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, wapiga kura wangu wanataka kufahamu sasa hasa wale ambao tayari wako nje wanasubiri

utaratibu kwa ahadi ya Rais aliyoitoa kule Kilimanjaro, ni nini kinafuata baada ya hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimsikia Mwenyekiti wa Kamati anasema kutakuwa na hiyo asilimia 33 kwa miezi sita na baadaye kuangalia kama hakuna tena ajira nyingine, basi mtu analipwa pesa yake, anaondoka. Tulione hili kwenye utaratibu ili liwasaidie watu kuweza kujipanga na maisha yao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tufahamu kwamba tunapoiunganisha mifuko hii tunaondoa ushindani kwa kupunguza gharama, pia kuna madhara ya kuondoa ushindani. Mara nyingi sana huko nyuma kabla ya mifuko hii kuwa mingi, pia hata *customer care* ilikuwa *very poor*. Lazima tulitambue hili kwamba baada ya mifuko hii kuunganishwa, watu watakuwa hawana *option*; wa umma watakwenda huku na wa upande wa binafsi atakwenda huku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa *option* kunaweza kukawafanya watendaji wakalala usingizi. Kwa hiyo, lazima tuweke mfumo ambao utaendelea kuifanya mifuko hii kuendelea kuhakikisha kwamba inajali huduma za *members* wake, lakini pia inatoa huduma kulingana na mikataba ambayo ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, kwa sasa ndiyo tuishie hapo.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana. Kitu ambacho mimi kukaa hapa leo nimejisikia vizuri sana, ni michango yenu wote mmejielekeza kwenye muswada. Mmechangia ya jumla, lakini unakwenda kwenye Muswada, kwa sababu katika hatua hii ndiyo muhimu sana. Tutakapoingia sasa kwenye Kamati ya Bunge Zima, *issues* zote ambazo mlidhani kwamba Serikali ipate nafasi ya kuziona, zimo kwenye muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge wote, nawashukuruni sana mliopata nafasi ya kuchangia. Ni matarajio yangu na wengine watakaofuata wachache ambao watapata nafasi jioni na wenyewe wafuate nyayo hizi. Hizi ndiyo shughuli za Wabunge, tunapofika kutunga sheria. Nawashukuruni sana kwa hilo.

Sasa baada ya kusema hayo, sina matangazo, lakini niwatangaze tu wale ambao tutaanza nao mchana ili wakajiweke vizuri. Tutaanza na wawili wa mwanzo, kwa sababu tutashauriana na Serikali kwa jinsi ya muda nitakavyoona saa 11.00, lakini kwa uamuzi tuliochukua wa dakika saba, ile saa moja itatupatia kama wachangiaji nane. Siyo haba lakini tutaona.

Sasa niwataje tu hawa wa mwanzo; tutakuwa na Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Mtolea na Mheshimiwa Pascal Haonga. Tuanze na hao, halafu tutaona baadae.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.30 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimewataja wale tutakaoanza nao. Tunaanza na Mheshimiwa Allan Kiula, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Mtolea na Mheshimiwa Pascal Haonga. Tutaona muda unavyokwenda.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia muswada huu muhimu. Pili, naipongeza Wizara na watendaji wote waliofanyia kazi Muswada huu kwa sababu umekuja kwa wakati muafaka

kabisa. Kwa hiyo, wale wanaoona kama ungeahirishwa au haujatimia, mimi nasema muswada huu umetimia na ndiyo wakati wake kuwasilishwa na ninasema umechelewa sana kuletwa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, lakini yako mambo kadhaa ambayo inabidi tuyaangalie sisi kama Bunge na kuyatolea maamuzi. Mambo mengi yameshazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, lakini nami nitajazia baadhi ya sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *section 19* inazungumzia suala zima la mwajiri kama atakuwa hajapeleka michango, yaani fursa ya mwajiri kutokupeleka michango. Uhalisia sasa hivi ni kwamba inapotokea hali kama hii uyo mfanyakazi ambaye amestaafu anastahili kulipwa mafao yake, huwa anapata shida kubwa. Kwa hiyo, hatutakiwi kutoa nafasi au fursa ya mwajiri kuchelewesha michango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sheria ingesema tu kama mwajiri anatakiwa apeleke michango kwa wakati inapo-*fall due*, basi, tukaishia hapo hapo. Kwa sababu nafahamu kwamba kwenye mifuko wako ma-*inspector* ambao ndio kazi yao kufuatilia michango hii. Kwa hiyo, siyo kazi ya mwanachama kufuatilia mchango. Kwa hiyo, hilo ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipengele namba 22 kinasema: "*money paid in excess.*" Hili lilivyoingia tu kidogo lilinipa ukakasi, kwa sababu kama sasa hivi tuko kwenye mambo ya teknolojia (*IT*), kwa nini michango iende *in excess* halafu tuanze kuangalia inarudishwa kwa utaratibu upi? Kwa hiyo, hili jambo lingeweza kuangaliwa kwa sababu wao wanaopeleka michango wanatakiwa wawe makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo lingine kwenye kuunganisha mifuko ambalo na lenyewe lipo lakini sijaliona vizuri, labda Waziri mhusika atalifafanua. Wako wafanyakazi ambao walikuwa wafanyakazi, wameshachangia kwenye mifuko hii inayounganishwa, lakini sasa hivi sio wafanyakazi

na hawachangii, lakini pesa zao bado zipo kwenye mifuko na hawajachukua. Walikuwa wanasubiri muda wa miaka 60 au 55 waweze kudai mafao yao. Sasa sijaona kwenye *transition* au hili jambo litakuwa *handled* vipi? Wako wengi sana wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ile *section 29* inayozungumzia ile *list* ya mafao, Waheshimwia Wabunge wameshazungumza suala la *health benefit*, ni jambo muhimu sana likawekwa. Bunge hili lisikubali kupitisha sheria hii kama hilo jambo halitawekwa, kwa sababu jambo hilo ni muhimu na tumeona faida zake na wananchi wanahangaika. Mifuko mingine ilianzisha *involuntary contribution*, lakini kwenye *involuntary contribution* watu wanapata mafao na limeweza kusaidia sana Watanzania. Kwa hiyo, ni fao muhimu na ambalo ni muhimu likawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuunganisha mifuko, huko nyuma tulizungumza kwamba litapunguza gharama za uendeshaji. Kwa maana hiyo tulitarajia kwamba gharama zilizopungua na wanachama wakiwa *pooled* kwenye mfuko mmoja, kutakuwa na ongezeko la kuondoa michango na kwa sababu michango hii itawekezwa ina maana kutakuwa na ongezeko la uwekezaji. Kwa hiyo, mafao kama *health benefit* na mengineyo, fao la elimu wamezungumza, ni muhimu yakawekwa kwa sababu ni jambo ambalo linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muswada huu umezungumzia suala la kwamba mafao hayatatozwa kodi. Sheria ya Kodi (*Income Tax Act*) *section 10 (3)* nafikiri inaeleza kwamba iwe ina-*override* mambo yote. Kwa hiyo, jambo hili labda Mheshimiwa Waziri aliweke vizuri ili atuhakikishie kwamba kodi haitatozwa kwenye mafao ya mwisho. Ni rahisi tu, ni kuongezea pale kwamba "*not withstanding*", tunaongezea maneno pale, mambo yanakaa vizuri. Kwa sababu ni matarajio kwamba kwa kuunganisha mifuko, kutakuwa na manufaa zaidi na ndiyo imani ya Wabunge kwamba kutakuwa na manufaa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ndio ulikuwa huo na ningependa kusesitiza hayo mambo machache. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kiula kwa mchango wako, lakini pia kwa kututunzia muda. Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru, lakini namshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu ya kusimama hapa na kukupa nguvu wewe ya kuniona na kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo katika Muswada ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli zilikuwa kelele zetu za muda mrefu sana kutaka marekebisho haya yaje ili tuweze kufanya maboresho katika hii mifuko ili Watanzania walio wengi wale ambao wapo katika ajira waweze kuona mwanga wa maisha yao ya kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulihitaji kweli kupunguza utitiri wa mifuko, lakini tulihitaji kuboresha maslahi yaliyomo kwenye mifuko iliyopo. Sasa tungeweza kuipongeza Serikali kwa kuleta muswada, lakini kuuleta muswada peke yake bila kuzingatia vile vilio vyenyewe vilivyokuwa vikipigiwa kelele na sisi Wabunge kwa niaba ya Watanzania, haisaidii sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuja kugundua kwamba kuna mafao mapya ambayo yanaanzishwa, lakini kuna mafao ya muhimu yaliyokuwepo yameondolewa. Sasa hili siyo jambo jema sana, kwa sababu lengo ilikuwa ni kupunguza malalamiko ya watu. Sasa huwezi kupunguza malalamiko ya watu kwa kuondoa vile vitu vizuri ambavyo vilikuwa vikiwagusa katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona hapa limeondolewa lile fao la afya (*health benefit*). Utagundua kwamba katika kipindi kilichopita ambapo fao la kujitoa lilikuwa limeondoka, wanufaika hawa walikuwa angalau wanaenda wanapata

ile huduma ya afya. Sasa hivi hilo fao limeondolewa, kinaletwa kitu kinachoitwa *unemployment benefits* ambayo na yenyewe inaelea juu juu, hujui mtu huyu mnufaika atapata kitu gani? Unaambiwa kwamba kujua ni namna gani itakokotolewa, Waziri atakuja kutunga *regulations*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndio wenye kazi ya kutunga sheria na siyo vizuri tukatunga sheria ya kumruhusu Waziri aende akatunge sheria. Tunatakiwa tumalizie hapa, tuwekewe hiyo hesabu ya kukokotoa ili tujue mtu akiwa amepoteza ajira, wakati anatafuta ajira, anapata kiasi gani? Tunajijua wenyewe, ukiiacha tu hivi na kusema Waziri atatunga *regulations*, inaweza kuchukua miaka mitatu au minne hapa hiyo *regulation* haijatungwa. Tuna hiyo mifano. Sasa hapa hata ile kazi yetu ya Kibunge ya kutunga sheria yenyewe haikamiliki katika kuweka mafao ambayo yanaelea kiasi hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kifungu cha 31(2) kinatambua kwamba kuna Mtanzania kwa namna moja au nyingine atalazimika kuondoka hapa nchini, ama ataacha kazi au atapata kazi kwenye nchi nyingine na sheria inatambua kabisa kwamba mtu huyu anaweza akaenda akarudi au akaenda asirudi. Mnatuletea hiyo *special lump sum benefit* na yenyewe ni kiasi gani? Mtu kama anaondoka nchini, bado unataka akuachie hela yake, ufanye nayo nini? Kwa nini humpi hiyo hela yake akaondoka nayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaona muswada umekuja na mambo mengi ambayo hayajakamilika, yaani vitu viko nusu nusu. Miswada ya namna hii kwa kweli haitusaidii. Vilevile inatunyima fursa na sisi kama Wabunge kuitunga sheria ambayo tukimaliza tu, Mtanzania atakuwa anaguswa moja kwa moja. Sasa hata tukishaipitisha hii leo hapa, bado kazi kubwa anaachiwa Waziri. Kwa hiyo, sisi tunakuwa bado hatujafanya ile kazi yetu ya kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ukienda kwa mfano pale kifungu cha 57(1) kinasema hivi, kwa ufupi tu nikisome. Anasema: " *The board shall at interval of three year*

or at any other intervals... "sitaki kuendelea huko. Hivi ukisema "the body shall", halafu unasema *at interval of three year or any intervals*;" sasa hapo "shall" ilikuwa na kazi gani? Kwa sababu unapoweka "shall" ni lazima ukasisitize lile jambo, lakini kumbe jambo lenyewe bado linaendelea kubaki ni *discretion* ya mtu ambaye atafanya hayo maamuzi. Kwa nini tunatumia "shall"? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmekwenda mbali zaidi mkaongeza kifungu kingine cha 57(2), mnazidi kusisitiza hilo hilo kwamba kumbe hii *actuarial valuation* siyo jambo la msingi kwenu. Sasa kama siyo jambo la msingi, kwa nini mnalirudia, mnaliandika halafu mnalitoa? Mngechagua moja au kuliweka au kutoliweka kuliko kufanya namna hii. Maana yake hapa tutaonekana sasa kama tumekuja kupitisha mafao ya kijanja kijanja hivi, jambo ambalo siyo zuri kwa Bunge letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri, hiki kifungu, maana yake hata kwenye *drafting* tu ya mambo haya ya kisheria hapa inatudhalilisha. Kwa hiyo, mnaweza mkaenda kuifanyia marekebisho au mkaondoa kabisa hiyo *sub-section two*, kama hamtaki ku-*edit* hiyo *sub-section one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kusisitiza kwamba kitendo cha kutokuwa na kikokotoo katika Muswada huu kimeondoa ile maana nzima ya sisi kuja kutunga sheria na kuwasaidia hao wanufaika wa hii wa mifuko ili wajue ni kitu gani watakipata baada ya kuwa wamepoteza ajira kabla ya kutimiza hiyo miaka 50. Fao lao la kujitoa bado linahitajika sana na kelele za Watanzania katika hili hazitaisha. Nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nakushukuru kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Pascal Haonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ninaomba na mimi niweze kuchangia muswada wa kuunganisha mifuko ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, yale yote ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imewasilisha ni vizuri akayachukua na akayafanyia kazi kwa sababu yana faida kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine kama ulivyotangulia kuzungumza tunapokuwa tunatunga sheria za nchi yetu, ni vizuri basi hata yale ambayo yanatoka kwa mtu ambaye ni wa upande mwingine, ili mradi tu kama yana maslahi mapana kwa Taifa letu, ni vyema tukayafanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niungane na mchangiaji Mwalimu Kasuku Bilago kuhusu ile *formula* kutokuwekwa kwenye muswada huu. Mara nyingi sana wote tunajua kwamba mara nyingi sana kanuni zimekuwa ni kichaka cha Serikali kujifichia. Mara nyingi sana zimekuwa ni kanuni ambazo Waziri peke yake anaenda kujifungia, anaangalia nifanye nini, nadhani siyo sahihi hata kidogo. Kwa hiyo, nashauri kama alivyotangulia kuongea mzungumzaji wa kwanza kwamba jambo hili ni vema basi, kwa maana ya *formula* ingeweza kuweka kwenye muswada na badala ya Waziri kwenda mwenyewe kupeleka kwenye kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mbunge ambaye anashiriki kwenye kutunga hizo kanuni. Sasa Waziri anapokuwa amekosea na yuko peke yake na ukiwa peke yako ni rahisi kukosea, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba tu ni vizuri ingeweza kuletwa *formula* hapa tukajadili kwa pamoja, tujue sasa hawa wastaafu wetu watanufaika vipi tuweze kujadiliana kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu jambo lingine kwamba hata ile *denominator* ambayo inatumika kwa sasa ile 540 kwa 580 bado unaweza ukaona kwamba siyo nzuri kwa wastaafu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo 540 ipo tangu kipindi cha ukoloni, ni ya muda mrefu sana. Kwa hiyo, kama lengo

ni kui-merge mifuko hii ili kuboresha mafao ya wastaafu, basi ingekuwa ni vema tungeboresha hata tuweke *denominator* ya 520. Tukiweka *denominator* ya 520 wastaafu wetu watanufaika vizuri, watapata *pension* ya kutosha na mwisho wa siku tutakuwa angalau na sisi tumeingia historia ya kutengeneza ya kwetu kuliko ile ambayo tulitengenezewa na Wakoloni miaka hiyo ambayo ni 540 ambayo siyo nzuri, inawanyonya watumishi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, nashauri hapa Mheshimiwa Waziri katika jambo ambalo ukilifanya naamini utakuwa umetendea haki Watanzania ni pamoja na kuweka hii *denominator* 520 ambayo itakuwa ni jambo jema na wastaafu wetu wataenda kupata *pension* ya kutosha na mwisho wa siku wataishi bila *stress* hapo watakapokuwa wamestaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni jambo ambalo linahusu wale watumishi ambao wako kwenye mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii. Huyu Mheshimiwa Waziri anahusika na mambo ya kazi na ajira, siyo ajabu kesho na keshokutwa akaleta tatizo lingine la ajira. Kwa sababu hawa watu wameajiriwa kwenye mifuko mbalimbali, atakapokuwa ana-*windup* atuhakikishie hapa kwamba je, wale ambao wameajiriwa kwenye mifuko mbalimbali watachukuliwa kupelekwa kwenye mfuko mpya, hii mifuko ambayo itakuwa imeunganishwa? Kwa sababu tusipolichukulia vizuri hili, mwisho wa siku wale wote walioajiliwa watakuwa wamepoteza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye kupoteza ajira, tunaweza tukapoteza watu wengi sana. Kwa mfano, ukichukua *PSPF*, iko karibu kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ngazi ya mkoa kuna mtu mmoja anaitwa Afisa Mfawidhi, pia kuna kuna mwingine anaitwa Afisa Mfawidhi Msaidizi na kuna madereva. Sasa hawa wapo kwenye kila ngazi ya mkoa, je, watawachukua wote hawa kwenda kuwapeleka kenye mifuko mingine hii au ndiyo watakuwa wameshawatelekeza?

Unapowatelekeza maana tafsiri yake ni kwamba badala ya kutatua tatizo, unakuwa umesababisha tatizo kubwa la ukosefu wa ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba baada ya mwanachama kufariki wategemezi watanufaika kwa miezi 36 tu. Sasa jambo hili labda naomba Mheshimiwa Waziri atusaidia mwishoni hapa, *criteria* ipi ilitumika kusema kwamba hawa wategemezi anufaike kwa miezi 36? Kwa nini isiwe miaka mitano? Kwa nini isiwe miaka 10? Kwa nini isiwe miaka nane? Maana yake hii miezi 36 ni sawa na miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri atuambie ni *criteria* ipi ilitumika kuweka miezi 36 na siyo miaka mitano au 10 na kadhalika? Atuambie aliangalia kitu gani? Kwa sababu siku moja nimewahi kumsikia akisema mifuko yetu itafika mahali itakosa fedha za kujiendesha. Sasa kama itakosa fedha na kuna mtu alikuwa anachangia, tusije tukawatesa wategemezi ambao mara nyingi unajua kabisa wengi wanakuwa wanateseka kwa sababu tu watu wao waliokuwa wanafanya kazi wamefariki, tunakuja kuacha miezi 36 tu. Kwa kweli hii naomba tu watusaidie, kwa nini isiwe miaka mitano au 10?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu madeni makubwa ambayo mifuko hii inaidai Serikali. Kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani tumesikia wote kwamba kwa mfano *PSPF* waidai Serikali karibu shilingi trilioni tatu. Sasa kama hili jambo ndivyo ilivyo, hebu tuambiwe vizuri: Je, hii mifuko italipwa hizi fedha kabla ya kwenda kuiunganisha au yale madeni yatahamishwa kutoka kwenye mifuko tuliyokuwa nayo sasa kwenda kwenye ile mifuko mingine ambayo sasa tutakuwa tumeshaipata ile miwili kwa maana ya *PSSF* na ile mingine ya *NSSF*? Kwa hiyo, kama tutahamisha madeni, hiyo pia tutataka tuambiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kama hayo madeni yakihamishiwa kule kwenye mifuko mingine hii mipya, kama

Serikali itaendela kukopa mifuko hii, hii mifuko haita-*survive* kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaangalia utaratibu mwingine wa kutafuta fedha kuliko kwenda kukopa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Inafika muda watumishi wengi wanataka kustaafu, Serikali imeshakopa fedha wanahangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Serikali...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea Mheshimiwa Hawa Mchafu, atafuatiwa na Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Mwita Mwikabwe ajiandae. *(Makofi)*

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya uchache wa muda, niende moja kwa moja kwenye Ibara ya 29 ambayo imeweka orodha ya mafao pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali yangu ione sasa umuhimu ili iweze kuja na *amendment* iongeze fao la elimu. Kwa mujibu wa *ILO, minimum standard* ya haya mafao ni tisa, sisi hapa tuna saba, haitakuwa mbaya sana tukiongeza fao la elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukiacha hivyo, Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, tayari inatoa elimu bila malipo kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne. Kwa hiyo, itapendeza kama mfuko utatoa fao la elimu ili kuweza kusaidia kwa Kidato cha tano na cha sita, mwanafunzi huyu akimaliza, anakutana

na Bodi ya Mkopo kuweza kupata mkopo kuendelea na elimu yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili uko hapo hapo kwenye Ibara ya 29 kuhusiana na *unemployment benefit*. Naipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuja na fao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana nchini kwetu kumekuwa na taharuki au sintofahamu ya *withdrawal benefit*. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuliona hili. Ukichukua ripoti ya Upinzani ambapo katika ukurasa wake wa 12, wao wanavyoona, fao la kujitua linaenda kuchukua nafasi ya *withdrawal benefits*. Hivi ni vitu viwili tofauti, unapuzungumzia *withdrawal benefit* ama fao la kujitua kwanza kwa mujibu wa *ILO*, hakuna fao la kujitua au hakuna *withdrawal benefit*. Kwa wao hilo siyo fao, ukienda kwenye orodha ya mafao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia *withdrawal benefit*, tafsiri au maana yake mwanachama aliyechangia kwa muda wa miaka nane akaja akapata janga la kupoteza ajira, maana yake anaenda kwenye ule mfuko anatoa yale mafao yake. Baada ya mwaka mmoja au miaka miwili, akipata ajira anaenda tena kuanza sifuri ama kuanza moja. Sasa hapo tunamsaidia mwanachama ama tunamuumiza huyu mwanachama? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuja na hili fao la *unemployment benefit* litaenda kuwasaidia wenzetu ambao katikati ya ajira yake amepata bahati mbaya ya kupoteza ajira.

TAARIFA

MHE. HALIMA J. MDEE: Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa tu nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Mchafu, ni muhimu akasoma vizuri taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Kambi Rasmi ya Upinzani hakuna mahali popote kwenye hotuba tulikosema *withdrawal benefit* ni sawa na *unemployment benefit*. Hakuna mahali tuliposema, kwa hiyo, ni muhimu arejee vizuri ili kutokupotosha maelezo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa Mchafu, unaikubali taarifa au unaikataa?

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa yake, achukue ripoti yake, sitaki kupoteza muda, dakika ni saba. Asome mstari wa mwisho. lmeandikwa tu kwa kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kuwapa elimu ya *withdrawal benefit*. Unapoenda kumwambia mtu aka-*withdraw* mafao yake unacho...

MHE. HALIMA J. MDEE: (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Hiyo siyo sababu, nawe umekaa mwaka mmoja *exile* ndiyo maana huelewi nini tunafanya humu ndani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomwambia mwanachama aka-*withdraw* mafao yake aliyochangia kwa miaka nane, unaenda kuumumiza huyu mwanachama. Kwa sababu ili u-*qualify* kupata *pension* ni miaka 15. Kwa hiyo, kama leo ana-*withdraw* mafao yake, akija baada ya miaka miwili akipata ajira, tafsiri yake anaanza sifuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuja na *unemployment benefit*, maana huyu mwanachama ikitokea bahati mbaya amepoteza ajira, kutokana na fao hili, ataenda atalipwa asilimia 33.3 ya michango yake kwa muda wa miezi sita. Ikipita miezi sita ikitokea hajapata ajira, atahamishwa kutoka kwenye *mandatory scheme* atapelekwa kwenye *supplementary* au

voluntary scheme. Ataendelea kupewa michango yake kwa muda wa miezi 18 tukiamini baada ya hiyo miaka miwili atakuwa amepata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu sasa iboreshe tu hapa kwa kuangalia baada ya ile miezi sita na ile miezi 18 ambayo amehamishiwa kwenye *voluntary scheme*, ikitokea amepata ajira, je, tutamrudisha tena kule kwenye *mandatory*? Tukimrudisha, tunaanzaje kuhesabu? Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu ikiweke hicho kifungu kizuri kabisa cha *unemployment benefit* ili kuweza kuwasaidia watumishi wa Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Ibara ya 35. Ibara hii pia inazungumzia suala hili la *unemployment benefit*. Ili tukae vizuri kabisa na tuondokane na hizi kelele za *withdraw*, naona kile kifungu cha 35(2)(e) ambacho kinasema; *“proves to the Director General that he has not secure, another employment.”* Ni ngumu sana kuli-*prove* hili kwamba sijapata ajira. Hili limekaaje? Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*windup*, alitolee ufafanuzi hili ili kuondoa huo ukakasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuzungumze kuhusiana na suala la *formula* kuwepo kwenye muswada huu. Suala la kutumia moja chini ya 520 ama moja chini ya 540 ama 580 hatukurupuki tu kwa utashi wa kiasiasa na tukasema twende tutumie hii. Ni lazima tukafanye *actuarial report*, hii ndiyo itatuongoza tunaenda na mtindo gani ambapo tutaangalia namba ya wachangiaji, namba ya wastaafu, namba ya uwekezaji na kadhalika. Hiyo ndiyo itakayosema tunaenda kwenye *formula* ipi? Siyo tu mtu unaamka unataka ile *formula* ambayo unaitaka wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kinachosemekana kana kwamba Serikali imekuja na *merging as if haijafanya actuarial report, no*, Serikali imefanya. Pengine labda mwende mkasome, mkatafute. Tukienda na hii 100 chini ya 540 maana yake, *contribution rate* iende ikapande mpaka asilimia 35?

Sasa *are we ready* kwa wafanyakazi wetu wachangie kutoka asilimia 20 mpaka...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. *(Makofi)*

Nakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Mbarouk.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Asubuhi wakati unamalizia kipindi cha asubuhi, uliwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuchangia vizuri na ukasema katika utungaji wa sheria ni jambo muhimu sana, ni muhimu watu wakajielekeza kwenye hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kujielekeza huko kwenye hoja, ni pale ambapo mimi kama Mbunge nasema yangu. Tukianza kusema Mbunge wa upande huu ametoa hoja wewe unamjibu kama Serikali, kwa kweli hatuendi mbele. Nadhani hilo ni jambo la msingi sana kuzingatia. Tuache Serikali iwajibu hoja ambazo wamepewa ili watusaidie twende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii sheria, kimsingi huko mtaani na wananchi wetu na hasa watu ambao wanafanya shughuli za kimikataba wanatarajia kwamba sheria hii inapopitishwa leo wapate ahueni ya kupata tiba ya malalamiko mengi ambayo wanayo mtaani kule. Kuna watu ambao wanafanya kazi migodini, wameachishwa kazi, hawana ajira wamekuwa *blacklisted* maeneo mengi wanataka hii suluhu wapate wafao yao waanze maisha mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao wameajiriwa wakamaliza mkataba wao, fedha zao

wamezuiliwa, wanaambiwa ni baada ya miaka 55, wanatarajia tupate majibu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona ni jambo ambalo ni muhimu sana na ndiyo maana Wabunge wakaomba hii sheria ilipaswa ipewe siku mbili mpaka tatu kujadiliwa kwa sababu tunajadili maisha ya watu wetu katika Taifa hili. Hapa ndiyo mahali pekee tunaweza kuwasaidia. Sasa nitashangaa tunaanza kulumbana kwa vitu ambavyo havina maana sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 27(b) kama wenzangu walivyozungumza kwamba inatajwa kutakuwa na kulipa mafao ya jumla, lakini hapa ambacho tungeomba, tungetaka *formula* ambayo itatumika kutengeneza fedha hizi ijulikane kwenye sheria. Tunataka hii iingizwe kwenye sheria tufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mtindo wa kumwambia Waziri atakaa peke yake, atengeneze sheria, halafu atatoa kiasi gani kwa kweli ni kama tunawaambia watu kwamba huo utaratibu watapata fedha lakini hawajui kiasi gani na hakuna namna ambayo tutarudi kuja kujadili tena hapa. Kwa hiyo hili jambo lingewekwa kwenye sheria na *formula* hapa tuzi-*testify* kwamba kama mtu anapewa milioni kumi, *formula* hiyo inampa *outlet* shilingi ngapi, ijulikane hapa! Lakini hili jambo kulificha kwenye kanuni kule, Waziri aende akakae na wenzake atengeneze halafu alete, sisi Wabunge hatutamhoji, hatutaiona ataweka kwenye *gazette*, wananchi wetu hawataona, wataendelea kupiga kelele na kulalamika mtaani bila majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili kwakweli ni kubwa kwelikweli lilipaswa liwekwe wazi kila Mtanzania ajue na Wabunge wajue, tupitisha kitu ambacho tunakijua kwamba hii *formula*, inawezekana. Kama inashindikana, wataalam wa hesabu tupo hapa, tulete, tusaidiane, tuitoe hadharani ijulikane ili watu wapate majibu, hakuna sababu ya kuficha *formula* hii ya kupata fedha ya Watanzania wetu ambazo kimsingi ni jasho lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niliona kwenye Bodi pale ambayo wameweka kwenye *schedule* namba moja, *provisions relation rating to the Board*. Hapa kuna mambo yafuatayo; moja, wametaja Wajumbe wote, sikuona kama watazingatia *gender balance* katika eneo hili. Wametaja nafasi, lakini kwa sababu kwa namna ya kuboresha kwamba angalau jinsia nyingine ishirikishwe, kwa kulazimisha ilitakiwa itajwe kwamba katika Bodi itakapokuwa ina-*appoint* hawa wahusika, watazingatia *gender*. Hilo jambo sikuliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wamesema kutakuwa na uwakilishi wa taasisi ambazo zina ajira kubwa, *most employee organizations*. Hapa unapozungumzia ajira katika nchi hii, kuna watu ambao wana mahitaji maalum, sikuona uwakilishi wao katika eneo hili kwamba angalau wale wenye mahitaji maalum na wenyewe angalau mtu mmoja ambaye atawawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana wasipokuwepo hapa, madai yao mbalimbali hayatazungumzwa. Watazungumza mtu kama mimi ambaye sina mahitaji maalum, nina viungo kamili, sina ulemavu wowote. Hawa watu wanahitaji wapate mtu hapa wa kuwasemea kwenye Bodi hii kwa kuzingatia mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, hii sheria ambayo inayojadiliwa leo kwamba inapitishwa, ndiyo sheria ambayo kila Mbunge, *message* ambazo mnatumiwa kwamba watu wanalalamika mtaani hawana haja, wanataka fedha zao; wale watu wanauliza, kwa nini mimi nifanye kazi, nimemaliza miaka sita au kumi, unaniambia nisubiri miaka 55, nina watoto ninasomesha; na mwingine ni mgonjwa, angefanya biashara aanze maisha yake mengine. Kwa nini unamlazimisha? Yaani kazi ya ajira imekuwa tena ni utumwa kwake, analazimishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili nadhani Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla na Wabunge wa Bunge hili Tukufu ni muhimu tujielekeze tukitoka humu ndani,

wananchi wanaolalamikia fedha zao ambazo wamefanyia kazi tusiwalazimishe matumizi yao. Tuwa-*guide* lakini tutoe tiba ya jumla katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anajua, mara nyingi tumekwambia sana watu wanalalamika mtaani, tupate majibu! Kwa mtindo ambao nauona huu ambapo watu wanajigeuza kuwa upande wa Serikali, kazi ya Bunge tunatunga sheria, sisi tunaishauri Serikali, tunaiwajibisha. Humu ndani tumejigeuza, tumejipa vyeo, Mawaziri, Kamati, tunazungumza hapa. Ndiyo picha inayoonekana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mimi Mbunge hakuna tofauti na Waziri, wala hakuna habari ya chama hapa. Hapa ni kwamba sisi Wabunge tuisimamie Serikali, wananchi wetu wanalalamika, sheria hii inawaumiza, wanataka fedha zao wajenge nyumba, wakopeshwe, watibiwe na wasomeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishie hapa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nakushukuru kwa kuokoa na muda pia. Naelekea kwa Mheshimiwa Mussa Mbarouk, halafu bado nina muda kidogo. Baada ya Mheshimiwa Mbarouk nitamwita Mheshimiwa Sonia Magogo.

Mheshimiwa Mbarouk, huwezi kusema, hujawa tayari! Mimi nimekuita, kama huwezi kusema nafasi imepotea. Mheshimiwa Sonia Magogo.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia...

MWENYEKITI: Samahani kidogo. Mheshimiwa Halima, naomba utulivu tu Bungeni. Msijibishane huko, kama una hoja ielekeze kwenye kiti. Mheshimiwa Sonia.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa, napenda kuipongeza Serikali kwa

kuleta muswada huu wa kuunganisha mifuko. Ninaona ni wakati muafaka kabisa kwa kuwa hiki kilikuwa ni kilio cha muda mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali, nilikuwa napenda kutoa angalizo, kwa vile tunakwenda kuunganisha mifuko na kunakuwa kuna *monopolization*, kwa hiyo hakuna ushindani kati ya mfuko mmoja na mfuko mwingine kama ilivyokuwa mwanzo, napenda kuishauri Serikali iwe makini sana katika huduma zinazokwenda kutolewa na mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo kulikuwa na mafao ambayo yanatolewa ambayo yalikuwa yanatumika kama kichocheo cha kuvutia wanachama kutoka mfuko mmoja kwenda mfuko mwingine. Vilevile mifuko ilikuwa inajitahidi kila mfuko utoe huduma bora zaidi ya mwingine ili kuweza kuvutia wanachama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kuweka hili suala la kuwa na mifuko miwili ambapo mwanachama hatakuwa na nafasi ya kuchagua aende mfuko gani, nilikuwa naishauri Serikali iwe makini sana kuhakikisha kwamba wanachama hawa hawapati usumbufu katika huduma wanazokwenda kuzipata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kuongelea kuhusu suala la fao la *unemployment* ambalo limekuwa *introduced* kwenye muswada. Hili fao kwa kweli nami naliunga mkono. Mimi ni mmoja wapo wa watu ambao walikuwa wanatoa huduma kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Kwa hiyo, wakati mwingine nilikuwa nakutana na wanachama ambao walitamani kuwepo na fao kama hili ili liweze kuwasaidia kulinda *credit* zao pindi watakapostaafu. Kwa kuwa kulikuwa hakuna hili fao, ilibidi kipindi kingine wa-*withdraw* hata bila kupenda pamoja na kwamba walikuwa bado wana *credit* chache ili waweze ku-*qualify* kuwa *pensioners*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunakwenda kulitoa hili fao la *unemployment*, naishauri Serikali iangalie hili fao linakwenda kutolewaje na litawasaidiaje wale waathirika wa hii *unemployment* kwa kipindi kile ambacho watakuwa hawana kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo naishauri Serikali iangalie, kuna makundi kadhaa ambayo sidhani kama hii *unemployment benefit* ambayo ni sehemu tu ya mafao itaweza kuwasaidia. Mathalani wale wanaofanya kazi kwa mikataba mifupi na hawana tena *room* ya kwenda kupata kazi sehemu nyingine na vilevile kuna wengine ambao wanapata ugonjwa ambao kwa ripoti ya Daktari unaona kabisa huyu mtu hawezi kuja kuendelea na kazi au labda ile pesa angeweza kusaidiwa kupata, ingeweza kumsaidia katika matibabu au shida anayoipitia.

Kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na kuondoa fao la *withdrawal*, lakini naomba waangalie makundi. Kuna kesi ambazo ukiliweka hili fao la *unemployment* na wakashindwa kupata ile pesa yao, bado tutakuwa hatujawatendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningependa kuishauri Serikali, kwa kuwa sasa hivi tunakwenda kuwa na mifuko miwili, sioni tena sababu ya mfuko mmoja unakata asilimia 15 kwa asilimia tano na mfuko mwingine unaendelea kukata asilimia 10 kwa asilimia 10. Naiomba Serikali, kwa kuwa sasa hivi tunakwenda kuwa na mifuko miwili, mifuko yote iwe *uniform*; wote wawe wanakata asilimia 15 kwa mwajiri na asilimia tano inakatwa kutoka kwa mfanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa upande wa mafao, nilikuwa naishauri Serikali iyapite upya mafao ambayo wameyapendekeza. Ukiangalia vitu vikubwa ambavyo vinamuumiza mwanachama, ni elimu na afya na mimi napendekeza kama wenzangu waliotangulia kwamba tuangalie fao la elimu. Fao la elimu ni muhimu sana kwa wanachama na tutakwa tumewasaidia kutua mzigo na vilevile tutakuwa tunatengeneza kizazi ambacho baadaye

kitakuja kuwa wanachama wetu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishauri Serikali kwa sababu tayari wafanyakazi watakuwa ni wanachama wa *NSSF*, sioni sababu tena ya yule mwanachama kukatwa pesa kwa ajili ya matibabu ya *NHIF*. Kwa hiyo, ni vyema mwanachama ambaye atakuwa tayari yuko kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii akaunganisha moja kwa moja kupitia ile michango yake kikawa ndiyo kigezo cha yeye kumfanya atibiwe kupitia *NHIF*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho naomba kuishauri Serikali ni hili suala la kusema kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Umma utachanganywa na yale makampuni ya *private*. Kwangu mimi hili naona kama litakuja kuleta mkanganyiko, kwa sababu *terms* za *public service* ukiangalia na *private* ziko tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hawa wafanyakazi wa *Private Sector* watakwenda kwenye *Public Sector* baadaye itakuja kuleta shida hata kwenye suala la *unemployment*, kwa sababu *terms* zao hawa, anaacha kazi hapa leo, anahamia hapa. Kwa hiyo, itakuwa badala ya ku-*concentrate* kuendeleza hii mifuko, kila siku itakuwa ni ku-*deal* na hilo fao la *unemployment*.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea, Mheshimiwa Richard Mbogo. (*Makofi*)

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. kwanza naomba nishukuru kwa hii nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa uhai mpaka dakika hii.

Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kufanya kazi na Kamati hii na wameweza kufanya vizuri sana kwanza kwa kuchukua maoni ya Kamati na kuweza kuyafanyia kazi na kwa ushahidi, ukiangalia muswada huu

hatuna *schedule of amendment* mezani za Wizara, inaonesha jinsi gani walikuwa wasikivu na wameweza kuchukua maoni ya Kamati na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache tu; la kwanza ambalo naomba nisisitize upande wa Serikali, kwamba baada ya kuunganisha hii mifuko, naomba sana tuangalie suala la kulinda hizi ajira za watumishi waliopo katika hii mifuko. Kama tukiangalia suala la wastaafu wangapi ambao ni wafanyakazi ndani ya hii mifuko, basi tuzilinde ajira kwa watu waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili limezungumziwa kuhusu suala la kujitoa. Kuna sekta nyingine ambayo hatujaiangalia kwa umakini. Kwa mfano, mtu labda ana miaka 50, anajitoa katika mfuko kwa sababu tu amepata ajira au kwa mfano, mtu amechaguliwa kuwa Mbunge, anaenda kwenye sheria nyingine ya wastaafu kwa upande wa kisiasa, ambapo kuingia kwenye hii mifuko inakuwa ni hiari.

Sasa kwa mtu ambaye ameacha kazi, ameingia kwenye Ubunge, kwa nini mtu kama huyo asifikiriwe kwenye fao la kujitoa aliye tofauti zaidi ya kukaa miezi sita ile na kusubiri na kuingia kwenye ule mfuko ambao ali-serve. Kwa hiyo, tuangalie na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la michango kwa upande wa asilimia tano kwa 15. Tumeona kwamba kuna hiari, mtu anaweza akaongeza lakini azidi asilimia 50. Sasa ni bora kwa wakati mwingine tunaweza kubadilisha, tuache tu asilimia tano kwa 15; asilimia tano kwa mwajiriwa na asilimia 15 kwa mwajiri, kuliko ile *section 18(6)* ambayo imeweka uhiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la *section 25*, tumezungumzia kuhusu umri wa kustaafu. Umri wa hiari ni miaka 55 na umri wa lazima ni miaka 60. Tukumbuke kwamba ni jana tu tumeipitisha ile sheria kwa zile kada za Madaktari na Wahadhiri, lakini sasa huku kwenye mifuko hakuna haja

ya kuongeza kipengele kikatambua ile sheria ambayo tumepitisha jana kuhusu hizo kada za Madokta pamoja na Wahadhiri ambao ni Maprofesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda *section 39(1)*, inazungumzia endapo mnufaika ambaye ni mstaafu amefariki kwamba warithi watalipwa kiasi alichokuwa analipwa cha mwezi cha huyu mstaafu, watalipwa kwa miezi 36. Sasa endapo mtu amestaafu ana miaka 62, bahati mbaya amefariki, halafu *beneficiaries* wanalipwa miezi 36: Je, kama mtu kastaafu kwa lazima miaka 60 halafu akaendelea kuishi mpaka miaka 75, angeweza kulipwa shilingi ngapi katika hiyo miaka 15 ya uhai wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii *beneficiaries* tunawapa fao la miezi 36 tu. Hatuoni katika *probability* ambayo tunaiangalia hapa, kwa namna nyingine hatujui sasa siyo Mungu wa kujua kwamba lini mtu atakufa, lakini nashauri tuweke *categories* tuwe na *range* kama tatu; kama mtu amefariki ana zaidi ya miaka 70 ndiyo hiyo miezi 36, lakini kama mtu amefariki kati ya miaka 60 na 65, hii miezi ya kuwalipa hawa wanufaika iongezeke ifike hata miezi 72 au 60 ili wanufaika waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tunaunganisha hii mifuko, lakini imezungumziwa kwenye hii sheria, bahati nzuri imebeba vizuri suala la kama la makato haya ya lazima hayakuwasilishwa katika hii mifuko, yeye mwajiriwa itakuwa siyo mzigo wake. Kuna mashirika mengine ya Serikali, mengine yaliweka madeni na hasa hizi *statutory deductions* za nyuma, sasa Serikali inabeba vipi? Kwa mfano, *Air Tanzania* unakuta ilikuwa inadaiwa na *TRA*, inadaiwa na mifuko, inadaiwa na *SACCOS*mbalimbali, kama za wanahewa, sasa madeni kama haya yanabebwaje kuja kwenye hii mifuko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kukubali kufanya mabadiliko ambayo Kamati imewashauri kwa kipindi cha siku nane. Kwa kuwa Kamati ya Bunge inafanya kazi kwa niaba ya Bunge, haya yanayokuja katika muswada huu, kwa asilimia zaidi ya 99 Kamati imeshiriki katika mabadiliko haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa dhati kabisa na yapo mabadiliko ambayo tumeyafanya. Moja, uwepo wa *unemployment benefit*; pili, mabadiliko kwenye kifungu cha 29 ambacho kinaelezea mafao na kuipa mamlaka bodi kuweza kufanya maamuzi juu ya aina ya mafao ambayo bodi husika itaona inaweza kuyaongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna *crykubwa* ya *public* juu ya *withdraw benefit*. Sisi tumeangalia nini? Tuliangalia *sustainability* ya mifuko hii. Sote tunafahamu mifuko ya hifadhi hii kama ingeendelea kwa utaratibu ambao tumekuwa nao, kuna mfuko kama *PSPF* uhai wake ulikuwa hauna zaidi ya miaka miwili, ulikuwa unaanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *denominator* ya 540 ilikuwa ni *dialogue* kubwa, lakini sisi kama Kamati vilevile tuliona kwamba tu-*provide* nafasi kwa Serikali na kuiruhusu kutumia kanuni kwenda kuweka *equation* na kwa kufuata utaratibu wa utatu kwa maana ya waajiriwa, vyama vya wafanyakazi, waajiri na Serikali katika mchakato wa kutengeneza kanuni ili mjadala wa *equation* itakayotumika kama *benefit* ya wafanyakazi iweze kuwa *considered*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeangalia suala la ku-*safeguard interest* za mifuko ya hifadhi kwa maana ya *investment*. Kumekuwa kuna uwekezaji mwingi sana ambao ulikuwa ukifanyika huko nyuma ambao umepoteza fedha za wastaafu. Kwa sheria hii, *Management, Board of Directors* watakuwa *accountable* juu ya uwekezaji wowote utakaofanyika na wataadhibiwa mpaka kifungo cha miaka mitano juu ya uwekezaji wowote watakaofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliamua mapendekezo ya Serikali yalikuwa ni kwamba wafanyakazi walioko kwenye *private sector*, wanaolipa katika mifuko ya kiserikali kama *PPF* wahame na michango yako. Uhai wa mifuko ungekwisha! Tuliamua kuweka *demarcation* na kusema kwamba kuanzia sasa mashirika yote ya umma ambayo Serikali ina *interest* yachangie katika mfuko wa umma. Hii ni ili kuweza kuipa uhai mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba maamuzi ya kisiasa ambayo yalikuwa yakifanyika huko nyuma katika mifuko ya hifadhi, hayatafanyika tena na Serikali. Tumeitaka Serikali kwamba watakapotunga kanuni, ziletwe kwenye Kamati ya Bunge ili Kamati ya Bunge iweze kuzipitia kanuni zile, ili tuone maslahi ya wafanyakazi kama yameweza kutazamwa inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu ambalo naendelea kuiomba Serikali na tumeiomba hata kwenye Kamati, sheria hii imetambua watu wa kada mbalimbali ambao wapo Kikatiba, ambao wametwajwa na sheria, lakini Makatibu Wakuu wameachwa kwa hoja kwamba Makatibu Wakuu ni wengi, lakini vilevile waliokuwa *considered* ni wale waliotajwa katika Katiba tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kila *Executive* ni *Permanent Secretaries*. Kwa hiyo, ni vizuri kabisa *Permanent Secretaries* wakaweza kuwa *considered* kama alivyotajwa *IGP*, kama alivyotajwa *Chief Secretary*, kama alivyotajwa Katibu wa Bunge na sheria hii, ili hawa watu ambao ndio *custodian* wa taasisi zetu za umma waweze kuwa na uhakika wa kesho yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* nimalizie tu kusema jambo moja kwamba *attitude* iliyooneshwa na Wizara katika mchakato wa kuipitisha sheria hii ni *very positive attitude*. Tunaamini Serikali inapoenda kutunga kanuni ambazo zitatumika ku-*govern* sheria hii na kufanya utekelezaji wa sheria hii, kanuni zile zitatumwa katika misingi ile ile ambayo sheria hii imepitia. Misingi ya *dialogue*, misingi ya kusikiliza

vyama vya wafanyakazi, misingi ya kusikiliza vya waajiri ili tuweze kuwa na sheria ambayo itaipa uhai mifuko yetu ya hifadhi ya jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kusema kwamba naunga mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bashe. Mheshimiwa Rehema Migilla. Mheshimiwa Mbarouk.

Nawashukuruni sana. Nahamia kwenye upande wa mapito ya mwenye hoja. Kwa sababu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Naibu Mawaziri hawa wawili; Mheshimiwa Ikupa na Mheshimiwa Mavunde, tutaanza na Mheshimiwa Ikupa Alex dakika kumi, halafu Mheshimiwa Mavunde dakika 20; na mtoa hoja mwenyewe nadhani dakika 30 zitakuwa zimekaa vizuri ndani ya muda wetu wa saa moja. Tunaanza na Mheshimiwa Ikupa, dakika kumi, karibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia hii nafasi. Awali ya yote naomba niunge mkono hoja hii ambayo iko mbele yetu na moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada kuunga mkono hoja hii na kama ambavyo hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu imeelezea, hiki kilikuwa ni kilio cha wafanyakazi kwa muda mrefu sana kama ambavyo imeelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida zake kwenye hotuba imeelezwa pia kwamba ni kwa nini sasa hii mifuko inaunganishwa ama kwa nini wafanyakazi walikuwa wakillia kwamba mifuko hii iunganishwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilitokana na kwamba kulikuwa kuna utofauti mkubwa wa mafao kati ya mfuko mmoja na mwingine, lakini pia gharama za uendeshaji wa hii mifuko na mengine mengi ambayo yameongelewa kwenye hii hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafafanua kwa ufupi tu fao la kifo. Fao hili ni fao ambalo linatolewa pale ambapo mtumishi bado anakuwa yuko kwenye utumishi na bahati mbaya akafariki. Fao hili limewekwa siyo kama tunataka watu wafe kabla ya umri, lakini kwa hali ilivyo ni lazima liwepo kwa sababu ni hali ambayo imekuwa ikijitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili fao ni zuri kwa maana ya kwamba kwa jinsi ambavyo limewekwa, yaani wanufaika pale ambapo huyu mtumishi anapofariki akiwa kwenye utumishi. Ukiangalia kwenye hii sheria inafafanua kabisa na inaonesha kwamba ni akina nani ambao wanakuwa ni wanufaika pale ambapo mtumishi anafariki akiwa bado kwenye utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kuna watoto, lakini pia kuna mjane, kwa maana ya mgane ama mjane; pia kwa upande wa watoto wanaendelea kuhudumiwa mpaka pale wanapofikisha umri wa miaka 21. Pia watoto hawa ama mtoto anaweza akaendelea kuhudumiwa endapo atakuwa na ulemavu wa aina yoyote. Kwa hiyo, huyu ataendelea kuhudumiwa kwa muda wake wote, yaani kwa maisha yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili fao ni zuri kwa maana kwamba linanufaisha wale ambao wanakuwa wamebaki ama ambao walikuwa ni wategemezi wa Marehemu. Siyo hilo tu, kama Marehemu alikuwa hana mke wala watoto wanaomtegemea, lakini ana wazazi, hili fao pia linakuwa lina umuhimu kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, muunge mkono hoja hii iliyoko mbele yetu ili iweze kupitishwa kwa maslahi mapana ya Watanzania wote na kwa maslahi mapana ya nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba niendeleo kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea, Mheshimiwa Mavunde, una dakika zako 20.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa michango yenu ambayo kwa namna moja ama nyingine imekuwa ni sehemu ya kuboresha muswada huu wa sheria ambao umewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema asubuhi, hata sisi ambao tulikuwa tunasikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge, unasikia kabisa ni michango ambayo inakwenda kuongeza thamani, ni michango ambayo iko *very positive*; na tunaamini kabisa kama Serikali iko michango ambayo tumeona ina umuhimu na sisi tutaichukua kwa ajili ya kuona namna bora ya utekelezaji wa sheria hii hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na jambo ambalo siyo muhimu sana lakini ni kwa sababu ya kumbukumbu. Nataka niweke kumbukumbu sawa. Wakati Msemaji wa Kambi ya Upinzani hajaanza kusoma hotuba yake, alizungumza ya kwamba ikumbukwe kwamba hoja hii ya kuunganisha mifuko ni hoja ambayo imeletwa na upinzani na akawataja baadhi ya Wabunge ambao walianzisha hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumbukumbu tu ili Bunge lako liweke kumbukumbu sawa, nimepata mkanganyiko mkubwa sana wakati nasoma taarifa hii na mkanganyiko wenyewe ni kwamba sehemu moja inakubali, sehemu nyingine inakataa. Wakati maelezo ya msemaji anasema kwamba hoja hii imeanzia kwao, lakini ukisoma ukurasa wa pili, aya ya pili, naomba ninukuu kidogo tu kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa. Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani anasema; "Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba badala ya Serikali kung' ang' ana kuweka

sheria za kupunguza na kuibana mifuko ya jamii, ingepanua fursa za ajira kwa Watanzania na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuajiri kwa wingi ili kupunguza umasikini wa kipato kwa Watanzania.”

“Pili, ni kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanawekewa akiba itakayowasaidia pindi umri wao wa kufanya kazi utakapokoma.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona kabisa *contradiction* hapa kwamba mwanzoni anasema hoja hii imetokea Upinzani, lakini ukisoma katika ripoti hii wanashangaa kwa nini tunaendelea kung’ang’ana kupunguza idadi ya mifuko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kumbukumbu hii ibaki sawa ni kwamba hoja hii kama walivyosema wachangiaji waliopita, ni hoja ambayo imeletwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (*TUCTA*) na sisi kama Serikali tuliona ina umuhimu mkubwa ndiyo maana tumeichukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuweka hiyo kumbukumbu sawa, niko katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Moja ya jambo ambalo limesemwa katika taarifa hii, limezungumzwa vyema kabisa kwamba tusiunganishe mifuko hii na badala yake tupanue fursa za ajira na kuweka mazingira wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mtoa hoja alielezea umuhimu wa kuunganisha mifuko hii na namna ambavyo itakwenda kuboresha mazingira ya wafanyakazi katika nchi yetu ikiwemo pamoja na mafao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inayozungumzwa hapo na Kambi Rasmi ya Upinzani ni kutuambia kwamba badala ya kuunganisha mifuko, ni afadhali mtengeneze fursa zaidi za ajira kuliko kufanya jambo hili, ambayo inapingana na hoja ambayo aliitoa Mheshimiwa Zitto Kabwe ya kuongeza wigo wa sekta ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunaamini kabisa uunganishaji wa mifuko hii inakwenda kuongeza tija kubwa sana kwa wafanyakazi wa nchi hii, lakini unapozungumzia suala la kuweka mazingira wezeshi na kuongeza fursa za ajira, mipango ya Serikali iko dhahiri, inafahamika. Tunayo miradi mikubwa katika nchi yetu ambayo itakwenda kutengeneza ajira nyingi sana ikiwemo ujenzi wa reli ya kati (*standard gauge*), likiwemo bomba la mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukienda katika falsafa ya uchumi wa viwanda ambayo inakwenda na ufungamanisho na maendeleo ya watu moja kati ya mambo ambayo tunayapigia kelele sana katika uchumi wa viwanda ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa ajira hasa katika kundi kubwa hili la vijana. Kwa hiyo, sioni kabisa kwamba ile hoja iliyoletwa hapa ya kusema kwamba, tuendelee kutengeneza nafasi tu za ajira na mifuko hii isiunganishwe, sikuona kama ina umuhimu mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya jambo lingine ambalo katika ripoti hii katika Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani wamesema ni msemaji anazungumza kwamba lazima mwanachama huyu anayechangia basi anufaike na michango yake kwa sababu kuna wengine unakuta hata michango hii hawajaitumia na tayari ameshafariki na hajaona utamu wa michango yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Msemaji leo wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Dada yangu Mheshimiwa Ester, kidogo alipitiwa leo na kama hakupitiwa basi hakuusoma vizuri muswada huu wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu wa sheria ambao tunaupendekeza katika kifungu cha 29, imeainishwa bayana mafao ambayo yatakwenda kutolewa. Hata katika *previous position*, kwa sheria zilizopo hivi sasa mwanachama ananufaika na mafao mbalimbali ambayo muda mwingine tunayasema ni mafao ambayo hata kabla hajafikia muda

wake wa kustaafu, lakini anayapata kuanzia hivi sasa.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mafao ya uzazi, mafao ya kuumia kazini, ugonjwa na mikopo. Kwa hiyo, unapozungumza hoja ya kwamba, michango yake imsaidie ndio inavyomsaidia katika namna hii na ndio maana katika muswada wa sheria ambayo tunaipendekeza kifungu namba 29 kimeeleza bayana aina ya mafao ambayo sheria hii inayapendekeza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini alikwenda mbali zaidi akazungumza kuhusu suala la *life expectancy* ya miaka 61.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Taarifa hii ya Kambi Rasmi ya Upinzani...

MWENYEKITI: Wheshimiwa Wabunge, samahahi sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge, Idara ya *Hansard* inashindwa ku-*capture* anayosema Mheshimiwa kwa sababu tunachangia na sisi kwa mashauriano. Naomba uende chini na ndio shughuli za Kibunge, msikilize mwenzako, yeye alikusikiliza. Tuendelee.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, hoja yangu ni kwamba, katika Taarifa hii ya Kambi Rasmi ya Upinzani imezungumzwa hoja ya kwamba umri wa kuishi Mtanzania hivi sasa unakadiriwa kuwa ni miaka 61 kwa hiyo, na ndio maana ilikuja hoja kwamba ni afhadhali mtu anufaike na mafao yake haya kabla kwa sababu sio wote ambao wanakuwepo katika mda huo ambao aliusema hapa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimpe tu taarifa kidogo kwamba, najua alikwenda kuchukua takwimu hii katika Taarifa ya *NBS* ambayo inazungumzia *General Life Expectancy* ambayo hii inamhusisha mpaka mtoto wa umri wa chini ya mwaka mmoja. Lakini nataka nimsaidie taarifa nyingine ambayo itamsaidia pia katika taarifa nyingine

ambazo zinakuja. Ni kwamba kwa mujibu wa *Acturial Valuation Report* ambayo ilifanywa na *ILO* ambayo inazungumzia kuhusu wastani wa kuishi wa mstaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastani wa kuishi wa mstaafu kwa mujibu wa taarifa ile inasema, mstaafu wa kiume ana uwezo wa kuishi miaka 20.9, lakini wa kike kwa miaka 22.3. Lakini kubwa zaidi kuliko yote tukichukulia kwa mfano tu wa *PSPF* ambao mpaka hivi sasa una takribani ya wastaafu 72,000 ni wastaafu asilimia nne tu waliofariki mpaka leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa pia katika taarifa hii kwamba hoja ya kwa nini tunamuingiza Mwanasheria Mkuu pindi pale Bodi inaposhitakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 inamtamka Serikali kama ndiye *guarantor*. Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaingia kwa sababu ya kulinda maslahi ya Serikali. Ndio maana kwa mujibu wa sheria inayopendekezwa kifungu cha 60 kinatoa wajibu wa Serikali kama sehemu ya *guarantee* kwa mfuko huu, maana yake ni nini; maana yake ni kwamba Serikali lazima ilinde maslahi yake katika mfuko huu. Ikitokea jambo lolote limetokea mfuko huu una-*collapse* mwisho wa siku mzigo mzito inabeba Serikali na ndio maana Mwanasheria Mkuu wa Serikali likitokea jambo lolote la kushitakiwa kwa Bodi hii anaingia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu hiki cha 60, inakwenda mbali zaidi ikitokea kwamba, kuna jambo ambalo linasababisha *insufficiency* katika *fund* kwenye mfuko huu, Mfuko Mkuu wa Serikali unaguswa kwa namna moja, kwa hiyo, ndio maana nafasi ya Mwanasheria Mkuu inakuwepo katika Sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa pia, hoja hapa na Waheshimiwa Wabunge ambayo na sisi kama Serikali tunaikubali ya kuongeza wigo wa ku-*cover* mpaka *informal sector* na hoja hii, ukiifuatilia katika ripoti iliyotolewa

mwaka 2014 inaitwa *Intergrated Labour Force Survey* inasema, nchi yetu ya Tanzania tuna takribani ya nguvu kazi ya watu milioni 22.3. Watu milioni 22.3 maana yake ni watu kuanzia miaka 15 na kuendelea mbele ambao ndio *the working age population* (watu wenye uwezo wa kufanya kazi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mujibu wa takwimu zilizofanyika, utafiti uliofanyika inaonyesha kwamba, ni asilimia 10 tu ya nguvu kazi yetu ndio wapo katika hifadhi ya jamii. Ndio maana na sisi tunakubaliana na hoja hii kwamba, ni lazima, kama Serikali, tuje na mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba, tunaendelea kuwa-*cover* watu wengi zaidi kuingia katika mfumo wa hifadhi ya jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yamefanyika pia katika marekebisho ya kifungu cha 30 cha Sheria ya *SSRA* ambayo imekwenda kutambua wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kama wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii. Lakini vilevile kwa sheria hii ambayo leo tunaijadili hapa ndani na ikipitishwa inakwenda kupeleka mabadiliko katika Sheria ya *NSSF* ambapo *NSSF* sasa inapewa jukumu mahususi la kushughulika na *private sector* na *informal sector*.

Kwa hiyo, katika mpango na mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, kupitia *NSSF* tunaifikia *informal sector* kwa eneo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na sera yetu imezungumza jambo hilo. Ukisoma sera yetu, Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003, kifungu cha 3(2)(b) na chenyewe kinaelezea umuhimu wa kuwepo na *informal sector* katika *coverage* ya *social security* hasa katika maeneo ya kilimo, uvuvi, madini na biashara ndogondogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 95 cha Muswada kinakwenda kurekebisha kifungu cha 6 cha Sheria ya *NSSF* kuongeza maneno ya mtu aliyejajiriwa katika sekta binafsi na mtu ambaye amejajiri ikiwa ni sehemu ya kwenda kutekeleza takwa hili la kusaidia *coverage* ya *informal sector* kwenye hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa pia hoja hapa ambayo imewagusa Waheshimiwa Wabunge wengi sana kuhusiana na Fao la Bima ya Matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa fao hili tumeshuhudia Wabunge wengi wamkisimama wakilisema jambo hili. Niseme tu kama Serikali kwa kufahamu umuhimu wa jambo hili, tusingekuwa tayari kuliondoa kwa sababu ni jambo ambalo kwa kiwango kikubwa sana linagusa maisha ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ilikuwa tu ni makosa ya kiuchapaji na ndio maana tumerekebisha. Fao hili la Bima ya Matibabu lipo palepale na marekebisho yetu ya Jedwali ambalo linakuja na Serikali lengo lake ni kupitia kifungu cha 97 kwenda kufuta kifungu cha 21(f) cha Sheria ya *NSSF* na kuingiza badala yake *unemployment benefit*, lakini kukiacha kifungu 21(g) cha sheria ile ambacho kinazungumzia masuala ya Bima ya Afya ya Matibabu. Kwa hiyo, jambo hili halijaondoka lipo palepale na kwa kweli, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa *concern* yenu kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilizungumzwa pia, hoja na Mheshimiwa Mtolea, Mheshimiwa Mtolea alikwenda *specific* kwenye kifungu namba 57 na akawa anastaajibishwa na matumizi ya neno *shall* ambalo kwa tafsiri yake anasema ni kama inatoa *discretion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nafikiri rafiki yangu mwanasheria msomi Mheshimiwa Mtolea hakujiielekeza vyema katika kifungu hicho. Kifungu hiki cha 57 kipo wazi kinasema, neno alilolisema yeye la *shall* katika kifungu hiki cha 57 neno hili linalenga kuweka sharti la lazima kwa bodi kuandaa ripoti ya uthamini kila baada ya miaka mitatu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ukisoma vizuri pale utaona imezungumzwa *shall*, lakini kwenye zile koma zile imekwenda kutoa jukumu kule mbele kwa hiyo, Mheshimiwa Mtolea ukikisoma vizuri

bado hakijaharibu maana. Na uzuri katika Kifungu cha 57(2) imekwenda kueleza pia, kwamba, iwapo itatokea kwamba, kuna sababu za msingi za Bodi kutokuandaa ripoti ya Uthamini inaweza kuomba *waiver* kwa mujibu wa kifungu hicho kwa hiyo, nafikiri kabisa hapa Mheshimiwa Mwanasheria Msomi Mheshimiwa Mtolea hakujiielekeza vyema katika kifungu hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimebakiza hoja moja ya mwisho, hoja hii imesemwa na Kambi Rasmi ya Upinzani na baadhi ya Wabunge kwamba, hawaoni tena umuhimu wa *SSRA* kwa sababu mifuko hii inakwenda kuunganishwa, itakuwa miwili, kutakuwa hakuna ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera yetu ya Hifadhi ya Jamii inajielekeza katika taa ya tatu ambazo naomba nizataje kwa ufupi, taa ya kwanza inazungumzia kuhusu *social assistance*, taa ya pili inazungumzia kuhusu *mandatory schemes* na taa ya tatu inazungumzia kuhusu *voluntary schemes*. Sasa sisi kwa hoja inayosemwa hapa ni kwamba tayari tuna mifuko mwili *SSRA* anabaki kufanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niweke vyema kabisa hapa, hii mifuko miwili ambayo tunaizungumzia ipo kwenye taa ya pili ya *mandatory scheme*, lakini tunayo taa ya tatu ambayo ni ya *voluntary scheme*. Iko mifuko midogomidogo mingi sana, hauwezi leo kumuondoa *SSRA* ukaacha mifuko hii ikajiendesha yenyewe, hapo ndipo hasa umuhimu wa *SSRA* unaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hivyo tu ukiacha mifuko hii miwili hapa kinachozungumzwa inazungumzwa Sera ya Hifadhi ya Jamii ambayo ndani yake pia inajumuisha mifuko mingine ikiwemo Mfuko wa *CHF*, ikiwemo Mfuko wa *NHIF*, ikiwepo Mfuko wa *WCF*. Hii yote pia inahitaji kuwa *regulated* kwa hiyo, hayo hasa ndio yanafanya na kuleta *relevancy* ya kwa nini *SSRA* iwepo. Lakini pia bado chombo hiki ni muhimu kuwepo katika kushughulikia malalmiko ya wanachama hasa katika kipindi hiki cha mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, hata uzoefu wa nchi za jirani Kenya wana mifuko mikubwa miwili, kama kazi ambayo tutakwenda kuifanya hapa, lakini Kenya wana kitu kinaitwa *Retirement Benefit Authority* ambayo kazi yake kubwa ni kama kazi inayofanywa na *SSRA*. Sasa kwa Kenya mifuko iko miwili, lakini Kenya wana *voluntary schemes* zaidi ya 10,000 ndio maana wenyewe wakaona umuhimu kwamba pamoja na mifuko hii mikubwa miwili, lakini bado mifuko hii midogo lazima iwe ina mtu wa kui-regulate. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nichukue fursa hii tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Na kwa kweli, Muswada huu unakwenda kutibu matatizo mengi sana yaliyokuwa yanakabili wananchi wafanyakazi wa Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi tu niseme naunga mkono hoja. Asante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Asante sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Mavunde kwa mchango wao. Sasa nimuite mtoa hoja, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. (Makofi)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba nichukue nafasi hii niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia muswada huu ni pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, lakini pamoja na Maoni ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Wabunge walioweza kuchangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ni Waheshimiwa Wabunge 17 na waliochangia kwa maandishi ni Wabunge watano. Naomba niwashukuru sana Wabunge kwa michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwa kusema kwamba, nichukue nafasi ya pekee kwa niaba ya Serikali kuwahakikishia wafanyakazi wote wa Tanzania kwamba, Serikali yao inawapenda sana na niwaombe sana wafanyakazi wa Tanzania wasifikiri kuletwa kwa muswada huu wakayasikiliza maneno ya uchonganishi kutoka mahali kokote kwamba muswada huu una lengo la Serikali kudhulumu maslahi ya wafanyakazi, si kweli, kwa sababu wafanyakazi wanajua chanzo cha muswada huu ni nini. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie tuko pamoja wafanyakazi wote na tunaendelea kuwaheshimu na tutaendelea kufanya kazi nao kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa kilichonifurahisha katika majadiliano ya muswada huu ni kwamba Wabunge waliochangia wengi wamedhihirisha kabisa kwamba, wanaunga mkono muswada wetu ikiwa ni pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani na yeye anasema hoja hii hata wao waliitafakari tafakari hivi. Kwa hiyo, hiyo inadhihirisha kabisa kwamba kwa kweli, Waheshimiwa Wabunge wa Kambi zote mbili wanaunga mkono hoja hii, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema toka asubuhi kwamba, haki ya hifadhi ya jamii katika nchi yetu ya Tanzania imwekwa katika misingi ifuatayo; msingi wa kwanza ni Mkataba wa *ILO* Namba 102, lakini msingi wa pili ni Pendekezo Namba 202 la mwaka 2012 ambalo linaweka utaratibu na mfumo wa ulipaji wa mafao katika nchi zote wanachama wa Umoja wa Mataifa. Pendekezo namba 202 linatoa nafasi kwa kila nchi mwanachama kuangalia mafao yale ambayo yametajwa na *ILO* katika muongozo na mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi inao uwezo wa kuamua kutengeneza aina ya mifumo na sheria ambazo zitatafsiri mahitaji ya hifadhi ya jamii katika nchi husika na ndio maana sisi katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 11(1) kimejieleza wazi mamlaka ya nchi yetu haina budi sasa kwa kutafsiri miongozo hiyo, lakini vilevile

kwa kutafsiri mikataba tunao uwezo wa kutunga sheria mbalimbali zitakazowahifadhi Watanzania watakapokutana na majanga yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada wa leo ni utekelezaji wa mikataba, lakini ni utekelezaji wa mapendekezo ya Shirika la Kazi Ulimwenguni. Kwa hiyo, wale Wabunge waliounga mkono ninawashukuru sana kwa sababu tunaendana na Umoja wa Mataifa unavyotaka na hasa Shirika la Kazi Ulimwenguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo tunapoendelea kuyatekeleza matakwa haya wote tunaona kwamba sekta ya hifadhi ya jamii katika nchi yetu ya Tanzania imeendelea kuwa na mabadiliko makubwa na imeendelea kuchangia katika kukua kwa Taifa letu ukiachia mbali suala zima la kuwahifadhi wananchi wa Tanzania wakiwemo wafanyakazi kwa kutumia misingi ambayo tumejiwekea kisheria lakini kwa kuzingatia sera ambayo tumeiunda ya hifadhi ya jamii katika nchi yetu ya Tanzania. Na hivyo hivyo imetupelekea tukakutana leo kwenye Bunge lako tukufu, tukaja kuangalia umuhimu wa kuunganisha mifuko na mifuko hii tunapoiunganisha leo ziko sababu za kimsingi za kuunganisha mifuko hii nitarejea kwa ufupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Kazi Ulimwenguni lilishatuagiza baada ya kufanya utathimini wa mifuko lilishatoa mapendekezo ya kuishauri nchi yetu ya Tanzania toka mwaka 2013 kufikiria namna bora ya kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii kwa kuiunganisha mifuko hii ya hifadhi ya jamii ambayo nchi yetu ya Tanzania ilionekana ina mifuko mingi kulinganisha na nchi nyingine. Shirika la Kazi Ulimwenguni kama mdau mkubwa anayesimamia vigezo vya hifadhi ya jamii katika mataifa mbalimbali na yeye alitushauri hivyo. Lakini na sisi kupitia mdhibiti wa sekta katika nchi yetu ya Tanzania tuliona kwamba iko hoja ya msingi ya kuhakikisha kwamba mifuko hii tunaiunganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo ya utangulizi sasa nitajikita katika kujibu hoja za

Waheshimiwa Wabunge lakini ambazo zimezungumzwa kwa ujumla. Labda nianze na hoja ambayo ni hoja kubwa sana. Ninaona Bilago mwalimu mwenzangu na jirani yake Haonga Kambi Rasmi ya Upinzani wameizunguza kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hoja yao kubwa kikokotoo ambacho kinatakiwa kielekeze mfumo wa malipo ya pensheni kiingizwe kwenye sheria. Hiyo ndiyo hoja kubwa, na Mheshimiwa kaka yangu Bilago mwalimu mwenzangu amekwenda mbali zaidi akasema ni lazima kikokotoo cha moja chini ya mia tano arobaini (1/540) kijionyeshe pale dhahiri. Lakini alipokuja kuchangia jirani yake ndugu yangu Haonga akasema tena hiyo moja chini ya mia tano arobaini (1/540) haitoshi twende moja chini ya mia tano ishirini (1/520). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema mambo yafuatayo; ningeomba sana wafanyakazi tusiwapotoshe, wafanyakazi tusiwajengee mtazamo kwamba Bunge hili ndilo Bunge linaloweza kuwahurumia sana katika suala la mafao yao. Ninasema hivyo kwa sababu gani ninazo sababu za msingi. Kabla hatujafikia kuunganisha hii mifuko nimesema pale mwanzo *ILO* walifanya tathimini wa sekta ya hifadhi ya jamii katika nchi yetu ya Tanzania. Wamefanya utathimini mwaka 2010; wamefanya utathimini mwaka 2016 nilitegemea kaka yangu Haonga anapokuja kuleta hilo pendekezo na kaka yangu Bilago na Kambi Rasmi ya Upinzani wasingeishia kwenye eneo la kikokotoo peke yake, wangeenda mbele kwenye zile *findings* zote ambazo zililetwa baada ya kufanya utathimini wa mifuko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu yafuatayo; baada ya kufanya utathimini wa mifuko mwaka 2010 na 2016 yafuatayo ndiyo yaliyojitokeza; la kwanza, ni *funding level* ya mifuko yote katika nchi ya Tanzania. Mfuko wa *NSSF* ambao kikokotoo chake ni moja chini ya mia tano themanini(1/580); mwaka 2010 *funding level* yake ilikuwa asilimia 75.8 mwaka 2016 *funding level* ikaendelea kupanda. Mfuko wa *PPF* walipofanya utathimini wa mfuko mwaka 2010 *funding level*

ya PPF ilikuwa asilimia 47.1 mwaka 2016 ikawa 49.6. LAPF ambayo inatumia kikokotoo cha moja kwa mia tano arobaini (1/540) *funding level* ilikuwa asilimia 46.7 mwaka 2010 ilipofika mwaka 2016 kwa sababu ya kikokotoo cha moja chini ya mia tano arobaini *funding level* ya LAPF ikaanza kushuka na ikafika asilimia 27.7. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, PSPF mwaka 2010 *funding level* ilikuwa asilimia 10.1 ilipofika mwaka 2016 *funding level* ikawa asilimia 6.2. Lakini hatukuishia hapo matokeo ya utathimini baada ya kupata hizi *findings wakatoa* ushauri, ushauri wa wazi kabisa tukitaka kuendelea na kikokotoo cha moja chini ya mita tano arobaini (1/540) kwa mfuko wa LAPF na mfuko wa PSPF ni lazima *contribution rate* itoke asilimia 20 iende asilimia 30.

Sasa ninataka kumuuliza kaka yangu Bilago anapopendekeza kikokotoo cha moja chini ya mia tano arobaini achotaka kuwaambia wafanyakazi wa Tanzania anakubaliana na mapendekezo ya ILO yaliyofanywa mwaka 2010 na 2016 kwamba sasa kikokotoo kiondoke asilimia 20 kiende asilimia 30. (Makofi)

Ninaomba nitoe ufafanuzi wa maana ya asilimia 30. Mfanyakazi huyo sasa akipelekwa asilimia 30 ina maana mwajiri atachangia asilimia 15 mfanyakazi atachangia asilimia 15 na mwenye kalamu aanze kushika karamu yake aorodheshe. Mfanyakazi atachangia asilimia 15 ya Mfuko wa Pensheni, atachangia asilimia 15 ya Bodi ya Mikopo, atachangia asilimia tatu ya Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa atachangia mbili, Chama cha Wafanyakazi, achangie asilimia tisa ya Kodi ya Mapato, achangie asilimia tano labda ya mkopo ambao ameukopa labda binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli kwa asilimia 15 kwa *funding level* ya moja chini ya mia tano arobaini (1/540) ambayo itampelekea mfanyakazi huyu kukatwa makato ambayo yanazidi Sheria ya Utumishi wa Umma vigezo vilivyowekwa. Mfanyakazi huyu mshahara wake utabaki takribani kama asilimia 23 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuliona hilo lakini pia kwa kuyatazama na mengine ambayo nitayasema *TUCTA* (Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi) ambao hoja hii ndiyo hoja yao pamoja na Kamati walikuja Serikalini na ushahidi wao ninao hapa, wakaomba Bunge lisiwaamulie kikokotoo, hayo ndiyo maoni ya *TUCTA* na *TUCTA* ndiyo wenye sheria yao na ndiyo waliyoiomba Serikali na ndiyo wadau namba moja. Kikokotoo hiki turudi kwenye kanuni na kwa kuzingatia sheria za kazi tulizo nazo na utaratibu wetu wa *collective bargaining* katika dhana ya Utatu tuende tukatafakari jambo hili kwa pamoja na mwisho wa siku tukubaliane sisi kule na wadau wa mfuko huu kikokotoo kiwe ni kikokotoo kipi.

Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba sana kama tutaamua sisi kuwapangia wafanyakazi tutakuwa tumewapangia wafanyakazi na *contribution rate* ambayo itakuwa ama inawaumiza ama haitawasaidia. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo tutakuwa hatujawatendea haki wafanyakazi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana ndugu zangu wa upinzani muelewe kabisa hoja hii kwa msingi huo ambao nimeusema. Sheria yetu sisi tumeamua kuweka bayana kikokotoo ili tusiwaumize wafanyakazi kibakie kuwa asilimia 20 mfanyakazi achange asilimia tano, Serikali inachangie asilimia 15. (*Makofi*)

Sasa kaka yangu Bilago unapotaka kung'ang'ania twende katika mfumo huo kabla hatujarudi kukaa pamoja na kutafakari na kuwabebecha hao wafanyakazi mzigo wakuchangia asilimia 30 unawasaidia ama unawaingiza kwenye matatizo zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge jambo hili ni jambo zito wala siyo jambo la kuliambia tuhumu ndani wenye Maulid yao ni wafanyakazi wa Tanzania watakaokutana na Waziri wa Kazi. Na Maulid kaka Bilago siyo ya kwako usiyavali kanzu, acha wenye maulid wayafanyie kazi, tutarudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge mmesema hapa kwamba hamumwamini Waziri wenye dhamana kurudi kukaa na wadau katika kutengeneza vikokotoo. Waziri wa Kazi haongozwi na sheria moja katika nchi ya Tanzania. Uzoefu wa Kimataifa na mikataba niliyoisema Waziri wa Kazi anaongozwa na sheria nyingi, mimi ninaongozwa na Sheria Namba 7 ya mwaka 2014. Sheria hiyo inaunda Baraza la *LESCO* na Baraza la *LESCO* kazi yake ni kumshauri Waziri kama kubadilisha sheria lazima nitarudi kwenye Baraza la *LESCO* na Baraza la *LESCO* lina Wajumbe ambao ni wafanyakazi, mwajiri lakini na Serikali tunakuwa mle ndani kwa pamoja na hiyo niwaondoe tu shaka kwamba jambo hilo tatalifanya kwa pamoja na wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niongeze pia katika kufanya pia utathimini wa mifuko tulichogundua hii mifuko ambayo inatumia kikokotoo cha moja kwa mia tano arobaini (1/540) imeendelea kushuka hata kwa uwiano na uwiano wa walipwaji wa pensheni. *Standard* za kimataifa inatakiwa katika mfuko mwanachama mmoja aliyesitaafu achangiwe fedha ya kustaafu na wanachama 25, lakini tukirudi kwa sababu ya kikokotoo kile kile, mifuko ambayo kikokotoo chake ni hicho ambacho Kaka Bilago unasema twende tu hata bila kufanya utathimini tuamue tu unaona kwamba wameshindwa kufikia *standard* hizi za Kimataifa. Mfuko wa *PSPF* uwiano ni mwanachama mmoja kwa wanachama watano tu. Lakini ukienda kwenye mfuko wa *LAPF* ni mwanachama mmoja kwa wanachama 19. Lakini ukienda kwenye mfuko wa *NSSF* ni mwanachama mmoja kwa wanachama 32.

Kwa hiyo, unaona kabisa hali ya sekta ilitakiwa tufanye maamuzi haya, ninarudia kusema Waheshimiwa Wabunge tupitisheni sheria tutakwenda kufanya *actuarial* mpya. Kwa sababu hata hapa tunapongea wako wanachama ambao mpaka sasa wanaendelea kujiunga na mifuko hii na wako wanachama wanaostaafu. Sasa niulize hivi tukiamua tu hapa ndani hawa wanachama wanaojiunga leo. Wanachama wanaoendelea kustaafu wakati sisi tuko na huo muswada, hao nao tutafanya nini.

Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema tumalize sheria hii, turudi tukafanya *actuarial* yetu tutapata picha nzuri tutatengeneza *regulation* kwa taratibu wa sheria za kazi tulizonazo, tuna Sheria Namba 6 na Sheria Namba 7 na hizi zote zitatusaidia kutuhakikishia kwamba jambo hili tunalifikisha salama na wafanyakazi. Wafanyakazi nieleweni Waziri wenu nipo hakuna kitakachoharibika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa fao la kukosa ajira, kwanza niwashukuru Wabunge wote ambao wameunga mkono fao hili ninawashukuru sana. Fao hili nisema labda maneno machache ya utangulizi, kwenye mafao ambayo yanatambulika na Umoja a Mataifa hakuna fao la kujitoa. Fao hili la kujitoa liliingizwa na mifuko yetu mingi kwa kulazimishwa ama sheria ama kulitoa fao bila kuwa na *mandate* za kisheria kwa sababu ya ushindani kwenye sekta. Lakini hakuna fao la kujitoa katika mafao duniani halipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sikivu ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli baada ya kusikiliza kilio cha wafanyakazi kwa muda mrefu na hasa wafanyakazi wa kwenye migodi ndiyo maana tumekuja na fao hili sasa *unemployment benefit* ili tutibu tatizo la wafanyakazi hao. Nilitegemea Wabunge leo mngeshangilia sana fao hili kwa sababu linaenda kusaidia sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema hivi fao hili kwenye sheria tumelipa masharti, baada ya kulipa masharti kaka yangu Mtolea alisema kitu kizuri sana hapa ni lazima wakati wa kuliangalia hili fao la kujitoa tukajue aina za wafanyakazi walioko katika sekta mbalimbali na tujue watalipwa je hayo mafao yao kwenye hili fao la kukosa ajira kama mbadala wa fao la kujitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili utaweza kulifanya tu kama utarudi kwenye *regulation* ukamaliza utathimini wako wa mfuko ukaangalia mahitaji halisi ya wafanyakazi kwenye fao hili la kosefu waajira na baada ya hapo ukalitengenezea mfumo wa malipo mzuri ambao utakuwa endelevu.

Ninaomba Waheshimwa Wabunge muamini hapa tulipofika tumefika kwa sababu tumefanya kazi kwa pamoja na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini na hii siyo hoja ya Serikali peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hofu ya hatima ya wafanyakazi ambao wako kwenye mifuko yetu mpaka sasa. Kifungu cha 87 kiko wazi kabisa na sisi tumesema kwamba hatuwezi kuwaacha Watanzania wenzetu ambao wamehudumia kwenye sekta ya hifadhi ya jamii kwa miaka hii yote eti kwa sababu ya kuunganisha mifuko tukawaacha wapotee tu hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wafanyakazi waliopo kwenye sekta mpaka sasa mpaka Septemba mwaka jana ni wafanyakazi 2,147. Lakini idadi ya wanachama hai na wanachama wastaafu mpaka mwezi Septemba, 2017 ilikuwa ni 1,448,861. Baada ya kuunganisha hii mifuko kwa takwimu sahihi ambazo tunazo idadi ya wafanyakazi kwenye mfuko wa umma watakuwa 988 na idadi ya wafanyakazi kwenye mfuko binafsi watakuwa 1,159. Sasa ili uweze kujua wafanyakazi hawa unawachukua ama huwachukui ni lazima uzingatie uwiano wa wafanyakazi na uwiano wa wanachama na wastaafu katika kila mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya hiyo kazi kwa kiasi cha kutosha na naomba niwaombe wenzetu Wabunge wa Upinzani hatujaja hapa tumekurupuka, jamani tumefanya kazi kwa ajili ya wafanyakazi wa nchi hii ya Tanzania. Ni tofauti na mtu aliyekutana tu na muswada huu bila kujua kazi iliyofanyika. *SSRA* baada ya kuangalia sekta itakavyokuwa huko mbele tunapokwenda tumegundua uwiano unaonatakiwa kwa mfuko wa umma utakuwa ni 1:675 na kwa hali hiyo wafanyakazi wote 988 watahitajika na tutahitaji ziada ya wafanyakazi 114. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hiyo tu inatosha kabisa kukuambia kwamba pamoja na kifungu cha 87 lakini bado sekta itahitaji wafanyakazi wa ziada na hivyo basi ninaomba niwahakikishie wafanyakazi, ambao wako kwenye sekta ya jamii mpaka

sasa tumeshafanya hesabu yao, tunajua waliko, tunajua wanafanya nini, na sisi tumejipanga kuwachukua ili waimarishe sekta ya hifadhi ya jamii.

Lakini hata hivyo kwenye sekta ya hifadhi ya jamii bado tunayo mifuko mingine tunao Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa unahitaji wafanyakazi, tunao Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi wanapoumia kazini tunahitaji wafanyakazi na mfuko huo wa *private* wa *NSSF* tuliouanzisha unahitaji wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kifungu cha 87 ninaomba niwahakikishie kabisa kabisa ndugu zangu Wabunge wafanyakazi wako salama. Labda kutokee jambo ambalo kati ya hao wafanyakazi lazima utakuta kuna wengine labda maadili yao hayafanani na sekta yetu na inawezekana tu lazima watakuwa wapo, ama aina moja au nyingine ya mfanyakazi ambaye hatakuwa anaendana na sekta tunayokwenda kuijenga. Sheria za utumishi wa umma zimeweka ufafanuzi wa kila jambo na kwa namna hiyo basi tutaweza kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitolewa hoja hapa kwamba hii mifuko wakati mwingine imekuwa inakufa kwa sababu ya madeni.

Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani tulikuwa na madeni ya aina tatu kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Deni la kwanza kubwa ambalo ni la msingi lilikuwa ni malimbikizo ya michango ya wanachama yenye thamani shilingi za kitanzania trilioni 1.3, naomba kuwaarifu Wabunge fedha hiyo yote imekwisha kulipwa kwenye mifuko, fedha yote trilioni 1.3 tumekwisha kuilipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebakiza madeni mengine ambayo ni lazima yahakikiwe lakini vilevile yatengenezewe mfumo wa kuyalipa. Lakini wakati tunafanya utathimini wa mfuko tulijiuliza swali lingine moja la msingi, je, madeni haya ni sababu ya mfuko kama wa *PSPF* kutokufanya vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo hapa taarifa ya utathimini ambayo imejonyesha wazi. Ukiacha hata hayo madeni mengine kwa mfano ukauacha mfuko wa *PSPF* kama vile una kila kitu, mfuko huo maisha yake ni mafupi sana na Mfuko wa *PSPF* ulitakiwa uwe umekwisha kufa mwaka 2018 hata kama madeni yangekuwa yamelipwa yote. Lakini vilevile Mfuko wa *LAPF* na Mfuko wa *GEPF* ulikuwa unakufa mwaka 2049 na mifuko hiyo ndiyo ile mifuko ambayo pendekezo lake ilikuwa ichangiwe sasa kiwango cha uchangiaji kifike asilimia 30. Lakini Mfuko wa *PPF* maisha yake yalikuwa yanakwenda mpaka mwaka 2075 kwa kikokotoo cha moja chini ya mia tano na themanini (1/580). Mfuko wa *NSSF* uhai wake ni miaka 75 mpaka 85.

Sasa Waheshimiwa Wabunge ukishapata *data* kama hizi utabebaje hoja ambayo haina uchambuzi wa kitafiti kama uchambuzi ninaoutoa hapa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda mbali zaidi tukajiuliza hivi kwenye Mfuko wa *PSPF* wale wanachama ambao wako kwenye mfuko huo, kwa mwezi wanachangia shilingi ngapi na malipo ya pensheni zao kwa mwezi ni shilingi ngapi, tulilolikuta michango yao kwa mwezi ni shilingi bilioni 44 lakini mafao wanayolipwa ni shilingi bilioni 77. Sasa Waheshimiwa Wabunge hebu fanya huo ulinganishi na kwa sababu kikokotoo kilikuwa kimewekwa kwenye sheria unapokuja na matokeo sasa ya utathimini wa mfuko hali ilikuwa ni tete ya kutokuelewana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka sasa hivi turudi kama nilivyosema tukakae kwa pamoja, tujue mwenendo mzima wa namna tutakavyofanya kwa kukubaliana na wafanyakazi wenyewe na hiyo itatusaidia kutuweka mahali pazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba suala zima la deni la malimbikizo la michango ambalo lilikuwa kwa Serikali na baada ya kulipwa, inakupa nafasi ya kutathimini sekta na mifuko ilivyo hali yake ilivyo na nini cha kufanya, lakini sasa

kwa kutumia sheria ulizonazo za kazi ni lazima urudi ukakae na wafanyakazi wenyewe na mkishafanya utathimini mtakaa mtakubaliana, mtaelewaa na safari itakuwa salama zaidi. Ninaamini kwa maneno haya hata Mheshimiwa Bilago sasa ananielewa vizuri na nitamshukuru kama ataelewa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo tumepata pendekezo toka kwa Mheshimiwa Bashe linalohusu kuangalia kifungu cha 40 na 41 na kuona ni namna gani tunaweza kufanya ili kuona Makatibu Wakuu nao wanakuwa *considered* kwenye mfuko wetu na kwenye sheria ambazo zinaenda kueleza mfumo wa mafao yao. Jambo hili Waheshimiwa Wabunge naomba mtuachie ili turudi na tukalitafakari na tuone ni watu wengine wa aina gani ambao watashiriki na wao watahitaji kushirikishwa katika kufanya utathimini na kuja na pendekezo ambalo litabeba dhana zima ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie na fao la elimu tumewasikia Waheshimiwa Wabunge. Tutakachokifanya kwa sababu kifungu cha 29(3) kinatuelekeza kuangalia namna nzuri ya kuendelea kulipa mafao, kwanza niwahakikishie watoto wote ambao wanalipiwa fao la elimu hakuna mtoto atakayeacha kuendelea kulipiwa fao la elimu, hiyo tutaendelea kuwalipia na kama tutaona fao hili baada ya utathimini ni fao ambalo ni zuri ambalo linaweza kuwasaidia wanachama kwa kutumia kifungu cha 29(3) tutafanya hivyo na ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge muwe na imani na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango iliyoletwa na Wabunge ni mingi niseme tu labda tutaijibu ile ambayo tutashindwa kujibu, tutaijibu kwa kutumia maandishi.

Nimalizie kwa kusema Waheshimiwa Wabunge Muswada huu ni muswada unaowahusu wafanyakazi wa nchi Tanzania na kwa kuwa muswada huo toka tulipoanza tumefanya kazi ya kutosha kwa kushirikiana na wafanyakazi wenyewe kupitia Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania yaani *TUCTA*. Na kwa kuwa *TUCTA* wenyewe kwenye

barua niliyonayo na maoni haya wameridhia vipengele ambavyo vipo kwenye muswada huu. Ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa shughuli hii ina wenyewe na wenyewe ni wafanyakazi wa Tanzania, yale tuliyomesema tunakwenda kujadiliana na wafanyakazi, mridhie mtuache tukajadiliane na wafanyakazi na tutayarudisha ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana tusije tukatumia nafasi hii kuwaamulia wafanyakazi mambo ambayo ama hawatoyapenda ama yatakiuka misingi na taratibu zetu za kisheria za kutekeleza matakwa ya wafanyakazi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo niwashukuru sana sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa mara nyingine ninawaomba sana muunge mkono muswada huu. Muswada huu umefanyiwa kazi nzuri sana na Kamati, muswada huu unahitajika sana na wafanyakazi wa Tanzania, muswada umeweka mafao mengine mapya mengi ambayo wafanyakazi walikuwa wanayahitaji, muswada huu hatma yake ni makubaliano kati wafanyakazi na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana, hoja imetolewa, imeungwa mkono na Wabunge zaidi ya kumi. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

MWENYEKITI: Kamati ya Bunge Zima!

Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa
Watumishi wa Umma wa mwaka 2017
(*The Public Service Social Security Fund Bill, 2017*)

Ibara ya 1

Ibara ya 2

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 3

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwalimu Bilago, tuko
kwenye eneo la tafsiri.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti,
ahsante, kwenye kifungu hicho cha 3 naomba niisome; *"In
clause three by adding the word full pension and giving it
interpretation as follows: means an annual amount equal to
one divided by 540 of a members monthly pensionable
emolument for each completed monthly of each his
pensionable service multiplied by annual pensionable
emolument and this also shall be a competition formula."*
(Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa

MHE. KASUKU S. BILAGO. Naomba nieleze sababu.

MWENYEKITI: Hebu ngoja kidogo, unachopendekeza
yaani maana yake ndio unanza na maneno *means* si ndio
unakuja kuishia nayo wapi zile *comma*, mabano.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti,
kifungu hiki kilifutwa.

MWENYEKITI: Nakuelewa sasa nataka tu maana
umeingiza *this also shall be a competition formula*.

MHE. KASUKU S. BILAGO. Baada ya hii *definition* inayoongezeka ya hii *full pension* na ndiyo hiyo hiyo sasa itumike kama *formula*.

MWENYEKITI: Haya.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Ndiyo maneno hayo nataka yaongezeke hapo kwenye *three*.

MWENYEKITI: Maelezo sasa

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, maana nzima ya dhana ya kuunganisha hii mifuko na kwa maelezo Waziri ilikuwa ni kuboresha mafao ya wafanyakazi. Mafao ya wafanyakazi yaliyokuwepo kwenye mifuko yalikuwa na *formula* zake. Sheria nzima hii kifungu hiki kinalenga kuingiza *formula* kwenye muswada ili sheria inapotongwa iwe tayari ina kikokotoo chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati hii *full pension* inafutwa, ilifutwa kwa maana kwamba haikutajwa mahali popote lakini ina-*appear* kifungu cha 30. Kifungu cha 30 kinaendelea kuitaja *full pension* wakati haina *definition* mahali popote.

Kwa hiyo, iingizwe na kwa maana tu kwamba ili sheria inatungwa sasa iwe na kikokotoo cha 1/540 na kama haitaingizwa na kwa maelezo ya Waziri tunayoyasikia yanalenga kwenda kuipunguza 540 waathirika ni wale wote waliokuwa wanalipwa kwa kikokotoo walichoingia nacho mkataba wa ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wao wa ajira waliingia kwa 540; sasa kama 500 inapotea na kwa maelezo ya Waziri niliyopata sasa hivi, inaenda kupotea baada ya *actuarial evaluation* na nimeshauri kabla ya kufanya *actuarial evaluation* hakukutakiwa kuja *bill* humu Bungeni walitakiwa wawe wamekaa wote na *TUCTA* na hao wafanyakazi na watu gani ili watuletee walisha-*determine* kikokotoo halisi kitakachotumika kwenye sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo kuleta ikiwa hivi hivi kimya na tunaipitisha kimya wanaomba tuwaamini wakati mwingine huwa hawaaminiki hii ni kuwaumiza wafanyakazi. Kwa hiyo, hatuwezi kwenda kwa kuaminiana tu tuwaamini tutunge sheria ambayo itawasaidia wafanyakazi.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa hoja kama sitaridhika na majibu wa Waziri.

MWENYEKITI: Haya ngoja upewe maelezo tena. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutokuelewa vizuri mfumo wa uandishi alioutumia na hasa katika kuweka *comma* ina ina ina inasumbua kidogo kuelewa, sasa unapata shida ya kuelewa, lakini hata hivyo, nitarudi kwa Mheshimiwa Bilago kumwambia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naendelea kumsihi sana Mwalimu Bilago, anapopendekeza hiki kikokotoo nimesema toka mwanzo, anafahamu pia utathimini wa mifuko uliofanyika, sambamba na kikokotoo hicho kulikuwa na vitu gani vingine vya msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu anapotaka kukirudisha kikokotoo hiki kwa utathimini ambao umekwisha kufanyika na nataka kumkatalia kwamba anasema hatujafanya utathimini. Tumeshafanya na nimesema tumefanya mwaka 2010; tumefanya mwaka 2016 na tunajua tunachokifanya. Sasa mapendekezo ya kikokotoo hiki yanaendana sambamba na kuongeza *contribution rate* kwenda 30%. Sasa naomba kujua Mheshimiwa Bilago, umeshajadiliana na wafanyakazi na mmeshakubaliana kwamba *contribution rate* ya 30% wafanyakazi wanao uwezo wa kuilipa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tulipokaa na *TUCTA* na kuangalia utathimini ulivyo, tukakubaliana kwa pamoja na hawa wafanyakazi ambao ndiyo wenye Mfuko na hao ndiyo wenye hizo *pension* zao. Wakaomba sana ili tuendane sambamba, ili sheria hii iwe na manufaa ya kikokotoo chenye tija kwao, turudi kwenye *regulation* tukajadiliane alafu tumalize huo mjadala, tuwe na kikokotoo halisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, unapoendelea kuweka kikokotoo kwenye sheria, pale ambapo mfuko utakuwa umekuwa ama umepungua kwa hiyo kila siku kazi itakuwa ni kurudi kufanya tena mashauriano? Kwa sababu wenye uhitaji wa huu mfuko wamesharidhiana na sisi, na nimewaambia hata Mheshimiwa Bilago alikuwepo kwenye Kamati, *TUCTA* walisema nini na ninayo *document* ya *TUCTA* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasihi Waheshimiwa Wabunge, tuacheni Serikali kwa kutumia sheria za Kazi tulizonazo. Tukakae na wenye muswada wao wafanyakazi, wakiridhia kikokotoo kiende 30% tutarudisha hiyo moja chini ya 540. Lakini wakisema kwamba tuitazame *industry* nzima tutafanya yale ambayo mwisho wa siku yatakuwa na tija kwa wafanyakazi. Mimi na Serikali yangu tunawajali wafanyakazi na ndiyo maana tunataka kuwapa nafasi ya majadiliano. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kabla Mheshimiwa haujaendelea, hebu isaidie Kamati. Endapo Kamati itakubaliana na pendekezo lako kwamba tuwe na *definition* hiyo, nichukue basi kwenye *main body* ya muswada ni wapi tunatumia neno hilo ili wakuelewe vizuri.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kifungu cha 30 kimeelezea vizuri kabisa kwamba itakuwepo *full pension* na itakuja kwenye *movement* yangu ya pili, kwa hiyo kwa sababu ipo kwenye *section 30* iki - *appear* kwenye *distribution* kwenye fasili ni sahihi zaidi. Lakini sambamba na hilo Mwenyekiti kama kuunganisha mifuko

kunaokoa gharama, gharama hizo hizo ndizo zinaweza zikashusha uendeshaji ulikuwa mkubwa, kwa hiyo, inakwenda kumuweka Waziri pazuri zaidi kuliko kung'ang'ania kwamba gharama zitakuwa kubwa mifuko itakufa mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni sababu ya kama tunaokoa gharama ma-*MD* wote wanastaafu, tutakuwa na *MD* mmoja tu. Kwa hiyo, naomba nitoe hoja Mwenyekiti Wabunge waweze kunisaidia kujadili hoja hii.

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Taarifa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Wewe tupo kwenye Kamati, Kamati hamna taarifa wewe, unafikiri tunachunga ng'ombe hapa wewe. (*Kicheko*)

MWENYEKTI: Kwenye Kamati hakuna taarifa, Mheshimiwa sjavaa miwani yangu, niwie radhi kwa nyuma hapo nani? Haya tuitendee haki hoja ya Mheshimiwa Mwalimu Bilago. Tunaanza na Mheshimiwa Grace Tendega.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bilago kama alivyoelekeza .

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukijadili katika Kamati yetu kulikuwa na *full pension* ambayo ilikuwa ni *definition* imewekwa vizuri kabisa pale, ikiwa inaonyesha ni moja kati ya 580 na katika hiyo tunaona kwamba katika kifungu cha 30 maelekezo tuliyopewa ni kwamba itafutwa wataielekeza kwenye Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini, katika hii, *bill* iliyoletwa tumeiona bado ipo pale na kikokotoo chake bado imewekwa *full pension* na kwenye *definition* hakuna. Kwa hiyo, naunga mkono Mheshimiwa Bilago anavyosema kwamba tuiweke lakini kikokotoo kiwe 540 kama ambavyo

wadau walikuwa wametoa mapendekezo na kwa sababu mifuko hii lengo lake ni kuboresha maslahi ya wafanyakazi na kwa sababu tunataka tuwaboresha ni vema wakapata kikokotoo ambacho walikuwa wakikitumia mwanzoni kuliko sasa hivi tukiweka kikokotoo cha 580. (Makofi)

Kwa hiyo, naunga mkono hoja ili hiyo *full pension* iwekwe kwenye *definition* na iwekwe badala ya 580 iwe 540. Kusema kwamba *actuarial valuation* itafanyika tena na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba walikwishafanya *actuarial valuation*, sawa *actuarial valuation* kama ilifanywa lakini anasema tutaweza kushusha tukiweka kwenye kanuni inaweza ama ikapata ama ikashuka. Kwa nini mmewahisha *bill* ikaja kabla ya kuweka *actuarial valuation*?

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani jambo jema kwamba tungemaliza kabisa *actuarial valuation*, ndiyo *bill* ije tuweze kuijadili na kujua hicho kikokotoo. Bila kuweka kikokotoo kwenye hii *bill* ... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako, Mheshimiwa Richard Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Serikali ndiyo inapashwa kuungwa mkono kwa sababu kwanza Wajumbe ambao wanachangia hapa walikuwa kwenye Kamati husika. Sijui nashangaa kwanini hawakumaliza kule. Narudi kwenye hoja, kifungu cha 30 kimetoa ruksa ya kwenda kwenye *regulations* na kule kwenye *regulations* kwa maelezo mazuri ambayo yametolewa na Serikali kwamba wadau watashirikiswa wote na Waheshimiwa Wabunge unavyofanya *actuarial evaluation* sio kwanza *evaluation* ni *valuation*. *Factors* zipo nyingi za kuangalia na inafanywa na wataalam husika, sasa katika vigezo vya kwenda kuangalia lazima uangalie mtu huyu kwa miaka aliyofanya kazi amestaafua amewekeza shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, makato ambayo amechangia ni Milioni 15, katika *formula* ambazo mtakazozileta ambazo hazina tija anapewa labda milioni 40. Hii milioni 25 zimewekezwa wapi mpaka akafikisha pale? Ndiyo matokeo yake Mifuko inakuwa kwamba sio stahimili, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Serikali, Kifungu kibaki hivyo hivyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na mimi ninaunga hoja mkono ya Mheshimiwa Bilago kwa sababu kuu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza maelezo ya Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba wamefanya *actuarial valuation*, sasa suala ni kwamba kama wameshafanya wamegundua hii mifuko *life span* yake ni muda gani? Na kama wameshagundua hiyo *prediction* kwani kurudi baada ya miaka 50 kwa mfano, kurudi tukabadilisha sheria kutakuwa na shida gani? Kwa hiyo, nasema kikokotoo hiki ni muhimu sana kwa sababu kitaonesha ni jinsi gani huyu mtu, huyu *pensioner* mwisho wa siku anapata kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe najua ni mtaalam wa Sheria kwa sababu hili jambo kwenye Kamati, ukiangalia muswada wetu wa awali hii tafsiri ilikuwepo na hicho kifungu 30 kinaelezea *full pension*. Sasa kama hakipo kwenye *interpretation*, hatuoni kwamba hili ni tatizo kubwa?

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba kwa kuwa wamefanya *valuation*, kama bado maana nimeongea na Waziri bado anasema wanataka kufanya *thorough actuarial valuation*. Kama wanataka kufanya hiyo *thorough* kwa nini wametuletea muswada kabla hawajakamilisha hiyo *thorough valuation* ili sasa wananchi wajue kikokotoo chao au wafanyakazi ni cha nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme huu muswada sio ni wafanyakazi lakini sisi Wabunge ndiyo tunajua pia ni mambo

gani ambayo tunataka tuwasaidie wafanyakazi wa nchi hii. Kwa hiyo, nadhani kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba hiki kikokotoo kinakuwa *interpreted* kama ilivyokuwa awali na watu waje, wafanyakazi hao waelewe wanapoingia kwenye hii mifuko watapata nini baada ya kustaafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja ya Mwalimu Bilago, mwalimu mwenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anazungumza mwanzoni na alipokuja kumaliza amepiga siasa sana kwa kweli. Kwa sababu anajichanganya. Wewe umesema umeshakutana na Wafanyakazi mmekubaliana, tunataka makubaliano hayo hapa. Kwa nini hayawekwi *no*, hayo sio makubaliano. Unasema mrudi mkajadili eti mlshakutana mkajadili mkakubaliana, mnarudi kujadili kitu gani tena? Karatasi hiyo Mheshimiwa Waziri unayo peke yako, yaani unaweza ukaamua ukaichana na ukabadilisha unachotaka kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yetu ni kwamba kama *issue* yakusema kwamba inaweza ikapanda ikashuka sio hoja ki-*mathematics*. Kihesabu inahesabugwi wote kama ni moja ya 540 umesema mshahara wake ni X ukizidisha utapata *product* pale mbele. Haina shida, yaani hii ndiyo hoja ambayo ukiwa na *formula* huna malalamiko yoyote na mfanyakazi yoyote. Kwa sababa *formula* inafahamika *value* yake ikibadilika thamani imeshuka, imepanda anajua yaani huna mgogoro naye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya kutunga sheria ambako hatutakua na nafasi ya kuja kujadiliana mrudi kujadili kwa kweli maana yake ni kwamba ama kazi hajifanywa au kazi imefanywa unaficha ukweli au Bunge halitungi kitu hakieleweki. Na kwa kweli sina muda mrefu

sana sijawahi kuona sheria ambayo tunapitisha hapa wakajadiliane waandae wenyewe ukaache na wadau. Na hoja ya kutuambia kwamba hii ni kazi eti hii sheria ni wafanyakazi wenye ngoma hizi ni mbwembwe za mtaani, haina maana yoyote humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Sheria tujadiliane kwa maana na mujibu wa sheria tutunge, hao wafanyakazi hawawezi kutunga ndiyo maana wameleta kwenye Bunge. Kwa hiyo, tufanye kazi ya Kibunge tusifanye kazi ambayo kuna maswali ya kuuliza, *formula* ilipaswa iwekwe hapa tupitische ili tusiweze kuuliza.

Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mwalimu Bilago na Mheshimiwa Waziri na Wabunge wenzake wa CCM wasilete msimamo ambao kimsingi haupo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waitara. Mheshimiwa Nchambi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: *Wabheja* sana Mwenyekiti!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunajadili mambo ya msingi ni bora tukaweka siasa pembeni na tukaweka maslahi ya Taifa mbele. Nimemsikiliza kwa makini shemeji yangu kutoka Kigoma na kule kuna msemu unasema *maghambo Bukhebukhe* (mambo ni polepole). Kilio hiki, cha wafanyakazi naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, kila sherehe za Mei Mosi zinapofanyika, moja ya kilio kikubwa cha wafanyakazi katika Taifa letu ni kuleta ombi la kuunganisha mifuko hii kwa pamoja. Maombi haya yamekuwa yakitoka, kwa bahati nzuri Mtemi Chenge Mheshimiwa Mbunge wewe unajua mimi nimelelewa katika chama hiki na nimekuwa mstari wa mbele katika kushiriki shughuli mbalimbali za Serikali.

Kwa hiyo, hoja yangu ni kuonesha hisia kwa wenzetu wageni ambao wanakurupuka na waliodandia treni kwa mbele. Sisi tuliingia wakati treni ile ikianza safari, enzi ya Mwinyi Mheshimiwa Mwinyi, Mheshimiwa Jakaya Kikwete,

Mheshimiwa Mkapa na sasa juzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ni namna wafanyakazi wanautashi na ushawishi mkubwa wa kuona mifuko hii inaunganishwa kwa pamoja. Tukipata msingi wa jambo hili kuwa umetokana na wafanyakazi wenyewe, ndipo tutakapojenga hoja ya msingi ya kuona namna ni gani tatizo hili tunalitatu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu pia nikufahamishe kuwa wenzetu ni wavivu wa kusoma. Hata, katika nyumba za Ibada tunazokwenda, nyaraka nyingi ambazo wanatakiwa kuzisoma waumini wanakuwa wavivu na wanaishia kulalamika. Wenzetu hawajasoma, ukisoma ripoti ya *ILO actuarial valuation* ya mwaka 2016...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa ... (Makofi/Vigelegele)

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Naunga mkono hoja ya Serikali. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea, Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ni nioneshe kwa nini siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Bilago.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uweze kupata kikokotoo lazima uwe na *guidelines*, na ili ufanye *actuarial valuation* lazima uongozwe na *guidelines*, na *guidelines* zinapatikana pale tu ambapo utakuwa umeiunganisha hii mifuko na ukisha unganisha hii mifuko utapata *new guidelines* ambazo zitakueleza sasa unawezaje kutengeneza hiyo *formula*. (Makofi)

Sasa mifuko haijaunganishwa ili ije na hizi *guidelines* mpya, unapataje hiyo *denominator* unaipataje sasa. Lakini Mheshimiwa Bilago hapa ametumia ujanja mkubwa, na mimi nikupongeze we ni mjanja. Anataka kuturudisha nyumba

tuiharibu kabisa hii Sheria yote, sasa sidhani kama kuna mtu yupo tayari hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kazi iliyofanyika ni kubwa na Kamati imefanya kazi kubwa. Nataka nikuhakikishie kwamba hauwezi ukapata hicho kikokotoo kwa sababu hiyo *section 30* imekuwa *coached* katika utaalum ambao sasa inatengeneza sheria nzuri zaidi kulliko ile ilivyokuwa zamani. Maana inasema itazingatia *The Regulatory Authority Act, section number 25A* ambayo inaelezea namna ya kupiga hizo hesabu. Sasa ukishazingatia hiyo ile maana yake utakuwa salama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti nimalizie, hivi dhana ya kwamba Sheria Ndogo ni mbaya inatoka wapi? Yaani kwamba *by-laws* sheria nzuri! Hapana kwa sababu Bunge hili lina Kamati inayoshughulikia sheria ndogo na kwamba zikitungwa zinaletwa huku huku Bungeni zinaangaliwa kwamba zimezingatia Katiba, zimezingatia Sheria nyingine, zimezingatia matakwa na maelekezo ya wakati wa utungaji wa sheria zingine ikiwemo sheria hii. Maana lazima tunapotaka kutafsiri sheria ndogo lazima tuianze kwenye sheria mama zinazozalisha kutungwa kwa Sheria hii. Katiba inasema, sheria nyingine zinasema ndiyo unapoi-*verify* kwamba hii Sheria hii imekidhi matakwa ya utungwaji wake hata kama inatungwa na *Executive*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo dhana hii ya kuondoa mfumo ambao upo kwamba hatuaminiani kwa kiasi hicho...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Simbachawene. Mheshimiwa Haonga.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Naunga mkono msimamo wa Serikali. *(Makofi)*

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimegundua kwa nini kuna watu walipoteza Uwaziri kwa

sababu haya mawazo... (Makofi) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa RAsmi za Bunge]

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mheshimiwa Haonga.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Kuhusu Utaratibu.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo.

MWENYEKITI: Futa kauli hiyo.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeifuta hiyo, nimeshaifuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mwalimu Bilago hapa ni kwamba hicho kikokotoo (*denominator 540*) kiingizwe kwenye kanuni. Na kama tunakubali kwamba kuna *by -laws* kwa nini sasa tusikubali kuiweka hiyo kama ikileta matatizo baadaye tunaweza pia kutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutunga sheria mkishatunga sheria kwenye Bunge hili, hizi sheria wakati mwingine zikisha tumika tukiona kwamba kuna shida baadaye hamna ubaya wowote kuja kurudi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni maslahi mapana ya watumishi. Watumishi wetu amezungumza Mheshimiwa Mhagama pale, watumishi wetu wamekuwa wakilalamika sana Mheshimiwa Mhagama wanalalamika sana kwa sababu *pension* yao inaonekana kwamba wanapata kidogo kwa sababu ya kile kikokotoo, sasa kumruhusu Waziri peke yake akakae peke yake chumbani na anatengeneza kile kitu, halafu tunadanganywa kwamba anaenda kukaa na wale wawakilishi kwa mfano vile Vyama vya Wafanyakazi hii sio sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba Mheshimiwa Jenista Mhagama naomba ukubali tu, kwamba tuingize kikokotoo hiki cha 540 ili tuwasaidie watumishi wetu wamelalamika wa muda mrefu sana kama ikaleta matatizo bado tutarudi tu nafasi hiyo bado tunayo, Ahsante sana lilikuwa ndilo hilo tu.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea, Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Bilago, lakini pia nimeshangaa kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumelijadili sana kwenye Kamati, na naomba leo niseme mbele ya Bunge hili, walioleta maoni ya kuomba kikokotoo kisiwekwe kwenye sheria ni watu wa *TUCTA*. Sasa huyu nani ambaye kiatu asicho vaa yeye kinamuhangaisha? Na waliokuja na hoja hukuwepo kwenye kamati usipige kelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliokuja na hoja hapa ya kikokotoo hiki ni chama kimoja *ATE* wakawajibu msitrudishe nyuma na *TUCTA* wakawajibu msitrudishe nyuma, tukakaa kama kamati tukakubaliana tukasema jambo hili liondolewe kwenye sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu kama tumemsikiliza vizuri Mheshimiwa Jenista, mimi nashangaa mtu leo akihangilia jambo hili. Tumeambiwa *funding level unless* hatuelewi maana ya *funding level*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *funding level* ya *PSPF* ilikuwa imefika asilimia 6.2 maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba leo ukiwaambia *PSPF* tunafunga hawawezi kulipa *liability* zaidi ya asilimia 6.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa *PSPF* ilipofika ilikuwa mtu akistaafu anachangiwa na watu watano. Lakini *ILO* inasema ili mtu apate *pension* lazima achangiwe na watu

25, mnataka tukae hapa Bunge hili na sisi tuwe sehemu ya kutunga sheria inaenda kuua mifuko naomba nisiwe sehemu ya sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasema *actuarial valuation* hakuna, *actuarial valuation* mwaka 2010 ilikuwepo, *actuarial valuation* 2016 na unaona wanakimbia suala la kuongeza asilimia 30 hamna anayesema. Wewe ni Mwenyekiti wa Kamati Ndogo unajua Serikali ikishatunga kanuni wanazileta kwenye kamati yako, kwa hiyo bado *role* ya Bunge ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wewe unajua umekuwa *Attorney General* wa nchi hii huwezi Waziri ukatunga kanuni peke yako chumbani, ukishamaliza kutunga kanuni unawapelekea wadau. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa umechangia vizuri.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashawishi Wabunge tusikubali hoja ya Mwalimu Bilago. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, ahsante tumsikilize Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, nadhani kama Serikali imefanya *actuarial valuation* kama wanavyosema, jukumu la msingi lilikuwa baada ya hiyo *valuation* kikokotoo ni kiasi gani, mkiweke kikokotoo kiwe kizuri ama kiwe kibaya ili Wafanyakazi wa Watanzania waweze kupima utendaji kazi wenu kwenye hii mifuko kwa kipindi cha miaka 56 ya utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, jukumu la Bunge ni kutunga sheria, Kamati imefanya kazi nzuri, lakini kazi kubwa ambayo Kamati imefanya ni kutoa mamlaka makubwa kwa Waziri na kwa *SSRA* kwenye mambo ya msingi sasa Waziri tu anisaidie, kama kikokotoo ilikuwa ni shida kwa

nini kwenye muswaada wa kwanza mlikionyesha kikokotoo?
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbaya zaidi Kifungu cha 57 kipitie. Kifungu cha 57(1), 57(2) kina ainisha wazi kabisa kwamba *actuarial valuation* ambayo inatusaidia kujua *assets* na *liability* ya shirika letu likoje, uhai wa shirika ikoje. Hapa imeonekana kwamba inaweza isifanyike soma kifungu cha 57(1) kimetoa *mandatory* kufanya miaka mitatu, lakini kikaenda mbele sana au muda mwingine wowote. Kifungu kidogo cha (2) kinasema kabisa kwamba bodi inaweza ikaomba ruhusa na ikiomba ruhusa *actuarial* isifanyike.

Sasa tupo kwenye mazingira ambayo *actuarial valuation* ndio itatu-*guide*, lakini sheria hii hii inatoa kificho, kwa hiyo, matokeo yake mashirika yetu yatakuwa yanaendeshwa tukitaka kwenda kutaka wataalam wa masuala ya *risk* ili tujue *assets* na *liability* kuna kifungu kinasema sio lazima tuangalie. Kwa hiyo, tutafunika kombe mwana haramu apite mifuko inazidi kupata, wananchi wanazidi kuumia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sio sahihi kusema eti *TUCTA*, wametuingia, nchi hii ina Vyama vya Wafanyakazi vingapi? Kwa hiyo, *TUCTA* wakija ndio wame *represent* wafanyakazi wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme hivi, nashukuru Mheshimiwa Serukamba alisema hivi *the law does not apply retrospective* ulisema vizuri, hoja nyingine ya Mwalimu inasema, kwa wale wafanyakazi ambao waliingia mikataba, mikataba wakasema... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa
Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa ahsante sana, Mheshimiwa muda wako umekwisha ahsante, Mheshimiwa Bashe tumalizie.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyiko juu ya 540 ama 580 ulikuwa ni *dialogue* ya *almost* siku mbili ndani ya Kamati na tukafikia *consensus* kwa *actuarial valuation* iliyofanyika, Serikali ikafanye tena baada ya kuunganisha mifuko yote kuangalia *asset and liability* ili iweze ku-*determine* itumike *denominator* ya ngapi? Tuliuliza swali *why 540, why not 520, why not 400, why not 580?* Swali hili litaenda kujibiwa baada ya kufanyika kwa *evaluation* ya mifuko hii baada ya kuunganisha *assets and liability*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili Mheshimiwa Dada yangu Halima ametumia kifungu cha 57 tukisome tu wote na mimi nilipata mchanganyiko kama wa kwake. Kinasema; *"The board shall at interval of three years or at any other intervals as the authority..."* na tunapo zungumzia *authority* tunamzungumzia *regulator SSRA*, *"...may direct and subject to guidelines issued by the authority..."* zipo *clear guideline* zilizokuwa *issued* na *authority* ya *SSRA* namna gani ya kufanya *valuation*. (Makofi)

Lakini *sub section (2)* ambayo inasema *notwithstanding subsection (1) the board may not shall owing to the natural and circumstances. This is very clear*, suala ya *actuarial valuation* liko *very clear* na linasimamiwa na utaratibu wake, kwa hiyo, *we expect* Serikali haitovunja sheria, lakini kama tunakuja Bungeni tunataka kupitisha sheria ambayo sote tunafahamu kwamba itaenda kuua hii mifuko *we are not going to be fair for this country* na kikubwa ni kutokuaminiana, lakini ipo kamati ndogo ya sheria ambayo ina jukumu la kupitia hizi kanuni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye mchakato huu kuna utatu mtakatifu wa mwajiri, Serikali na Vyama vya Wafanyakazi, hatuamini kwamba Serikali itaenda kutunga kanuni bila kupitia mchakato huu wa kisheria ulioko, hatudhani kwamba Mheshimiwa Jenista atajifungia chumbani lakini niseme na niseme hapa kwenye Bunge hili, hakuna njia nyingine *we have two choices* kufanya maamuzi kwa moyo tukaue mifuko, hii tunayotaka ya kwenda kuweka 540 ambayo leo *PSPF* ime-*suffer* na ina *create* shimo la zaidi

ya 300 billion shilling a year. This is the only best way ambayo tunayo kama nchi kusaidia mifuko hii na kusaidia wafanyakazi wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa sote wafanyakazi wapate 540, 520, 500 *whatever good denominator* ambayo itatupatia mafao makubwa. Kwa hiyo, ningemuomba kaka yangu mwalimu Bilago...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, ili tuweke mambo sawa kifungu cha 57(1) kama mnataka tukisome mimi nitawasomea mkielewe tu, tunasema hivi; *The board shall sikiliza sasa, The Board shall cause asset liability of the fund to be evaluated by an actuary.* Lini ndiyo unarudi *at intervals of three years or at any other intervals as authority may direct any subject guideline issued by the authority.* (Makofi)

Ukisoma ndio maana *comma* hizi zina maana sana ile *shall* inabaki pale pale *interval* lini wafanye na kuzingatia sasa utaratibu ambao *regulator* ameweka, bila kujali kifungu kidogo cha kwanza *board* yaweza, yaweza sio lazima, sasa katika mazingira yanayokutegemea na hali ya biashara ndio nilikuwa nasema ukiisoma kwa namna hiyo wala mkanganyiko wowote hasa. Nimuite Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu sasa naye aseme yale ya kisheria ili tuweze sasa kuiamua hoja hii kabla sijamwita mtoa hoja.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuchangia kwenye hoja hii, na ninaunga mkono moja kwa moja hoja ya Serikali kama ilivyo kwenye muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wote tunavyofahamu muswada huu una maslahi makubwa sana kwa wafanyakazi, ni muswada ambao moja kwa moja unagusa maslahi

muhimu ya wafanyakazi na wafanyakazi wana taasisi muhimu ya kuwasemea na taasisi hiyo ni Shirikisho la Wafanyakazi la Chama cha Wafanyakazi Tanzania (TUCTA).

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Bunge lako Tukufu, limeweka utaratibu kwenye kanuni ya 84(2) kwenye kamati kuwashirikisha wadau kwenye mchakato wa kuunda sheria na Shirikisho hili wameitwa wameleta maoni haya lazima tuheshimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo sheria ya kwanza ambayo tumewashirikisha wadau, kila sheria inatungwa tunawashirikisha wadau, leo kwa sababu tuna hoja fulani tofauti tunasema tunataka ku-*down play role* ya wadau kwenye hii tena wadau ambao wameleta haiwezekani sisi tukaguswa sana na maslahi ya wadau/wafanyakazi wale kuliko wafanyakazi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni hili, kwanza sio kila neno kwenye sheria lazima lipate tafsiri sasa utatunga sheria ya aina gani hiyo kama *full pension* kwa mfano unatafuta tafsiri, *can't you take it seven so much literary*, lakini kama unataka tafsiri pia ipo kwenye kifungu chenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu chenyewe cha 30 kinaitoa hiyo tafsiri kama unaitaka tafsiri ya *full pension* sema; *a full pension* naisoma *a members who has attained the age of retirement and has contributed to the fund for the period of not less than one hundred and eight months shall be entitled to a full pension constituted of commuted pension and monthly pension calculated and payable in accordance with the formula prescribed in regulations this is in itself a definition.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani hii yenyewe ni tafsiri inakupa tafsiri ndio, kwa sababu *formula* si ndio *formula* inakuongoza inakupa tafsiri, *that is it* na hii siyo sheria ya kwanza pia inayotoa mamlaka kwa Waziri kwenda kutengeneza *formula*, tunatunga sheria chungu mzima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, hizi sheria ndogo hizi ni sehemu ya sheria ni sawa ni sehemu ya sheria mama kwa mujibu wa kifungu cha 41 na cha 42 cha Sheria ya Tafsiri ya sheria na sababu za msingi zimetolewa na Mheshimiwa Waziri na Wabunge wamesema kwa nini hii haiwezi kuwekwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi kwamba moja kama ambavyo Katiba ya nchi inatafsiriwa na sheria hizi mama, kanuni ndizo zinatafsiri sheria na hiyo inasababisha utekelezaji wa sheria.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja hii ya Serikali kama ilivyo kwenye muswada na hili la pili ibara 57 ya muswada kiti chako kimeitolea tafsiri sahihi kama ambavyo na Serikali imeshakwisha kutoa na ni kwa hekima yako kwa sababu tungetegemea kwamba kama kungekuwa na *schedule of amendment* ambayo imekuwa *moved* kujadili ibara ya 57 *then could have considered in this one accordingly*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aendelee kukubariki sana kwa hekima uliyonayo baada ya mwongozo huu ambao nakubaliana nao naomba kuwashauri Waheshimiwa Wabunge wote tuunge mkono hoja hii, huu ni muswada muhimu kwa maslahi ya wafanyakazi na watumishi wote wa umma. Ninayezungumza, pia ni mtumishi wa umma na mimi najulikana kama kitu hiki kingekuwa cha hovyoyo ningekataa tu hapa hapa, na mimi nawafanyakazi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hoja hizi za Mheshimiwa Waziri ameeleza sana wakati wa *winding up*, Waheshimiwa Wabunge wanaounga mkono hoja hii ya Serikali wamelifafanua vizuri sana, Mheshimiwa Mwenyekiti umetoa mwongozo kwamba kwa mara nyingine kwa nidhamu kubwa sana naomba kuishauri Wabunge wote tukubali hii hoja ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukikubali tu *assuming* kwamba tunakubali hivi *proposal* hii ina kichwa wala miguu, hii *definition* yenyewe hii hapa ...

MWENYEKITI: Tulianza nayo. (*Kicheko*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti Mungu akubariki sana, naunga mkono hoja ya Serikali. (*Makofi*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Ahsante sana AG, ahsante sana. Hapana Waheshimiwa Wabunge tupo kwenye *process* ya msingi sana hapa, na mniwie radhi *sometimes* na mimi naghafirika kidogo.

Lakini tuone sasa, narudia na jamesemwa na ninyi mliokuwa mnachangia, Bunge hili haliwezi likafanya kazi zote na ndio maana tunafanya kazi nyingi kwenye Kamati, mmeipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Huduma ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri ambayo inaonekana, kwa siku nane kama ripoti inavyosema wamefanya kazi na tunaona.

Sasa kwa vile muswada huu pia una maslahi mapana ya wafanyakazi wa nchi hii, ndio maana ule utatu wao umeshirikishwa kikamilifu na mpaka wakafika kwenye eneo la sasa la kikokotoo wakasema bwana hapa twende hatua kwa hatua ndio ninavyoliona mimi kwa maelezo ya Serikali hasa sisi kama Bunge sasa hivi tupo kwenye kamati tusipoisikiliza au kuyasikiliza maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge iliyoleta taarifa yake Bungeni tutakuwa tunafanya vitu ambavyo kusema kweli ni ... mimi naomba tullione hili, na sitaki kushawishi Kamati hii ya Bunge Zima lakini nataka mlione hili kwamba... (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Kamati hizi zinafanya kazi kubwa ya kuchambua haya kwa niaba ya Bunge ili sasa *unless* kuna hoja ambayo wame-*over look* ndiyo unaweza sasa Mbunge ukasema hapa Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti suala hili halijakaa vizuri naomba ni-*move amendment*. Hiyo ni haki yako lakini kama limefanyiwa kazi kama katika hali ambayo tunayo sasa hivi, mimi nadhani tuendelee kuheshimu taarifa

za Bunge zinazowasilishwa Bungeni. Niliona niyaseme hayo sasa nitamwita mwenye hoja aweze kuhitimisha hoja yake halafu twende mbele tuiamue.

Sasa naongeza muda kwa mamlaka niliyonayo kwa nusu saa, tumalize kazi iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwalimu Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tunaingia kwenye historia ya kutunga sheria inayokwenda kumaliza mafao ya wafanyakazi na kama kuna mtu anapingana na hili kwa kuiona sheria ina maslahi mapana, upana wa maslahi ungeonekana kama kuna *formula*. Kama hakuna *formula* unajuaje huo upana wa maslahi? Na ninawahakikishia Wabunge wenzangu, wale wafanyakazi waliokuwa wanalipwa *540 denominate* na hawataipata. Hiyo dhambi tutabeba wote humu. Kama itakuja 540 waliokuwa wanalipwa 580 watashangilia. Lakini kwa dalili zilizopo hakuna 540, itakuwa *above that* na ninawashangaa Wabunge wa CCM kabla ya leo tulikuwa tunaelewana hili vizuri tu, sasa leo sijui mmelishwa nini! Walikuwa wanasema hili tutakomaa nalo hawawezi kukomaa leo. (*Makofi/Kicheko*)

Naomba kwa wingi wenu, niombe kwa sababu ya wingi wenu tuliamue hili kwa kura mimi ni-*keep record* ya kutetea wafanyakazi wa nchi hii mpaka mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba liamuliwe kwa kura. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa nawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Mwalimu Bilago. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kukataliwa*)

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
kwa kuwa Serikali yenyewe ilikiri ni *typing error* peke yake basi
nimeondoa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu cha 30 inasema hivi; *by deleting the words prescribed by the Authority pass one to section 2 A of the Social Security (Regulatory Authority) Act.* Nilitaka isome hivi kama mngekuwa mnakubaliana na mambo mazuri; *“A member who has attained the age of retirement and has contributed to the fund for the period of not less than One hundred and eight month shall be entitled to a full pension constituted of a commuted pension and a monthly pension calcuted and payable in accordance with the formula prescribed in the regulations,”* ingeishia hapo.

Haya maneno ya *prescribed by the authority pursuant to section 25A of Social Security (Regulatory Authority) Act* yangefutika na kwa vile yangefutika haya maneno basi hii ingekuja kufanana na ile tuliyokuwa tume-*define* kwenye *full pension*. Kwavile ile imegoma kwa wingi wenu basi na hii niache haitakuwa na maana kama hii itaondoka na ile haikuwepo tena.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bilago, kwanza utungaji wa sheria tu tuelewane, ukiishia tu *the regulations* haina maana, inapoteza kabisa maana. Hatuwezi kutunga sheria ambazo hazieleweki kwa watumiaji na hili ni Bunge hapa ndio tunatunga sheria. Hata kama ungekuwa una-*accept* hiyo uliyoanza nayo huwezi ukaishia hapo. *Made* na nani lazima ziwe *made by a certain authority* ambalo Bunge hili linakasimu madaraka ya kwenda kutengeneza kanuni hizo.

Kwa hiyo, lazima utaje Waziri, sasa Waziri anazitengeneza zile kwa mujibu upi, inakuelekeza sasa nenda kwenye sheria nyingine inaitwa *The Social Security Regulatory Authority Act* kifungu cha 25A, ndio tunachohama. Tena ni uandishi rafiki kabisa. Hivyo usifike huko kwamba kwa sababu hili limekufa na hili sasa hapana, hapana, hapana. Kwa uandishi wa sheria mapendekezo yako hayawezi kukubalika

kwa sababu yatakuwa yanapoteza maana tu inayokusudiwa. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati yaBunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64

Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71
Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74
Ibara ya 75
Ibara ya 76
Ibara ya 77
Ibara ya 78
Ibara ya 79
Ibara ya 80
Ibara ya 81
Ibara ya 82
Ibara ya 83
Ibara ya 84
Ibara ya 85
Ibara ya 86
Ibara ya 87
Ibara ya 88
Ibara ya 89
Ibara ya 90
Ibara ya 91
Ibara ya 92
Ibara ya 93
Ibara ya 94
Ibara ya 95
Ibara ya 96

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 97

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 98
Ibara ya 99
Ibara ya 100
Ibara ya 101
Ibara ya102
Ibara ya103
Ibara ya 104

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 105

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 106
Ibara ya 107
Ibara ya 108
Ibara ya 109
Ibara ya 110
Ibara ya 111
Ibara ya 112
Ibara ya 113
Ibara ya 114
Ibara ya 115
Ibara ya 116
Ibara ya 117
Ibara ya 118
Ibara ya 119
Ibara ya 120
Ibara ya 121
Ibara ya 122
Ibara ya 123
Ibara ya 124
Ibara ya 125
Ibara ya 125

Ibara ya 126

Ibara ya 127

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Jedwali la 1

(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imekamisha kazi yake.

(Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa hoja taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imeupitia Muswada Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa mwaka 2018 yaani *The Public Service Social Security Fund Act 2018* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono na zaidi ya Wabunge kumi. Nitawahoji sasa muiamue hoja hiyo. *(Makofi)*

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

MWENYEKITI: Katibu!

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kwa madhumuni ya kutoa Mafao ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi Walio katika Utumishi wa Umma na kufuta Sheria ya Mfuko wa Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Watumishi wa Umma, Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa LAPF, Sheria ya Mfuko wa PPF na Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa *GEPF* pamoja na mambo mengine yanayohusina na hayo *(A Bill for an Act provide for establishment of Public Service Social Security Scheme to provide for contribution and to the payments of social security benefits in respect of the service of the employee in The Public Service Retirement Benefit Act, The LAPF Pension Fund Act, The GEPF Retirement Benefits Act and The PPF Pension Fund Act and to provide for other related matters).*

(Kusomwa Mara ya Tatu)

(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Ahsante, hapo ndio tumepitisha huu Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kwa mwaka 2017 *(The Public Service Social Security Fund Bill 2017)* ndio umepitishwa na Bunge rasmi katika hatua yetu ya Bunge kama *National Assembly*. Itaenda kwa hatua za Kikatiba na kwa mujibu wa Kanuni kwa Mheshimiwa Rais kama sehemu ya pili ya Bunge kwa idhini yake.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwashukuruni sana ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa kazi ya kihistoria mliyoifanya leo, mtakumbukwa kwa Bunge la Kumi la Kumi na Moja mtakumbukwa na Taifa hili kwamba mlifanya maamuzi ya Msingi sana katika maslahi mapana ya watumishi wa umma katika mifuko hii na ninaamini kazi hii na jasho lililotolewa tangu kwenye Kamati husika na wadau mbalimbali kwamba jasho hilo halikupotea bure.

Niishukuru sana Serikali kupitia Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa aliyofanya. Wataalam wote waliokuwa nyuma ya hii, *a lot of thinking and hardwork* imeendana na kazi hii. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na timu yako yote, nawashukuru sana na mimi huwa sifichi, si mchoyo kwa kutoa au kumegea wenzako.

Waheshimiwa Wabunge, mimi nimemwambia AG mchana tulipomkuta anatoka, katika Miswada michache ambayo nimeona imeandikwa vizuri na kwa mtiririko ambao unauona kabisa hupotei msituni ni huu, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Tunatarajia sasa hayo ambayo yanaenda kukamilisha katika kupitia Kifungu cha 30 kuandaa zile kanuni yatafanyika kwa ushirikishi ule ule ambao umetufikisha katika hatua hii na Kanuni maana sasa hivi Bunge limekasimu madaraka yake, kwa Waziri mwenye dhamana ya mifuko hii akatengeneze kanuni ni Bunge limekasimu, lakini halijajivua madaraka yake ya kuangalia ni nini kinachoenda kutekelezwa katika kukasimu.

Kwa hiyo, tunaamini watakapokamilisha Kanuni hiyo au Kanuni hizo zitawasilishwa humu humu Bungeni na baada ya pale kwa taratibu za kawaida zitapelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo watazipitia na kama wataona kuna masuala ambayo hayajakaa vizuri wataiita Serikali kwenye Kamati na kama haijakaa vizuri watatoa taarifa Bungeni kwamba tumegundua kitu ambacho ni tofauti na matarajio yetu katika kupata kile kikokotoo.

Lakini siamini kwamba itakuwa hivyo kwa sababu wataalam ninaowafahamu ndani ya Serikali na Mifuko ni wengi na ni wazuri na weledi ni wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Tuliongeza muda tumefika hapo vizuri, Mheshimiwa Bilago nakushukuru *as a Parliamentarian* umefanya kazi nzuri na wote mlijenga hoja. *(Makofi)*

Sasa kwenye taratibu hizi wengi wape, umeyasema ya kwako, Kamati imesikia na Watanzania wamesikia, lakini kwa sababu hoja hii ni ya msingi na Serikali imeyaeleza vizuri kwanini hoja yako haukuweza kuichukua, siyo kwa sababu ya wingi tu wa upande huu hapana, ile mantiki yenyewe. Kwa hiyo, niwashukuruni sana, sina mengine ya ziada kwa leo sina matangazo. *(Makofi)*

Nimalizie tu kama nilivyoanza kwa kuwashukuruni sana kwa ushirikiano mlionipatia kwa siku ya leo kwa kufanikisha kazi iliyokuwa mbele yetu.

Baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Alhamisi Saa Tatu Asubuhi.

(Saa 2.05 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 1 Februari, 2018 Saa Tatu Asubuhi)